New Testament Survey – updated 01/07/2015

UTANGULIZI WA AGANO JIPYA

Kwa miaka 400, sauti ya Mungu haikusikika. Huu ndio wakati ya Agano la kale na Agano Jipya. Wakati huu ambapo sauti ya Mungu hakusikika, historia inasema, mambo mengi yalifanyika. Wamedi ndio walikuwa watu wenye nguvu na utawala mkubwa wakati wa mwisho wa Agano la Kale. Alexander mkuu ndiye alikuwa kiongozi wa Ugiriki, nchi ambayo ilikuwa na nguvu nyingi. Baadaye Warumi walitokea ambao walitawala wakati wa Agano Jipya. Tutazame historia fupi ya watu wa Mungu kutoka wakati wa Solomoni hadi Agano Jipya.

1. Nchi ya Israeli ambayo ilijulikana kama nchi ya kasikazini ilikuwepo kati ya 930 BC hadi 722 BC. Kwa jumla taifa hili lilikuwepo kwa miaka 208. Taifa hili liliancha kuwepo wakati Waashuru walikuja na kuwapeleka watu wa taifa hili katika utumwa. Huu ndio ulikuwa mwisho wa taifa hili hadi leo. Taifa la Yuda lilikuwepo katika mwaka wa 930 BC hadi 597 BC. Kwa jumla taifa hili lilikuwepo kwa miaka 333. Yuda baadaye alipelekwa katika utumwa na Wababeli.

2. Miaka 70 baadaye baadhi ya Wayahudi walirudi Yerusalemu na waliendelea kuishi humo chini ya utawala wa Wamedi.

3. Wagiriki na wale ambao walikuja baada yao, walitawala Israeli kutoka 331 BC hadi 164 BC. Mwanzoni, Wayahudi waliendelea vyema na kunawili chini ya uongozi wa watu hawa. Jambo hili lilibadilika katika mwaka wa 198 BC wakati kikundi kingine cha Wagiriki kilichukua hatamu za utawala wa taifa la Israeli. Hawa walikuwa wakatili sana kwa Wayahudi, na waliwalazimisha wayahudi kuabudu miungu na kula nyama ya wanyama ambao walikatazwa.

4. Utawala huu mbaya ulifanya kuwe na uasi ambao ulifaulu. Kati ya mwaka wa 166-63 BC, vikundi viwili ambavyo vilikuwa vikipingana vilijitokeza huko Yuda. Hawa walikuwa Mafarisayo na Masadukayo, hawa ni watu ambao kila mara walikuwa wanampinga Kristo. Mafarisayo walikuwa watu wa sheria na Masadukayo walikuwa watu ambao hawakuamini katika maisha baada ya kufa, kwa sababu hii, hawakuamini katika jahanum. Vikundi hivi viwili Kristo alivikemea sana. Wakati Masadukayo walikuwa wakiongoza, waliwasulibisha Mafarisayo 800.

5. Kwa sababu ya kuwepo kwa Wagiriki, Agano la kale lilitafsiriwa katoka Kiebrania kwa Kigiriki. Jambo hili lilifanyika na wasomi 70 ambao walihakikisha kwamba tafsiri hizi ni sahihi.

6. Kwa sababu ya kupingana kwa vikundi hivi viwili, Warumi walikuja na kutawala Israeli na huu ndio ulikuwa wakati wa mwisho wa kujitawala hadi baada ya vita vya dunia vya pili.

7. Inadhaniwa kwamba Kristo alizaliwa 6 BC na kifo chake mwaka wa 30 AD. Ukweli ni kwamba hakuna yule ambaye anajua kabisa siku wakati Yesu aliishi humu duniani.

8. Baada ya kifo cha Kristo, Wayahudi waliasi dhidi ya serikali ya Warumi na wengi waliuliwa. Mwaka wa 70 AD, walishindwa vibaya sana na Hekalu na mji wa Yerusalemu viliharibiwa vibaya sana. Wale wayahudi ambao walibaki, walilazimishwa kutoroka Israeli na kutawanyika ulimwenguni kote. Kwa sababu hii, hawakuwa na mahali pa kutolea sadaka zao kwa Mungu kwa zaidi ya miaka 2000.

Warumi walitawala ulimwengu wote isipokuwa sehemu ya kusini mwa Afrika na mashiriki ya bara la Indi. Waliweka sheria ambazo zilihakikisha kuwepo kwa amani. Waliwalazimisha watu wazungumze lugha ya Kigiriki ambayo ni lugha imetumika katika uandishi wa Biblia.

Lugha ya Kigiriki ina maneno mengi ambayo yanamaanisha upendo. Kwa mfano neno mume, linamaanisha upendo, upendo wa undugu na upendo wa baba. Walikuwa na barabara nzuri sana ambazo ziliwawezesha kueneza injili ya Kristo. Mungu alipanga kwamba wakati huu ndio ulikuwa wakati bora wa Kristo kuzaliwa katika ulimwengu huu na ujumbe wa Injili kuandikwa, na dini ya Kristo kuenea sana. Kwa mfano, wakati Paulo alifika Roma alikuta wakristo wakimgoja. Kumaanusha kwamba injili ilikuwa imefika huko tayari.

Agano Jipya linatuelezea maisha ya Kristo Yesu hapa ulimwenguni. Tunasoma kutoka kwa Kristo kwamba kuna njia moja tu ya sisi kufika mbinguni, ambayo ni kumwamini Yeye na kuishi maisha yetu tukiongozwa na Roho Mtakatifu. Tunapaswa kutubu dhambi zetu na kumfuata Kristo kwa utiifu. Agano Jipya limejawa na maagizo kwetu jinsi tunapaswa kuishi maisha yetu tukiwa wakristo. Kuna mafundisho kuhusu maisha ya mbeleni kama kurudi kwa Kristo Yesu.

MAFUNDISHO YA JUMLA YA VITABU VYA INJILI

Kuna vitabu vinne katika Biblia ambavyo vinajulikana kama vitabu vya Injili: Mathayo, Marko, Luka na Yohana. Vimepewa majina yake kutokana na wale ambao wameviandika na vinatueleza kuhusu maisha ya Kritso. Mathayo aliandika akiwaeleza Wayahudi kwamba Yesu ndiye Mesaya na Mfalme wa milele. Marko aliwaandikia wakristo ambao walikuwa katika mji wa Roma akiwaeleza kuhusu Kristo ni nani, kazi ya Kristo na

mafundisho ya Kristo ni gani. Luka hakuwa Myahudi kwa hivyo yeye aliwaandikia watu wa Mataifa akiwaeleza kwamba Kristo ni mwanadamu kamili na mwokozi kamili. Yohana aliwaandikia wale ambao walikuwa wameokoka na wale ambao hawakuwa wameokoka kuwaeleza kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu na kwamba wale wote ambao wanamwamini Kristo watapata uzima wa milele.

Vitabu vitatu vya Injili, yaani Mathayo, Marko na Luke vina matukio sawa na kwa hivyo huwa vimewekwa pamoja na kuitwa fanani injili (Synoptic gospels). Kitabu cha Yohana kinamaandiko ambayo hayapatikani katika vingine vitatu. Wengi wamesema kwamba kama vitabu vingi vya Biblia vyote vingepotea na tubakishe Yohana na warumi, ukristo ungeendelea.

Tutazame baadhi ya vifungu kutoka katika vitabu hivi vya injili. Tutazame kwa karibu sana Mathayo 5-7 ambacho ni kifungu cha hotuba ya Kristo mlimani. Tutatazama mambo ambayo yanafanana katika kitabu cha Mathayo, Marko na Luka na halfu tutatazama Yohana ambacho uandishi wake ni tofauti na vingine. Kwa mfano Yohana ana mifano, na miujiza saba ambayo haipo katika vitabu vingine vya injili. Kitabu cha Yohana kinamafundisha ya ndani sana kwa sababu kinashughulika na hali ya Kristo, jinsi alivyo na maana ya kuwa na imani katika Kristo.

Mathayo

Mwandishi wa kitabu hiki Mathayo, alikuwa mtoza ushuru. Kazi hii ilikuwa ni kazi ambayo wale ambao waliifanya walichukiwa sana na watu kwa sababu waliwatoza watu kiwango cha pesa ambacho kilikuwa kikubwa kama ya njia ya kuwanyanyasa. Yeye aliitwa na Kristo na akamfuata Kristo. Hii inaonyesha kwamba mtu yeyote anaweza kuwa mfuasi na mfanyakazi wa Kristo, akimwamini Kristo. Wokovu hauna mipaka ya kabila, rangi, masomo, utajiri au umaskini; wote ambao wanamwamini Kristo wanaokolewa na kutumika na Kristo katika ufalme wake.

1. Mathayo 1:1-17, tunasoma kuhusu ukoo ya Kristo. Mstari wa 1 unatukumbusha kwamba Yesu ni mwana wa Abrahamu na ni mwana wa mfalme Daudi. Hili ni jambo la muhimu sana kwa sababu linatimiza ahadi ya Mungu kwa Abrahamu (Mwanzo 12:1-9) na kwa Daudi (Isaya 11:1 na 1 Samweli 7:12-16).

A. Mwanzo 12:3, Mungu alimwahidi Abrahamu kwamba watu watabarikiwa kupitia kwa uzao wake. Hizi baraka zinakuja kupitia kwa Kristo. Baadaye katika 1 Mambo ya Nyakati 17:14, Mungu alimwahidi Daudi kwamba kiti chake cha ufalme kitadumu milele. Hata hii ahadi inamhusu Kristo. Zaburi 132:11 na Yeremia 23:5, tunasoma kwamba watu walikumbushwa kuhusu hii ahadi kutoka kwa Mungu.

B. Katika ukoo huu pia tunasoma kuwahusu wanawake watano ambao wanatukumbusha kwamba wakati mwingine Mungu anafanya kinyume na matarajio ya wanadamu. Kumbuka kwamba katika ukoo wanawake hawakuwa wakihesabiwa.

i. Mathayo 1:3, tunakumbushwa kuhusu Tamari ambaye tunasoma hadith yake katika Mwanzo 38:1-30. Huyu Yuda ambaye alifanya uashareti na Tamari, kutoka kwake, tunapata kabila la Yuda ambamo Kristo alitoka.

ii. Mathayo 1:5, tunasoma kumhusu Rahabu ambaye alikuwa kahaba. Kristo habagui katika kazi yake ya kuokoa. Wale wote ambao wanamwamini Kristo wanaokolewa, haijalishi wao ni kina nani, wametoka wapi wamekuwa wakiishi maisha ya aina gani, wote wakimwamini Kristo kama Rahabu, wote wanaokolewa.

iii. Pia tunasoma kumhusu Ruthu katika mstari wa 5 ambaye pia anahesabiwa katika ukoo wa Daudi. Ruthu alikuwa anatoka Maobu. Katika Kumbukumbu la Torati 23:3-5, tunasoma kwamba watu wa nchi hii Mungu alikuwa amewalaani. Ruthu na Boazi walikuwa wazazi wa baba wa Daudi. Tena tunakumbushwa kwamba katika Kristo hakuna kizuizi. Wayahudi na watu wa mataifa wote ni watoto wa Mungu wanapomwamini Kristo. Pia ni kutuonyesha kwamba Kristo hakuja tu kuwaokoa Wayahudi alikuja kuwaokoa watu wa ulimwengu ambao watamwamini (Yohana 3:16).

iv. Mathayo 1:6, tunasoma kwamba Bathsheba ambaye alikuwa mke wa Uriya pia anahesabiwa katika koo hii. Yeye na mfalme Daudi walifanya uasherati. Fundisho ni kwamba hakuna dhambi ambayo Yesu hawezi kusamehe. Yesu alisema, “sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi” (Mathayo 9:13).

v. Mathayo pia anataja Maria mama wa Yesu. Maria alitimiza ahadi ya Mwanzo 3:15.

2. Mathayo 1:18-23, tunasoma kuhusu utabiri wa kuzaliwa kwa Kristo. Mari ambaye alikuwa bikira alikuwa mjaa mzito. Hii ilitimiza unabii katika Isaya 7:14.

A. Yesu kuzaliwa na bikira ulikuwa muujiza mkubwa sana. Yesu, mama yake na baba yake walikuwa na Roho Mtakatifu. Yesu alikuwa mwanadamu kamili na pia alikuwa Mungu kamili. Yesu hakuwahi tenda dhambi kwa sababu alichagua kumtii Mungu na kifo chake kilimtosheleza Mungu.

3. Mathayo 2. Hadithi inapatikana katika kitabu cha Mathayo pekee. Hii ni hadithi kuwahusu wachungaji ambao walifamishwa kuhusu Yesu wakati alizaliwa. Wao walikuja kumwabudu Yesu. Herode alikuwa anamtafuta Yesu amwue lakini Mungu alimlinda kwa kuamuru Yusufu atorokee Misri.

4. Pia tunasoma kumhusu Yohana Mbatizaji ambaye alikuja mbele ya Kristo. Kazi ya Yohana Mbatizaji ni timizo la unabii wa Agano la Kale (Isaya 40:1-5 na Malaki 4:5-6). Kazi ya Yohana Mbatizaji ilikuwa kutangaza kuja kwa Kristo Yesu (Mathayo 3:1-3).

A. Ubatizo wa Yohana Mbatizaji ulikuwa umekusudiwa kutangaza kuja kwa Kristo Yesu na Agano Jipya. Kwa hivyo ubatizo huu uliwandaa watu kwa ajili ya kuja kwa Kristo. Yesu alibatizwa kama njia ya kujitambulisha pamoja na Wayahudi na kutangaza kwamba amekuja kuchukua na nafsi ya wenye dhambi kwa kuadhibiwa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu.

5. Mathayo 4, tunasoma kuhusu hadithi ambayo inapatikana katika vitabu vya Mathayo, Marko na Luka, Mathayo 4:1-11, tunasoma kwamba Yesu aliongozwa katika jangwa na Roho Mtakatifu kufunga siku 40. Baada ya kufunga, Yesu alijaribiwa. Jambo la kwanza shetani alimjaribu nalo ni chakula kwa sababu alikuwa na njaa. Yesu aliyashinda majaribu yote. Kujaribiwa si dhambi. Tunatenda dhambi wakati tunaanguka katika dhambi. Yesu Kristo alishinda majaribu yote ya shetani na hakufanya dhambi yoyote.

Yesu alijaribiwa kwa mambo matatu: chakula, mamlaka, na mali ya ulimwengu. Hivi ndivyo vitu hata leo ambavyo tunajaribiwa navyo, na wengi wameanguka katika dhambi kwa sababu ya haya mambo matatu. Pia wengi wameendelea kukataa ujumbe wa Injili kwa sababu ya mambo haya matatu.

6. Yesu alianza huduma wake baada ya Yohana Mbatizaji kuwekwa gerezani. Mathayo 4:17, tunasoma kwamba ujumbe wa Yesu ulikuwa ujumbe wa toba ambao Yohana pia alihubiri. Pia aliwaita wanafunzi wake. Katika mstari wa 18, tunapewa majina yao: Simoni Petro na Andrea ambao walikuwa wavuvi. Mstari wa 19 tunasoma sababu ya Kristo kuwaita; aliwaita ili wawe wavuvi wa watu kumaanisha kwamba aliwaita ili wawahubirie wengi na kuwaleta katika Ufalme wa Mungu.

Hii ndio kazi ya kila mhubiri wa Injili. Kuhakisha kwamba anahubiri Kristo kwa watu wote, kwamba Kristo ndiye njia ya kuingia mbinguni. Hivyo ndivyo Ufalme wa Mungu unajengwa kupitia kwa kuhubiri Kristo kwa uaminifu.

7. Mathayo 5-7, tunasoma kuhusu hotuba ya Kristo mlimani. Tunasoma kwamba Kristo alienda mlimani na umati wa watu ukaketi na akaubiria. Haya ni mafundisho mazuri sana ambayo kila kanisa lafaa kufundisha.

A. Soma sura ya 5:2-12, hizi zinaitwa sifa za aliyebarikiwa. Someni na mjadili kila moja.

i. Mstari wa 3, tunasoma kwamba wale ambao ni maskini wa kiroho wamebarikiwa. Hii inamaanisha kwamba ni baraka kubwa sana kufahamu umasikini wako wa kiroho mbele za Mungu ili uweze kubarikiwa na Mungu.

ii. Katika mstari wa 4, tunasoma kwamba, wale ambao wanahuzunika wamebarikiwa. Huzuni huu ni huzuni kwa sababu ya dhambi. Huwa tunafarijiwa na ujumbe wa injili ambao unatupatia tumaini la msamaha wa dhambi kupitia kwa Kristo Yesu.

iii.Katika mstari wa 5, tunasoma kwamba wale ambao ni wapole wamebarikiwa. Hii haimaanisha upole wa uoga. Kitabu cha Hesabu kinatukumbusha kwamba Musa ndiye alikuwa mtu mpole sana. Mstari huu unatokana na Zaburi 37:11 na unamaansiha kukubali kile ambacho Mungu anapatia kila mmoja wetu na kufurahia kile ambacho ametupatia. Hatufai kuanza kupigana kwa sababu ya kupata vingi.

iv. Wamebarikiwa wale ambao wako na njaa na kiu cha utakatifu. Watu hawa wamebarikiwa kwa sababu wanataka kuishi kwa njia ambayo inamletea Mungu utukufu. Hii inawezekana tu wakati mtu ameokolewa na Kristo. Tamaa yetu inafaa kuwa watakatifu kama Kristo Yesu.

v. Mstari wa 7 tunasoma kwamba wale ambao wako na huruma wamebarikiwa. Hii ni kwa sababu huruma ndio kitu ambacho tunakipata wakati tumeokolewa. Hili ni jambo la ndani na ni baraka sana ikiwa pia tutawahururmia wengine. Mathayo 18:21-35, ni mfano kuhusu kuwahurumia wengine. Kwa sababu tunataka Mungu na wengine watuhurumie pia tunapaswa kuwa tayari kuwahurumia wengine. Soma Mathayo 6:12, tunaona jambo hili likisisitizwa. Kumbuka kwamba msamaha, huruma na upatanisho ndio moyo wa kila mkristo.

vi.Wamebarikiwa wale ambao wako na moyo safi. Hili ndilo fundisho la Zaburi 24:3-4. Wale ambao tumeokoka tumebarikiwa kwa sababu tuko na mioyo safi na tumeletwa katika Ufalme wa Mungu.

vii. Mstari wa 9, wamebarikiwa wale ambao ni wapatanishi. Hii inamaanisha wakati tunatangaza injili ya Kristo, huwa tunatangaza upatanishi kati ya watu na Mungu na pia miongoni mwa wakristo.

viii. Mstari wa 10, amebarikiwa yule ambaye anateswa kwa ajili ya haki. Kumbuka kwamba Bwana Yesu Kristo haahidi afya mzuri kila wakati, utajiri na ufanisi. Mistari ya 11-12, tunasoma kwamba tutazawadiwa kwa sababu ya uhusiano wetu na Kristo. Mstari wa 12, unasema kwamba ni vyema kuteswa kwa ajili ya Kristo kwa sababu tutazawadiwa mbinguni milele.

B.Mistari ya 13-16, sisi ni chumvi na nuru. Sisi ni chumvi wakati tunafanya kazi ya kuzuia ulimwengu usianguka katika giza. Sisi ni nuru wakati tunatangaza nuru ya injili kwa watu wote. Ushuhuda wetu ni wa muhimu sana.

i. Je, tunawezaje kupoteza ladhaa yetu kama chumvi? Tunapoteza wakati tunakata kuishi maisha matakatifu kwa ajili ya Kristo.

ii. Tunakuwa chumvi na nuru wakati tunatii na kumtumikia Mungu kwa uaminifu. Tunakuwa nuru wakati tunatangaza ujumbe wa Injili kwa wengine.

C. Mathayo 5:20, tunasoma kuhusu maisha ya wokovu. Yesu anasema kwamba, “Kwa maana nawaambia, haki yenu isipozidi haki ya walimu wa Sheria na mafarisayo, kamwe hamtaingia katika Ufalme wa Mbinguni” Fafanua jinsi tunaweza kuishi maisha haya. Je, tunafanya jambo hili kwa nguvu zetu?

D. Mafundisho mengine katika surah hii yanahusu mambo kama hasira, tamaa, talaka, kulipiza kisasi na kuwapenda maadui wetu. Kuna mafundisho mengi kuhusu jinsi tunapaswa kuishi maisha yetu. Tusome na tujadili msitari 21-48.

8. Mathayo 6, kuna mafundisho ya aina mbili lakini lengo ni moja. Tusome vifungu hivi vitatu halfa tuvijadili.

A . Mistari ya 1-4, tunafundishwa jinsi ya kutenda matendo mazuri.

B. Mistari ya 5-8, tunafundishwa kuhusu maombi

C. Mistari ya 16-18,tunafundishwa kuhusu kufunga. Mstari wa 16, unasema, mnapofunga na wala si ikiwa unafunga.

D. Haya yote yanatufundisha jambo moja. Tunafaa kufanya mambo haya yote, lakini tunapaswa kuyafanya kwa siri. Hatufai kuyafanya kwa ajili ya kuheshimiwa na wanadamu. Si kwa sababu ya kuonyesha hali ya ukristo wetu kwa wengine au kwa sababu tunajaribu kumtii Mungu. Jinsi unavyomba na jinsi unavyotoa ni siri kati yako na Mungu.

E. Katika mistari ya 9-15, Yesu anatufundisha jinsi tunapaswa kuomba. Katika mstari wa 14, tunafundishwa jinis mioyo yetu inapaswa kuzingatia jambo la msamaha wa dhambi.

F. Mistari ya 19-24, tunafundishwa kuhusu mali na pesa. Hakuna mtu ambaye atatoka humu duniani na pesa, lakini tunatoka na matendo yetu mazuri.

G. Mistari ya 25-34, tunafundishwa kwamba hatufai kuwa na wasiwasi juu ya lolote, bali tunapswa kumwamini tu Mungu. (Warumi 8:28).

9. Mathayo 7, tunasoma kuhusu kuhukumu wengine (Luka 6), kuomba mambo fulani kutoka kwa Mungu, na kuhusu mti na matunda yake.

A. Mstari wa 12, tunasoma kuhusu kanuni kuu ya maisha; yaani tunapaswa kuwafanyia wengine jinsi tunataka wengine wa tufanyie.

B. Mistari ya 21-23, tunasoma kuhusu Kristo akizungumza juu ya wale ambao wanafundisha neno lake. Tunapaswa kuhakikisha kwamba sisi tumeokoka, na wala si kuzingatia yale ambayo tunayafanya. Kwa sababu mtu ni mhubiri wa neno la Mungu hiyo haimfanyi kuwa mtoto wa Mungu. Kuna uwezekano kwamba kuna wengi ambao wanahubiri neno la Mungu lakini wao hawajaokoka. Kwa hivyo tuhakikishe kwamba tumeokoka, kwa sababu hili ndilo la muhimu zaidi.

C. Katika mistari ya 24-27, tunasoma kuwahusu watu wawili ambao walijenga nyumba zao. Mmoja alijenga kwa mwamba na mwingine kwa mchanga. Yule ambaye alijenga kwa mwamba ni yule ambaye alimwamini Kristo na msingi wa matendo yao yote ni Kristo. Hawa ndio wako na tumaini la kweli la kuingia mbinguni. Wale ambao walijenga kwa mchanga ni wale ambao walitegemea matendo yao kuingia mbinguni badala ya kuwamini Kristo. Je, wewe unajenga kwa mwamba au kwa mchanga?

D. Mstari wa 29, tunasoma kwamba Kristo alihubiri kwa mamlaka. Je, ni kwa nini? Jibu ni kwamba Yeye ni Mungu.

10. Mathayo 8, tunasoma kuhusu miujiza nyingi ambayo ilifanywa na Kristo Yesu. Mathayo 7, inamalizikia kwa kusema kwamba Kristo alikuwa na mamlaka. Katika Mathayo 8, tunaanza kwa kuona jinsi Kristo alivyodhihirisha mamlaka haya. Yeye alifanya miujiza ambayo ilidhihirisha kwamba Yeye ni Mungu.

A. Mistari ya 18-22, kuna mafundisho ambayo wengi huwa wanapenda kuyapuuza. Kuwa mkristo haimaanishi kwamba hatuwezi kuwa wagonjwa, au kwamba hatuwezi kukosa. Ukweli ni kwamna kuwa mkristo ni gharama ambayo kila mmoja anapaswa kulipa.

11. Mathayo 9:35-38, tunsoma kwamba kuna wengi ambao wanapaswa kufikiwa na ujumbe wa injili lakini kuna machache ambao wako tayari kuwafikia na ujumbe huo. Kwa sababu tunahimizwa kwamba tuombe. No vyema wakati tunaomba kwamba Mungu awalete wengi wahubiri Injili, pia umwombe kwamba hata akutumia wewe katika kazi hii. Je, uko tayari kuenda?

12. Mathayo 10:6-15, tunasoma kuhusu kutumwa kwa wanafunzi wa Kristo kwa Wayahudi wawahubirie injili. Je, ni kwa nini walitumwa kwa Wayahudi pekee yao na wala si kwa watu wa Mataifa mengine? Jibu kwamba wakati wa kuwafikia watu wa mataifa memngine na injili ulikuwa haujafika.

A. Mistari ya 16-33, Yesu anafundisha kwamba injili ya pesa na uponyaji ni mbaya sana. Pia anasema kwamba wale ambao wanafuata kwa ukweli, wao watateswa. Hili fundisho la muhimu sana kwetu, hatufai kutarajia

kupendwa na kila mtu au kuwa na kila kitu au kukosa kuwa wagonjwa. Wale ambao ni waamini kwa Kristo, watateswa n ahata kuuliwa kwa sababu ya Kristo.

i. Kila mmoja wa wale ambao tumemwamini kristo, tunapaswa kutarajia mateso. Lakini hata bhivyo, Yesu anatuhimiza kwamba tunapaswa kuwa wavumilivu (19-20) kwa sababu Roho Mtakatifu aatakuwa hapo akitusaididia. Soma pia Matendo ya Mitume 1:18. Roho Mtakatifu atatupatia nguvu za kufanya kazi ya Mungu.

ii Mstari wa 28, kuna ushauri mzuri sana. Mateso yetu ya humu duniani ni ya muda mfupi sana kwa sababu karibuni tutatoka humo na kwenda mbinguni.

iii. Mistari ya 32-33, tunafundishwa kwamba tunapaswa kuwa wajasiri katika kuhubiri Kristo na kuwaeleza wengi kwamba sisi ni wafuasi wa Kristo.

13. Mathayo 11:1-15, tunasoma kwamba hata Yohana Mbatizaji alipokuwa gerezani, alikuwa na shaka kumhusu Kristo. Ili kuwahakikishia wanafunzi wa Yohana kwamba Yesu ndiye Kristo, Yesu aliwaambia watazame miujiza yake ambayo ilidhibitishia huduma wake kwamba kweli Yeye alikuwa ametumwa na Mungu. Katika mstari wa 11, tunasoma kwamba yule ambaye ni mdogo sana katika mambo ya mbinguni, yeye ana nafasi kubwa sana minguni kuliko yule ambaye ni mkuu katika ulimwengu huu.

14. Mathayo 12:1-21, upinzani dhidi ya Kristo uliendelea kukua haswa kutoka kwa Mafarisaya ambao walimshutumi Kristo kwamba hazitii sheria ambazo wao walikuwa wameongeza juu ya neno la Mungu. Jambo kuu lilikuwa kuhusu siku ya sabato. Katika mstari 1-8, unahusu kuhusu kuvuna na kula siku ya sabato. Katika mistari ya 9;13, Yesu alimponya mtu siku ya Sabato. Kwa sababu hii, Mafarisayo walitafuta njia ya kumwua Kristo.

A. Siku ya sabato

i.Mwanadamu ni mtu wa muhimu sana kuliko kutii sheria ambazo si ya Biblia (Luka 14:5). Maisha ya mwanadamu ni ya muhimu sana.

ii. Siku ya sabato ni zawadi ya Mungu kwa mwadamu (Marko 2:27).

iii. Marko 2:28, Yesu Kristo ndiye Bwana wa Sabato. Hapa Kristo alikuwa anasema kwamba Yeye ni Mungu. Kwa ufupi Kristo ndiye sheria zake zinafuata kufuata kuhusu siku ya Sabato.

James Boice anasema kwamba siku ya Sabato inafaa kutumika kwa njia mabayo inamleta Kristo utukufu. Ni siku ya wale ambao wameokoka. Tunapaswa kufurahia siku ya Sabato kwa ushirika na pamoja na kuwa pamoja na jamii zetu. Tunapaswa kuacha kazi zetu za kila siku na kupumzika.

C. Mafarisaya walikuwa wameongeza sheria nyingi kuhus siku ya sabato ambazo zilifanya maisha kuwa magumu sana. Hizi sheria za mafarisayo zilikusudiwa kuonyesha kwamba wao walikuwa watu ambao walitii mafundisho ya siku ya sabato. Kwa njia walionekana kuwa watu ambao walitiii sheria, lakini kwa ndani walikuwa wasi wa Mungu.

Yafuatayo ni baadhi ya mambo ambayo Mafarisayo waliongeza kwa neno la Mungu.

"Mafarisaya walikuwa wameongeza kanuni za wanadamu kwa neno la Mungu. Wao waliwafanya watu wasitii yale ambayo Mungu alikuwa amesema badala yake watii kile ambacho wao walitaka."

1. Sheria ya Mungu ilisema kwamba mtu hakufaa kusafiri siku ya Sabato (Kutoka 16:29). Je, kusafiri ni kufanya nini? Mafarisayo waliuliza? Jibu lao lilikuwa kwamba mtu hafai kusafiri zaidi ya mita 300. Kwa hivyo walikubali kwamba mtu anaweza kusafiri huo umbali na ikiwa ataenda zaii basi atakuwa anatenda dhambi. Lakini ikiwa kambi ilikuwa imefungwa kando ya mji, basi mita 300 ilikuwa inahesabiawa baada ya kambi. Pia ikiwa mtu huyo alikuwa ameweka chakula chake mahali fulani siku ya ijumaa, basi alikubaliwa kuenda kukichukua siku ya sabato.

2. Sheria pia ilikataza kubeba mzigo siku ya sabato (17:21-27). Lakini swali lilikuwa mzigo wa aina gani? Je, ulikuwa kipande cha nguo? Mafarisay walijibu jibu kwa kusema kwamba ilikuwa haikuwa nguo ambayo ilivaliwa bali ile ambayo ilikuwa imebebwa. Kwa hivyo njia ya kubeba nguo moja kutoka chumba kimoja hadi kingine ilikuwa ni kuvaa kwa mwili.

3. Sheria ya Mungu alisema kwamba watu wasifanye kazi. Kwa hivyo waliuliza, je ikiwa mtu anaondoak na hakafu anathema mate, je hiyo ni kazi? Walijibu kwa kusema kwamba ikiwa mate hayo yanapotelea kwa hewa, hiyo si kazi lakini ikiwa yanaanguka chini basi utukuwa umefanya kazi. Kwa sababu hii kuwa Myahudia ilitegemea unatema mate wap siku ya sabato.

15. Mathayo 23:28, tunasoma jinsi tunapaswa kuishi maisha yetu kulingana na mafundisho ya Biblia kuhusu siku ya sabato. Biblia inafundisha kwamba tunapaswa kula na kufanya kazi za huruma. Yesu anasema kwamba inahusu hali ya moyo wa mtu ambayo itamwongoza kutekeleza mapezni ya Mungu na wala sit u mambo ya nje. Kwa Mafarisayo, ilijumlisha tu mambo ya nje. Kwa sababu ya Yesu kuweka wazi unafiki wao, wao walimchukia sana.

A. Je, ni kwa nini siku ya sabato ni JUmapili na wala si Juma Mosi?

i.Yesu Kristo alifufuka siku ya Jumapili na kwa sababu kanisa la kwanza lilianza kukutana siku hii.

ii. Matendo ya Mitume 20:7, tunasoma kwamba kanisa la kwanza lilikutana siku ya kwanza ya Jumaa ambayo ni Jumapili.

iii. Kanisa la kwanza lilikuwa na wakati mgumu sana wa kuwaongoza wale ambao walikuwa wameokoka miongoni mwa Wayahudi kuwasaidia kuishi maisha ya ukristo wa kweli. Wengi wao waliwaza kwamba walihitaji kuzifuata sherai za Agano la Kale za Wayahudi. Kwa sababu lilikuwa jambo la muhimu sana kwa kila mmmoja wao kuelewa kwamba dini ya ukristo ni tofauti kabisa na dini ya Kiyahudi. Walihitaji kuelewa kwamba Agano la kale lilikuwa limepita na sasa kulikuwa na agano Jipya. Kukutana siku tofauti na Wahayudi wa dini iliwasaidia sana kuelewa hili. Hata katika wakati wao wa kufunga, kanisa la kwanza lilifunga siku tofauti na dini ya Wayahudi kuonyesha kwamba Ukristo ni tofauti kabisa.

16. Mathayo 12:24-37, kifungu hiki kinazungymza juu ya dhambi ambayo haisamehiwi. Katika mstari 24, tunasoma kuwahusu Mafarisayo wkimtusa Kristo. Wao walisema ni kwa nguvu za Belzabebuli alikuwa anafanya miujiza. Katika mstari wa 31, tunasoma kuhusu dhambi ambayo haisamehewi ambayo ni kumkufufru Roho Mtakatifu. Je, dhambi hii ni dhambi ya aina gani? Jibu ni, Roho Mtakatifu ndiye huwa anatudhibitishia dhambi na kutufanya tuupokee Ujumbe wa Injili. Kwa hivyo dhambi ambayo haisamehewi ni dhambi ambayo mtu anakata kazi ya Roho Mtakatifu na kwa sababu hii, Mungu anaufanya moyo wake kuwa mgumu sana. Kwa kukataa Roho Mtakatifu, huwa tunamkataa Kristo Yesu mwenyewe.

Wale ambao wanatenda dhambi hii, huwa hawajali kabisa. Kwa wale wote amabo wameokoka, wao hawajatenda dhambi hii.

17. Mathayo 13, kuna mifuno mingi ambayo tunaisoma. Mfano ni hadithi ambayo ukweli umefichwa ndani ya hadithi hiyo. Ili mtu aweze kuufahamu mfano wa Kristo, yeye anapaswa kuwa mfuasi wa Kristo. Ili tuweze kueelewa mfano, lazima mtu ajue unazungumza juu ya nini. Katika mistari ya 1-9, tunasoma kuhusu mfano wa mpanzi ambao tunaopata maana yake katika mistari ya 18-23. Mistari ya 44-46, mfano huu unafundisha kwamba watu hawa waliona umuhimu wa ufalme na kwa sababu hiyo walikuwa tayari kufanya lolote ili waweze kuupata ufalme. Waza juu ya maisha yako kulingana na fundisho hili.

18. Mathayo 14, tunasoma kuhusu jinsi Yesu alivyowalisha watu 5,000 katika mistari ya 13-21. Hadithi inaonyesha jinsi Kristo alivyo na huruma kwa wale ambao wako na njaa na Yeye anaweza kuwapa mahitaji yao.

19. Mathayo 16:21-23, tunasoma kumhusu Kristo akiwatayarisha wanafunzi wake juu ya kifo chake. Tazama jinsi Petro alimjibu Kristo na pia jinsi kristo alivyomjibu Petero. Kifo cha Kristo mslabani kilikuwa kimesudiwa na Mungu ili shetani ashindwe na sisi tupate kukombolewa. Kukataa hili, kutakuwa kumkataa Mungu. Kumbuka kwamba kila wakati Mungu anadhibiti kila kitu na kila hali.

20. Mathayo 16:24-25, tunasoma kwamba ni lazima kila wakati tuwe tayari kuteseka kwa ajili ya Kristo. Mfano ambao uko katika Mathayo 13:44-46, unasema kwamba ni lazima tuwe tayari kutoa kila kitu kwa ajili ya ufalme wa Mungu.

Hadithi hii ifuatayo ni kweli: Kulikuwa na msichana mmoja uko nchi ya Amerika. Msichana huyu alikuwa mwislamu na baadaye aliokoka. Wazazi wake walijaribu kumshawishi alirudi katika dini ya kiislamu. Kwa sababu alikataa, familia yake, walimtesa na kwa sababu hiyo alitoroka nyumbani kwao. Msichana huyu aliuliwa huenda na wazazi wake. Kile ninaonyesha hapa ni kwamba kama msichana huyu, ni lazima tujue kwamba kuna gharama kwa kumfuata Kristo.

21. Mathayo 17:1-8, tunasoma kuhusu kun'ga kwa Yesu na mavazi yake. Jambo hili tunalisoma katika Marko na Luka na katika 1 Petro 1:16-18. Kung'a kwa sura na mavazi ya Kristo kulidhibitisha Uungu wake. Pia kulidhibitisha utukufu ambao Kristo alikuwa anaenda kuingia na ule mabo atakuwa wakati wa kurudi kwake.

Lakini pia tukumbuke kwamba wakati huo Eliya na Musa walionekana wake naye. Je, hili linatufundisha nini? Agano la Kale limjumlisha maandishi ya Musa ambayo ni sheria na maandishi ya manabii. Musa alidhirisha sheria na Eliya manabii. Musa na Eliya walikuwa wanadhibitisha kwamba yote ambayo yaliandikwa na Musa na manabii kama Eliya, yote yalikuwa yanatuelekeza kwa Kristo. Kwa sababu ndipo sauti ilisikika ikisema, huyu ndiye Mwanangu sikizeni Yeye.

22. Mathayo 19:3-9, tunasoma kuhusu mafundisho ya ndoa na talaka. Katika Mwanzo 2:24, machoni pa Mungu wawili ambao wameoana wanakuwa kitu kimoja; yaani mume na mke wanakuwa kitu kimoja. Yesu Kristo ananukuu mstari huu kuonyesha kwamba anachukia talaka. Yesua nasema kwamba Musa alikubali talaka kwa sababu mioyo ya watu ilikuwa migumu kusameheana. Talaka ni kitu kibaya sana kwa sababu ni kutenganisha kile ambacho Mungu ameweka pamoja. Pia talaka huwa inasababisha maisha mabaya kwa watoto. Tunapaswa kila wakati kuwahimiza watu waombe na watafute usaidiza lakini wala si kuwahimiza ktalakiana. Tukifanya hivyo, tutakuwa tunashirika katika kazi ya shetani ya kutenganisha kile ambacho Mungu aliweka pamoja.

Tutazame mafundisho mengine kutoka katika vitabu vingine vya Injili. Kitabu cha Marko hatutakigusa si kwa sababu si cha muhimu bali ni kwa sababu ya muda. Kwa hivyo mwanafunzi anapaswa kukisoma na kuhakikisha kwamba anakielewa.

Kitabu cha Luka

Luka anatueleza kuhusu maisha ya kwanza ya bwana Yesu Kristo. Luka hakuwa Myahaudi, alkini yeye alikuwa daktari. Luka pia alikiandika kitabu cha Matendo ya Mitume. Luka katika maandishi yake, anatupatia picha ya

mbunguni na jahanumu. Yeye pia anatufundisha mengi kuhusu maombi. Kwa sababu ya wakati hatutakizama kitabu chote cha Luka. Lakini tutatazama mafundisho yake ambayo hayamo katika vitabu vingine vya injili.

1. Luka 1:26-56, tunasoma kumhusu Maraia ambaye ni mama ya Yesu. Yeye si mungu kama jinsi makanisa mengine yanavyofundisha. Yeye alikuwa mwenye dhambi kama mtu yeyote na alihitaji wokovu.

2. Luka 2:8-20, malaika walileta habari za kuzaliwa kwa Yesu kwa wachungaji ambao ndio walikuwa wakudharauliwa kabisa katika jamii.

3. Luka 4:16-30, Yesu alianza huduma wake baada ya kujaribiwa katika jangwa. Yeye alianza kwa kufundisha katika Sinagogi huku Nazareti. Hii inatuonyesha umuhimu wa kukutana pamoja na kuabdu Mungu kwa sababu hapa tunamwona Kristo akiwa ameenda kuabudu.

A. katika mistari ya 16-21, tunasom kumhusu Kriso akisoma maandiko kwa watu. Yeye alinukuu kifungu kutoka kwa saya kuhusu kuja kwa Mesaya. Aliotangaza kwamba Yeye ndiye anatimiza unabii huo. Anasema kwamba Yeye ndiye Mesaya.

B. Katikas mstari wa 25-26, Yesu anaeleza hadithi ya Eliya na jinsi alivyoenda kwa mjane ambaye hakuwa Myahudi huku Zerafati na kumhudumia.

C. Katika mstari wa 27, Yesu anazungumza kuhusu Nahamani ambaye hakuwa Myahaudi jinsi alivyoponywa. Ujumbe kwa wayahudi ni kwamba Mungu hakuwa Mungu wa Wayahudi pekee. Mungu ni Mungu wa watu wote.

D. Katika mstari wa 28-29, maneno ya Yesu Kristo yaliwakasirisha Wayahudi sana. Kwanza walikasirika kwa sababu Yesu alisema kwamba Yeye ni Mungu. Pia walikasirika zaidi kwa sababu Yesu alisema kwamba Mungu ni watu wote na si wa Wayahudi pekee.

E. wayahudi walitaka kumwua Kristo lakini katika mstari wa 30, tunasoma kwamba Kristo alitoka tu akaenda. Hii ni kwa sababu wakati wake ulikuwa haujafika wa kufa. Hapa tunaona kwamba Yesu alitawala kila kitu na wala si Wayahudi. Tukumbuke kwamba Yesu alikufa msalabani kwa sababu alitupenda. Alijitolea kufa kwa ajili yetu. Yeye hakulazimishwa na mtu yeyote kufa msalabani.

4. Luka 5, tunasoma kuhusu Yesu akiwaita baadhi ya wanafunzi wake. Tunaona kwamba aliwaita watu wa kawaida kama wavuvi wa samaki.

A. Mistari ya 27-32, tunasoma kwamba Yesu alimwita moza ushuru kuwa mwanafunzi wake. Lawi ambaye ndiye mathayo alimkaribisha Yesu na watoza ushuru wengine kwake na kula nao pamoja. Mafarisayo walimkemea Kristo kwa kula na wenye dhambi.

i. Mistari ya 31-32, tunafunzwa funzo muhimu kuhusu kazi ya kueneza ujumbe wa injili. Ni lazima tuhakikishe kwamba tunawahubirie wenye dhambi injili ya Kristo. Tunapaswa kufanya kazi hii kama tu vile Yesu alivyoifanya.

B. Mistari ya 33-39, tunasoma kuhusu yafuatayo:

i. Katika mstari wa 35, hatuja amurishwa kufunga, lakini ni jambo jema wakristo kufunga.

ii. Bwana Yesu anatumia mfano wa divai mpya kutuifunza kwamba kuhusu furaha ambayo inaambatana na Agano Jipya. Agano la Kale halikuwaletea furaha kwa sababu ya sheria zake, lakini Agano Jipya ambalo liaanzishwa na Yesu ni zuri sana. Kwa hivyo hatupaswa kuchanganya haya mawili.

5. Luka 6:37-38 na 41-42 pamoja na also Mathayo7:1, tunasoma kuhusu kuhukumu. Hii ni mistaria ambayo mara kwa mara huwa inanukuliwa vibaya. Tunasoma hili pia katika mahubiri ya Kristp Msalabani. Kuna wakati ambapo tunapaswa kuhukumu na tunapaswa kufanya jambo hili kulingana na mandishi ya Biblia. Tunapaswa Ni lazima tuhakikishe kwamba neno la Mungu linatuongoza katika kuhukumu kwetu. Yaani hatupaswi kunyamanza wakati tunaona dhambi.

A. Pia tunaonywa kwamba hatufai kuwa watu ambao kila wakati tunawashitumu wale ambao ni viongozi katika makanisa yetu kwa msingi ambayo si ya Biblia. Tusiwe watu wa kuleta mafarakano au wa kuwasengenya wengine. Katika mstari wa 41-42, tunaoma kwamba sisi sote tuna kasoro. Tuko na mambo ambayo tunapaswa tuhukumiwa nayo kwa sababu kila wakati tunatenda dhambi Tuhakikishe kwamba sisi hatuna hatia katika lile ambalo tunawahukumu wengine. Hatufai kuhukumu kwa haraka na kwa njia mbaya. Tunapaswa kuhukumu jinsi hata sisi tunapaswa kuhukumiwa.

6. Luka 6:39-40, tunapa mfano wa shida katika kanisa ambayo hata leo tuko nayo. Tunafundishwa kwamba tunapaswa kuwa na wachungaji ambao wanayafahamu maandiko vizru ili waweze kulisaidia kanisa la Mungu kufahamu ukweli wa neno la Mungu.

A. Katika mstari wa 39, tunaona wachungaji ambao hawajafunzwa wakijaribu kuwa wafundisha washirika wa kanisa neno la Mungu. Huu n mfano wa kipofu kuongoza kipofu.

B. katika mstari wa 40, kusudi la kanisa katika kuhubiri na kufunza neno la Mungu ni kwamba kumtukuza Mungu. Mungu anatukuzwa wakati watu wanaishi maisha yao kwa utukufu wa Kristo. Ikiwa mchungaji amejifunza vyema neno la Mungu, basi ni wazi kwamba ataweza kuwafundisha wengine vizuri. Yeye atawafaidi sana kiroho. Hili ndilo kusudi la ATA kuona kwamba kanisa la Kristo linajengwa na nuru ya Kristo inang'a hapa Afrika.

6. Yesu kila mara alitabiri kufa kwake, na kwa sababu kifo chake hakikuwa cha kushangaza. Yesu mwenyewe alizungumza kuhusu kifo chake katika Mathayo 9:21-27 na 43-45. Hii pia inatuonyesha kwamba Mungu anatawala kila kitu.

7. Luka 16:19-31, tunasoma kuhusu mbinguni na Jahanumu na pia tunasoma kuhusu kuzawadiwa hapa duniani n ahata kule mbinguni. Tajiri aliji furahisha wakati alikuwa hapa duniani lakini yeye hakuwa na Amani na Mungu. Wakati alikufa Yeye alipelekwa jahanumu mahali pa mateso. Lazaro ambaye alikuwa maskini alikuwa ameokoka. Wakati alikufa, Biblia inasema kwamba malaika alimpeleka katika kifua cha Abrahamu. Hapa tunaona mafundisho yafuatayo.

A. Mbinguni na jahanumu ni mahali pawili pa kweli. Mbinguni ni mahali pazuri na jahanumu ni mahali pabaya.

B. Mateso ya jahanumu yatakuwa mabaya sana kwa sababu wale ambao wako jahanumu watajua kwamba kuna mbinguni ambao wanaishi maisha mazuri sana. Wao watajuta kwamba kwa nini hawakuingia humo. Mimi ninawaza kwamba wale ambao wako mbinguni hawatajua wale ambao wako jahanumu kwa sababu hii itwaletea huzuni na Biblia inasema kwamba mbinguni si pahali pa huzuni (Ufunuo 21:4).

C. Kama tajiri, tusiishi katika anasa za Ulimwengu huu kwa sababu vitu vya ulimwengu vinapita. Utajiri wa ulimwenguni si ishara ya baraka za milele za Mungu juu ya mtu. Mtu anaweza kuwa tajiri sana lakini anaenda jahanumu. Lakini pia tukumbuke kwamba mtu akiwa ni tajiri na amwamini Kristo ataokoka. Si matajiri wote wanaenda jahanumu, wale ambao wameokoka wataenda mbinguni ikiwa watamwamini Kristo.

D. Kuwa maskini si ishara ya kwamba unaenda mbinguni. Lazaro ambaye alikuwa maskini hakuingia mbignuni kwa sababu alikuwa maskini, yeye aliingia kwa sababu alimwamini Kristo. Unaweza kuwa sana na hata uwe wakuhurumiwa na watu wote, na ujulikanane wewe ni maskini, lakini usipomwamini Kristo, wewe utaenda jahanumu kama tu tajiri ambaye alikuwa hajaokoka.

i. Mbinguni ni mahali pa furaha ya milele. (v 25).

E. Mstari wa 26, tunasoma kwamba mahali ambapo mtu ataenda baada ya klufa, hapa ndipo ataishi milele. Hakuna kutoka huko. Kuna wengine ambao wanafundisha kwamba mtu anaweza kuenda jahanumu na baada

ya muda fulani atoke humo, huo ni uongo kabisa. Kuna mahali pawili mtu ataenda akiondoka humu duniani; mbinguni au jahanum, hakuna pengine.

F. Mstari wa 31, tunasoma kwamba Biblia inatosha kuwamleta mtu kwa Kristo. Biblia inasema imani huja kwa kusikia neno la Kristo ambalo ni Biblia (Warumi 10:17). Pia tunaona kwamba wale ambao wanakataa kuokoka, wanakata hata kufufuka kwa Kristo.

G. Hadithi hii inatuonyesha kwamba vyeo au mali yetu katika ulimwengu huu si kitu cha maana. Kile cha maana ni hali yetu mbele za Mungu. Hakuna ubaya wa mtu kuwa tajiri katika maisha haya ya duniani ikiwa utajiri wake ni halali na kwamba yeye awe ana mwamini Kristo. Pia awe anafahamu kwamba Mungu anamtarajie awasaidie wale ambao hawana.

H. Pia kuna faraja kwa yule ambaye ameokoka na ni maskini katika ulimwengu huu. Maisha ya hapa ulimwenguni ni ya muda mfupi sana. Katika uzima wa milele, wale yule ambaye ameokoka, anazawadiwa vizuri. Kuna malaika ambaye anaongoja kutubeba na kutuingiza mbinguni. Ni lazima tuwe waaminifu katika kila jambo.

8. Luka 18:1-8, tunasoma kuhusu mfano ambao unatufundisha kuhusu ukakamavu. Mjane hakukubali uamuzi wa hakimu ambaye alikuwa mwovu. Mjane aliendelea kumweleza huyu tajiri hadi wakati alipomtendea haki. Tunapaswa kuendelea katika maombi kila wakati bila kukataa tamaa. Usikate tamaa katika maombi juu ya jambo fulani. Huenda wakati mwingine itabidii uombe kwa miaka mingi sana kabla Mungu akujibu na kwa wakati mwingine Mungu hataleta kile ambacho unataka. Lakini lazima tuendelea kuomba.

9. Luka 22:14-23, wakati walipokuwa katika chumba cha juu wakati wa chakula cha pasaka, Yesu alianzisha meza ya Bwana na aliwaambia wanafunzi wake wakula meza hiyo kwa kumkumbuka Yeye. Tutazama jambo hili kwa urefu katika 1 Wakorintho 11.

10. Tunapoendelea kusoma kuhusu masaa ya mwisho ya Kristo, tunaona kwamba alikuwa peke yake. Wanafunzi wake wote walimwacha. Katika marko 14:32-42, wakati aliwasihi wanafunzi wake wakeshe kwa maombi, lakini tunasoma kwamba wao hawakuweza, walilala. Katika Luka 22:44, tunaosma kwamba yesu alikuwa katika huzuni mwingi na aliomba hadi jasho lake likawa damu.

Yohana

Hiki ni kitabu cha Muhimu sana cha Biblia ambacho kiliandikwa na Yohana mwanafunzi wa Yesu. Yeye alikuwa mtume ambayo inamaanisha yule ambaye ametumwa. Yohana anaandika akimdhihirisha Kristo kwamba Yeye ni Mungu.

Tunasoma mengi kumhusu Kristo na Yeye ni nani (Mungu) katika kitabu hiki cha Yohana. Asilimia 90 ya kitabu hiki cha Yohana ni tofauti kabisa na vitabu vingine vya Injili. Katika kitabu hiki hakuna mifano.

1. Yohana 1:1-5, hii ni msitari ya muhimu sana. Yohana ataeleza kwamba Neno ambaye ni Kristo Yesu ni Mungu. Anasema kwamba Kristo ni Mungu ambaye ni wa milele na Yeye pia ni mwumbaji. Maisha yetu yanatokana na Kristo. Yeye nuru ambayo imeshinda nguvu za giza.
A. Swali kuu katika maisha ni, Je, Yesu Kristo ni nani? Je, yeye ni mwanadamu tu kwako au ni Mungu? Ndipo uwe mkristo ni lazima uamini kwamba Yesu ni Mungu na kwamba ni Yeye ambaye utamfuata. Je, hii inamaanisha nini kwako? Inamaanisha kwamba ni lazima umtii, umpende na umtumikie. Ni lazima utubu dhambi zako na umpokee Kristo.

B. Yohana 1:10-13, tunasoma kwamba ulimwengu ambao ni watu, walikataa kumpokea Kristo ambaye aliwaumba. Hadi leo ulimwengu bado unampinga Kristo. Isaya 1:3, nasema kwamba ngombe na punda wanaweza kujau bwana wao ni nani, lakini mwanadamu hawezi.

C. Yohana 1:12, wale ambao wanamwamini Kristo, wanafanyika wana wa Mungu. Wale wote ambao wamemwamini Kristo, tuko na kibali cha kuja kwa Mungu kwa maombi na Mungu kutushughulikia kwa sababu yeye ni baba wetu.

D. Yohana 1:13, tunasoma kuhusu jinsi mtu anafanyika mwana wa Mungu. Yaani jinsi mtu anapata imani ya kumwamini Kristo. Hali hii inaitwa kuzaliwa mara ya pili. Wokovu ni kazi ya Mungu. Ni mugnu ambaye anatupatia imani ya kumwamini Kristo. Hatuokoki kwa kuzawaliwa na wazazi wetu wa kimwili, tunaokoka kwa kazi ya Mungu mwenyewe. Ni Mungu ambaye anatuza mara ya pili.

E. Yohana 1:14, tunasoma kwamba Mungu amnaye ni kristo alikuja humu duniani na kuishi na wanadamu. Yeye aliacha utajiri wa mbinguni na alikuja hapa duniani na kuishi pamoja nasi. Yeye aliteseke na alijaribiwa kama tu sisi, lakini bila dhambi yoyote.

2. Yohana 2:1-11, tunasoma kuhusu muujiza wa kwanza wa Kristo Yesu alipogeuza maji yakawa divai. Yesu hapa alionyesha kwamba anajali maisha ya mwanadamu. Je, ni kwa nini Yesu alifanya miujiza? Sababu kuu ilikuwa kudhibitisha huduma wake. Sababu ya pili ni kwamba Yesu aliwahurumia sana watu na alifurahia kuwasaidia watu sana.

A. Yohana 2:12-17, Yesu alilisafisha kanisa kama tu vile Nehemia alifanya katika Nehemia 13:8. Hapa tunajifunza kwamba, tunafaa kuwazuia wale ambao hawajaokoka kujihusicha na mambo ya makanisa yetu. Tunapaswa kuwa waangalifu kwamba wale ambao ni wakristi wenye ushuhuda mzuri ndio peke yao wanahusishwa katika kazi ya kanisa. Hatufai kuwaacha watu kwa sababu wako na pesa kuzungumza katika

makanisa yetu. Tunapaswa kuwakubali tu wahubiri ambao wanahubiri neno la Mungu kwa uangalifu peke yao kuwazungumzia watu na wala si wanasiasa.

B. Yohana 2:18-22, Kristo ahapa alizungumza juu ya kifo na kufufuka kwake lakini hakuna hata mmoja ambaye alielewa wakti huo.

3. Yohana 3:1-15

A. Yesu alijua moyo wa Nikodemo kama tu vile anavyoijuwa miyo ya wanadamu wote. Nikodemo alitafuta kutosheka kiroho kulingana na jinsi yeye mwenyewe alijua na si kulingana na mapenzi ya Mungu.

B. Mistari ya 1-2, Nikodemo alikuwa kiongozi tajiri ambaye alikuja kwa Kristo Yesu. Yeye alitaka majibu kutoka kwa Kristo kwa sababu alijua kwamba Kristo alikuwa mtu muhimu lakini hata hivyo hakuwa tayari kukubali yale ambayo Kristo alimwambia. Katika mstari wa 13, Nikodemo alibishana na Kristo. Tukumbuke kwamba tunaweza kuja kwa Kristo Yesu kulingana na jinsi Yeye mwenyewe anataka na wala si jinsi sisi wenyewe tunataka. Kwa sababu hii, hatufai kuwa na mabishano na Mungu. Tukubali tu yale ambayo amesema.

C.Mistari ya 3-5, tunasoma kuhusu kuzaliwa mara ya pili. Wale ambao wameokoka, ni watu ambao wamezaliwa mara ya pili.

D.Mstari wa 5, tunasoma jambo la kuzaliwa kwa maji na Roho. Maana ya hii ni neno la Mungu. Mahali pengine katika Biblia tunasoma kwamba, “kwa maana mmezaliwa mara ya pili; siku kwa mbegu iharibikayo; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele” (1 Petro 1:23). Roho Mtakatifu hutumia Biblia ambalo ni neno la Mungu kutudhibitishia dhambi.

E.Mstari wa 6, tunasoma kwamba mwili huzaa mwili na Roho huzaa Roho. Mwanadamu huwa anamzaa mwanadamu mwenye dhambi. Roho wa Mungu humzaa mtu ambaye anaongozwa na Roho wake. Maisha matakatifu yanatokana na Roho Mtakatifu ambaye anaisha ndani mwa mtu. Ni lazima kuwa na mabadiliko katika maisha ya mtu ikiwa huyo mtu atwweza kuishi maisha yake kwa utukufu wa Mungu.

F. Mistari ya 14-15, hatuokolewi kwa matendo yetu mazuri bali kwa kumwamini Kristo.

4. Yohana 3:16, huu ni mstari ambao unajulikana na wengi sana leo. Wengi hawaelewi upendo wa Mungu.

A. Neno amini katika Kigiriki kinamaanisha imani. Kwa sababu hiyo tunasema kwamba yeyote ambaye anamwamini Kristo, ataokolewa. Imani si kitu ambacho kinaweza kushikwa lakini kinaweza kuonekana katika maisha ya watu. Hii ndio sababu Yakobo anasema kwamba kuna imani ambayo inaokoa (Yokobo 2:17-18).

B. Upendo wa Mungu hauna kipimo, yaani ni mkubwa sana hauna mwisho (Waefeso 3:17-19).

C. Upendo wa Mungu ni upendo ambao unapeana. Upendo wa Mungu ulimgharimu sana. Mungu Baba alipeana Mwana wake Yesu Kristo akaja humu duniani ili ateseke vibaya sana kwa ajili yetu.

D. Hadithi ya kitabu cha Hosea inatuonyesha kuhusu upendo ambao unagharimu. Tunaona kwamba kuna kufanana sana wakati tunaona upendo wa Hosea kwa Gomeri na upendo wa Mungu kwa watu wake.

i.Hosea likuwa mujme mzuri na ambaye alishughulikia mke wake kama tu vile Mungu alivyo.

ii.Hosea alikuwa na mke ambaye hakuwa mwaminifu. Gomeri alikuwa na wapenzi wengine kama tu vile watu wa Mungu walivyogeuka na kuanza kuabudu miungu. Lakini Hosea alienedelea kumshughulikia kwa sababu Mungu alimwamuru hivyo. Mungu anye aliendelea kuwashughuilikia watu wake ambao hawakuwa waaminifu. Hosea alimkomboa mkewe wakati alikuwa ameuzwa ka mtumwa kama tu vile Kristo anavyotukomboa sisi kutoka katika utumwa wa dhambi na shetani.

iii. Upendo wa Mungu kama tu ule wa Hosea ni upendo ambao unapenda kila wakati. Hata kama sisi ni wenye dhambi, Mungu hututafuta na kutukomboa kutoka kwa hatari ambayo tumejiingiza ndani.

E. Yohana 3:16-17, tunasoma kwamba Kristo alikuja humu duniani kutuokoa. Wokovu unapatikana kupitia kwa Kristo Yesu.

5. Yohana 3: 18-21, Je, ni kwa nini watu hawataka kumwamini Kristo ili waokolewe? Watu wwengi hawamtaki Kristo kwa sababu wanapenda na wafurahia dhambi zao. Wale ambao hawajaokoka wanawaza kwamba ikiwa wataokoka, furaha yao yote intaisha. Wao wanawaza kwamba wacha wafurahie anasa za dunia halfu baadye wao wataokoka. Hatari ya hii ni kwamba wao wanaweza kufa wakati wowote. Wanawaza kwamba watakufa wakati wao wamekuwa wazee. Huu ni uongo wa shetani. Anawapumbaza wawaze hivi. Wanapoendelea kutookoka, Mungu anafanya mioyo yao iendelee kuwa migumu sana na kwa nji hii hawataweza kuokoka kamwe na watakufa katika dhambi zao na kuingia jahanumu mahali pa mateso. Farao ni mfano mzuri sana.
A. Mistari ya 22-30,tunaosoma kuhusu unyenyekevu wa Yohana Mbatizaji na jinsi alivyomtukuza Kristo. Yohana Mbatizaji alikuwa mtu ambaye alikuwa amefanya huduma wake vyema lakini alikubali kuacha kazi hiyo kwa sababu Kristo alikuwa amekuja. Yohana macho yake yalikuwa kwa Kristo Yesu pekee.

B. Mistari ya 31-36, inadhibitisha huduma wa Kristo. Ni Yesu pekee ambaye alitoka kwa Mungu. Hakuna mwingine ambaye ametoka kwa Mungu akiwa na mamlaka kama Kristo. Yeye ana mamlaka haya kwa sababu Yeye ni Mungu. Ikiwa unamkataa Kristo, unakataa uzima awa milele na unachagua hukumu na ghadhabu ya Mungu. Huu ndio ukweli wa mstari wa 36.

6. Yohana 4:1-14, tunaona unyenyekevu wa Yesu. Katika mistari ya 5-7, tunaosma kwamba Yesu alikuwa amechoka na pia alikuwa na kiu. Yeye alikuwa Samaria mahali ambapo Wayahudi walichukia sana kwa sababu waliwaona Wasamaria kama watu ambao walichukua nchi ya ndgu zao. Yesu hakuja kwa ajili ya Wayahudi pekee, bali kwa ajili ya watu wote.

A. kama tu katika bustani la Edeni, Mungu alizungumza na Adamu kwanza akitaka kurekebisha uhusiano wao. Sisi wanadumu huwa hatumtafuti Mungu, bali ni mMungu ambaye mara kwa mara hututafuta ili tuwe na uhusiano na ushirika naye.

C. Mstari wa 10, Yesu aliahidi kumpa yule mama msamaria maji ya uzima. Je, maji hayo ni gani? Hii ni neema ya Mungu ambayo ni kama mto wa maji ambao unafanya maisha yaendelee kuwepo. Yesu leo anatuahidi uzima wa milele ambao hauishi kamwe kwa wale ambao wanamwamini.

Katika Agano la kale, tunasoma kuhusu maji haya ya uzima katika Isaya 12:3 na Zaburi 42:1 na Yeremia 2:13.

C. Mistari ya 23-24, tunasoma kuhusu jambo moja la pekee ambalo Mungu anataka kutoka kwa mwanadamu. Yeye anataka tumwabudu kwa Roho na kwa kweli. Kusudi la Mungu kwa mwanadamu ni mwanadamu amwabudu na Mungu chanzo cha furaha yake katika maisha yake yote. Mungua lituumba tumwabudu. Mungu anataka tumwabudu. Yeye hataki kingine kutoka kwetu isipokuwa kumwabudu pekee.

7. Kitabu cha Yohana kinatupatia mambo matatu ya muhimu sana ambayo yatatufanya tumwabudu Mungu kwa njia ambayo inatupasa.

A. Yohana 3:7, ni lazima tuzaliwe mara ya pili. Mtu ambaye hajaokoka, hawezi kamwe kumwabudu Mungu.

B. Yohana 3:14, Yesu lazima ainuliwe juu. Ni lazima neno la Kristo lihubiriwe kwa kweli ikiwa kutakuwa na kuabudu kwa kweli.

C. Yohana 4:23, ni lazima tumwabudu Mungu kwa Roho na kwa kweli. Je hii inamaanisha nini? Kuabudu inamaanisha kumtambua Mungu katika ukuu wake na kwamba Yeye anastahili kuabudiwa.

i. Kuabudu katika Roho inamaanishi wakati nafsi zetu zinamwabudu Mungu na kuzungumza naye.

ii. Kuabudu katika kweli:

a. Kuja mble za Mungu kwa uaminifu na kwa mioyo yeu yote.

b. Kumwabudu Mungu kulingana na neno Lake. Ni lazima tumsifu Mungu, tumwombe Mungu na tuhubiri neno la Mungu kutoka kwa Biblia.

C. Tunaweza tu kumwabudu Mungu kupitia kwa Kristo (Yohana 14:6).

D. Mistari 25-26 Yesu anasema kwamba Yeye ni Mungu

E. Yohana 4:27-30, Wanafunzi wa yesu alishangaa sana kwakati walimkuta Yesu anazungumza na mama masamaria kwa sababu Wayahudi hawakuwa wanazungumza na wasamaria. Pia halikuwa jambo zuri kuzungumza na mwanamke wazi hivvyo. Hizi sheri mbili hazikuwa katika neno la Mungu, ni sheria ambazo zilikuwa zimetungwa na wanadamu. Yeye alionyesha kwamba ni sawa kuzungumza na wamasaria na wanawake waza wazi. Leo tunaweza kuzungumza leo na wale wote ambao hawajaokoka bila kujificha. Kwa njia hii tunaweza kuwafikia na ujumbe wa injili.

i. Yesu alimwokoa huyu mama na baadaye huyu mama aliwaita wa mji waje wamwone Yesu ambaye alimwambia kila kitu.

E. Yesu alikuja kwaokoa watu wote na wala si Wayahudi peke yao. Jambo liliwakasirisha Wyahudi. Mara ya kwanza Yesu alitamka jambo hili, wayahudi walitaka kumwua (Luka 4:26-30). Hapa Yesu alikuwa anawaambia kwamba kama tu vile Eliya alienda kumwokoa mtu wa mataifa, vivyo hivyo Yesu alikja ulimwengu kuwaokoa watu wa Mataifa na wale wayahudi ambao wataamini. Agano la Kale pia lilifundisha jambo hili kwa wazi kabisa (Mwanzo 12:3).

F. katika mistari ya 31-34, Yesu anasema kwamba kutosheka kwa kweli kunatokana na kufanya mapenzi ya Mungu. Ikiwa hatufany mapenzi ya Mungu, basi ni mapenzi ya nani ambayo tunayafanya? Tunapaswa kufanya mapenzi ya Mungu pekee na wala si ya mtu mwingine au kiumbe kingine. Je, tunajua kwamba haya ni mapenzi ya Mungu? Biblia inatufundisha wazi kabisa mapenzi ya Mungu ni gani na pia tuombe Mungu atuongoze katika mapenzi yake. Pia tutumie karama ambazo Mungu ametupatia.

G. Yohana 4:35-38, tunasoma kuhusu amri ya Mungu ya kutangaza injili kila mahali.

H. Mistari ya 39-42, huyu mwanamke aliwaambia watu waje wamwone Kristo ambaye alikuwa amemwabia mambo yote.

9. Yohana 5, tunafundishwa kuhusu siku ya sabato.

A. Mistari ya 1-9, Yesu alimponya mtu siku ya sabato na kwa kufanya hivi, viongozi wa wayahudi walimkasirikia sana. Katika Mathayo tulizingatia mafundisha ya sabato sana.

B. Mistari ya 17-23, tangu wakati huu wayahudi walimchukia sana Kristo na walijaribu sana kumwua Kristo. Yesu na Mungu Baba hakuna tofauti ni moja, kwa sababu Kristo mwenyewe ni Mungu. Yesu ana mamlaka na kwa hivyo Yeye anapaswa kuabudiwa. Yesu ni Mungu Baba ni moja.

C. Mstari wa 18, tunasoma kwamba Wayahudi walimtafuta Yesu ili wamwue. Ni kweli kwamba leo wengi hawatamkubali Kristo kwa sababu wanataka miungu ambayo inakubali tabia yao ya dhambi.

D. Mistari ya 24-29, tunasoma kuhusu Mamlaka ya Kristo Yesu. Tunaona kwamba Yesu Kristo ana mamlaka ya kuokoa na kwamba tunaokoka kwa kumwamini Kristo (mstari wa 24).

i. This is a matter of life and death and many don't believe this teaching. There are three doctrines here:

ii. Kifo si mwisho wa maisha (Mwanzo 25:8, 1 Wathesalonike 4:16 and Waebrania 11:35).

iii. Kuna mahali pawili ambapo mtu anaweza kuenda: mtu ataenda mbinguni au jahanum (Ufunuo 21:8; 21:4).

iv. Mahali ambapo utaenda inategemea uhusiano wako na Kristo.

E. Je, Mungu atapeana na nafasi nyingine kwa wale ambao wanakufa bila kuokoka? Jibu ni la. Mungu ameweka sheria zake na ikiwa zinavunjwa, hakuna nafasi nyingine. Kumbuka Luka 16:19-26. Kumbuka kwamba mojawapo wa hali ya Mungu ni kwamba habadiliki kamwe.

F. Yohana 5:39-44, Wayahudi waliyatumia vibaya maandiko. Katika mstari wa 39, kusudi la Biblia ni kwamba tuongozwe kwa Kristo. Wayahudi walisoma Biblia si kujifunza kutoka kwake bali kuitumia katika uovu wao. Wao walimwona Kristo kuwa mwanadamu tu na wala si Mungu. Je, wakati unaisoma Biblia, inasoma kwa njia gani? Hatufai kuabubu Biblia tunapaswa kuabudu mwenye Biblia. Tunafaa kusoma Biblia ili tumjue Mungu zaidi na zaidi. Wayahudi walisisitiza sehemu fulani fulani tu za Biblia na wala si Biblia yote. Wao waliwaza kwamba ikiwa watakariri Biblia, hilo ndilo litawaokoa. Wao walifurahia kutii kanuni fulani fulani na hawakuelewa kwamba ukristo ni kuwa na uhusiano na Kristo.

D. Mistari ya 45-47, Yesu anasema kwamba Biblia itawahukumu wengi. Watu walipuuza mafundsisho ya Mungu ambayo Musa alifundisha na kwa sababu hiyo, wao walikuwa wamehukumiwa tayari.

10. Yohana 6:1-14, tunasoma kuhusu muujiza ambao uko katika vitabu vyote vinne vya injili. Watu walikuwa wanafuata Yesu kwa sababu walitaka kufaidika kutoka kwake na sin a mambo ya kiroho, bali ya kimwili..

A. Watu walikuwa na njaa na pia walijua kwamba hakluwa na njia yoyote ya mwanadamu kutosheleza hitaji lao la chakula. Kwa hivyo walimgeuka Kristo. Yesu pekee ndiye alikuwa na uwezo wa kutosheleza hitaji hili, na kweli aliwatosheleza.

B. Yohana 6:30-35 na 48 na51, tunasoma kwamba watu wako na hitaji lingine la muhimu sana ambalo ni wokovu. Kila mtu anapaswa kufahamu kwamba hakuna njia nyingine au mwanadamu ambaye anaweza kukutana na hitaji hili la wokovu. Kila mtu anapaswa kuja kwa Kristo ikiwa kweli atapata wokovu kwa sababu ni Kristo pekee ambaye anaweza kuokoa. Yeye ameahidi kwamba wale wote ambao wanakuja kwake kwa ajili ya wokovu, Yeye atawaokoa. Yesu anatosha. Jinsi tu anavyotupatia mkate wetu wa kila siku, vivyo hivyo ana nguvu zote kutupatia mkate wa kiroho ambao ni uzima wa milele.

i.Kila siku tunahitaji chakula cha kimwili. Vivyo hivyo tunahitaji chakula cha kiroho ikiwa tutakuwa na tumaini la mbinguni.

ii.Kila siku tunapaswa kuendelea kukua katika maisha yetu ya kiroho, na ndilo hili lifanyike, ni lazima tusome neno la Mungu kila siku. Je, wewe unasoma Biblia yako kila siku?

iii. Mstari wa 48, watu wanakumbushwa kuhusu wale ambao walitoka Misri kwamba jangwani Mungu aliwapatia mkate wa kimwili na walipata nguvu lakini hata hivyo wao walikufa.

iv. Mstari wa 51, Yesu alifundisha kuhusu mkate wa uzima ambao unafanya tuishi milele kiroho. Mkate huu pia unatoka kwa Mungu, na mkate huo ni Kristo ambaye anatupatia uzima wa milele.

v. Mwisho wa mstari wa 51, yesu anasema kwamba atatoa sadaka ambao ni mwili wake.

C. Katika mstari wa 37, Mungu anasema kwamba atawakubali wote ambao watakuja kwake kupitia kwa Kristo na Yeye hatawahi kuwakataa.

E. Yohana 6:40, tunapata ahadi ya uzima wa milele.

F. Mistari ya 6:41-47, tunasoma kwamba Wayahudi walinung'unika kwa sababu alisema, Yeye ndiye mkate wa uzima ambao umekuja kutoka mbinguni. Yohana 6:42, waliulizana, je huyu ndiye Yesu mwana wa Yusufu, ambaye babake na mamake tunawajua? Je, sasa anawezaje kusema kwamba ametoka mbunguni?

G. Yohana 6:43, Yesu aliwajibu, "Achane kunung'ukiana ninyi kwa ninyi." Yesu aliwaeleza kuhusu njia ya kuja kwa Mungu (mistari ya 44-47). Wengi hawako tayari kumkubali kristo jinsi alivyo. Huwa tunataka kumgeuza awe jinsi wenyewe tunataka awe. Shida ni kwamba ikiwa tutafanya hivyo, Yeye hatakuwa Mungu tena.

11. Yohana 6:51-59, kuna wengine ambao hawaelewi mistari hii ni kuwaza kwamba wakristo ni watu ambao wanakula nyama mbichi. Hii mistari ilimaanisha kuamini na wala si kula kwa kawaida. Huwa tunwamini Kristo nan aye anakuwa mmoja katika maisha yetu.

A. Yohana 6:66-68, tunasoma kwamba ni wachache ambao walibaki na Kristo. Hii inatufundisha kwamba kila wakati Yesu atakuwa na watu wake, hata kama wengi watamwacha, kuna wale ambao hawataondoka hata hali iwe ya aina gani.

B. Yohana 6:69-71, tunasoma kuhsu maneno ya Petro baada ya wengi kumwacha Kristo. Petro alikuwa mwaminifu, lakini pia yesu alitabiri kwamba mmoja wa wanafunzi wake atamsaliti, na huyu alikuwa Yuda Iskariote.

12. Yohana 7:53-8:11, Kuna mafundisho mengi katika hadithi hii.

A. Dhambi ya zina lazima kuwa na mwamume. Je, ni kwa nini mwanamke adhibiwe pekee yake?

B. Tukumbuke mstari wa 7, wakati tunataka kumwadhibu mtu. Tunapaswa kuadhibu mtu kwa sababu sheria inasema hivyo lakini si kwa sababu ya hisia zetu wenyewe.

Hii ni sheria mzuri kufuata wakati tunawadhibu watoto wetu. Kumbuka kwamba sisi sote kuna mengi ambayo tunapaswa kuadhibiwa nayo. Wayahudi walikuwa wamemtega Kristo na wala si kwamba sheria ilikuwa inasema hivyo.

13. Yohana 8:12-59.

A. Yesu anasema kwamba Yeye ni Mungu. Katika mstari wa 13, Mafarisayo wanasema kwamba Yesu ni mwongo. Kwa sababu hii walianza kumshitumu Kristo kwamba:

i. Mstari wa 15 hakuelewa wanadamu.

ii. Mstari wa 19 hawakuelewa Mungu ni nani. Isaya 1:3, inafundisha jambo hili.

iii. Mistari ya 21 na 24, Yesu anawaambia kwamba wataangamia katika dhambi zao.

iv. Mstari ya 23, wao watu ambao wanapenda ulimwengu na vitu vyake.

v. Mstari wa 34, wao walikuwa watumwa wa dhambi.

vi. Mstari wa 44, tunasoma kina nani ndio wana wa shetani. Mtu anaweza kuwa mwana wa Mungu au wa shetani. Kabla tuokoke, tulikuwa wana wa shetani (Waefeso 2:1-3).

B. Hili ni jambo la kweli lakini Wayahudi hawakulipenda na kwa sababu hiyo walimkasirikia Yesu. Wacha tutazame baadhi ya hisia zao.

i. Mstari wa 41, walisema kwamba Yeye alikuwa mwana wa haramu.

ii. Mstari wa 48, Walimkashifu kwamba Yeye alikuwa Msamaraia na wala si Myahudi na kwamba Yeye alikuwa shetani.

C. Mstari wa 59, tunasoma kwamba wao walijaribu kumwua Yesu lakini hawangeweza kwa sababu hawakuwa na nguvu za kufanya hivyo hadi wakati Mungu alipokubali.

14. Yohana 9:1, tunasoma kwamba baada tu ya Yesu kutishwa na kifo, Yeye alimhurumia mtu. Je, ni wangapi ambao tunaweza kufanya hii? Hii inadhihirisha upendo mkuu wa Yesu kwetu.

A. Mistari ya 2-3, tunasoma kuhusu wanafunzi wa Yesu ambao waliwaza kwamba mateso ya kila mtu imesababishwa na dhambi za mtu huyo. Hili lilikuwa jambo ambalo wengi waliwza juu yake. Watu waliwaza kwamba kwa sababu mtu ni mgonjwa au kiwete au kipofu au kiziwi, hii ni kwa sababu alikuwa amefanya dhambi na Mungu alikuwa anamwadhibu. Sivyo hata kidogo. Lakini pia tukumbuke kwamba kuna wengi ambao wako katika hali kama hizi kwa sababu ya dhambi zao wenyewe. Kwa mfano, ikiwa mtu anaiba, halafu anashikwa na kukatwa masikio au mguu, hiyo ni kwa sababu dhambi zake atakosa mguu au maskio.

B. Tazama Luka 13:1-5.

C. Ni ukweli kwamba kila aina ya mateso imesababishwa na dhambi. Lakini mateso ya mtu binafsi si lazima yawe wamesababishwa na dhambi ambayo amaifanya mwenyewe. Huwa walimu wengi wa uongo wanatumia jambo hili kuwadanganya wengi. Ni jambo bay asana kumweleza mtu ambaye anaumia kwamba anaumia kwa sababu ya dhambi zake haswa ikiwa huna uhakika.

D. Kuna magonjwa ambayo yanaletwa kwa sababu ya dhambi za mtu mwingine. Kwa mfano ikiwa mtu anafanya uasherati na anapata miba na ukimwi. Ni wazi kwamba atamzaa mtoto ambaye ana ukimwi.
15. Yohana 10, tunasoma kuhusu Kristo ambaye ndiye mchungaji Mwema. Mchungaji analinda kondoo wake vyema kabisa. Hii inamaanisha kwamba Kristo Yesu ndiye njia ya wokovu na kwamba Yeye ndiye mchungaji ambaye anayatoa maisha yake ili aokoe watu wake.

A. Mistari 27-29, hapa tunapata faraja kubwa sana kwa wale ambao tumeokoka. Yesu anasema kwamba hatawahi kuwaacha kamwe wale wote ambao wamemwamini. Kwa ufupi ni kwamba ikiwa umeokoka, wewe kamwe hatuwahi kupotea kwa giza. Wewe ni mtoto wa Mungu milele.

B. Kwa sababu ya kusema kwamba Yeye anaweza kuwaokoa watu, wayahudi tena walitafuta njia ya kumshika ili wamwue. Mara nyingine tena hawakuweza kwa sababu wakati wa kufa kwa Kristo ulikuwa haujafika.

C. Mistari ya 19-21 na 42, tunasoma kuhusu migawanyiko miongoni mwa Wayahudi na kwamba wengi walimwamini Kristo.

16. Yohana 11:1-44, hii ni hadithi ya kufa na kuzikwa kwa lazaro na baadaye Kufufuliwa na Kristo.

A. Hadithi hii inatuonyesha kwamba Yesu ako na nguvu juu ya maisha na kifo na kwamba Yeye ni Mungu ambaye ana nguvu zote. Katika smtari wa 15, tunasoma kwamba sababu ya muujiza huu ni kwamba watu waweze kumwamini Mungu.

B. Mstari wa 35, tunasoma kwamba Yesu alilia. Je, ni kwa nini Yesu alilia ilhali alijua kwamba alikuwa amfufue lazaro?

i. Yesu alionyesha upendo wake kwa watu kwa sababu aliwaona wakiwa wamehuzunika.

ii. Alionyesha kwamba ni vyema watu kuomboleza kwa sababu ya kifo cha wapendwa wao hata kama walijua kwamba hao wapebdwa wao wako mbinguni. Kuna wale ambao wanahubiri kwamba hatufai kuomboleza wale ambao wameenda mbinguni.

iii. Kuna wale wanafundisha kwamba alilia kwa sababu kifo kinaleta huzuni.

C. Mistari ya 4 na 40, tunasoma kwamba sababu nyingine ya hadithi ni kudhihirisha utukufu wa Kristo Yesu.

D. Mstari wa 45, tunasoma kwamba baadhi ya watu walianza kumwamini Kristo kwa sababu yay ale ambayo waliona. Wengine waliendelea kuwa vipofu na kupuuza ukweli kwamba Kristo amejidhihirisha kwamba Yeye ni

Mungu. Katika mistari ya 46-53, tunasoma kwamba wale ambao waliendelea kupuuza kristo, walipanga jinsi ya kumwua. Hii inaonyesha jinsi watu walivyovipofu katika dhambi na jinsi wanaweza kupuuza ukweli hata kama wanauona kwa macho yao ya kiasili.
17. Yohana 12:1-8, tunasoma kuhusu Mari ambaye alimpaka Yesu mafuta ya bei ya juu sana. Hili lilifanyika ili kumpa Kristo heshima kwa karama ambayo ilikuwa imeandaliwa kwa heshima yake Yesu.

A. Mistari 9-11, tunasoma kuhusu watu wakianza kuwamini Kristo kwa sababu ya kumfufua Lazaro kutoka kwa wafu. Jambo hili liliwafanya Mkuhani wakuu kupanga njia ya kumwua Yesu n ahata Lazaro.

B. Mistari ya 12-19, tunasoma kuhusu kuingi kwa Yesu Kristo katika mji wa Yerusalemu akiwa juu ya mwana-punda. Katika Luka 19:33-38, tunasoma kwamba umati wa watu ulimkaribisha. Hii ilikuwa jumaa moja kabla ya Kristo kufa msalabani. Hii inatuonyesha kwamba kwa wakati moja wanadamu wanaweza kukusifu na wakati mwingine kukuua. Ni Mungu pekee ambaye habadiliki. Hadithi hii akiwa juu ya mwana punda inatimiza unabii katika Zekaria 9:9.

18. Yohana 13-17, inajulikana kama mazungumzo katika chumba cha juu. Usiku kabla ya kusulibishwa kwake, Yesu alikutana na wanafunzi wake katika chumba cha juu na akawapa majukumu mapya ambayo walifaa kutekeleza wakati Kristo amekufa. Huu ulikuwa wakati wa wanaunzi wa Yesu kuanza kufanya kazi ya ufalme wakiwezeshwa na Roho Mtakatifu. Katika matendo ya Mitume, tunasoma kwamba jambo hili lilifanyika.

A. Yohana 13:3-20, tunasoma kwamba Yesu Kristo aliosha miguu ya wanafunzi wake. Tunafundishwa kuhusu unyenyekevu. Mungu mwenyewe aliosha miguu yay a wanadamu. Tunapaswa kumwiga Kristo na kuwa watu wanyenyekevu. Hapa hatuambiwi tuoshana miguu kwani hiki kilikuwa kitendo cha kuonyesha tu unyenyekevu katika tamaduni za wakati huo.

B. Katika mstari wa 10, Yesu alisema kwamba mmoja wa wanafunzi wake alikuwa amsaliti.

C. Mstari wa 16, tunafundishwa kwamba uongozi katika kanisa ni jambo la muhimu sana. Washirika wa kanisa hawatakua katika ukristo wao, ikiwa wale ambao wanawaongoza hawajakua kiroho wenyewe. Kwa sababu hii ATA imeanzishwa na inaendelea kuwepo. Wachungaji wanapswa kuwa waaminifu sana kwa kuhubiri neno la Mungu. Ni neno la Mungu ambalo litawafanya wengi wakue kiroho. Kumbuka kwamba mwalimu lazima kwanza yeye mwenyewe asome kwa makini sana kwa sababu ni lazima ajue zaidi kuliko mwanafunzi.

i. Mistari ya 34-35, Yesu anapeana amri jinsi tunapaswa kupendana wenyewe kwa wenyewe. Katika Marko 12:31, tunaona umuhimu wa jambo hili.

ii. Mistari ya 37-38, tunasoma jinsi Petro alijigamba kuhusu ujasiri wake na jinsi Kristo alivyotabiri kwamba Petro angemkana. Ni lazima tuwe waangalifu sana kuhusu kujivuna. Kile ambacho Mungu anasema kutuhusu ndicho ukweli na wala si kile ambacho tunajiwazia sisi wenyewe.

19. Yohana 14:1-4, yesu aliendelea kuwaanda wanafunzi wake kwa ajili ya kifochake. Yeye aliwafundisha ujumbe wa kuwafariji wakati ataondoka.

A. Mstari wa 1, Yesu aliwaambia kwamba wa mwamini Mungu nao watapa kufarijiwa.

B. mstari wa 2, Yesu aliwaambai kwamba mbinguni kuna viumba kwa kila mmoja wao na Yeye alikuwa anaenda ili awatayarishia viumba huko.

C. Mistari ya 3-4, Yesu aliwafariji kwa kuwaambia kwamba atarudi na atawapeka huko mbinguni. Huu ulikuwa ujumbe wa kuwafariji kwa sababu wakati mgumu sana mabo walikuwa wanaenda kupitia. Huu ujumbe ni wa wakristo wote kukumbuka wakati tuko katika hali mbaya za maisha.

D. Katika mistari ya 5-6, tunapata mafundisho ya muhimu sana. Je, unamwaimi Kristo pekee? Katika Yohana 14:6, “Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kupitia Kwangu.”

i.Mkristo ni mtu ambaye anamwamini tu Kristo kwa ajili ya wokovu wake. Ukristo ni dini ya kipekee kwa sababu Mungu wetu ni Mungu mwenye wivu. Yeye hagawana utukufu wake na mtu mwingine yeyote (Isaya 48:11). Hatufai kuwaamini waganga au mtu mwingine yeyote isipokuwa Kristo pekee.

ii.Kuna makanisa mengi katika ulimwengu ambayo yanafundisha kwamba wale wote ambao wanaishi maisha mazuri, wataenda mbinguni haijalishi wanaamini nini. Haya ni mafundisho ya uongo na hatufai kuyakubali kamwe katika makanisa yetu. Biblia inafundisha kwamba njia moja tu ambayo tunaweza kuingia mbinguni ni kupitia kwa Yesu Kristo.

E. Mstari wa 9, Yesu anasema kwamba Yeye na Mungu Baba ni moja. Yaani Kristo Yesu ni Mungu. Tunaposoma kuhusu Mungu wa Utatu, ukweli unadhihirika wazi kabisa.

F. Yohana 14:12-14, watu wengi huwa wanakosea kufahamu mistari hii.

i.Katika mstari wa 12, anasema kwamba wakati atakapaorudi mbinguni, wanafunzi wake watapata nguvu zaidi. Wakati yesu alipokuwa hapa duniani, alikuwa tu katika nchi ya Israeli na aliwafikia watu wachache na ujumbe wa injili. Lakini wanafunzi wake watapewa Roho Mtakatifu amabye atawasaidia kuhubiri injili na kupanda makanisa katika ulimwengu wote.

iii. Hii ni kwa sababu mamobi yote yatafanywa katika jina la Kristo pekee.

iii. Tunapaswa kujua kwamba Mungu atayasikia maombi yetu na kuyajibu ikiwa tutaomba katika jina la Kristo.

iv. Wanafunzi wa yesu waliendlea kufanya mambo makuu. Tunasoma kwamba waliugeza ulimwengu juu chini wakati walihubiri injili ya Kristo na kupanda makanisa mengi (Soma kitabu cha Matendo ya Mitume).

G. Yohana 14:15, tunapewa maagizo kuhusu kupenda Kristo. Tunaonyesha upendo wetu kwa Kristo kutii neno lake. Kuna mafundisho mengi katika Agano Jipya kuhusu kuonyesha upendo wetu kwa Mungu kwa kutii neno lake.

H. Yesu aliahidi kwamba Roho Mtakatifu ambaye ni Mungu atakuja baada ya Yeye kuondoka humu duniani (Mistari ya 16-17).

i. Kazi ya Roho Mtakatifu ni kutusaidia (matendo ya Mitume 1:8). Roho Mtakatifu anatupatria nguvu za kufanya kazi ya Mungu. Maisha ya ukristo ni maisha ambayo yanongozwa na Roho Mtakatifu. Hizi ndio nguvu ambazo zinatuoatia ujasiri wa kuhubiri Kristo na hata kukumbana na mateso katika ulimwengu huu.

ii.Mtsri wa 16, tunaambiwa kwamba wakati Roho Mtakatifu atakuja ndani mwetu, Yeye hatawahi kuondoka. Hii inamaansiha kwamba mapepo hayawezi kuingia mtu ambaye ameokoka. Mungu hawezi kuishi na mapepo kwani moyo wa yule ambaye ameokoka ni makao ya Mungu.

iii.Hii inamaansha kwamba wakati tunaokolewa, Roho Mtahkatifu huja ndani mwetu (1 Wakorintho 6:19). Kwanzia wakati huu, Yeye hatawahi kutuacha. Yeye ndiye anatulinda katika wokovu wetu milele. Kwa sababu hii hakuna lolote ambalo litatuzuia kuingia mbinguni (Warumi 8:35-39).

I. Katika mstari wa 20, tunafundishwa kuhusu umoja wa Mungu na kanisa.

J. Katika mistari ya 21-24, tunasisitiziwa upendo kwa Mungu kwa kutii neno lake.

20. Yohana 15:1-17, Yesu anasema kwamba kuna uhusiano mpya kati yake na wanafunzi wake na wakristo wote, yaani Kristo na watu wake wote wako pamoja. Yesu ndiye mzabibu sisi ni matawi.

A. Hii inatufundisha kwamba wakristo wanapaswa kuwa watu ambao wamejitolea katika kumtumikia Mungu na kwamba nguvu za kufanya kazi hii zinatoka kwa kristo Yesu mwenyewe. Tumebarikiwa kwamba tunaweza kumtumikia Mungu, lakini tukikata kumtumikia Mungu, tutapoteza nafasi hiyo.

B. Mistari ya 9-10, tunasoma kuhusu upendo wa Mungu ambao ni kutii neno lake.

C. Mistari ya 12-13, tunasoma kuhusu upendo mkuu wa Mungu. Ni upendo mkubwa sana kiwangi kwamba Kristo alijitoa kufa kwa ajili yetu (Warumi 5:7-8).

D. Katika mistari ya 14-15, Yesu anasema kwamba sisi ni marafiki wake na ni wafanyi kazi wenzake katika ufalme wake. Hii ni baraka kubwa sana kwetu (1 Wakorintho 3:9).

E. Mstari wa 16, tunasoam kwamba ni Kristo ambaye alituchagua sisi kuwa marafiki wake na wafanyikazi wenzake.

F. Katika zingine za sura, Yesu anafundisha kwamba, tunapaswa kutarajia kuteswa kama Yeye kwa ajili ya wokovu wetu. Tunasoma kwamba yesu alichukiwa bila kumfanyia mtu yeyote makosa. Hivi ndivyo itakuwa kwetu. Katika mistari ya 18-19, tunasoma kwamba dunia ilimchukia Kristo na kwa hivyo itachukia hata sisi leo.

21. Yohana 16:1-4, tunasoma kuhusu sababu ya kutuonya kwamba lazim tutarajie mateso, ni kwamba kwa uwezo na nguvu za Mungu tujue kwamba hatutashindwa kamwe. Kuna mafundisho mengi katika Agano Jipya ambayo yanatuandaa kuhusu jambo hili la kuteseka kwa ajili ya Kristo. Leo kuna wengi ambao wanateswa kwa ajili ya imani yao ndani ya Kristo.

A. Yohana 16:5-8, tunafundishwa kumhusu Roho Mtakatifu.

B. Yesua ansema kwamba anaenda lakini atamtuma msaidizi ambaye ni Mungu Roho Mtakatifu.

C. Mungu Roho Mtakatifu ataudhibitishia ulimwengu juu ya dhambi. Pia Roho Mtakatifu atatufundisha.

D. Yesu anafundisha hapa kwamba wanfunzi wake watahuzunika sana wakati ataondoak lakini hata hivyo, huzuni wao utageuka na kuwa furaha kwa sababu watajua kwamba wao wataushinda ulimwengu.

22. Yohana 17, hili ombi zuri sana la kanisa. Ombi hili linajulikana sana kama ombi la Kristo Yesu amabye ndiye Kuhani Mkuu. Yeye anatuombea sisi ambao ndio kanisa lake la kweli.

A. Hili ni ombi zuri. Katika Ombi la Bwana, Kristo alitufunza jinis tunapaswa kuomba. Lakini hapa tunaona sasa Yeye mwenyewe akiomba. Yeye alituombea.

B. Mstari wa 1-5, Yesu anaomba kwamba atarejeshwa katika utukufu wake ambamo alikuwa kabla ya kuja humu duniani.

C. Kuanzia katika mstari wa 6, Yesu anatuombea sisi ambao tumeokoka. Katika mistari ya 9-10, anawaombea wale ambao tumeokoka na wala si wale ambao hawajaokoka. Wale ambao tumeokoka sisi ni watu wake ambao anawapenda sana.

D. Katika msitari ya 11-15, Yesu anamwomba Mungu kwamba atulinde tuendelea kuwa waaminifu hata wakati wa majaribu makali sana. Katika mstari wa 15, Yesu haombi kwamba Mungu atuondoe katika ulimwengu huu, bali kwamba atulinde tuwe waaminifu kwake na pia atulinde kutokana na hatari za shetani. Nimewasikia wakristo ambao waliomba ombi kama hili. Wao waliomba kwamba mpango wa Mungu ukamilishwa katika mateso ambayo walikuwa wakiyapitia na kwamba wao waendelee kuwa waaminifu.

E. Katika mstari wa 17, Yesu anaomba kwamba sisi tuwe watakatifu na katika mstari wa 22, anaomba kwamba sisi tukue na umoja. Pia anaomba kwamba tuwe pamoja naye (24).

F. Mistari ya 14-16, tunasoma kwamba ulimwengu utatuchukia kwa sababu sisi si wa ulimwengu huu. Hapa ulimwengu ni pahali pa shetani na sisi kwetu ni mbinguni. Watu wa familia au jamii yako wao watawaza kwamba wewe ni wazimu kwa sababu ya maisha yako ya ukristo. Wao hawawezi kukuelewa.

23. Yohana 18:1-11, tunasoma kuhusu kukamatwa kwa Yesu Kristo ambako kulifanyika katika bustani la Gethsemane. Yesu alikubali kukamatwa. Tunapaswa kuelewa kwamba Kristo Yesu hakulazimishwa kufa msalabani. Alikubali kufa kwa sababu alitupenda mimi na wewe.

A. Mistari ya 12-27, tunaosma kwamba Yesu aliposhikwa, alipelekwa mbele ya baraza la Wayahudi. Nao walimpeleka katika mahakama ya Warumi.

B. Ni wakati huu Petro alimkana Yesu mara tatu. Katika mistari ya 25-27, jogoo aliwika kama tu vile Kristo alikuwa ametabiri katika sura 13. Baadaye, Yesu alimhimiza Petro na tunaona Petro akiwa mstari wa mbele katika kufanya kazi ya Mungu.

C. Balaza la wayahudi walitaka kumwua Yesu lakini hawakuwa na mamlaka, kwa sababu hiyo walimpeleka kwa Pilato ili amhukumia kifo.

D.Pilato alijua kwamba Yesu hakuwa na hatia yoyote (Yohana 18: 38 na 19:4-6). Pilato alijaribu kiumwachilia Kristo (12), lakini Wayahudi walikata kwa sababu hiyo, Pilato alimtoa Yesu asulibishwe hata kama Yesu hakuwa na makossa yoyote. Kwa kufanya hivi, Pilato alionyesha kwamba yeye alikuwa mtu mdhaifu n ahata hivyo, yeye alifanya makossa na kwa sababu hiyo aliajibika mbele za Mungu.

E. Yohana 19, tunasoma kuhusu kusulibishwa na kuzikwa kwa Yesu Kristo. Tunaona kwamba baadhi ya ahadi za Agano la Kale zilikamilishwa. Hakuna mtu ambaye ana kijisababu kwa nini yeye anafanya dhambi.

A. Zaburi 22:18 ilikamilishwa katika Yohana 19:24

B. Kutoka 12:46, hakuna hata mfupa wake ulivunjwa ilikamilishwa katika Yohana 19:33,36.

C. Zekaria 12:10 ilikamilishwa katika Yohana 19:37.

D. Yesu aliteseka kimwili na kimawaza wakati alipokuwa mslabani. Kusilibishwa ilikuwa njia mbaya sana kwa mwanadamu yeyote kufa. Haya yalikuwa mateso makali sana. Pia wakati huu moja, Mungu Baba alimwacha Yesu. Soma Zaburi 22:1-22, na utaona jinsi Kristo aliteseka sana.
E. Yohana 19:30-33, tunasoma kwamba Yesu alikufa. Tunapaswa kufahamu hili vyema kabisa kwa sababu maadui wa kanisa wengi walidai kwamba Kristo hakufa kweli na kwamba Yeye aliumizwa tu na baadaye alipona. Ukweli ni kwamba Biblia inatuhakikishia kwamba kweli Kristo alikufa.

i. Mslabani Kalivari, Yesu alishinda vita dhidi ya Shetani.

ii. Msalabani Kalivari, Yesu alilipia dhambi zote za watu wake milele.

iii. Shetani bado anapigana lakini ukweli ni kwamba ameshaa shindwa. Msalaba wa Kristo Yesu ni wa muhimu sana kwetu.

iv. Yohana 19 inamalizikia kwa kutuleza kwamba Yesu alizikwa. Baadaye madui wa kanisa walidai kwamba Kristo hakuwa amekufa kweli.

24. Yohana 20:1-10, tunasoma kwamba Yesu hakuwamo katika kaburi. Wanafunzi wa Yesu hakukumbuka kwamba Yesu alikuwa amewaeleza kwamba Yeye atafufuka kutoka kwa wafu. Jambo hili lilikuwa limetabiriwa mbeleni katika zaburi 16:10 na pia na Yesu mwenyewe katika Luka 24:46.

A. Yohana 20, baadaye tunasoma kumhusu Yesu akiwatokea watu tofauti tofauti. Yesu kwnza alimtoke mwanamke na baadaye Luka anasema kwamba aliwatokea wanawake wengi.

25. Yohana 21:1-14, tunasoma kumhusu Yesu akijitokeza kwa wanafunzi wake wakati walipokuwa wanavua samaki.

A. Yohana 21:15-19, tunasoma jinsi Yesu alivyomrejesha Petro. Petro alihisi vibaya sana baada ya kumkana Kristo. Tunasoma hapa jinsi Yesu alimchukua Petro na kumrejesha katika huduma wake. Tunajifunza hapa kwamba, haijalishi unaweza shusha moya kwa njia gani au kuanguka vibaya sana, ikiwa tunatuba, Yesu atatusamehe na ataturejesha. Petro alikuwa mojawapo wa watu ambao walitumika sana Kristo katika kulijenga kanisa.

B. Tunasoma kuhusu Yesu akizungumza kuhusu jinsi Petro alivyokuwa anenda kufa. Historia inasema kwamba Petro aliteswa sana kabla ya kuuliwa.

C. Yohana anamalizia kuandika kitabu chake kwa kutueleza kwamba Yesu alifanya mengi sana ambayo hayajaandikwa kwa sababu hakuna kitabu ambacho kingetoshea hayo yote.

Tunapomalizia vitabu vya injili, ni vyema kuelewa kwamba Yesu alikufa na alifufuka. Kifo chake msalabani, kilikuwa kwa ajili ya dhambi zetu. Na wale wote ambao wanamwamini Kristo, wao wataingia mbinguni. Kwa kifo chake msalabani, shetnai alishindwa kabisa. Kwa kufufuka kwake, Yesu alidhihirisha ushindi wake dhidi ya nguvu za giza.

Maadui wa kanisa, kila mara wamejaribu sana kueneza uongo kuhusu Kristo ambao ungeangamiza kanisa vibaya sana. Katika Historia kanisa limeandika kueleza ukweli kumhusu Kristo na Biblia. Maandishi haya yamekuwa msingi wa imani ya kanisa. Moja wapo ya maandishi haya ni Apostle's Creed ambayo inasme kwamba:

> Ninaamini katika Mungu, Baba mwenye nguvu, mwumba mbingu na nchi.
>
> Ninaamini Yesu Kristo, Mwana wa pekee wa Mungu, ambaye ni Bwana wetu, ambaye alizaliwa kwa nguvu za Roho Mtakatifu kupitia kwa Bikira ambaye ni Maria. Yesu aliteseka chini ya Pilato, alisulibishwa, akafa na akazikwa; siku ya tatu alifufuka. Yeye alipaa na akarudi mbinguni ambapo ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba na atarudi tena kuhukumu wanaoishi na wale ambao wamekufa.
>
> Ninaamini katika Roho Mtakatifu, kanisa katika la Mungu, katika ushirika wa wandugu, katika msmaha wa dhambi, katika kufufuka kwa mwili na katika maisha ya milele. Amen.

Matendo ya Mitume

Kitabu hiki kinazungumza kuhusu kuwepo kwa Yesu mara ya mwisho humu duniani na kupaa kwake mbinguni. Pia kinazungumza kuhusu kuanzishwa kwa kanisa la kwanza. Kwa sababu ya barabara nzuri na lugha ya Warumi, kanisa liliweza kupanuka na kuwa kubwa mno katika ulimwengu wote. Kitabu cha Matendo ya Mitume ni kitabu rahisi sana kusoma na pia kimejawa na mambo mengi ambayo yalifanywa na Kristo kupitia kwa watu wake. Tunajifunza mambo

mengi sana kutokana na kitabu hiki kuhusu kuabudu na jinsi ya kufanya mambo katika kanisa. Makanisa ya kwanza yalianzihswa na mitume na tunajifunza mengi kutokana na jinsi walivyofanya kazi hii.

Tunasoma kuhusu afisi ya mchungaji nay a shamanzi katika kanisa na majukumu yao. Pia tunasoma mengi kumhusu Mungu Roho Mtakatifu ambaye ndiye msaidizi wetu, mlinzi wetu na mwalimu wetu.

Kama tu leo, Kanisa la kwanza liliteswa sana. Wale ambao walitesa kanisa la Kristo wakati huo walikuwa Wayahudi. Warumi hakulisumbua kanisa sana kwa sababu wao waliliona kuwa mahali ambapo hapa kujiusha na mambo ya serikali yao bali mambo ya kiroho.

Kanisa la kwanza lilikumbana na upinzani mkubwa sana kutoka kwa wayahudi nje n ahata ndani. Katika Matendo ya Mitume tunasoma jinsi Wayahudi walijaribu kuliangamiza kanisa na kwamba mtume Paulo alikuwa mmoja wa wale ambao walikuwa wamejitolea kuangamiza kanisa. Wayahudi ambao walikuwa wameokoka walikuwa wanataka kuleta tamaduni za kiyahudi katika kanisa. Tutatazama vita ambavyo vilikuwepo katika kuetnganisha tamaduni kiyahudi na Ukristo wa kweli. Ukristo ulifundisha kwamba wokovu ni kwa watu wote ambao wanamwamini Kristo na kwamba wale ambao walimwamini Kristo, hata watu wa mataifa walikuwa wote sawa machoni pa Mungu.

Katika kitabu cha Matendo ya Mitume, tunasoma kuhusu miujiza 25. Miujiza hii ilijumlisha kuwafufua wafu na kufunguliwa kwa Malanga ya gereza. Miujiza hii, ilisaidia katika kukua kwa kanisa. Miujiza hii ilishuhudia ukweli wa ujumbe wa Injili ambao ulikuwa unahubiriwa.

Matendo ya Mitume 1:1-11, tunsoma kuhusu siku za mwisho za Kristo hapa ulimwenguni kabla ya Yeye kupaa na kurudi mbinguni. Yeye alimaliza siku 40 hapa ulimwenguni baada ya kufufuka kutoka kwa wafu na Yeye alionekana na wengi. Katika mistari ya 1-2, tunasoma kwamba alimaliza siku hizi akifundisha neno la Mungu.

1. Mstari wa 8, tunasoma maneno ya mwisho ya Kristo kabla ya Yeye kurudi mbinguni. Kwa kawadia tunajua kwamba mtu huwa anazungumza maneno ya muhimu sana wakati anajua kwamba haya maneno ndio ya mwisho kwake; haswa wakati anatoka akatika ulimwengu huu. Katika maneno haya, Bwana Yesu Kristo anatuamuru tueleze ulimwengu kuhusu Yeye. Ni jukumu la kanisa kuhakikisha kwamba ujumbe wa injili unaenezwa kila mahali. Mstari wa 8, ni mstari mzuri sana kuwazia. Mstari huu unatueleza kwamba tunapaswa kueneza injili ya Kristo katika nyumba zetu, vijijina mwetu, miji yetu na ulimwenguni kote.

A. Mitume na kanisa la kwanza walizingatia sana amuri hii kwa sababu tunasoma kwamba walijitoa kabisa katika kuhubiri Injili. Leo tuna wengi kwamba hawana tamaa ya kueneza injili na kwa sababu hii, wengi leo hawajaokoka.

2. Katika mistari ya 9-11, tunasoma kumhusu Kristo akipaa juu mbinguni, aliinuliwa na mawingu. Katika mstari wa 11 tunasoma kwamba kwa njia hiyo hiyo, Yesu atarudi. Tunajua kwamba Yesu atarudi, lakini hatujui atarudi lini.

3. Mistari mingine katika suri hii inaeleza yale ambayo yalikuwa yanatendeka wakati wanafunzi wa Yesu walipokuwa wanamsubiri Roho Mtakatifu. Katika mstari wa 14, tunasoma kwamba walimaliza muda wao wakiomba. Tunajifunza hapa kwamba Kanisa linapaswa kuomba kwa pamoja.

A. Katika mstari wa 15, tunamwona Petro akichukua uongozi katika kanisa. Yeye alikuwa mtu tofauti tofauti kabisa wakati huu.

B. Mstari wa 26, tunasoma kuhuus kuchaguliwa kwa Mathiya ambaye alichukua nafasi ya Yuda. Hatujui mengi kumhusu isipokuwa kwamba alichukua nafasi ya Yuda Iskariote.

C. Mitume walikuwa watu ambao walikuwa na mamlaka ya kipekee kutoka kwa Kristo. Kwa mfano katika warumi 11:13, tunasoma kwamba Paulo alikuwa mtume kwa watu Mataifa. Katika Biblia mtume ni mtu ambaye alikuwa mfuasi wa Kristo ambaye alimwona Kristo kwa macho macho.

F. Wanafunzi ni wafuasi wa Kristo n ahata wakristo wote ni wanafunzi na wafuasi wa Kristo lakini si mitume. Kukusanyika pamoja na kuomba, ni jambo la muhimu sana katika maisha ya mkristo. Jambo hili limetajwa mara mingi katika Biblia: Matendo ya Mitume 2:46; 4:24; 5:12; Warumi 15:6 na Waefeso 5:18.

G. Matendo 2:1-13, tunasoma kumhusu Roho Mtakatifu akija. Hili ni tukio la muhimu sana. Tukio hili litukio siku 50 baada ya siku ya Pasaka.

1. Mistari ya 1-3, tunasoma jinsi Roho Mtakatifu alivyowashukia wanafunzi wa Yesu.

2. Mistari ya 4-13, tunasoma jinsi wale ambao walikuwa wamekusanyika walivyoweza kuwasikia wanafunzi wa Yesu wakizungumza katika lugha ambyo walifahamu wao vyema. Jambo hili linajulikana kama kuzungumza kwa ndimi. Kusudi la jambo hili ilikuwa kuwawezesha watu

wasikilizaji kufahamu ujumbe ambao walikuwa hawawezi kuufahamu. Katika 1 Wakorintho tunasoma kuhusu maagizo juu ya kutumia.

A. Matendo 10:46, tunasoma kuhusu kutumia lugha kuzungumza na Mungu. Lugha au ndimi zilitumika katika Biblia kuzungumza na Mungu.

3. Katika mistari ya 14-36, tunasoma kuhusu mahubiri ya Petero.

A. Alihubiri kwamba nyakati ambazo walikuwa wakikishi zilikuwa nyakatia ambamo unabii ulikuwa utimike. Pia alihubiri kuhusu unabii tofauti tofauti ambao ulitimika katika kuja kwa Yesu Kristo.

i. Kwanza Petero alisema kwamba watu hawakuwa wamelewa. Kuja kwa Roho Mtakatifu ni jambo ambalo lilikuwa limetabiria katika Yoeli 2:28-32.

ii. Katika Matendo 1:16-20, Petero alisema kwamba kusalitiwa kwa Kristo Yesu ni jambo ambalo lilikuwa limetabiriwa katika Zaburi 41:9.

iii. Matendo ya 3:18, Petero alihubiri kwamba ilikuwa imetabiriwa kwamba Kristo angeteseka (Zaburi 22 na Isaya 53).

iv. Matendo 2:23-28, Petero alihubiri kwamba kufufuka kwa Kristo Yesu kulikuwa pia kumetabiriwa katika Zaburi 16. Zaburi inasema kwamba Mwili wa Kristo haungeozea kaburini ambalo ni jambo la kawaida kwa mwili ya wale wote ambao wamekufa.

v. Matendo 2:33-35, Petero alihubiri kwamba kupaa kwa Kristo mbinguni pia kulitabiriwa katika Zaburi 110:1.

4. Matendo 2:41, tunasoma kuhusu matokeo ya mahubiri ya Petero ambapo watu 3000 waliokolewa na Mungu.

5. Katika mistari ya 42-47, tunasoma kuhusu ushirika wa wale ambao waliokoka. Tunaona kwamba walijitolea kwa mafundisho ya neno la Mungu na ushirika wa wandugu. Huu ni mfano mkubwa sana kwetu leo. Katika mstari wa 47, tunasoma kwamba ni Mungu ambaye huwa anawaokoa watu na kuwaongeza kwa kanisa lake.

Matendo 3:6, tunawaona Petero na Yohana wakiwa wapewa ngunvu na Roho Mtakatifu. Wao hwakufanya lolote ili waweze kumponya yule mtu. Katika mistari ya 11-26, tunasoma sababu wao walipewa nguvu za kumponya yule mtu. Hii ilikuwa kwa sababu ya kumshuhudia Kristo.

Matendo 4:1-3, viongozi wa dini walikasirika kwa sababu waliona kwamba kwa sababu ya kupona kwa yule kiwete, watu walikuwa wameanza kumwamini Kristo. Kwa sababu hii, wao waliwashika Petro na Yohana na kuwaweka gerezani. Je, ni kwa nini kulikuwa na upinzani mkubwa hiv?

1. Katika mstari wa 4, tunasoma kwamba watu 5000 waliokolewa na Mungu. Pia katika Matendo 2:41, tunasoma kwamba 3000 pia waliokolewa siku ya Pentekote. Viongozi waliwaonya na kuwakataza mitume wasizungumze kumhusu Kristo. Katika mistari ya 19-20, Petero na Yohana walisema kwa ujasiri kwamba wataendelea kuzungumza ukweli wa Kristo. Hata leo wale ambao tumeokoka, tunapaswa kuwa na ujasiri huu na kuwaeleza watu wote kumhusu Yesu hata kama maisha yetu yataharishwa.

Matendo 5:1-11, tunasoma kuhusu hadithi ya Anania na Safira. Hadithi ilifanyika wakati ambapo watu walikuwa wanauza aridhi zao na kuleta pesa zao kanisani. Anania na Safiri waliahidi kuuza aridhi yao na kuleta pesa hizo kanisani. Lakini wakati waliuza aridhi yao, hawakuleta pes azote, bali walibakisha pesa zingine. Wao hawakulazimishwa kuleta pesa zozote kanisani. Hakuna mtu ambaye aliwaambia kwamba walifaa kuuza aridhi yao. Wao wenyewe walifanya uamuzi huo.

Walipoahidi kuleta pesa hizo, basi pesa hizo zilikuwa na Mungu. Kwa sababu ya kuiba pesa za Mungu, adhabu yake ilikuwa kifo. Ni lazima tuwe waangalifu sana kutekeleza ahadi zetu kwa Mungu. Je, ni kwa nini Anania alihidi pesa kwa Mungu ilhali alijua kwamba hataleta zote? Hii ilikuwa sababu alitaka kujivuna kwamba hata yeye alitoa pesa kwa kanisa. Moyo wake haukuwa na nia ya kumtukuza Mungu bali kujiletea sifa mwenyewe. Alitaka ajulikane kuwa mtu mkarimu. Tunapaswa kujitahidi na kutekeleza ahadi zetu kwa Mungu. Ikiwa hatutaweza kutekeleza ahadi zetu kwa Mungu kwa sababu hatuwezi, Mungu atatusamehe. Mungu ndiye anajua mioyo yetu na atatuadhibu ikiwa hatutatekeleza ahadi zetu kwake.

1.Matendo 5, tunasoma kuhusu jinsi Mitume walishikwa na kuweka gerezani. Katika mistari ya 18-20, tunasoma kwamba malaika aliwafungulia malango ya gerezani na kuwatoa nje na aliwamuru kwamba waende katika ukumbi wa hekalu na wahubiri injili huko.

Mara nyingine tunasoma kwamba, Mitume waliletwa kwa viongozi wa Wayahudi. Katika mistari ya 28-29, tunasoma kuhusu funzo muhimu sana kwetu. Tunapaswa kutii sheria za nchi

isipokuwa tu zile ambazo ni kinyume na mafundisho ya Biblia. Tunapaswa kufanya hivyo hata kama maisha yetu yatakuwa hatarini. Katika mstari wa 40, tunasoma kwamba hao viongozi waliwapiga mitume. Katika mistari ya 41-42, tunasoma kwamba mitume waliendelea kuhubiri Kristo. Hawa mitume hawangeruhusu lolote liwazuie katika kuendelea na kazi ya Mungu.

Matendo 6:1-7, tunasoma kuhusu kuanzishwa kwa afisi ya shamanzi. Tunasoma kwamba wale 7 walichaguliwa kufanya kazi ya kuwashugulikia watu ili mitume wazingatia tu kazi ya kuhubiri neno la Mungu na kuomba. Afisi ya shamanzi niafisi ambayo imeanzishwa na Mungu.

A. Mstari wa 7, kuhusu matokeo ya Mitume kujitoa tu kwa kazi ya kuhubiri na kuomba. Tunaosma kwamba idadi ya wale ambao waliokoka iliongezeka.

Matendo 6:9-7:60, tunasoma kuhusu kuuliwa kwa Stefano.
1. Matendo 6:9-7:1, Stefano alishikwa na kuletwa mbele ya kamati ya viongozi wa Kiyahudi.

A. Matendo 6:12-14, tunasoma kuhusu ushahidi wa uongo ambao walisingizia nao Stefano.

B. Mistari ya 10-15, tunasoma kwamba Stefano alipewa nguvu na Roho Mataktifu na kwamba alikuwa na Amani katika moya wake wakati alikumbana na wale ambao walimwua.

C. Matendo 7:1, Stefano aliulizwa kama yale ambayo yalikuwa yanasemwa yalikuwa ya kweli. Katika mstari wa 2, Stefano alianza kuwaeleza historia ya wayahudi alianza na Abrahamu na akamalizia na ujenzi wa hekalu.

2. Katika mistari ya 51-53, Stefano aliwashituma viongozi wa Wayahudi, jambo ambalo liliwakasirisha sana. Mara moja walipiga mawe na kumwua.

A. Je, Stefano alitoa wapi ujasiri huo? Katika mstari wa 55, tunasoma kwamba ni Mungu Roho Mtatifu ambaye alimpa ujasiri huo. Funzo kwetu hapa ni kwamba, tunapaswa kuwa tayari kufa kwa ajili ya kazi ya Ufalme wa Mungu. Lakini pia tunapaswa kumtegemea Mungu atupatia hekima ya kutekeleza lolote kama tu vile Stefano alivyofanya. Wengi wamekufa kwa sababu ya kazi ya Mungu (Matendo 12:2; mathayo 14:10).

B. Katika mstari wa 58, tunaona Paulo ambaye aliitwa sauli akiwa hapo wakati Stefano alikuwa akiwauliwa.

Matendo 8 na 9, tunasoma kumhusu Sauli ambaye baadaye aliiitwa Paulo.

1. Matendo ya Mitume 8:1-3, tunasoma kumhusu Paulo akiwa na ghadhabu dhidi ya Wakristo.

2. Matendo 9:3-8, tunasoma kuhusu Paulo akikutana na Bwana Yesu Kristo akiwa njiani akielekea Damasku. Paulo aliokolewa wakati huu. Katika mstari wa 15, Mungu anasema kwamba amemchagua Paulo kuwa chombo chake cha kueneza ujumbe wa Injili. Katika mstari wa 16, Mungu anasema kwamba Paulo atateseka kwa ajili ya kumtumikia Mungu. Historia inadhihirsha kwamba kweli Paulo aliteseka sana n ahata aliuliwa.

3. Matendo 9:20, tunsoma kwamba mara moja Paulo alianza kufundisha kuhusu Yesu. Mara kwa mara wale ambao wameokoka, huwa wanakuwa na tamaa kubwa sana kueneza injili ya Kristo. Lakini baada ya muda mfupi, wao hupoteza tamaa hiyo. Tunapaswa kuiga kutoka kwa Paulo amabye hakupoteza tamaa kuwaeleza wengi habari ya Kristo. Tunapaswa kujitolea kabisa kuwaeleza watu wote hadithi ya Yesu Kristo.
Matendo 9:36-42

1. Matendo 9:36-42, Petero alimfufua Dorkasi. Mistari inasema kwamba wengi walikuaj kwa Kristi kutokana na muujiza huu.

2. Katika mstari wa 41, tunasoma kwmamba jina lingine la wakristo ni watakatifu.

3. Matendo 10-11:18, kuna mambo mawili ya muhimu ambayo tunayasoma hapa.

A. Katika mistari ya 10:9-16 na 11:5-10, sheria za sherehe kuhusu chakula kisafi na kile kichafu, ziliondolewa. Katika Marko 7:14-19, Yesu alifundisha kwamba kile ambacho kinaingia ndani ya muda siyo ndio kinachomchafua. Bali ni kile ambacho kinachotoka ndani mwake ndicho kinachomchafua. Mawazo yote mabaya yanatoka ndani ya moyo.

B. Jambo hili lilifanyika kuandaa petero na Mitume ili waweze kuwapokea watu wa mataifa ambao walikuwa waokoke. Petero alitumwa kwa Kornelio na alienda na akamhubiria ujumbe wa wokovu ambao unapatikana kwa imani ndani Kristo Yesu. Biblia inasema kwamba Kornelio na wenzake waliokolewa. Matendo 10:44, tunasoma kwamba Roho Mtakatifu aliwajia watu hawa.

C. Matendo 11: 2-3, Petero alikashifiwa na wakristo Wayahudi ambao hawakufahamu kwamba Yesu alikuja kwa ajili ya watu wote. Shida kubwa ambayo ilikuwepo katika kanisa la kwanza ni kwamba wengi wa wakristo Wayahudi hawakutaka kuchanganyika na watu wa mataifa ambao walikuwa wameokoka. Wengine waliwaza kwamba watu wa mataifa walihitaji kutahiriwa kwanza kabla ya kujiunga nao. Petero aliwajibu kwa kuwaeleza ujumbe ambao aliupata kutoka

kwa Mungu. Katika mstari wa 11, anasema kwamba Mungu anapeana msamaha wa dhambi kwa watu wote ambao wanatubu na kumwamini. Mungu anawapenda watu wake wote sawa. Yeye hawapendelei kabila au rangi au watu wa taifa fulani, wote ambao wameokoka anawapenda sawa.

3. Matendo 11:26, tunasoma kwamba wanafunzi waliitwa wakristo kwanza katika mji wa Antiokia.

4. Matendo 12, tunasoma kuhusu mateso makali sana ambayo yaliwatokeo wale ambao walikuwa wamemwamini Kristo. Mateso haya yalitoka kwa Wayahudi na hii ilisababisha wakristo watawanyike ulimwenguni kote. Kwa sababu hii pia sehemu nyingi ulimwenguni zilipata kusikia ujumbe wa Injili.

A. Katika mstari wa 2, tunasoma kuhusu kuuliwa kwa mtume Yakobo ambaye alichinjwa na mfalme Herode Agripa. Mstari wa 3, tunasoma kuhusu kushikwa kwa Petero. Lakini pia tunasoma kwamba kwa nguvu za Mungu, Petero aliachiliwa kutoka gerezani. Herode alifanya haya yote kwa sababu alitaka kuwapendeza Wayahudi hata kama yeye alijua kwamba ni vibaya kuwashika na kuwaua wanafunzi wa Yesu.

B. Mistari 21-23, tunasoma kwamba Herode alikubali kuitwa na kusifiwa kama Mungu na kwa sababu hiyo, Mungu alimwua Herode. Kifo cha Herode kilikuwa kifo kibaya sana na uchungu mwingi sana.

Matendo 13-14, tunasoma kuhusu safari ya kwanza ya Paulo ya kitume akiwa na Baranabasi. Tunajua kwamba Paulo alikuwa na safari 3 za kitume.

1. Matendo 13:2, tunasoma kwamba Roho Mtakatifu aliwaita Paulo na Baranabasi watengwe kwa ajili ya kazi ya kueneza injili kwa mataifa. Mstari wa 3, kuna fundisho hapa kuhusu umuhimu wa kuomba na kufunga kabla ya kuanza kazi ya Mungu. Ni vyema kuomba na kufunga na kuwa na wakati na Mungu ili tujue kama kweli Mungu ametuita au la. Pia tukumbuke kwamba ni kazi ya kanisa kuwatuma wahubiri katika sehemu zingine ili wahubiri huko. Kanisa leo linapaswa kujihusisha na kazi hii.

2. Safari ya kwanza ya Paulo ya Kitume ili kuwa kwa mataifa mengine katika Asia. Huko watu waliokoka walipowahubiria injili na pia kulikuwa na upinzani mkubwa sana. Wayahudi ambao walikuwa huko mara kwa mara waliwapinga. Katika Matendo 14:19-20 tunasoma kwamba Paulo alipingwa sana na hata karibu kuuliwa. Lakini tunsoam tena kwamba Paulo aliweza kuenda katika mji mwingine na huko pia alihubriir Injili. Paulo alimpenda sana Mungu na

hangeweza kuacha kuhubiri injili hata kama maisha yake yalikuwa katika hatari kubwa sana. Je, sisi ambao tumeokoka tuko na tamaa kama ya Paulo leo? Paulo alitoa maisha yake yote kwa ajili ya kumtumikia Mungu. Je, sii tuko kama Paulo au tunamfuata tu Mungu kw asababu yay ale ammabo mazuri ambayo anatuptaia? Tunapaswa kuwa kama Paulo.

3. Matendo 14:23, kanisa la kwanza walifunga walipowateua wachungaji wao. Tunasoma kwamba, “Nao baada ya kuwateua wazee katika kila kanisa, kwa kufunga na kuomba wakawakabidhi kwa Bawana waliyemwamini.” Tunapaswa kuiga kutoka kwao.

Matendo 15 tunasoma kuhusu kutokubaliana katika kanisa.

1. Wayahudi ambao walikuwa wameokoka walisisitiza kwamba wale ambao walikuwa wameokoka na ni watu mataifa walipaswa kutahiriwa kwanza. Hii haikufaa hata kidogo. Paulo baranabasi na viongozi wengine wa kanisa walisema kwamba kutahiriwa hakukufaa hata kidogo kwa sababu kusisitiza kutahiriwa ni kufanya wokovu uwe kazi ya mwanadamu. Biblia inafundisha kwamba tunaokoka kwa imani pekee katika Kristo Yesu kwa sababu ni Kristo ambaye amefanya kazi yote ambayo ilihitajika ili sisi tupate kuokoka.

2. Kwa hivyo walikubaliana kwamba kutahiriwa hakukuhitajika hata kidogo. Katika mistari ya 19-20 tunasoma kwamba waliandika barua na kuzipeleka kila mahali kuhusu uamuzi wao juu ya kutahiriwa. Lakini hata hivyo wao pia walisema kwamba watu mataifa hawakufa kula vyakula fulani ili wasiwakosee wayahudi ambao walikuwa wameokoka. Hii haikuwa kweli.

3.Katika mstari wa 28, tunasoma kuhusu jambo la muhimu sana. Wakristo wanapaswa kufuata tu Biblia pekee. Hatupaswi kuongeza kanuni na tamaduni za wanadamu kama mafarisayo ambao walimkasirisha Kristo kwa sababu ya kanuni na sheria zao. Kwa mfano kuna makanisa ambayo yanasema kwamba siku ya Jumapili hatupaswi kupika chakula.

4. Katika mistari ya 36-40, tunasoma kuhusu Paulo na baranabasi wakipingana kuhusu kuenda na Marko kwa safari yay a Kitume. Kwa sababu hii, wao walitawanyika na kila mmoja akaenda sehemu yake kuhubiri huko. Wao hawakupigana kama jinsi tunavyoona leo katika makanisa tofauti tofauti. Ni jambo la kawaida kutokubaliana juu ya mambo fulani katika huduma. Lakini hata hivyo hatupasi kupigana. Kulikuwa na faidi katika kutawanyika kwao, kwa sababu waliweza kuwafikia watu zaidi wakiwa katika vikundi viwili.

Matendo 16-20, tunasoma kuhusu safari ya Paulo ya kitume ya pili nay a tatu. Tutatazama mambo machache kuhusu safari hizi. Ni vyema kwamba usome sura hizi zote.

1. Matendo 16:7, tunafundishwa kwamba tunapaswa kuwa waangalifu katika kuongozwa na Roho Mtakatifu. Mungu ndiye anaongoza kila jambo na wala si sisi.

2. Matendo 17:23, tunasoma kuwahusu watu ambao walikuwa wanamwabudu miungu ambaye alikuwa hajulikani badala ya kumwabudu Mungu ambaye amejidhihirisha kwetu kupitia kwa Biblia. Katika historia tunasoma kwamba watu wamekuwa wakiabudu miungu ambayo wao wenyewe wamejitengenezea. Leo wengi wanasema kwamba hakuna Mungu na miungu wao ni sayansi. Wanamwabudu Mungu ambaye wenyewe wamejitengenezea. Wanaabudu miungu ambayo hawaijui.

3. Matendo 17:29-31, tunasoma kwamba kabla ya Yesu kuja, Mungu alipuuza dhambi za watu. Lakini sasa kwa sababu kila siri kuhusu wokovu imefunuliwa, Mungu anwamuru watu wote watubu dhambi zao na wamwamini. Katika mistari hii 3, Paulo anatupatia sababu 3 kwa nini tunapaswa kutubu na kuwamini Mungu. Katika Agano la kale, watu waliokolewa kwa kutazamia kuja kwa Mesiya. Leo tunaokolew kwa kuutazama msalaba wa Kristo.

A. Mungu amekuwa mvumilivu nasi, lakini uvumilivu wake unaweza kuishi wakati wowote na awadhibu wale wote ambao wanakata kutubu na kumwamini.

B. Mungu ameamuru watu wote watubu na waokoke (Matendo 2:38).

iii. Mungu ameweka siku moja ambapo atahukumu watu wote na yesu Kristo ndiye atakuwa hakimu.

4. Matendo 20:7, tunasoma kwamba kanisa la kwanza lilikutana siku ya kwanza ya Juma ambayo ilikuwa Jumapili.

Matendo 21-26, tunasoma kumhusu Paulo akiwa Yerusalemu.

1. Matendo 21, tunsoma kuhusu Paulo akishikwa na kuwekwa gerezani kwa sababu msimamo wake mkali wa injili ya Kristo.

2. Matendo 23, tunasoma kuhusu Paulo akiwa mbele ya baraza ya Wayahudi ambalo pia lilitoa uamuzi mbaya kuhusu Kristo.

3. Wayahudi walipigana wenyewe na ikaonekana kana kwamba vurugu mbaya sana ingetokea kwa hivyo Warumi walimwondoa Paulo hapo. Katika matendo 23:11, Mungu alimwambia Pualo

kwamba haya yote yalitokea ili Mungu kama njia ya Mungu kumpeleka Paulo Roma ili atangaze Kristo huko.
4. Katika mistari 12-14, tunasoma kuhusu hasira ya Wayahudi dhidi ya Paulo kiwango kwamba hata kuna wengine ambao walihapa kwamba hawatakula au kunywa hadi wamehakikisha kwamba Paulo ameuliwa. Lakini hata hivyo Mungu hakuwakubali kumwua Paulo.

5. Paulo alikuwa mwenyeji wa Roma na jambo hili lilifanya akapewa ulinzi mzuri chini ya sheria ya warumi. Paulo alipelekwa kwa gavana Felix ambaye alimhoji Paulo na baadaye kuangizwa kwamba afungwe gerezani mahali ambapo alikuwa kwa miaka miwili. Gavana mpaya ambaye aliiitwa Festua alimpa Paulo na nafasi nyingine ya kujitetea mbele ya hakimu Wayahudi lakini Paulo alikataa. Kwa sababu Paulo alikuwa mwenyeji wa Roma alikuwa na haki ya kuitisha kusikizwa tena kwa kaisari. Katika Matendo 25:11. Tunasoma kwamba aliitisha jambo hili.

5. Mfalme Agripa akiwa na Festus walikuja pamoja na kumhoji Paulo. Katika Matendo 25:25, Festua alikubali kwamba hakuona makossa yoyote ambayo Paulo alikuwa ameyafanya. Sasabu moja ambayo ilimfanya Festus asimwachilie Paulo ni ile ile ambayo ilifanya Yesu asiachiliwe. Yeye alitaka kuwapendeza Wayahudi hata kama alijua ukweli. Hawa wote wawili pamoja na Pilato walikataa kumwachilia mtu ambaye walijua kweli kwmba hakuwa na makossa yoyote. Kila wakati tunapaswa kufanya kile ambacho tunajua kwamba kinamletea Mungu utukufu na wala si kumfurahisha mwanadamu.

6. Matendo 26, tunasoma jinsi Paulo alivyojitetea akizungumza kuhusu hali yake ya zamani akiwa farisayo, jinsi aliokoka na jinsi alivyokuwa anafanya kazi ya kuhubiri injili ambayo ndio sababu wayahudi walikuwa wanampinga na kutafuta kumwua.

A. Paulo alizungumza ujumbe wa injili kwa Mfalme Agripa. Katika mstari wa 24, Agripa anasema kwamba Paulo ni mwanda wazimu. Paulo alijaribu kumshawishi mfalme kwamba anaopaswa kuokoka.

B. katika mstari wa 27, Paulo anamalizia ujumbe wake kwa Agripa. Agripa alikataa kuamini ujumbe wa injili kwa kuufanya moyo wake kuwa mgumu sana. Baada ya hili, Agripa alikufa kwa hivyo hakuweza kuokoka.

7. Mistari ya 31-32, tunasoma kwamba Festus na Agripa wote hakuweza kupata Paulo na makossa yoyote. Paulo angekuwa amewekwa huru lakini alikuwa ameitisha kusikilizwa na Kaisari huko Roma. Hii ndio njia Mungu alitumia kumwondoa Paulo kutoka Yerusalemu hadi Roma.

Matendo 27-28, tunasoma kuhusu Paulo akienda Roma.

1. Safari ya kuenda Roma alifanyika wakati mbaysa sana wa mwaka wakati kulikuwa na mawimbi makali sana kwa bahari. Tunasoma kwamba kwa sababu ya mawimbi makali, meli ambayo Paulo alikuwemo alivunjika na walibaki katika kisiwa cha Malta. Meli ilihabiwa kabisa lakini Mungu aliokoa maisha ya Paulo na wale owte ambao walikuwa katika meli hiyo. Jambo hili Paulo alikuwa amelizungumzia katika Matendo 27:34.

2. Paulo alikwama katika kisiwa cha Malta ambacho kiko karibu sana na Italia. Mungu aliendelea kumlinda hata wakati aliumwa na nyoka. Tunajifunza hapa kwamba tunapaswa kufanya kazi ya Mungu kwa ujasiri sana. Yeye Mungu atatulinda wakati wowote anapotutuma kufanya kazi yake. Pia atatupeleka mbinguni.

3. Wakati msimu wa baradi ulipoisha, Paulo alienda Italia. Matendo 28:14, huko italia kuliwepo na dini ya ukristo.

4. Tunaona pia kwamba hata kama Paulo alikuwa gerezani, alikubali kuwafundisha wale ambao walikuwa wakija kumwona kuhusu Yesu Kristo. Tunapaswa kufahamu kwamba hakuna jambo ambalo litazuia mipango ya Mungu kukamilika. Hata huko gerezani, Mungu alitaka Paulo aendelee kuhubiri injili ya Kristo.

Warumi

Hii ndio barua ya kwanza ya Paulo. Kuna barua 21 kwa ujumla ambazo zimeandikwa kutufundisha kuhusu kile ambacho tumeamini na jinsi ya kuishi maisha ya ukristo. Barua zingine ziliandikwa kusahihisha makossa ambayo yalikuwepo katika makanisa au katika maisha ya watu fulani. Paulo aliandika barua 13.

Barua ya Warumi aliandikwa kwa kanisa la Roma kabla ya Paulo kuenda Roma. Hii ni barua nzuri sana kwa sababu inafundisha misingi ya imani ya kanisa la Kristo. Katika barua hii tunaona kwamba kila mtu anapaswa kuajibika mbele za Mungu na kwa sababu hiyo, kila mtu anahitaji kuokoka. Paulo anafundisha jinsi ya mtu anayohesabiwa kuwa mwenye haki na jinsi ya kuishi maisha yetu tukiwa wakristo. Pia anafundisha jinsi Mungu atakavyowashughulikia Wayahudia. Paulo hatufundishi tu jinsi tunapaswa kuishi tukiwa tumeokoka, lakini pia yeye mwenyewe anatupatia mfano kwa jinsi yeye mwenyewe alivyojitoa kabisa kwa Mungu hata wakati wa majaribu makali sana katika maisha yake.

Hii barua ambayo inadhihirisha maisha ya mkristo ni maisha ya aina gani. Tunaweza kumaliza mwaka mzima tukisoma kitabu hiki, lakini hata wakati huo hatutamaliza mafundisho yake yote. Ninajua mchungaji mmoja ambaye alimaliza miaka 9 akifundisha barua hii. Barua hii ya Warumi ikna mafundisho ya msingi mengi ambayo yalifundishwa katika Agano la Kale haswa katika kitabu cha Isaya. Kwa mfano tunasoma katika barua hii kwamba Mungu ndiye anatawala kila kitu. Katika Isaya 43:1, Mungu ndiye anayetukomboa; Isaya 43:21,25, Mungu alituomba kwa ajili ya kusudi lake na anatukomboa kwa utukufu wake; Isaya 44:1-2, Mungu ndiye anachuagua ni nani atakayemwokoa. Isaya 45:1-7, tunasoma kuhusu ukuu wa Mungu. Haya ndio baadhi ya mafundisho ambayo yamo katika barua ya Warumi. Biblia inafundhsa jambo moja yote.

Augustine na Martin Luther wote wawili waliyatumia mafundisha ya barua hii kufahamu na kufundisha kumhusu Mungu. Luther alifahamu kutokana na barua ya Warumi kwamba hatuokolewi kwa matendo yetu mazuri na kwamba kile ambacho kanisa la katoliki linafundisha kuhusu dhambi si kweli kwa sababu ni kinyume na Biblia. Tunafanywa wenye haki kwa kazi ya Mungu pekee.

Martin Luther ni mmoja wapo wa baba wa kanisa la kiprotestanti. Makanisa yote ambayo si ya kikatoliki au Kigiriki, ni ya Kiprotesitante. Martin Luther alikasirishwa sana na tabia ya malipo kwa ajili ya msamaha ambayo yalikuwa yanadaiwa na kanisa la kikatoliki wakati huo. Tabia ilihimiza watu kufanya dhambi kwani waliwaza kwamba unaweza kununua msamaha wa dhambi zako ambazo unaenda kutenda kesho yake. Pia ungeweza kulipa ili dhambi za mtu ambaye alikufa zisamehewe. Wakati Luther alisoma barua ya warumi, aliona jinsi kanisa la kikatoliki lilivyokuwa linafundisha mambo ya uongo.

I. Sehemu ya kwanza ya barua ya warumi inazungumza kuhusu hali ya wanadamu wote mbele za Mungu. Wanadamu wote ni wenye dhambi na kwa sababu hiyo wote wako na hatia mbele za Mungu (Warumi 1-3:20).

1. Paulo anaanza kwa kutoa salamu zake kwa watu wote. Katika mstari wa kwanza anasema kwamba yeye ni mtume wa Bwana Yesu Kristo. Katika mstari 13, Paulo anasema kwamba anatamani sana kuja Roma. Katika matendo ya Mitume tunajua kwamba baadaye alienda huko.

2. Warumi 1-14:20, tunasoma kwamba Mungu amejifunua kwa wanadamu wote na kwamba wanadamu wako na hatia mbele za Mungu.

A. Katika mistari 14-15, Paulo anasema kwamba kazi yake na ujumbe wa Injili si kwa Wayahudi pekee yao, bali pia kwa watu mataifa. Hii mada kubwa sana katika barua hii kwa Warumi na Biblia nzima. Machoni pa Mungu hakuna tofauti kwa mzungu au mwafrika, kabila au kitu kama

hicho. Kila mkristo ni maana sana machoni pa Mungu. Mchungaji wa kanisa lako si wa muhimu sana machoni pa Mungu kuliko msishirika. Mchungaji si mtu ambaye ako karibu sana na Mungu kuliko wakristo wengine.

B. katika msitari 16-17, Paulo anaandika akisema kwamba hatufai kuonea aibu ujumbe wa injili kwa sababu katika ujumbe huo kuna maagizo ambayo yanaleta wokovu wa nafsi. Wale ambao wameokoka tunapaswa kuishi maisha yetu kwa imani katika Kristo. Mungu alipeana wokovu kwanza kwa Wayahudi halafu klwa watu mataifa. Lakini wayahudi wengi walikataa wokovu huu.

D. Mstari wa 17, tunasoma kwamba wale ambao ni wenye haki wataishi maisha yao kwa imani.

i. Ili mtu aweze kufika mbinguni ni lazima kwanza ahesabiwe mwenye haki mbele za Mungu. Kuhesabiwa kuwa mwenye haki ni kitendo cha Mungu wakati anawasamehe dhambi wenye dhambi na kuwakubali kwa msingi wa kazi ambayo Kristo aliifanya. Kufanyika mwenye haki, inamaanisha kwamba machoni pa Mungu, hatuna dhambi hata kidogo. Kufanywa mwenye haki ni jambo ambalo linafanyika mara moja katika maisha ya mtu na hii ni kazi ya milele.

ii. Tunapokea msamaha wa dhambi kwa imani ndani ya Yesu Kristo. Pia msamaha huu ni wa bure ambapo Kristo anatupatia haki yake. Msalabani Kalivari Kristo alizibeba dhambi zetu zote na akadhibiwa ili sisi tuweze kupata haki yake ya wokovu.

iii. Sisi sote tunaamani katika mambo mengi kama kuamini kwamba kiti ambcaho tumekikalia kiko dhabiti na kwamba hakiwezi kutuangusha. Lakini hii si imani ya kuokoa. Imani ambayo inaokoa, ni imani katika Kristo Yesu ambaye hatumwoni. Ni imani katika mbingu na wala si katika ulimwenguni na vitu vyake. Ni imani ambayo inakuja kwa kusikia na kutii neno la Mungu.

3. Paulo sasa anataka kuzungumza kwa nini tunahitaji wokovu. Tunahitaji wokovu kwa sabau sisi ni wenye dhambi. Katika mistari ya 18-23, sisi sote tuko na hatia mbele za Mungu kwa sababu ya dhambi zetu. Mungu anajidhihiorsha kwetu kupitia kwa kazi yake ya kuumba kila kitu lakini hata hivyo, tunachagua kumpuuza na kuabudu miungu. Huwa tunachugua kuabudu kiumbe badala ya kumwabudu Mwumbaji ambaye ni Mungu. Katika mstari wa 26, Mungu aliwaachilia watu katika dhambi zao. Shida kubwa ni kwamba watu wanataka kumfanya Mungu awe jinsi wao wenyewe wanataka, badala ya kumkubali na kumwabudu jinis alivyo na jinsi amejifunua kwetu.

A. Katika mstari wa 18, tunasoma kuhusu ghadahabu ya Mungu. Tunapaswa kuwafundisha watu kuhusu hatari ya ghadhabu ya Mungu. Tunapaswa kuwaonya watu. Agano la kale

linatufundisha sana kuhusu ghadhabu ya Mungu. Kuna wengi ambao hawataki kusikia kuhusu ghadhabu ya Mungu badala yake wanataka ujumbe ambao unawapendeza. Ujumbe huu ni kama jinsi walivyo watu wazuri, ujumbe kuhusu utajiri wa hapa duniani, miujiza ya kuponywa na mambo kama hayo (2 Timotheo 4:3-4).

i.Kuna maknisa mengi ambayo yanafundisha ujumbe ambao watau wanaupenda kuusikia. Ujumbe ambao si wa kristo. Makanisa kama haya yanakubali dhambi miongoni mwake kama dhambi za usenge au ushoga na talaka.

ii. Kuna wachunga wengi ambao hawapendi kufundisha kuhusu ghadhabu ya Mungu kwea sababu hawataki kuwapoteza watu ambao watatoa sadaka kubwa katika makanisa yao. Mungu anataka makanisa ambayo ni matakatifu. Mungu anajali sana ukweli na wala si idadi ya watu.

B. Jambo hili la kufundisha kuhusu ghadhabu ya Mungu ni la muhimu sana na tunahitaji kulisoma zaidi. Tunapswa kuwashawishi kwa kuwafundisha watu kuhusu jambo hili wakati huo tukiwaonya. Pia tukumbuke kwamba hatuwezi kamwe kufahamu wokovu wetu ikiwa hatufahamu ni nini ambacho Mungu ametuokoa kutoka ndani mwake ikiwa hatuelewi ghadhabu ya Mungu. Tunapoendelea kusoma zaidi kuhusu ghadhabu ya Mungu, tunapasw akuwa wenye shukurani kubwa sana kwa sababu Yesu ametuokomboa kutoka katika ghadhabu ya milele jahanum.

C. Kuna vifungu kadhaa katika Biblia ambavyo vinatuonya sana kuhusu ghadhabu ya Mungu kuliko upendo wa Mungu. Kuna zaidi ya vifungu 600 kuhusu ghadhabu ya Mungu (Kutoka 22:22-24 na Ufunuo). Mungu anataka kuhakikisha kwamba tumepata onyo ya kutosha ili tusienda jahanum. Ni jambo la muhimu sana kwa wachungaji kuhubiri kuhusu ghadhabu ya Mungu na wakati huo pia kufundisha wazi kuhusu neema ya Mungu.

4. Katima mstari wa 26, tunasoma kwamba kuna wakati Mungu anawaachilia watu kupotelea katika dhambi zao. Tunaona hili katika mataifa fulani fulani ya ulimwengu n ahata katika watu fulani ambao maisha yao ni ya dhambi na hawajali Mungu na mipango yake kabisa. Wao wanajali tu jinsi watakuwa matarjiri.

A. Katika mstari wa 26, tunasoma kwamba Mungu anaweza kuwaadhibu watu kwa kuwapatia viongozi wabaya ambao wataleta uangamizi kwa mataifa hayo kwa haraka sana (Isaya 3:1-8).

B. Je, unawaza nini juu ya taifa lako? Je, taifa lako liko chini ya hukumu wa Mungu?

6. Katika mistari ya 19-23, tunasoma kuhusu jinsi Mungu alivyotukasirikia. Tunaona kwamba Mungu amejidhihirisha kwetu na kwa sababu hatuna kijisababu ni kwa nini tusimwabudu au kumtii. Kuna ufunuo mara mbili.

A. Kuna ufunua wa jumla. Kiumbe kinamfunua Mungu kwetu (Zaburi 19:1-2). Kile ambacho tunastahili kufanya ni kujifunza kutoka kwa kiumbe na kuona utukufu wa Mungu. Ni mpumbavu pekee ambaye anasema kwamba hakuna Mungu baada ya kuona mambo haya yote. Mungu anajidhihirisha kwa watu wote.

i.Sisi sote tunajua kwamba mambo fulani ni mabaya. Kwa mfano, Mungu ameweka katika mioyo yetu kwamba kumnajisi mtu wa kike ni jambo bay asana au kumwua mtu.

ii. Ufunoa wa jumla ndio msingi wa ufunoa maalumu ili sote tuweze kufahamu na kupenda ufuao wa maalumu.
B. Ufunuoa wa malaamu n I ufunuo wa Mungu kwetu akitueleza Kristo ni nani nay ale ambayo Kristo ameyafanya. Mungu anajifunua kupitia kwa Biblia ambayo inazungumza kumhusu Yesu na jinsi ametukomboa kutoka kwa dhambi. Kufahamu Kristo Yesu ni jambo la muhimu sana kwetu ikiwa tutapata kuokoka (Warumi 10:9).

i. Ufunuo maalumu unatoka kwa Biblia.

a. Unajumlisha kudhihirika kwa Mungu katika Mwanzo 15:1.

b. Biblia inamfunua Mungu na ufahamu wetu unatoka kwa Mungu (2 Timotheo 3:16-17).
Tunamwona kristo Yesu katika Biblia na pia katika kuumbwa kwa kila kitu (Mwanzo 1:26; Yohana 1:1-3).

C. Ufunuo wa jumla hatosheliezi kwa wokovu kwa sababu hatuwezi kuja kwa Kristo kwa wokovu bila ufunuo maalumu. Mungu atawahukumu watu wote ikiwa watakataa kumwamini Kristo (Matendo 17:30).

F. Dhambi ya usenge inatumika kama mfano katika warumi 1:26-27. Mungu amewaachilia katika dhambi zao na wakati ufao, wao watapata adhabu ya dhambi zao. Hii kwa wote ambao wanaendelea katika dhambi hizi na wanakataa kutubu. Miaka ambayo imepita watu walikuwa hataji dhambi hizi wazi wazi, lakini sasa tunawaona wengi wakifurahia dhambi hizi na kuzitetea kuonyesha wazi uonvu ambao watu wako ndani na hukumu ya Mungu kwao.

i.Dhambi ya usenge ni mbaya sana machoni pa Mungu na Mungu anaichukia saa. Mara kwa mara Mungu anatangaza hukumu juu ya dhambi hii. Kwa sababu ya dhambi hii, Mungu aliichoma miji ya Sodoma na Gomora.

ii. Je, ni kwa nini Mungu anaichukia dhambi hii ua usenge? Mungu anaichukia kwa sababu dhambi hii ni madharau kwa familia ambayo Mungu anaipenda. Mungu ndiye alianzisha ndoa na familia (Mwanzo 2:24). Shetani huwa anajaribu kuharibu familia na katika sehemu nyingi sana amefaulu.

Je, hapa Afrika bado watu wanazingatia familia?

7. Warumi 1:28-32, tunasoma tena kwamba Mungu aliwaachilia katika dhambi zao na kwamba dhambi zao zingeongezeka na mwishowe Mungu angewahukumu. Katika maisha yao wao wanafamnya dhambi na kufikia kiwango cha kuona kwamba dhambi zao ni sawa. Wao hawahisi tena aibu juu ya dhambi zao. Kutenda dhambi zao ni maisha ya kawaida. Wao hawawazi kabisa kuhusu hukumu ya Mungu kwa sababu ya dhambi zao. Mtu anapoanza kufanya dhambi mara ya kwanza, atahisi kwamba kile anafanya ni kibaya sana. Lakini anapoendelea katika dhambi hizo. Dhambi zetu kama kudanganya au kuwapiga wake wetu zinakuwa za kawaida tu tunapoendelea kuzifanya na tunakata kutubu. Wakatu huu Mungu anatuachilia katika dhambi zetu na hili ni jambo la hatari sana.

8. Warumi 2:1-5, tunsoma kwamba hakuna mtu ambaye anakijisababu chohcote kwa ajili ya dhambi zake. Kila mmoja wetu anapaswa kuajibika mbele za Mungu kwa ajili ya dhambi zake. Hasira ya Mungu inaendela kuwaka juu ya wale wote ambao wanaendelea kutenda dhambi na wanakataa kutubu.

A. Usimwonee wivu mwenye dhambi ambaye maisha yake yanaonekana kuwa mazuri hapa ulimwenguni lakini anakataa kutubu. Kumbuka hadithi ya Lazaro na tajiri katika Luka 16. Jishughulishe na kuhakikisha kwamba unatembe na Mungu katika utakatifu.

9. Kwa wakati wa Mungu ufao, atawadhibu wale ambao wanakataa kuokoka. Warumi 2:6-16 tunasoma kwamba kila mtu atajibika mbele za Mungu kwa matendo na maneno yake. Hii inamaanisha kwamba wayahudi watajibika jinsi walivyomshughulikia Kristo na wala si kwa sababu kwamba wao ni Wayahudi (Ezekieli 18:30).

A. Mistari ya 9-11, tunasoma kwamba Mungu atatuhukumu kulingana na neno lake la kweli. Mungu hataonyesha upendeleo kwa mtu yeyote wakati atakuwa anahukumu wenye dhambi.

B. Katika mistari ya 12-15, Mungu atahukumu kulingana na sheria yake takatifu. Hakutakuwa na kijisababu cha kutojua sheria ya Mungu.

C. Katika mstari wa 16, hukumu itakuwa kwa sababu ya kila jambo hata siri za mioyo yetu. Mungu atahukumu mioyo kulingana na neno lake.

10. Warumi 2:17-29, Paulo anazungumza na Wayahudi. Anawaambia kwamba Mungu atawahukumu kwa sababu ya matendo yao. Wayahudi wengi waliwaza kwamba kwa sababu walikuwa taifa teule la Mungu, Mungu hangeweza kuwaadhibu. Paulo aliataka wayahudi wajue kwamba wao kama tu watu wengine hawakuwa na kijisababu cha kukosa kuhukumiwa na Mungu kwa sababu wao ni wayahudi. Huu ni mfano wa leo ni kwamba kwa sababu mtu ni mchungaji asiwaze kwamba mbinguni kwake ni lazima au awe amezaliwa katika jamii ya wakristo kwa sababu hiyo, mbingu ataingia lazima.

A. Latika mistari ya 17-24, Paulo anasema kwamba walifaa kuwa mfano kwa sababu wao walikuwa na sheria ya Mungu. Aliwakemea wayahudi kwa saabu wao walikuwa wanafundisha sheria lakini hawakuwa wanatii sheria hiyo. Anawaambia kwamba kwa kufanya hivyo, walikuwa wanamkosea Mungu heshima na hivyo ni kuwa wanafiki. Funzo kwetu ni kwamba tunapaswa kuwafundisha wengine kile ambacho tunakifanya hatufai kuwa wanafiki.

B. Katika mistari ya 25-29, Paulo anazungumza na wale ambao wanaamini katika dini kuingia mbinguni. Anazungumza kuhusu kutahiriwa ambako kunalinganishwa na kubatizwa au kuwa mshirika wa kanisa. Anasema kwamba mambo haya yote hayawezi kutufanya tukubalike machoni pa Mungu. Katik amistari ifuatayo tutatazama mawazo yake Paulo.

i.Katika mstari wa 25, anasema kwamba kutahiriwa au ubatizo ni ishara tu ya nje na bure ikiwa ndani mwa mtu hakuna ukweli. Ubatizo ni isgara kwamba wewe umekufa kwa dhambi na kufufuka kwa maisha mpya. Ikiwa mtu haishio maisha matakatifu, ni bure kabisa hata akibatizwa kwa sabau itakuwa wazi kwamba hajaokoka.

ii.Katika mstari wa 26, tunasoma kwamba ishara ya nje si ya muhimu sana. La muhimu kwanza ni kutii neno la Mungu na kuwa na moyo mpya. Nia ya moyo wako ni ya muhimu sana kuliko hali yako ya nje. Je, wewe unayapenda maisha ya ukristo?

iii. Katika mstari wa 27, matendo yetu yanatenga na wengine. Yule ambaye ni ameokoka na yule ambaye hajaokoka wanajulikana. Mtu mataifa ambaye ameokoka, atamwaibisha Myahudi ambaye anakataa kumtii Mungu.

iv. Mistari ya 28-29 inamalizia mafundisho katika kifungu hiki. Mambo ya nje ya si ya muhimu sana kama mambo ya ndani ya moyo kwa kuwa Mungu anaanglai moyo na wala si nje.
We see examples of this over and over again in the Bible. Let's look at the book of Amos:

1. Amosi 5:11-12, tunasoma kwamba uovu unatoka ndani ya moyo wa mtu.

2. Mstari wa 16, tunasoma kuhusu hukumu kwa sababu ya mambi ya nje.

3. Mstari wa 21, Mungu anachukia kuabudu ambako wenyewe dhambi wanatoa kwake kwa sababu hakutoka katika mioyo yao bali kutoka katika mabo yao ya nje.

4. Mstari wa 24, Mungu anataka haki na moyo safi. Tunapaswa kumwabudu Mungu kwa moyo msafi ambao umetubu dhambi.

Every person ever born is judged by their actions and not by anything else. The Christian is judged by his action of belonging to Christ, of his faith in Christ. Many people think that they will be accepted by God because they grew up in a Christian home or they are members of a church. Just like the Jew they will only be acceptable if they belong to Jesus.

11. Warumi 3.

A. Mistari ya 1-4, je kuna umuhimu gani kuzaliwa ukiwa Myahudi au kuzaliwa katika jamii ya kikristo? Paulo anajibu hili kwa kusema kwamba watu ambao wanazaliwa katika jamii hizi wako na neno la Mungu na kwa sababu hiyo wako na nafasi bora kuliko wengine kwa sababu wao wako na ufahamu kumhusu Mungu.

B. Mistari ya 9-18, tunasoma kwamba hakuna mwenye haki na kwamba sisi sote tuko chini ya hukumu wa Mungu. Jambo hili linazungumziwa zaidi katika Warumi 9.

i.Hapa tunapata mafundisho ya kuanguka kwa mwanadamu katika dhambi na ukose wa mwanadamu kujiokoa mwenyewe. Wanadamu wote ni wenye dhambi isipokuwa Kristo Yesu. Kwa asili hakuna lolote zuri ndani mwetu. Chochote ambacho ni kizuri kimetoka kwa Mungu au kinatoka kwa Mungu.

ii. kazi ya Mungu Roho Mtakatifu inadhihirika wazi katika maisha ya watu au kikundi cha watu. Mungu Roho Mtakatifu anaishi ndani mwa kila Mkristo na wale ambao wameokoka wanapaswa kuwashawishi wale ambao hawajaokoka. Kile ambacho ni kizuri kinatoka kwa Mungu (Yakobo 1:17).

12. Mistari hii inamalizia sehemu ya kwanza ya barua kwa Warumi. Tumeona mambo matatu ya muhimu katika mistari hii.

i. Kila anaajibika mbele ya kwa yale ambayo anayatenda.

ii. Kila mtu ni mwenye hatia mbele za Mungu kwa sababu ya dhambi zake.

iii. Hakuna mtu ambaye atafanywa mweny haki kwa matendo yake mazuri.

II. Tumemaliza sehemu ya kwanza ya barua kwa Waraumi ambayo inafundisha kwamba sis sote ni wenye hatia mbele za Mungu. Sasa tunataka kutazama sehemu nyingine ya baraua hii ambayo inatufundisha jinsi ya kuwa wenye haki mbele za Mungu. Yaani jinsi tunavyookolewa kupitia kwa imani ndani ya Kristo Yesu.

1. Warumi 3:21-31, haki kupitia kwa imani ndio njia ya pekee ya kupata wokovu.

A. katika mistari ya 21-26, tunasoma kuhusu haki ya Mungu.

i. Haki hii imedhihirishwa kwetu leo na ikon je ya sheria. Mstari wa 21.

B. Haki tunaweza kuipata tu kupitia kwa imani ndani ya Kristo na watu wote wanaihitaji (mstari 22-23).

i. Warumi 3:23, ni mojawapo wa mistari ambayo tunapaswa kukariri kila wakati kwa sabau ni jambi la muhimu sana ikiwa tutafahamu mafundisho ya mstari huu.

c. Wokovu ni zawadi ya bure kwetu kutoka kwa Mungu lakini tunapaswa kukumbuka kwamba kuna gharama ambayo ililipwa na Kristo Yesu.

D. Ghadhabu ya Mungu ilitoshelezwa na sadaka ya Kristo Yesu na ikiwa tutamwamini kristo, na kumwomba atuokoe kwa kutubu dhambi zate, basi tutaweza kupata haki hiki ya Kristo na kuzawadia na uzima wa milele (mstari 26).

E. Kuna mambo mawili ya ukweli ambayo tuyaona katika mistari ya 27-28.

i.Kwanza tunaona kwamba hakuna lolote ambalo tunaweza kufanya ili tujiokoe. Kwa sababu yah ii hakuna mtu ambaye anaweza kujivuna bali tunapaswa kuwa watu wenye shukurani (mstari 27-28).

ii. Pili tunaona kwamba Wayahudi na watu Mataifa wote wako sawa mmachoni pa Mungu. Mungu huwa anaona watu wa aina mbili humu duniani, wale ambao wameokoka na wale ambao hawajaokoka (mistari ya 28-29).

F. Je, ni kwa nini Sheria inahitajika? Inahitjika ili ifafanuwe zuri na lile baya. Tunaona kwamba kila mwanadamu amekosa kutii sheria ya Mungu na kwa sababu hiyio kila mwanadamu anahitjai mwokozi (mstari wa 31).

2. Paulo anatumia Abrahamu katika sura ya 4, kueleza tunafanywa wenye haki kupitia kwa imani katika Kristo Yesu. uses Abraham in chapter 4 as an example of the fact that our belief in Jesus is how we are justified. Abrahamu alihesabiwa mwenye kwa imani (Mwanzo 15:6) kabla ya yeye kufanya lolote zuri hama kutahiriwa.

A. Abrahamu alihesabiwa mwenye haki kwa imani (mistari ya 1-8). Paulo alitumia Abrahamu kwa sababu Wayahudi walimheshimu sana ili kuonyesha kwamba wanadamu wote wanaokolewa kwa imani.

B. Mistari ya 9-12, tunafundishwa kwamba matendo mazuri au kutahiriwa hakumwokowi mtu yeyote.

i. Mstari wa 11, kwa sababu ya imani, Abrahamu ni baba ya wale wote ambao wanaokoka. Jambo hili limetanjwa tena katika mistari ya 23-25. Baraka ambazo Abrahamu alipata kwa imani zilikuwa zetu pia ambao wanamwamini Mungu kupitia kwa Kristo Yesu.

ii. Katika mstari wa 11, tunaona kwamba kutahiriwa au matendo mazuri ni matokeo ya imani. Imani huza matendo mazuri.

iii. Kuna makanisa mengi leo ambayo yanafundisha kwamba kubatizwa ni kama kutahiriwa katika Agano la kale.

iv. Kutahiriwa ni kama ishara ya imani ya wokovu na wala si njia ya kupata wokovu kulingana na Yakobo 2:14,17-18. Wale ambao wameokoka huwa wanatenda matendo mazuri wala si kinyume kwamba matendo mazuri ndio chanzo cha wokovu. Tunaokolewa kwa imani pekee ndani ya Kristo.

C. Katika mistari ya 16-22, tunapata mafundisho kuhusu imani.

i. Wale wote ambao tumeokoka, sisi ni watoto wa Abrahamu (mistari ya16-17).

ii. Mistari ya 18-21, tunasoma kwamba hata kama mke wa Abrahamu Sara alikuwa mzee na pia alikuwa tasa, Abrahamu alimwamini Mungu wakati Mungu alimwambia kwamba angepata mtoto kupitia kwa Sara.

iv. katika mstari wa 22, tunaosma kwamba kwa sababu alimwamini Mungu, Abrahamu alihesabiwa haki.

E. Ahadi hii ya kufanywa mwenye haki pia inapewa wale wote ambao wameokoka.

Katika Biblia mtu anahesabiwa kuwa na imani ya kweli wakati mtu huyu anajua vyema kabisa njia ya wokovu na anaikubali na anaitegemea njia hiyo pekee na anaiamini njia hiyo tu. Ni vyema sana kujichunguza wenyewe ili tuone kama kweli tuko na imani kweli.

3. Warumi 5:1-11 Baraka ambazo zinaambatana na kufanywa wenye haki.

A. Baraka za hapo na hapo mstari wa 1-2.

i. Hii ni mistari ambayo inafariji sana. Hapa tunaonyeshwa kwamba kila mtu ambaye hajaokoka katika ulimwengu huu, yuko vitani dhidi ya Mungu. Wakati tunaokoka na kufanywa wenye haki, tunapata Amani na Mungu, uhasama na vita vyote vinaisha. Ni jambio la kutiosha sana kuwa vitani dhidi ya Mungu ambaye ni mwenye nguvu zote. Kwa sababu wale wote ambao wameokoka tunapaswa kuwa na furaha kwa sababu sasa tuko na amamnio na Mungu.

B. katika mistari ya 3-5 tunasoma kwamba injili ambayo inaahidi afya na mali, ni injili ya uongo. Hatufai kuacha kuamini Mungu kwa sababu ya shida nyingi ambazo zinatukumba. Tunasoma kwamba mateso huleta tumaini ndani mwetu kwamba kweli sisi ni wana wa Mungu. Tumaini hutuletea ujasiri kwamba sisi ni watoto wa Mungu.

C. Mistari ya 6-11, tunakumbusha juu ya upendo wa Kristo kwetu. Tunaosma kwamba Kristo alitoa maisha yake kwa ajili ya kutuokokoa. Kristo alikufa kwa ajili yetu wakati sisi tulikuwa vitani Naye. Hii ni dhihirisho tosha jinsi Kristo ametupenda.

D. Warumi 5:9-11, tunapata hakikisho kuhusu maisha ya mbeleni. Tunafundishwa kwamba tumefanywa wenye haki kwa damau ya Kristo na kwa sababu hii, ghadhabu ya Mungu

imeondolewa kwetu. Kwa ufupi ni kwamba Mungu hatuhukumu milele. Mstari wa 10, unadhihirisha hili na mstari wa 11, unatuhakikishia kwamba sasa tunaweza kufurahia kwa sababu tuko na Amani na Mungu.

E.Warumi 5:12-21, tunasoma kumhusu Adamu wa kwanza na Adamu wa pili ambaye ni Kristo. Kuna wengi ambao wanakaana kwamba Adamu hakuwahi ishi. Wale ambao tumeokoka tunaamini jambo hili. Tunaamini kwamba Mungu aliumba kila kitu na kwamba kila kitu kipo na kinaendelea kuwepo kwa nguvu za Mungu ambaye aliumba kila kitu.

i. Tunasoma kwamba dhambi iliingia duniani kupitia kwa mtu mmoja ambaye na Adamu na kwamba dhambi imedhuru kila mwanadamu. Kifo kiliingia duniani kupitia kwa dhambi ya Adamu (mistari ya 12-14).

ii. Mistari ya 15-21, sisi ni wenye dhambi kupitia kwa mtu mmoja ambaye ni Adamu na pia tunaokolewa kupitia kwa mtu mmoja ambaye ni Kristo. Zawadi ya wokovu kutoka kwa Mungu ni kuu mno kuliko dhambi ya Adamu.

a. Mistari ya 18-19, kitendo moja cha dhambi kilileta hukumu na kitendo kimoja cha haki kinaleta uzima wa milele.

b. Mistari ya 20-21, tunaona dhambi ni nini. Pai tunaona kwamba dhambi inapoongezeka, neema huongezeka zaidi. Hakuna dhambi kubwa ambayo Mungu hawezi kusamehe. Kumbuka kwamba dhambi ni kila kitu ambacho tunasema, tunakifanya, au kuwakiwaza ambacho hakimfurahishi Mungu. Pia ni chochote ambacho tunakosa kufanya ambacho Mungu anataka tukifanya.

III. Warumi 6-1, kwa sababu ya ujumbe wa Injili, mambo sasa yamekuwa tofauti kabisa. Kwa sababu tumeupokea ujumbe wa Injili, sasa sisi si watumwa wa dhambi tena. Sasa tunaishi maisha ambayo yanamtukuza Mungu ambayo hatukuwa tunayaishi.

I. Warumi 6:1-11, Kiumbe cha kale na kiumbe kipya.

A. Paulo anauliza swali katika mistari ya 1-2. Ikiwa maisha matakatifu hayatuokowi, basi kuna haja gani ya kuishi maisha haya? Je, ni kwa nini tusiendele kufurahia tu dhambi zetu? Jibu ambalo Paulo anapeana ni kwamba, hatufai tena kuishi maisha ya dhambi ikiwa tumekufa kwa dhambi. Tamaa ya mkristo ni kumpendeza Mungu na wala si kufurahia dhambi kwa kuishi maisha ya dhambi.

A. Mistari ya 1-2, Paulo anapinga wazo kwamba mkristo anaweza kuishi maisha yake jinsi anavyotaka kama tu mtu ambaye hajaokoka. Mojawapo wa baraka za kuwa mkristo ni kwamba sasa tunaweza kuishi maisha yetu kwa kumpendeza Mungu. Ikiwa mtu anaendelea kuishi maisha ya dhambi ni wazi kwamba mtu huyu bado hajaokoka. Mtu ambaye ameokoka, anaishai maisha yake kwa kumpendeza Mungu na hii ni ishara ya kweli kwambna yeye ni mtoto wa Mungu.

B. Paulo amezungumza kuhusu zawadi ya neema na kuna wale ambao waliwaza kwamba sasa tuko huru kuishi maisha mabyo tunataka wenyewe. Katika surah ii ya 6, Paulo anaonyesha kwamba wakristo wanafaa kuishi maisha kwa njia ambayo inadhihirsha kwamba sasa wao wako na Bwana mpya ambaye ni Mungu. Tunapaswa kumtii kuonyesha kwamba sasa sisi si watumwa wa dhambi.

2. Katika mistari ya 12-14, Paulo anaonyesha jinsi tunapaswa kuishi maisha haya. Anasema kwamba tulikuwa watumwa wa dhambi na shetani. Sasa tuko na Bwana mpya kupitia kwa imani ndani ya Kristo. Njia moja tunaweza kupinga dhambi ni kujitolea kabisa kwa kumtumikia huyo Bwana wetu Mpya ambayer ni Mungu. Hatufai kuacha dhambi na shetani kutawala mioyo na maisha yetu kwa sababu ikiwa tumeokoka, sisi ni wa Mungu na tunapaswa kufanya kila kitu kwa utukufu wa Mungu. Tunapaswa kujitahidi kumpendeza Mungu.

A. Hali ya dhambi kila wakati itakuwepo katika maisha yetu, lakini tunapoendelea kumkaribia Mungu zaidi na zaidi, ndipo tutaendela kupata nguvu za kushinda dhambi. Hivi ndivyo tunaweza kushinda dhambi.

i. Jiepushe na majaribu. Ikiwa kunywa pombe au utumiaji wa dawa za kulevya au kuwa karibu na wanawake ni jambo ambalo litakufanya uanguke, basi ni vyema kwamba usipatikane mahali ambapo pombe inakunywiwa au madawa ya kulevya yapo au mahali ambapo kuna wanawake ambao tabia yao inaweza kukuongoza katika dhambi ya zina.

ii. Jifunze kutokana na makossa yako ya zamani na umwombe Mungu akusaidie wakati unanguka katika majaribu ya dhambi.

3. Katika Warumi 6:5-23, Paulo anarudia tena, Je ni kwa nini tutii sheria ikiwa hatuko chini ya sherai? Paulo anajibu swali hili kwa kuuliza maswali na kuyajibu.

A. Katika mstari wa 16, Paulo anasema kwamba Bwana wetu ni yule ambaye tunamtumikia. Kumtii Mungu ni dhihirisho kwamba kweli tumeokoka.

B. Katika mstari wa 21, tunasoma kwamba tunapaswa kuwa watu ambao tunaonea aibu dhambi zetu za zamani na kwamba dhambi hizo zilikuwa zinatuongoza kwa kifo.

C. Katika mstari 22, tunasoma kwamba kwa sababu sisi ni watumwa wa Mungu, tuko na uzima wa milele.

D. Warumi 6:23, ni moja wapo wa mistari ambayo tunapaswa kukariri. Mstari huu unatufundisha kwamba kwa sababu sisi ni wenye dhambi, tunastahili jahanum. Lakini Yesu Kristo alikuja humu duniani kutupatia uzima wa milele kama zawad kupitia kwa imani.

4. Warumi 7:1-6, Paulo anafundisha kwamba wakati mtu mmoja amekufa, ndoa huwa inaishia hapo na yule ambaye amebaki huwa huru kumwoa au kuoleka kwa mtu mwingine. Jambo hili analilinganisha kwetu kwamba wakati tunaokoka huwa tunaondolewa katika nguvu za sheria. Huwa tunatolewa chini ya sheria na kuletwa katika maisha ambayo yanongozwa na Roho Mtakatifu. Sheria sasa haituhukumu sisi ambao tumeokoka. Hii haimaanisha kwamba sasa amri kumi hazina maana yyote katika maisha yetu. Bado tunastahili kuzitii.

A. Ili tusichangnyikiwa, tutazame mafundisho ya Paulo kuhusu uhuru wa mkristo na pia kwamba mkristo ni mtu ambaye hafai kutenda.

i. Ukweli ni kwamba kuna wakristo wanaanguka katika dhambi lakini dhambi si tabia ya maisha yake.

ii. Tunaweza tu kujua uzito wa dhambi kutokana na sheria. Yule ambaye ameokoka anapaswa kujitahidi katika kutii sheria ya Mungu.

iii. Yule ambaye ameokoka, huwa anatii sheria kwa sababu anapenda kutii Mungu. Kwa mfano ni kwamba huwa tunawafanyia watu wa familia zetu mambo mazuri kwa sababu tunawapenda.

5. Warumi 7:7-25, mistari hii inazungumza kuhusu maisha ya zamani na sasa ya mkristo.

A. Warumi 7:7, kusudi ya sheria ni kutambua dhambi. Sheria ni mzuri. Katika mstari wa 12, tunasoma kwamba sheria ni takatifu. Shida kubwa sana ni sisi kwa sababu hatuna uwezo wa kutii sheria.

i. Kusudi ya sheria ni kutusaidia kufahamu baya na zuri na kutusaidia kuona kwamba kwa nguvu zetu, hatuwezi kamwe kumfurahisha Mungu. Hadi tunapo fahamu kutoweza kwetu, ndipo tutajua kwamba kweli tunahitaji mwokozi.

6. Warumi 7:14-25, tunasoma kuhusu vita kati ya hali yetu ya dhambi ambayo inataka tuifuate na hali yetu ya kiroho ambayo inataka tumtukuze Mungu. Ni kutokana na ushawishi wa Mungu ndipo tunaweza kufanya yale ambayo ni mazuri. Vita hivi vitakuwepo katika maisha yetu yote. Kristo anavyoendelea kushawishi maisha yetu mara kwa mara, ndivyo tutaendelea kukua katika utakatifu na kuwa kama Kristo Yesu mwenyewe. Hii ndio sababu moja kwa nini tunapaswa kusoma Biblia zetu kila siku ili tusome kumhusu Mungu kila wakati.

A. Katika msiaha yetui yote, wakristo tutakuwa na vita dhidi ya dhambi kila wakati.

B. Tukamilishe haya: wale wote ambao tumeokoka hatuko chini ya sheria na kwa sababu hiyo, hatuhukumiwa chini ya sheria. Sheria ilikusidiwa kutuongoza kwa Kristo. Kazi yetu leo ni kuwaongiza wengi kwa kristo Yesu kupitia kwa ujumbe wa Injili. Hii inamaanisha kwamba lazima tuwafundishe watu kuhusu dhambi zao na jinsi wamepotea kwa dhambi zao ikiwa wanategemea matendo yao mazuri. Wao wanapaswa kufundishwa kwamba wao wamepotea kabisa ikiwa hamwamini Kristo.

7. Warumi 8:18-39, tunasoma kuhusu mateso ambayo yamekusudiwa kila mkristo ayapitie.

A. Katika mstari wa 18, tunasoma kuhusu ambayo tunafaa kuvumilia kwa sababu tunajua kwamba kuna utukufu mkuu ambayo umetusubiri. Kila mkristo lazima atarajie kuteseka kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Mateso haya ni ya muda mfupi sana na wala si ya milele. Kwetu leo mateso haya yanaonekana kuwa magumu sana na kuonekana kwamba ni ya milele, lakini Bibl;ia inatueleza kwamba mateso haya ya leo hayaweza kulinganishwa na utukufu ambao umetusubiri huko mbinguni.

i. Paulo aliteseka sana kwa ajili ya inji`li na kwa sababu `hii, yeye anauzoefu na ujunzi wa kutueleza kuhusu mateso kwa ajili ya ufalme wa Mungu (2 Wakorintho 11:23-28). Paulo ni mfano mkuu kwetu katika maisha. Yeye alikuwa kiongozi ambaye tunafaa kuiga kutoka kwake.

B. Katika mistari ya 19-27, tunasoma kuhusu vilio vitatu ambavyo vimeletwa na dhambi ya Adamu. Kama tu Adamu, dhambi zetu huwa zinaumiza wengine.

i. Katika mistaro ya 19-22, tunasoma kuhusu kilio cha kwanza ambacho ni kilio kutoka kwa kiumbe ambacho kinateseka wakati huu kwa sababu ya matokeo ya dhambi ya Adamu.

ii. Katika mistari ya 23-25, tunasoma kwamba hata sisi wanadamu tunalia na tunaseka kwa sababu ya dhambi ya Adamu.

iii. Katika mistari ya 26-27, tunasoma kwamba pia Roho Analia kwa ajili yetu. Yeye anatuombea na kuleta maombi yetu mbele za Mungu. Roho Mtakatifu ndiye msaidizi wetu.

C. Katika mistari ya 28-39, tunapewa sababu ya kufurahia kila siku katika maisha yetu ya wokovu.

i. Warumi 8:28 tunapaswa kuukariri mstari huu. Hii inamaanisha kwamba tunaweza kumwamini Mungu na tupate faraja katika maisha yetu. Katika kila majaribu na mateso ikiwa umeokoka, Mungu anatumia majaribu na shida hizo kwa ajili ya uzuri wako. Hatuwezi kabisa kufahamu kwa nini tunateseka na kwa nini mambo mengi yapo jinsi yalipo. Isaya 55:8, tunasoma kwamba Mungu hawazi jinsi tunavyowaza na njia zake si njia zetu. Katika Mwanzo 50:20, tunasoma kwamba Mungu anatumia kila hali katika maisha yetu kwa ajili uzuri wetu na utukufu wa Mungu.

ii.Katika mistari ya 29-30, tunasoma kwamba tunapaswa kufurahia kwa sababu Mungu atatulinda na kutuleta katika utukufu wa milele. Hatakosea katika hili.
iii. Katika mstari wa 31, tunasoma kwamba Mungu yupo upande wetu na kwa sababu hii, maadui wetu hawatushinda kamwe. Ni jambo la faraja sana kwamba Mungu mwenye nguvu zote yupo upande wetu.

iv. Mstari wa 32, tunasoma kwamba Mungu alimtoa mwanawe wa pekee kwa ajili yetu. Yeye pia atatupatia kila kitu ambacho tunahitaji kama neema, himizo n ahata mbinguni.

v. Katika mistari ya 33-34, tunasoma kwamba hatutahukumiwa kwa sababu Kristo amekufa kwa ajili na kwamba sisi pia tumemwamini.

vi. Katika mistari ya 35-39, tunasoma kwamba furaha yetu inatokana na upendo mkuu wa Mungu kwetu. Upendo huu ni mkubwa sana kiwangi kwamba hakuna lolote ambalo linaweza kututenganisha na upendo huu. Katika mstari wa 37, Biblia inasema kwamba sisi ni washindi na zaidi ya washindi katika Kristo. Tunapaswa kuishi kwa ujasiri huu.

8. Warumi 8 ni mojawapo wa sura zenye kutuhimiza sana katika Biblia. Katika Warumi 9, Paulo anatueleza mfano wenye huzuni mkubwa sana. Huzuni ni kwa sababu wa wale ambao wanaangamia katika dhambi zao. Paulo anazungumza kuwahusu Wayahudi. Leo mfano huu ni wale ambao ni majirani wetu na watu wa jamii zetu.

A. Warumi 9:1-5, tunasoma kwamba Paulo aliwapenda sana Wayahudi wenzake kiwangi kwamba alikuwa tayari kupeana na nafasi yake kwao ya mbinguni kama kweli hili lingewasaidie. Je, sisi tunawapenda sana wale ambao ni wa jamii zetu na majarini zetu kiwango kwamba tnajitolea kabisa katika kuwahubiria injili ya Kristo?

B. Mistari ya 10-18, tunasoma kwamba Mungu anatawala kila kitu. Tunasoma kwamba hata kabla ya Esau na yakobo kuzaliwa, Mungu alimpenda Yakobo na alimchukia Esau. Katika mstari wa 15, tunasoma kwamba Mungu atamhurumia yule ambaye anataka kumhurumia. Katika mstari wa 18, Mungu ataufanya moyo kuwa mgumu wa yule ambaye anataka moyo uwe mgumu.

C. Paulo anaeleza kwa nini Mungu aliwaokoa watu mataifa na kuwaacha Wayahudi wakiwa hawajaokoka. Katika mistari ya 30-33, tunasoma kwamba Wayahudi walikuwa wamekusudia kujiokoa wenyewe kwa matendo yao wenyewe kama kutii sheria. Wao walikataa kukubali njia ya Mungu ya pekee ya wokovu ambayo ni imani ndani ya Kristo. Wayahudi walikuwa na mioyo migumu kama tu vile Isaya 30:1 inavyosema. Watu wengi wako na kiburi na wanataka njia yao wenyewe ya wokovu na wala si ya Mungu.

9. Warumi 10 ni sura ambayo inafundisha kuhusu kazi ya kueneza injili.

A. Paulo anaanza kwa kuonyesha tamaa yake ya kuwaona Wayahudi wenzake wakiwa wameokoka. Anasema kwamba anaona jinsi Wayahudi walivyokuwa na tamaa ya kumpendeza Mungu, lakini hata hivyo walikuwa wamejitolea kufanya mambo kwa njia ambayo wao walipenda badala ya kufuata njia ambayo Mungu ameweka. Katika mstari wa 4, njia hiyo ni Kristo.

B. Mistari ya 9-10, tunasoma kuhusu njinsi mtu anavyookolewa. Hili ni jambo la waza kabisa na kila mtu anaweza kulielewa vyema. Tunaokolewa kwa imani ndani ya na pia tunauajibi kuwaeleza wengine kuhusu Yesu Kristo.

i. Mfano wa kueneza injili ni kuwaambia watu kuhusu Kristo Yesu.

ii. Mfano mwingine ni kueneza ujumbe wa injili kwa watu wote.

C. Katika mstari wa 11, tunaona kwamba Mungu ni Mungu wa Wayahudi na pia ni Mungu wa watu mataifa. Machoni pa Mungu hakuna tofauti kati ya watu hawa. Watoto wote wa Mungu wamebarikiwa sawa.

D. Ni lazima wale ambao hawajaokoka waelezwe kumhusu Kristo. Ni huzuni kwamba wakristo wengi hawaonyesha nia ya kuwa na tamaa ya kueneza injili ya Kristo. Ujumbe wa mistari ya 14-21, ni kwamba kueneza injili ni kazi ambayo inahitajika kufanywa ili wale ambao hawajaokoka wapate kuhubiriwa. Hii kazi ya kila mkristo.

A. katika mistari hii 14, tunasoma jinsi mtu anayoamini katika yule ambaye hajawahi kumsikia, mstari wa 15, tunasoma kwamba mtu anawezaje kuwaeleza wengine ikiwa hajatumwa kuwaeleza?

i. Hii inamaanisha kwamba kuna watu ambao wameitwa kufanya kazi ya kueneza injili katika sehemu mbalimbali za ulimwenguni.

ii. Kuna wale ambao wameitwa kuhubiri mahali ambapo walipo. Kila mkristo anapaswa kujiusisha na kazi ya kueneza injili. Tunaweza kuenda sisi wenyewe au kuomba au kuwatuma wengine.

iii. Kuna baraka kwa wale wote ambao wanatangaza ujumbe wa injili (Isaya 52:7). Mtu ambaye anasaidia katika kuwatuma wengine kuhubiri Kristo amebarikiwa kama tu yule ambaye anaenda kuhubiri.

B. Katika mstari wa 16, tunasoma kwamba si kila mtu ambaye anasikia ujumbe wa injili ataokoka. Ni kazi yetu ambao tumeokoka kuhubiri Kristo na kazi ya Mungu kuwashawishi wote na kuwaokoa.

C. Katika mstari wa 17, tunasoma kwamba neno la Mungu ndio chombo ambacho kinaleta imani ya kuokoka. Ni kupitia kwa Biblia tunapata kusoma kumhusu Mungu.

10. Warumi 11 tunasoma kuwahusu Wayahudi.

A. Katika mistari ya 1-2, Paulo anauliza swali kama Mungu amewachagua watu mataifa na kuwakatalia mbali Wayahudi. Paulo anajibu kwa kusema kwamba hilo si kweli kwa sababu yeye mwenyewe ambaye ni Myahudi ameokolewa na Mungu. Kwa hivyo kuna wale Wayahudi ambao wameokoka.

B. Mistari ya 25-32, Paulo anaendelea kuzungumza kuhus hali ya Wayahudi sasa na ktika maisha ya mbeleni.

i. Mstari wa 25, Paulo anasema kwamba kuna ugumu wa moyo mingoni mwa Wayahudi. Hii inamaanisha kwamba kuna wale wayahudi ambao wataokoka na wengi wao bado wanakata ujumbe wa Injili.

ii. Mstari wa 26, kuna mabishano mengi kuhusu mstari huu. Kuna mawazo ya aina mbili ambayo yanaegemewa na wengi.

a. Kuna wengi ambao wanasema kwamba ndipo mtu yeyote aweze kuokoka, lazima aokolewe kupitia kwa Myahudi ambaye ni Kristo.

b. Wengine wanasema kwamba mstari huu unahusu maisha ya mbeleni ambapo kutakuwa na kuokolewa kundi kubwa la Wayahudi kabla ya kurudi kwa Yesu Kristo. Hii haijulikani kabisa.

C. Mistari ya 33-36, tunasoma kuhusu furaha ya Paulo kwa sababu ya mpango mkuu wa Mungu wa wokovu.

IV. Warumi 12-16, sura hizi zinahusu jinsi ya kuishi maisha yetu kulingana na mafundisho ya sura za 1-11. Je, tunapaswa kuishi maisha yetu ya kila siku kwa njia gani bado ya kuokolewa na Mungu.

1. Jambo la kwanza tunalisoma katika Warumi 12:1, ni kwamba lazima tujitoe kabisa katika kumtumikia Mungu. Kutumikia Mungu linapaswa kuwa jambo la kwanza katika maisha yetu. Wale ambao tumeokoka tunapaswa kuwa tofauti kabisa na wale ambao hawajaokoka.

A. Sisi ambao tumeokoka tunapaswa kujitoa kabisa kwa Mungu. Tunapaswa kumwabudu na kumtumikia kwa nguvu zetu zote. Mungu anapendezwa sana wakati tunajitoe kabisa kwake na wala si wakati tunapeana vitu kama pesa. Chochote tunakitoa kwa Mungu kinapaswa kuwa msingi wake ni upendo kwa Mungu na wala si kwa sababu tunataka baraka zake. Tunapaswa kujua kwamba sisi ni watu wa Mungu na kwa hivyo maisha yetu yanapaswa kuwa maisha ambayo yanamwiga Kristo. Tunapswa kuomaba kila wakati kwamba tutakuwa kama Kristo mwenyewe. Tunapaswa kujitoa kabisa kwa Kristo.

2. Warumi 12:3-8, tunasoma kuhusu umoja katika kanisa. Wakristo wote ni mwili mmoja na kwa sababu hii tunapaswa kufanya kazi pamoja tukitumia vipawa vyetu kwa utukufu wa Mungu na uzuri wa kila mmoja wetu. Sisi sote tunapswa kujitolea katika kazi ya Mungu.
A. Mstari wa 3, tunapswa kujichunguza kuona ni karama gani ambazo Mungu ametupatia. Usiwaze tu kwamba una karama fulani, kuwa na uhakika kuhusu karama hizo. Je, wewe unajua karama ambazo Mungu amekupatia?

B. Warumi Verses 12:4-5, tunasoma kwamba kanisa la Kristo ni mwili mmoja na kwamba kanisa linafanya kazi pamoja wakati kila mshirika anajitoa kuchangia katika kazi ya kanisa. Mwili wa mtu unafanya kazi pamoja vyema wakati kila kiungo kinajihusischa katika kuufanya mwili uendelee kuwepo.

C.Warumi 12: 6-7, tunasoma kwamba lazima tutumie karama hizi vyema kwa ajili ya manufaa ya kila mmoja wetu.

3. Warumi 12:9-21, tunasoma kuhusu tabia ya mkristo.

A. Mistari ya 9-10, tunasoma kwamba tunapswa kuwa upendo wa kweli kwa kila mmoja wetu. Tunapaswa kuwaza sana juu yaw engine kuliko jinsi tunavyojiwazia wenyewe (1 Yohana 4:11-12).

B. Mstari wa 11, tunasoma kwamba hatupaswi kuwa watu ambao tunakaa tu na hatufanyi lolote kwa sababu tuna maisha moja ambayo tunapaswa kuishi kwa ajili ya Mungu.

C. Mstari wa 12, tunapaswa kila wakati kuwa katika ushirika na Mungu, kusoma Biblia na kuomba kila wakati.

D. mstari wa 13, tunapaswa kujitoa kuwasaidia wakristo wenzetu ambao wako na mahitaji.

E. Mstari wa 14, tunasoma jinsi tunapswa kufanya wakati tunayapitai mateso ambayo wakristo wote tunapaswa kuvumilia. Tufundishwa kwamba tunapaswa kuwaombea wale wote ambao wanatutesa. Jambo hili ni kinyume ya maisha yetu ambayo tuyaishi kila wakati. Tabia yetu kila wakati ni kutaka kulipiza kisasi wale ambao wanatutesa. Lakini Biblia inasema kwamba tuwabariki (Mathayo 5:44 na Luka 6:28).

F. Mstari wa 15, tunapswa kuwapenda wengine kwa dhati. Tunapaswa kufurahi na wengine wakati wanafurahia na kuomboleza wakati wanaomboleza (Waebrania 13:3).

G. Mstari wa 16, tunahimizwa kwamba tuishi katika Amani na wengine . hatufai kumdharau mtu yeyote haijalishi maisha yake ni ya aina gani. Haijalishi unajiwazi nini kama mchungaji, unastahili kumheshimu kila mtu. Wakristo wote ni sawa machoni pa Mungu (Mithali 3:7).

H. Mistari ya 17-19, tunahimizwa kwamba tunapswa kuishi kwa Amani na wengine. Tunaambia tuwasamehe wale ambao wanatudhurumu na kutuhumiza. Hatupaswi kulipiza kisasi kwa sababu Mungu ndiye hulipiza kisasi.

I. Mistari ya 20-21, tunapewa ushauri. Tunaambiwa kwamba tunapaswa kuwapenda maadui wetu. Biblia inasema kwamb tusiwalipishe mabaya kwa mabaya.

4. Warumi 13, tunafundishwa kwamba tunapswa kuwa watu wenye kutii sheria ya nchi. Tunapaswa kutii zile sheria zote ambazo hazivunji sheria ya Mungu. Haifai kiongozi yeyote kuwa mtu ambaye anawatesa wakristo kwa sababu wakristo ni watu ambao ni watiifu kwa sheria ya nchi.

A. Kila serilaki inapata mamlaka yake kutoka kwa Mungu na kwa hivyo kukosa kutii mamlaka ya nchi ni kama kukosa kumtii Mungu.

B. Kuna wakati ambapo hatufai kutii sheria za nchi. Huu ni wakati ambapo serikali inatuagiza kufanya kinyume na neno la Mungu (matendo 4:19; 5:29). Kwa mfano:
i. Warumi waliwaagiza watu wote kumwabudu kiongozi kana kwamba yeye alikuwa Mungu. Wakristo wote walikataa kutii amri hii.

ii. Katika nchi zingine kanisa linaagizwa kwamba liwaajiri watu ambao wanafanya usenge kufanya kazi na watoto wao.

iii. Kuna wakati serikali inamwagiza mchungaji kuhubiri kwa njia ambayo ni kinyume na Biblia.

C. Mistari ya 3-4, tunasoma kwamba Mungu ameweka serikali kwa uzuri wetu na kwa hivyo ni vyema serikali kutuahibu wakati tumefanya makossa hata kama adhabu ni kifo. Tunapaswa kutii serikali.

iv. Kunapokosekana serikali, kunakuwa na hali mbaya sana. Kwa mfano nchi ya Somalia nan chi zingine ambazo serikali hakuna au kuwepo mapinduzi ya mara kwa mara. Katika nchi hizi, watu wengin wanakosa chakula. Kila siku watoto wanakufa. Tunapaswa kuomwomba Mungu kwamba wale ambao wameokoka wachukue hatamu za uongozi katika nchi zetu.

D. Warumi 13:5-7, tunapewa mfano wa kutii sheria za nchi. Mojawapo ni kulipa kodi ya nchi.

i. ikiwa Biblia inatuagiza kutii sheria na kulipa kodi ya nchi, je, ni kwa nini serikali nyingi zinachukia Biblia na wale ambao wameokoka?

F. Mistari ya 8-9, tunafundishwa kwamba tunapaswa kuwapenda watu wote.

G. mstari wa 10, tunafundishwa uoendo nini na kwamba upendo ni jambo ambalo linamfurahisha Mungu sana.

H. katika mistari ya 11-14, tunaambiwa tuishi maisha matakatifu kwa sababu Yesu anakuja karibuni. Tunapaswa kuishi matakatifu kwa sababu hizi ni siku za mwisho.

5. Warumi 14, surah ii inahusu kuishi kwa pamoja katika umoja. Pia inahusu umoja katika kanisa. Wakristo wako na mawazo tofauti jinsi wanapaswa kuishi katika sehemu tofauti za maisha ambazo Biblia haijaweka wazi kabisa. Yule ambaye ameokoka zamani anawaza kwamba ni vyema kufanya lolote ambalo halijakatazwa katika Biblia. Kwa mfano anawaza kwamba ni vyema kunywa pombe bora asilewe au ni vyema mwanamke kuja kanisa akiwa katika longi au ni vyema kuenda kutazama mchezo na mambo kama hayo. Kswa yule ambaye ameokoka juzijuzi anasema kwamba mambo haya yote hayafai. Katika sura ya 14, katika kanisa la kwanza kulikuwa na kutokubaliana kuhusu ulaji wa vyakula fulani. Fundisho hapa ni kwamba hatufai kupingana juu ya mambo ambayo hayamo katika Biblia. Biblia imetupatia ruhusa katika mambo fulani fulani.

A. Mistari ya1-6, tunapaswa kufanya lolote kuwa na aman na kila mtu. Kwa mambo ambayo si muhimu tunapaswa kuwa watu wenye misimamo ambayo haiwadhurumu wengine. Lengo letu sote linapaswa kuwa kuishi na kila mtu kwa Amani ambyo msingi wake ni ukweli wa neno la Mungu.

i. Katika mstari wa 1, tunafundishwa kwamba tunapaswa kuwaheshimu hata wale ambao maoni yao ni tofauti nasi.

ii. Mistari ya 2-3, tunapaswa kumheshimu ndugu ambaye ni mchanga katika imani na wala hatufai kumdharau. Yale ambayo hayamo katika Biblia, tunapaswa kuwa tayari kuyaachilia kwa ajili ya kuwepo kwa umoja na upendo. Mfano mzuri ni ATA masoma ambayo yanafundishwa na kila mtu kutoka katika kila dhehebu.

iii. Mistari ya 3-4, Biblia inasema kwamba usmhukumu ndugu ambaye ni mchanga katika imani. (Mathayo 7:1).

iv. Mstari wa 5, tunapaswa kuhakiksha kwamba lolote ambalo tunalifanya ni zuri.

v. Mstari wa 6, tunapaswa kufanya kila kitu kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

B. Mistari ya 7-9, tunapswa kukumbuka katika kila jambo kwamba lengo letu ni kumletea Mungu utukufu. Tunapaswa kuwa na nia mzuri katika kila jambo.

C. Mistari ya 10-12, hatupaswi kuwa hakimu wa wengine. Mungu ndiye hakimu wa pekee. Tunapaswa kujishughulisha na maisha yetu na jinsi tunavyoishi kwa sababu siku moja tutatoa hesabu mebele za Mungu jinsi tulivyoishi maisha yetu hapa ulimwenguni.

F. Sehemu ambayo imebaki ya sura inashughulika na jinsi tunapswa kuwa na uhusiano mwema na wengine. Hatupaswi kkuwa kikwaso kwa wengine. Yaani hatupaswi kuwaongoza wengine katika dhambi kwa sababu ya matendo yetu. Mfano wa hili ni kama kucheza mziki wa sauti ambao jiarani wako hapendi na kwa sababu hii utasababisha jirana wako akasirike. Usifanye lolote ambalo litamfanya mwingine anguke katika dhambi.

6. Warumi 15, sura inaendelea wazo hilo ambalo tumelipata katika sura ya 14. Warumi 14:1-13, inazungumza kuhusu undugu wa kweli. Katika mistari ya 1-6, pauloa anaanza kwa kuzungumza na ndugu ambaye amekua katika imani na yule ambaye bado ni mchanga katika imani.

A. Mambo matatu ambayo yanapaswa kuzingatiwa.

i. Yule ambaye amekua katika imani anapaswa kumsadia sana yule ambaye aliokoka juzijuzi.

ii. Mstari wa 1, hatupaswi kuishi maisha yetu tukijifurahisha, bali tunapaswa kumfurahisha Mungu. Pia tunapaswa kuwafurahisha ndugu wetu katika Kristo.

iii. Mstari wa 2, tuwasaide wengine kwa kuwajenga katika maisha yao.

B. Sasabu ya kufanya mambo haya matatu ni kumfuata Kristo.

C. Matokeo ya maisha ya mkristo ambaye anaishi maisha haya.

i. Mstari wa 2, tunasoma kwamba jambo hili litawajenga ndugu zetu.

ii. Mstari wa 6, tunasoma kwamba jambo hili litaleta umoja katika kanisa.

iii.Mstari wa 6, tunaosma kwamba jambo hili litaleta utukufu kwa Mungu. Kusudi kubwa la maisha yetu ni kumletea Mungu utukufu na kufurahia Mungu katika kila jambo milele.

D. Katika kistari ya 7-13, Paulo alikuwa nazungumza na Wayahudi na watu Mataifa. Anasema kwamba ni kusudi la Mungu kwamba waokoke. Ili wote pamoja waweze kumsifu Mungu (Zaburi 117:1).

E. Sasa Paulo alianza kuandika mamabo ambayo yanahusu mtu binafsi. Anazumgumza kuhusu kazi ambayo Mungu alimpa aifanye. Yeye amepeleka ujumbe wa injili kwa watu mataifa na pia amefika mahali ambapo injili haikuwa imefika. Pia anazungumza juu ya mpango wake kuenda Roma. Katika kitabu cha matendo tunasoma kwamba Paulo alifika Roma lakini si kwa njia ambayo alitaka afike huko.

8. Warumi 16:1-16. Paulo alizungumza kuwahusu watu tofauti tofauti.

A. Paulo anatuonya kwamba kuna watu ambao watajaribu sana kuleta migawanyiko katika kanisa na hatufai kuwakubali wafanye hivyo. Katika kistari ya 17-18, anasema kwamba watu ambao wanaleta migawanyiko katika kanisa hawamtumikii Mungu, bali wanajitumikia wenyewe (3 Yohana 1:9).

B. Katika mstari wa 16, kuna fundisho ya jinsi tunapaswa kuelewa na kufundisha Biblia. Paulo hasemi kwamba tunapaswa kubusiana. Kile anasema kwamba tunapaswa kusalimia kwa njia ya urafiki wa kweli kulingana na makubaliano ya mahali ambapo tunaishi.

B. Maneno ya Paulo ya mwisho ya kitabu hiki, sifa kwa Mungu.

Kitabu cha 1 Wakorintho

Paulo aliandika kitabu hiki akiwa katika mji wa Efeso, mji ambao ulikuwa katika nchi ya Utururki ya sasa. Aliandikia kanisa hili ambalo lilikuwa katika nchi ya Ugiriki katika mji wa Korintho. Mji ulikuwa mji tajiri sana. Barua hii iliandika ili Paulo asahihishi makossa mengi ambayo yalikuwa katika kanisa hili la Korntho. Kusudi lake la Kuandika lilikuwa kusaidia kanisa liwe katika umoja.

1 Wokoritho 1:1-6, anajibu maneno ambayo yalimfikia kuhusu hali ya kanisa hili.

1. Paulo anasema katika mstari wa 2, kwamba anaandika barua hii kwa kanisa. Hii inaonekana wazi katika salamu zake kwa kanisa na himizo lake. Anafanya hivi wajue kwamba hata kama alikuwa anawasahihisha, bado alikuwa anawapendo na zaidi Mungu pia alikuwa anawapenda. Fundisho hapa ni kwamba hata wakati unawaadhibu wakristo fulani katika kanisa, unapaswa

kufanya hili kwa upendo na kwa sababu unawajali sana. Nidhamu katika kanisa inafanywa kwa sabau ya kutaka kurejesha ndugu au dada katika ushirika ambaye ameanguka katika dhambi.

2. Tatizo la kwanza ambalo Paulo analizungumzia katika 1 Wakorintho 1:10-17 ni migawanyiko katika kanisa. Katika kuandika kwake, Paulo hakumtaji mtu yeyote kwa jina. Tatizo lilikuwa kwamba,kulikuwa na watu ambao walikuwa wamejifanya kuwa viongozi katika kanisa na walikuwa wanasababisha migawanyiko katika kanisa. Paulo alisema kwamba kanisa linapaswa kuwa kama Kristo kwa sababu Kristo hajagawanyika. Paulo hapa anashighulika na shida ambapo watu huwa wanajifanya kana kanisa ni lao wanasahau kwamba kanisa la Kristo. Katika kiburfi chao, huwa wanajifanya kuwa kichwa cha kanisa.

3. Mistari ya 18-25, tunajifundisha kwamba ujumbe wa injili ni upumbavu kwa ambao wanakataa klumwamini Kristo. Wale ambao hawajaokoka huwa wanawaza kwamba wale ambao tumeokoka, sisi ni wapumbavu.

A. Katika mstari wa 25, tunasoma kwamba Mungu ni mwerevu na mwenye nguvu zote kuliko mwanadamu yeyote.

4. Paulo anamalizia sura ya 1 akisema kwamba Mungu huwa anafurahia kutumia vile vyombo ambavyo ni vidhaifu kufanya kazi yake. Kumbuka hadithi ya Gideoni! Ikiwa tutajitahidi kwa nguvu zetu, ni wazi kwamba hatutafaulu na katika mstari wa 27, Biblia inasema kwamba tutaibishwa. Ufanisi wowote ambao nimepata kama mfanyakazi wa mkristo ni kwa sababu ya nguvu za Mungu.

A. Katika mstari wa 31, tunasoma kwamba tunapaswa kujivunia nguvu za Mungu kwa sababu Mungu ndiye chanzo cha nguvu zetu. Sisi wanadamu hatuna nguvu za kufanya kazi ya Mungu na kufanikiwa kivyetu. Mungu anafurahia kutumia sisi ambao ni vyombo vidhaifu ili ajidhihirishe kwamba Yeye ndiye anayefanya mambo makuu ndani mwetu na kwamba utukufu wote unastahili Yeye. Tazama hadithi ya Gideoni katika Waamuzi 6-8.

5. Paulo anaendelea katika 1 Wakorintho 2:1-5, kuonyesha kwamba nguvu za ujumbe wa injili ambao alikuwa anahubiri hazikutokana naye kama mwanadamu bali zilikuwa nguvu za Mungu (mstari wa 5).

A. katika mstari wa 2, Paulo anafundisha kwamba Kristo ambaye aliyesulibiwa. Wakati mwingine wahubiri wazuri katika Biblia walikuwa watu ambao walikuwa maskini. Jonathan Edwards inasemekana kuwa mhubiri mzuri lakini wengi waliomsikia walisema kwamba alikuwa anahubiri kwa njia ambayo hakupendwa na wengi. Mhubiri huyu alihubiri mahubiri ambayo

yanaitwa wenye dhambi katika mikono ya Mungu ambaye amekasirika, mahubiri ambayo yanadhani kuwa yenye nguvu. Mahubiri haya aliyahubiri wakati alipokuwa mgonjwa. Wengi walimwamini Kristo kutokana na mahubiri haya. Baqada ya miaka 200 baadaye, mahubiri haya bado wengi ambao wanayasikia wanafaidika sana. Nguvu katika mahubri haya, ni nguvu za Mungu.

6. Sehemu nyingine katika kistari ya 6-14, tunasoma kwamba kumfahamu Mungu ni lazima tumwezeshwe na Mungu. Ufahamu wa kiroho umeondolewa kwa wale ambao hawajaokoka na kufahamishwa kwa wale ambao wameokoka kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu anatufunulia mafundisho ya Biblia kwetu wakati tunapokuwa tunasoma Biblia.

A. Mistari ya 11-12, tunasoma kwamba ni wale ambao wameokoka ambao wanaweza kufahamu Biblia vyema. Hii ni kwa sababu Roho Mtakatifu ndiye anayetusaidia kuelewa Biblia na ni wale tu ambao wameokoka wako na Roho Matakatifu ndani mwao.

7. 1 Wakorintho 2: 14-3:3, Pualo na anazungumza kuhusu aina tatu ya watu.

A. Kuna yule mtu wa kawaida ambaye hajaokoka (mstari 14).

B. Kuna yule ambaye ameokoka (mistari ya 15-16) ambaye anajua na kufahamu neno la Mungu na yeye amekua kiroho na anafahamu mapenzi ya kristo katika maisha yake.

C. Kuna yule ambaye ameokoka lakini hajakua kiroho (mistari ya 1-3). Huyu ni mtu ambaye ameokoka lakini hakukwi mwangalifu katikam kuongozwa na Roho Mtakatifu. YeyeTanajua machache sana kumhusu Mungu kwa sababu hajitolei katika kusoma Biblia na kufundisha kile ambacho Biblia inasema. Huyu ni mtu ambaye mara kwa mara huwa anasababihs matatizo mengi kanisa kwa saabu tabia yake huwa mara kwa mara inakuwa kama ya yule ambaye hajaokoka. Mtu kama huyu hawezi kamwe kuwa mchungaji kwa sababu hajui mengi kumhusu Mungu. Wale ambao pia hawajipi kwa neno la Mungu wao humfusta mtu kama huyu. Kanisa zuri sana ni lile ambalo mchungaji wake na watu wanajipa kwa kusoma neno la Mungu kwa makini.

8. Paulo anamalizia sehemu hii ya migawanyiko katika kanisa kwa kuwahimiza wakristo kwamba wanapaswa kufanya kazi kwa pamoja.

9. Paulo sasa anendelea kuzungumza kuhusu dhambi ya zina ambayo alikuwa ameelezwa kwamba ilikuwepo kanisani. Hii ni dhambi mabay sana n ahata leo ni dhambi ambayo imeleta matatizo makubwa sana katika kanisa. Katika mstari wa 13, Paulo anasema kwamba

tumwondoe katika ushirika ndugu ambaye anakataa kutubu dhambi ya zina. Yaani anapaswa kukubaliwa kuendelea kushirika kanisani lakini hawezi akahusika katika majukumu ya kanisa yoyote.

10. 1 Wakorintho 6:1-8, tunaosma kwamba wakristo hatufai kupelekana kotini. Tunapaswa kutatua mizozo yetu ndani ya kanisa. Katika mstari wa 7 anasema kwamba tunapaswa kuwa tayari kupoteza lolote badala ya kupelekana kotini.

A. Tunasoma kwamba sisi ambao tumeokoka tutahukumu ulimwenguni na malaika kwa sababu hii tunapaswa kutatua mizozo yetu badala ya kuenda katika mahakama ya wale ambao hawajaokoka.

11. Katika mistari ya 9-20, Paulo anakemea dhambi ya zina.

A. katika mstari wa 15, tunasoma kwamba miili yetu ni miili ya Kristo na kwa hivyo hatufai kuiusisha katika ukahaba. Tunapojihusisha katika ukahaba, tunakuwa miwli mmoja na kahaba. Hii ni dhambi ya ndani ya mwili. Dhambi ya zina ni dhidi ya mwilli.

B. Katika mistari ya 19-20, tunafundishwa kwamba ni lazima tuitunze miili yetu vyema kwa sababu miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu ambaye anaishi mwetu ambao tumeokoka. Tunafundishwa kwamba sisi ni mali yetu bali sisi ni mali ya Mungu kwa sababu Mungu ametununua kwa gharama kubwa sana. Gharama hiyo ni damu ya Yesu kristo. Ikiwa kweli tunafahamu jambo hili, basi tutabadili jinsi tunayoishi maisha yetu. Badala ya kuishi kwa ajili yetu wenyewe, tunaishi kwa utukufu wa Mungu.

1 Wakorintho 7-16, tunasoma kuhusu matatizo ambayo kanisa lilimwuliza Paulo awasaidie kuyatatua.

1. 1 Wakorintho 7:1-16, tunasoma kuhusu ndoa na mambo yan kukutana kimwili katika ndoa.

A. Wale ambao hawajaokoka huwaza kwamba hakuna shida wakati watu wawili ambao wamekua wanapokutana kimwili. Lakini Biblia inasema kwamba kukutana kimwili ni jambo la mke na mume katika ndoa. Leo kuna wengi ambao hawaamini katika ndoa.

B. Kukutana kimwili ni jambo ambalo halikubaliki nje ya ndoa. Paulo anasema kwamba watu wako na hisia za kukutana kimwili na hili si jambo baya kwa saabu ni Mungu ambaye anatupatia hisia hizi. Katika mstari wa 2, Bibia inasema kwamba ni vyema kuoa ili kutosheleza hisia hizi za kukutano kimwili. Paulo anaendelea kusema kwamba mke na mume wote wako na jukumu la

kuhakikisha kwamba wanatoshelezana kimwili. Mke na mume wanapaswa kuheshimiana. Dini ya ukristo inawaheshimu wanawake sana.

C. Katika mistari ya 8-9, tunasoma kwamba ni vyema mtu kuoa ikiwa hisia zake Mungu amempa uwezo wa kuzizibiti. Lakini ikiwa hawezi basi Biblia inafundisha kwamba ni vyema mtu huyu kuoa. Katika kanisa la kikatoliki, ni sheria kwamba wale ambao wanahudumu kama makasisi, hawafai kuoa. Kwa sababu hii kuna dhambi nyingi sana miongoni mwa hawa makasisi za zina. Mungu anawakubali wachungaji kuoa na si sheria kwamba hawafai kuoa.

D. Paulo anaendelea kupeana maagizo kuhusu ndoa haswa katika kwa yule ambaye amaeokoka na yule ambaye hajaokoka. Ikiwa mtu ameokoka na yule mwenzake hajaokoka, wanapaswa kuendelea katika ndoa yao. Yule ambaye ameokoka anapaswa kuishi matakatifu ambayo yanadhihirisha Kristo. Kwa njia hii huenda Mungu anatumia mwenendeo wake kumwokoa yule ambaye hajaokoka. Kuna wachuinagaji na wakristo fulani ambao hawaelewi jambo hili. Wao wanawaza kwamba ikiwa mtu ameokoka, basi anaweza kumwwacha yule ambaye hajaokoka. Biblia inasema kwamba hafai hivyo.

2. 1 Wakorintho 8, kuna fundisho hapa ambalo wengi tunaweza kupuuza kwa sababu tunawaza kwamba katika jamii zetu hakuna nyama ambayo imetolewa kama sadaka. Katika mstari wa 13, kuna funzo kwetu. Hatufai kuwa kikwazo kwa ndugu ambaye hajakua katika imani. Katika sura ya 9, Paulo anasema kwamba tunapaswa kuwa watu ambao tuko tayari kujitoa na kuacha mambo fulani kwa sababu ya ndugu ambaye ni mdhaifu katika imani.

A. Mfano huu ni kama, hatufai kunywa pombe hata kwa kipimo mbele ya ndugu ambaye ni ameokoka juzijuzi ambaye anaweza kujaribiwa kuwa mlevi.

B. Mfano mwingine katika 9:20, tunapaswa kuacha mambo ambayo yanaweza kuonekana ni ya kudharau wengine au ni kikwaso kwa wengine ikiwa tunataka kuwaleta kwa Kristo. Hadithi ifuatayo ili elezwa na mtu ambaye alikuwa katika dini ya kiindi na baadaye alifanyika mkristo. Akiwa katika dini ya kiindi aliamini kwamba kula nyama ni jambo baya lakini alipokuwa mkristo alifahamu kwamba kula nyama ni sawa. Lakini hata hivyo hakuwahi kula nyama kwa sababu ya heshima kwa jamii yake. Mara ya kwanza babake alimkataa kwa sababu ya kuwa mkristo. Lakini baadaye babake aliokoka kwa sababu ya heshima ambayo kijana wake alimwonyesha.

3. 1 Wakorintho 10, ni onyo kwetu kwamba tunapaswa kutoroka dhjambi ya zina na uabudu sanamu. Mfano hapa ni kuacha kuabudu roho.

A. Mstari wa 13, tunasoma kwamba hatufai kumlaumu yeyote kwa sababu ya dhambi zetu. Tunapaswa kuajibika kwa sababu ya dhambi zetu. Kila mmoja wetu kwa wakati mmoja atajaribiwa; hata Yesu alijaribiwa. Si dhambi kujaribiwa. Tunasoma kwamba hatufai kusingizia shetani au mtu mwingine kwa sababu ya dhambi zetu. Kwa mfano hufai kumsisngizia mtu mwingine kwa sababu ya dhambi yako ya zina kwa sababu ni wewe mwenyewe ambaye anachagua kufanya dhambi hiyo. Ikiwa tutamtegemea Mungu wakati tunajaribiwa, Biblia inasmea kwamba mtu atatupatia njia ya kuepuka dhambi na kuishinda. Adamu alisingizia Hawa kwa sababu ya dhambi yake na Hawa naye alisingizia nyoka.

B. Katika mstari wa 14, tunashuriwa kwamba hatufai kunaswa na dhambi yoyote. Je, unajaribiwa na ulevi? Usiende mahali ambapo pombe inakunyiwa. Je, unajaribiwa na dhambi ya zina? Usiende mahali ambapo dhambi hiyo ipo au usimkaribie yule mwanamke ambaye unapata kwamba unajaribiwa naye.

4. 1 wakorintho 11, inazungumza kuhusu kuzingatia tamaduni. Katika Agano Jipya, tamaduni ilitaka wanawake wafunike vichwa vyao wakati wanakuwa kanisani. Wanaume wao waliambiwa kwamba hawakufa kufunika vichwa vyao.

A. 1 Wakorintho 11, tunasoma kuhusu meza ya Bwana. Tunapasoma tutaona kile ambacho meza hii hufanya na kile ambacho meza hii haifanyi.

B. Sadaka ni mfano au sahihi ya Agano let na Mungu. Sahihi inadhihirisha kwamba uhusiano wetu kama wakristo unakubalika mbele za Mungu. Sahihi inafanya uhusiano wetu utambulike.

C. Meza ya Bwana haijakusudiwa kutosheleza njaa ya kimwili. Pia meza hii haileti miujiza kama uponyaji ay kupata pesa.

D. Meza ya Bwana haipatiani nguvu au kupeana baraka fulani. Bali tunakula kwa ukumbusho wa Bwana Yesu Kristo. Ni wakati ambao tunaikumbuka sadaka ya Bwana Yesu Kristo kwa ajili ya dhambi zetu.

E. Tutazame maagizo kutoka kwa Biblia kuhusu meza ya Bwana:

i. Mistari ya 24, tunasoma kwamba mkate ni mfano wa mwili wa Kristo ambao uliwekwa msalabani. Mkate huwa haubadiliki kamwe.

ii. Mistari ya 25, kikombe ni mfano wa damu ya Kristo Yesu ambayo ilimwagika msalabani kalivari kwa ajili yetu. Kile kilicho katika kikombe huwa hakibadiliki na kuwa kitu kingine.

F. Mistari ya 27-28, tunaonywa kwamba tunapaswa kuwa waangalifu wakati tunachukua meza ya bwana. Meza ya Bwana haifai kuchukuliwa na wale ambao hawajaokoka na wale ambao hawaelewi maana yake. Kanisa lina uajibu kuakikisha kwamba wale ambao hawajaokoka na wale ambao hawaelewi maana yake, hawachukui meza hii. Tunaonywa kwamba tunapaswa kwanza kujichunguza vyema kabla ya kula meza ya Bwana. Kwa mfano ikiwa tuko katika dhambi ambayo tumekataa kutubu au tuko chini ya nidhamu, hatufai kula meza ya Bwana.

5. 1 Wakorintho 12, tunasoma kuhusu karama za rohoni. Paulo alitaja baadhi ya karama hizi. Zingine tunazipta katika Warumi 12:6-8 na Waefeso 4:11.

A. Katika mstari wa 7, tunasoma kwamba kila mkristo ana karama za rohoni kutoka kwa Mungu na kwamba tunapaswa kuzitumia kwa ajili ya uzuri wa kanisa lote. Paulo hasemi kwamba karama moja ni maana sana kuliko nyingine. Mti ambaye anafagia kanisa, ni wa muhimu sana kama tu mchungaji. Ni wakati kila mkristi anatumia karama zake katika kanisa ndipo kanisa litaweza kukua.

B. Ukosefu wa wengine kujitlea na kutumia karama zao katika kanisa inamfanya mchungaji asitekeleze majukumu yake vyema.

6. 1 Wakorintho 13, huwa inajulikana kama sura ya mapenzi kwa sababu ya ujumbe wa surah ii. Soma sura hiyo na kuzingatia mifano ambayo inapeanwa. Chochote tunamfanyia Mungu, ikiwa tutakifanya bila upendo, ni bure na hakikubaliki na Mungu.

A. Mistari ya 1-3, tunafundishwa kwamba upendo ndio jambo la muhimu katika maisha ya mkristo. Kazi zetu zinakubalika tu wakati tunazifanya kwa upendo.

C. Mstari wa 13, tunasoma kwamba upendo ni wa muhimu sana kuliko imani na tumaini. Je, kwa nini? Sasababu ni kwamba upendo ni wa milele lakini imani na tumaini vitaisha wakati tutaingia mbinguni.

7. 1 Wakorintho 14, tunafundisha kuhusu kutumia karama ambazo tumepewa kama unabii na lugha kwa njia ambayo inafaa. Lengo la karama hizi ni kujenga kanisa na wala si kuleta migawanyika kanisani.

A. Mstari wa 1, tunasoma kwamba unabii ni jambo la muhimu sana. Unabii hapa unamaanisha kufundisha au kuhubiri neno la Mungu. Kuwahubiria au kuwafundisha watu neno la Mungu ni jambo la muhimu sana.

B. Jambo lingine hapa linahusu lugha. Katika mistari ya 26-33, Mungu anasema kwamba mahali ambapo lugha ambayo haieleweki na wengine inapotumika lazima kuwe na mtu mwingine wa kutafsiri ili wengine wafahamu. Katika mistari ya 33 na 40, tunasoma kwamba Mungu ni Mungu wa mipangilio na wala si Mungu kuleta kuchanganyikiwa.

7. 1 Wokorintho 15, sura iliandikwa kusahihisha mafundisho ambayo yalikuwa yanafundishwa na hakuwa ya kweli. Katika mistari ya 1-4, tunafundishwa kwamba tunapaswa kuamini kwamba tutafufuliwa kutoka kwa wafu kama tu vile Kristo alivyofufuliwa.

A. 1 Wakorintho 15:5-11, jadili swali hili kwamba watu wengi walimwona Yesubaada ya kufufuka kwake. Kila mkristo lazima aamini kwamba Yesu alifufuka kutoka wafu. Hata sisi tutafufuka.

B. Katika mistari ya 12-20, tunasoma kwamba ikiwa hatutafufuliwa kutoka kwa wafu, basi hata Kristo hakufufuka. Hii inamaanisha kwamba tunapaswa kuhurumiwa kwa sababu hatuna tumaini lolote na kwa hivyo tunamaliza tu muda wetu wa bure katika kuamini Kristo. Mstari wa 20 unasisitiza kwamba kweli kristo alifufuka kutoka kwa wafu na kwa hivyo tunapaswa kuwa na furaha kwa kutumainia kufufuka kwetu wakati Kristo atakaporudi.

C. Mstari wa 29, hauleweki na wengi. Kuna kutokubaliana kwingi miongoni mwa wakristo kuhusu maana ya mstari huu.

D. Paulo anafundisha kuhusu aina ya mwili ambao tutakuwa nao wakati tutafufuliwa. Katika mstari wa 42 tunasoma kwamba mwili wetu mpya hautaweza kuangamia au kuumizwa. Mstari wa 43, mwili huo utakuwa na nguvu na mstari wa 44 utakuwa mwili wa kawaida lakini pia utakuwa mwili wa kiroho.

E. Mistari ya 50-58, tunasoma kwamba wakati Kristo atakaporudi, wakristo watafufuliwa kutoka katika makaburi yao, pamoja na wale ambao watakuwa bado wako hai watakutana na Yesu kwa mawingu. Lakini kwa wale ambao watakuwa hai, miili yao itabadilishwa na watapewa miili ya kiroho.

F. Mistari ya 55, tunasoma kuhusu isaya na Hosea ambao walifundisha kwamba kifo kitashindwa wakati . Kifo hakitakuwa na nguvu zozote.

G. 1 Wakorintho 15, inamalizikia kwa kutuhimiza sana kuhusu kuwa waaminifu katika kufanya kazi ya ufalme wa Mungu. Kazi ambayo tunayoifanya ya Ufalme si kazi bure.

2 Wakorintho

Paulo aliandika barua hii kuonyesha furaha yake kwa kanisa la Korintho ambalo lilikuwa limetubu. Pia anaeleza mamlaka yake kwamba yeye ni mtume.

2 Wakorintho 1-2:11, Paulo anatetea tabia yake. Ni jambo la kweli kwamba viongozi wa Kikristo kila wakati watapingwa. Ni moja wa ishara ya kuonyesha ufanisi wa huduma ambazo Mungu ametupatia wakati shetani anatuvamia akiwatumia watu tofauti tofauti.

1. 2 Wakorintho 1:1 Paulo anasema kwamba mamlaka yake yanatoka kwa Mungu.

2. Mistari ya 3-11, tunasoma kuhusu mateso ambayo Paulo aliyapitaia. Mstari wa 8, Paulo anasema kwamba mates ohayo yalikuwa makali sana kiwangio kwamba aliwaza angekufa. Katika mstari wa 10, anasema kwamba ni Mungu ambaye alimwokoa kutonakana na mateso hayao yote. Katika mstari wa 9, anasema kwamba mateso haya yalimfundisha kwamba kila wakati alihitaji kumtegemea Mungu na wala si kujitegemea yeye mwenyewe.

Kuna mafundisho mengi kuhusu mateso katika sura za 11-12.

1. Hapa tunaona kwamba Paulo aliteseka kwa ajili ya kufundisha injili. Soma 11:23-29. Tunapaswa kuwa tayari kuteseka kama Paulo kwa ajili ya injili.

2. Tunaona katika 12:7-10, Paulo pia aliteseka kwa sababu ya shida zingine. Paulo anasema kwamba mateso haya yalimsaidia ili asiwe mwenye kiburi bali awe mnyenyekevu.

A. Katika mistari ya 8-9, tunasoma kwamba Paulo alimwomba Mungu amwondolee shida hizi lakini Mungu hakuindoa. Mungu alimwambia Paulo kwamba alifaa kumtegemea Yeye pekee na wala hakufaa kujitegemea wakati anamtumikia Mungu. Hatuwezi kuwa na kisingizio kwamba hatuwezi kwa njia yoyote kumtumikia Mungu kwa sababu ikiwa tunamtegemea Mungu pekee, basi hakuna lolote ambalo Mungu hawezi kutuwezesha kumfanyia.

B. katika mstari wa 10, tunapaswa kuiga kutoka kwa Paulo. Tabia ya Paulo ni mzuri sana kwa kila mkristo kuiga.

3. Kutokana na mateso ya Paulo, tunajifunza kwamba mtu hawezi kujiponya wenyewe asipoponywa na Mungu mwenyewe. Mungu alimtumia Paulo kuwaponya wengine lakini hata hivyo Paulo hangeweza kujiponya.

2 Wakorintho 2:12 hadi sura ya 9, tunasoma kumhusu Paulo akitetea huduma wake.

1. 2 wakorintho 3:6-18, Paulo anazungumza kuhusu Agano Jipya. Sisi sote tumepofushwa na ni Kristo ambaye anaweza kuondoa upofu huu na kututleta kwa Mungu. Mistari ya 16-18, wakati huu tunaweza kuuona utukufu wa Mungu na kubadilishwa katika mfano wa Kristo mwenyewe. Hii inamaanisha kwamba sisi ambao tumeokoka, tunaanza kumfanana Kristo kwa sababu hili ndilo lengo la maisha yetu kuwa kama kristo zaidi na zaidi. Ishara moja katika maisha yetu kwamba sisi ni wakristo ni mabadiliko haya na kuanza kuona tunda la Roho ndani mwetu (Wagalatia 5:22-23).

2. 2 Wakorintho 4:2, Paulo anasema kwamba yeye atakuwa mwaminifu katika kufunza na kuhubiri neno la Mungu kama tu vile Mungu amelipeana. Tunapaswa kufanya hivi. Yaani hatupaswi kubadilisha ujumbe wa neno la Mungu ili tuwapendeza wale ambao wanatusikiliza. Lengo letu kuu linafaa kuwa kumpendeza Mungu.

3. 2 wakorintho 5:1-10, Paulo anazungumza jinsi yeye haogopi kufa. Katika mistari ya 6 na 8 anasema kwa nini? Kulingana na mstari wa 6, wakati tuko hai, hatuko na Mungu katika utukufu lakini mstari wa 8, unasema kwamba wakati tunakufa, tunaingia katika utukufu na tunaishi na Mungu milele. Mara tu mkristo anapokufa, yeye huingia mbinguni mara moja.

A. Mistari ya 9-10, tunasoma kwamba tunapaswa kufanya lolote ili kumpendeza Mungu kwa sababu ni yeye ambaye tunasimama mbele Zake na kutoa hesabu jinsi tulivyoishi maisha yetu hapa ulimwenguni. Wakristo hawataadhibu kwa sababu yay ale ambayo waliyafanya mabaya kwa sababu Kristo ameadhibiwa tayari kwa ajili yao na Mungu hawahesabii makossa yoyote mbele zake. Badala yake Mungu atawazawadia mazuri ambayo wameyafanya. Huko mbinugni wakristo wote watazawadiwa. Biblia inasema kwamba kuna zawadi tofauti tofauti huko mbinguni (marko 10:29-30 na Ufunuo 22:12).

4. 2 wakorintho 5:17, ni mstari ambao unatuhimiza sana. Yafuatayo ndio mafundisho ya msatari huu:

A. Kuwa kiumbe kipya inamaanisha kwamba ya kale yamepita. Dhambi zetu za awali zimesamehewa haijalishi tulikuwa watu wa aina gani kabla ya kuja kwa Kristo. Wakati tulikja kwa kristo tulisamehewa na kufanywa watu wapya. Waza juu ya Paulo kabla aokoke.

B. wazo lingine ni kwamba kwa sababu sisi ni viumbe vipya, basi tunapswa kuishi maisha yetu kama watu wapya. Maisha yetu yanapaswa kudhihirisha Kristo. Katika sura ya 3:16-18, tulisoma

kwamba tunafaa kuishi maisha yetu tukiwa kama Kristo mwenywe zaidi na zaidi. Kila mkristo anapaswa kuona mabadiliko katika maisha yake tunapoendelea kukua katika imani.

5. 2 wakorintho 6:14-18, kuna mafundisha muhimu sana kwetu.

A. Mstari wa 14, tunasoma kwamba hatufai kushiriki na wale ambao hawajaokoka. Katika ndo, biashara na kanisani.

i. Katika mataifa ya magharaibu, hali ya ndoa ni tofauti sana na katika mazingari ya Afrika. Wakristo wengi huko nchi ya magharibu wanaona n ahata wale ambao hawajaokoka. Jambo hili limeleta madhara mengi katika familia haswa katika hali ya kuwalea watoto.

ii. Mkristo hafai kuwa namushirika na yule ambaye hajaokoka kwa sababu maisha yetu ni tofauti kabisa nay a wale ambao hawajaokoka. Bwana wa Kristo ni Kristo na bwana wa yule ambaye ahajaokoka ni sheatani.

iii. Tunapaswa kulinda makanisa yetu isije ikahusika na wale ambao hawajaokoka. Hatufai kuwaacha wale ambao tunawajua kwamba hawajaokoka kuhubiri katika makanisa yetu au kuzungumza katika makanisa yetu. Tunapswa kuhakikisha kwamba Biblia pekee ndio inafundishwa katika makanisa yetu.

B. Tazama mstari wa 16, ambao unafundisha kwamba sisi ni hekalu la Roho Mtakatifu kwa sababu hii hatuwezi kuwa na ushirika na wale ambao hawajaokoka. Hii ni kama kumkubali yule ambaye hajaokoka kuleta miungu yake miongoni mwetu.

C. Mstari wa 17, hatufai kuwa na uhusiano wa karibu na wale ambao hawajaokoka. Katika mstari wa 18 unasema kwamba tuna Mungu ambaye ni Baba wetu na kwa hivyo hatuhitaji wake au waume ambao hawajaokoka au yule ambaye hajaokoka katika biashara au yule ambaye hajaokoka kufanya naye kazi ya kumhudumia Mungu.

i. Tunaweza kuheshimiana na wale ambao hawajaokoka ili tuweze kuwafikia na injili ya Kristo.

6. 2 Worintho 8-9, Paulo anazungumza kuhusu pesa na kupeana kwa ajili ya kazi ya Mungu. Tunaposoma hivi, kumbuka kwamba Paulo anazungumza na watu ambao walikuwa maskini sana na anawahimiza kutoa kwa ajili ya kazi ya Mungu. Katika Luka 21:1-4, Yesu anafundisha kwamba lazima tutoe kwa ajili ya kazi ya kanisa. Yesu alifurahishwa na kutoa kwa mjane mmoja ambaye alikuwa maskini. Kutoa ni baraka, na ni zawadi kutoka kwa Mungu. Kumbuka kwamba yesu hahitaji pesa kwa sababu Yeye ndiye anamiliki kila kitu (Zaburi 24:1 na 50:10-12).

A. 2 wakorintho 8:1-7, tunasoma kuhusu mfano jinsi Mungu anataka kanisa lake linapaswa kushirika mali ambayo Mungu amepeana. Tunaona kanisa la Macedonia ambali lilikuwa kanisa maskini jinsi lilitoa kwa ajili ya kazi ya Mungu. Katika mstari wa 4, tunaona kwamba walijua kwamba Mungu aliwabariki sana kiwangi kwamba aliwakubali kutoa kwa ajili ya kazi yake.

B. Mistari ya 6-7, Paulo alilihimiza kanisa la Korintho kufanya jinsi kanisa la Macedonia lilifanya. Aliwahimiza watoe kwa moyo mkunjufu. Hivi ndivyo Mungu anataka kila kanisa lifanya.

C. 2 Wakorintho 9:5-7, tunaona sababu ya Paulo kuzungumza juu ya kanisa la Macedonia ilikuwa kuhimiza kanisa la Korintho kutoa ili mahitaji yao yapatikane (mstari wa 5). Paulo anatupatia kanuni ambayo tunapaswa kufuata. Mungu an ataka tutoe kwa moyo mkunjufu na kama sivyo, tusitoe. Mungu hahitaji pesa yako, lakini anakubali utoe kwa moyo mkunjufu na wenye furaha.

D. 2 wakorintho 9:15, Paulo anazungumza sasa juu ya jinsi Mungu ametupatia mengi. Ktika mstari wa 15, anasema kwamba Mungu ametupatia zawadi kuu sana. Zawadi hii ni Kristo. Je, tunaweza kufafanua Kristo kwa njia gani? Haijalishi tunampatia Mungu nini, ukweli ni kwamba hatutawahi kumpatioa zaidi ya jinsi Yeye ametupatia. Zawadi yakle kwetu ni ya milele.

E. Malaki 3:10-11, tunasoma kwamba tumjaribu Mungu kwa kkuwa waaminifu katika kutoa kwetu hata wwakati hatuna mengi. Biblia inatuhimiza tumjaribu Mungu katika hili. Yesu alimsifa yule mjane ambaye alitoa kidogo ambacho alikuwa nacho kwa Mungu (Marko 12:42-43).

Paulo anamalizia barua kwa kuwahimiza watu kwamba wanapaswa kukubali mamlaka yake kama mtume. Paulo alitaka kuja huko na kufurahia ushirika pamoja na kanisa na wala si kuwaadhibu. Nidhamu ya kanisa inapaswa kuzingatiwa wakati inahitajika. Katika 2 Wakorintho 13:9-10, Paulo anapeana sababu ya kutekeleza nidhamu kanisani, ambayo ni kuwarejesha wale ambao wametenda dhambi katika ushirika mzuri na kanisa lote.

A. Paulo anamalizia kwa kuwahimiza watu kwamba walifaa kuweka kandoo tofauti zao na kuishi na kufanya kazi kwa Amani na kwa pamoja.

Barua kwa Wagalatia na Waefeso.

Mji wa Galatia ni mji katika Uturuki. Barua hii iliandikwa kwa kanisa au makanisa ambao yalikuwa katika eneo hili la Galatia. Makanisa haya yalipandwa na Paulo wakati wa Safari yake ya kwanza ya kueneza injili. Barua hatusoma Paulo akiwasalimu wasikilizaji wake kwamba sababu alikuwa na nia moja ya kurekebisha uongo ambao ulikuwa unaenea katika kanisa. Yeye

alikuwa na kusudi moja, kundoa uongo. Watu walikuwa wanafundishwa ujumbe wa uongo kuhusu wokovu. Walifundishwa kwamba walifaa kuwa na matendo mazuri ikiwa kweli wangekubalika na Mungu. Matendo ambayo walikuwa wanaambiwa, yalikuwa ni ya Kiyahudi kama kutahiriwa.

Wagalatia

Sura za 1-2, Paulo anazungumza kusuhu mamlaka yake.

1. Mistari ya 1-3, Paulo anasema kwamba yeye amepewa mamlaka kutoka Mungu na wala si kwa mwanadamu.
2. Paulo anawakemea wale ambao wanafunidisha watu mafundisho ya uongo n ahata anawalaani (Mstari wa 9). Je, ni kwa nini mafindosho ya uongo ni mabaya sana? Sasabu moja kuu ni kwamba mafundisho ya uongo yanawatoa watu kwa Kristo na kwa ongoza watu jahanumu. Silaha kuu dhidi ya mafundisho ya uongo ni kufundisha ukweli wa Biblia wazi wazi. Usikubali lolote ambalo mtu yeyote anafundisho iki mafundisho hayo hayatoki kwa Biblia.

3. Paulo anaendelea katika mstari wa 10, kueleza ukweli. Anasema kwamba hatufai kuwa na wasiwasi yoyote ya kutaka kumpendeza mwanadamu yeyote na ujumbe wetu. Tunapaswa kumfuirahisha tu Mungu. Ukweli ni kwamba yule ambaye anataka kumpendeza Mungu mara kwa mara atapata upinzani mkubwa sana. Chaguo letu lipaswa kuwa kumpendeza Mungu hata kama tutachukiwa na watu wote. Mahubiri ya mali na afya ni mabaya sana kwa sababu huwa yanafanya mahitaji ya mwanadamu yapewa nafasi ya kwanza badala ya Mungu.

4. Mistari ya 11-12, tunapaswa kufundisha kile ambacho Mungu ametuamuru kufundisha pekee. Paulo alipata ujumbe wake kutoka kwa Kristo nasi leo tunapata ujumbe kutoka Kristo kupitia kwa Biblia.

5. Paulo katika sura ya 2, anasema kwamba miyume wengine walikubali ujumbe wake na mamlaka yake kama mtume na kwa sababu hiyo hawakuhitaji Tito kutahiriwa (mstari wa 3). Ikiwa lingekuwa jambo la muhimu kutahiriwa, basi mitume wengine wangemsihi Paulo kumtahiri Tito. Leo kutahiriwa si jambo la muhimu, lakini kuna makanisa ambayo yanafunidisha bado kwamba lazima tufanye mambo fulani ikiwa tutakubalika kama kubatizwa au kutoa sadaka.

Wagalatia 2:15 hadi sura ya 4, tunasoma kwamba tunaokolewa kwa imani pekee.
1. Tunaokolewa kwa imani pekee na wala si kwa matendo mazuri (2:16). Huu ndio ujumbe katika sura ya 3. Hivi ndivyo Paulo anavyojadili jambo hili:

A. Wagalatia 3:1-5, Paulo anawakumbusha Wagalatia kuhusu wokovu wao. Katika mstari wa 3, anawauliza kwamba kwa nini walionelea kwamba walifaa kuongoza juu ya wokovu wao ambao walipokea kwa imani pekee.

B.Wagalatia 3:6-9, Paulo anawakumbusha Wayahudi kwamba Abrahamu alihesabiwa mwenye haki kwa imani pekee (Mwanzo 15:6). Hii ilikuwa kabla ya kutahiriwa kwake na kabla ya sheria kupeanwa na Musa. Hili dhihirsho kwamba mtu anaokolewa kwa imani na wala si kwa matendo yake mazuri kama kutahiriwa. Kuna Wayahudi ambao waliokolewa na walikuwa bado wanataka kutekeleza matakwa ya sheria ya Wayahudi.

C. Katika mstari 10-14, Paulo anasema kwamba no vyema kutii shweria kwa sababu katika mstari wa 10 anasema kwamba amelaaniwa yule ambayer hatii sheria ya Mungu. Dhambi moja inatosha kutufanya tulaaniwe. Katika mstari wa 11, anasema kwamba tunahesabiwa haki kwa imani kwa sababu hakuna mtu amabaye atahesabiwa haki kuwa kuzingatia sheria.

2. Je, ikiwa sheria haiwezi kutuokoa, kwa nini Mungu alitupatia sheria yake? Paulo anajibu swali katika sura ya 3:19-4:7.

A. Mstari wa 19, kusudi ya sheria ilikuwa kudhihirsha dhambi ndani mwetu ili watu wajue Mungu anataka nini kutoka kwao. Jambo hili ni wazi kabisa katika warumi 4:15.

B. Kusudi nyingine ya sheria ni kufanya watu wao udhaifu wao na kutosweza kwao kujiokoa. Kwa njia hii wao wageuke na kumwamini tu Kristo kwa ajili ya wokovu wao.

C. Katika mistari ya 24-26, sheria ilikuwa kama kiongozi wetu wakati tulipokuwa chini ya sheria. Sasa sheria imebadilishwa na sasa sisi ni wana wa Mungu. Kwa hivyo hatuko chini ya sheria tena. Sasa wale wote ambao wameokoka wako chini uongozi wa Mungu.

D. Wagalatia 4:5-7, Paulo anaendelea kusema kwamba sisi ambao tumeokoka tumefanywa kuwa wana wa Mungu (Warumi 8:15). Tunaona hapa kwamba uhusiano wetu umebadilika na sasa tuko na uhusiano wa kipekee na Mungu. Sisi tuko katika jamii ya Mungu.

3. Paulo katika sura ya 4 anasema kwamba kwa sababu sasa wagalatia walikuwa wamewekwa huru kutoka kwa sheria, kurudi kwa sheria ni kurudi kwa utumwa.

1. Wagalatia 5:1, kwa sababu ya kristo, hatuhitaji tena kuwa chini ya nira ya utumwa kwa dhambi. Badala yake, tuko na huru wa kusihi kama wakristo, yaani tuko huru kuenenda kulingana kwa Roho. Paulo anafundisha jambo hili hili katika Wakolosai 3:5-17.

A. Paulo anafundisha kwamba hatufai kuenenda kwa mwili. Katika mstari wa 16, anaorodhesha mambo fulani ambayo hatufai kufanya. Dhambi ambazo Paulo anaorodhesha hapa ni dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu na wale ambao wanafanya dhambi hizo hawatauridhi ufalme wa Mungu.

B. Paulo anatueleza kuhus yale ambayo tunapaswa kuyafanya. Tunapaswa kufanya yafuatayo katika mistari ya 22-23: tunda la Roho Mtakatifu; upendo, furaha. Amani, uvumilivu, uzuri, uaminifu, ukarimu na kiasi.

Wagalatia 6:1-10, Paulo anaorodhesha baadhi ya tabia ya mtu ambaye ameokoka.

2. Wagalatia 6:1 anasema kwamba tunapaswa kumrejesha ndugu ambaye ameanguka katika dhambi.

3. mstari wa 2, tunapaswa kusaidiana. Njia moja ya kufanya hivi ni kuombeana.

4. Mstari wa 3, mtu ambaye anaongozwa na Roho hafai kuwa mtu mwenye kiburi.

5. Mstari wa 4, mtu ambaye ameokoka atajichunguza na kuchunguza matenda yake mbele za Mungu. Kusudi lake ni utukufu wa Mungu na wala si sifa za wanadamu.

6. Mstari wa 5, mtu ambaye ameokoka anajukumika katika majukumu yake ya kiroho.

7. Mstari wa 6, mtu ambaye ameokoka atahusika katika kukutana na mahitaji ya wale ambao wanamfundisha neno la Mungu.

8. Mistari ya 9-10, yanajumlisha mambo yote katika maisha ya yule ambaye ameokoka. Tunapaswa kuendeelea kwa uaminifu katika maisha yetu yote ya kiroho na hatupaswi kushushwa moyo. Katika mstari wa 10, tunaelezwa jinsi tunapaswa kuasaidia. Tunaambiwa tuwasaidie wote haswa na kwanza kabisa wale ambao wameokoka kama sisi.

Ephesians

Paulo aliandika barua hii wakati alipokuwa gerezani huko Roma. Hakuandika barua kwa sababu kulikuwa na shida katika kanisa, ni kwa sababu alitaka kufundisha mambo fulani fulani. Mji wa Efeso unapatikana katika Uturuki leo.

Waefeso 1-3 Utajiri wa kanisa.

1. Mistari ya 3-14, katika lugha la Kigiriki ni sentensi moja ambamo Paulo anamsifu Mungu. Mistari ya 3-5, anamsifu Mungu Baba kwa ajili ya baraka zetu za kiroho ambazo tunapokea katika Kristo. Baraka hizi za kiroho ndio utajiri wa kweli wa kanisa na kila siku tunapaswa kumsifu, kumtukuza, na kumshukuru Mungu kwa sababu ya baraka hizi.

A. Tunaona kwamba Mungu aliwachugua watu wake kabla ya kuiweka misingi ya ulimwengu. Mungu alifanya haya kwa kusudi lake pendo na kusudi lake mwenywe. Mungu alituchagua na hiki ni kitendo chake cha Upendo.

2. Katika msitari ya 7-11, Paulo anazingatia sifa zake kwa Mungu kwa kazi ambayo Mungu Baba ameofanya kupitia kwa Kristo. Katika mistari ya 7-8, tunaona kwamba tunapewa wokovu kupitia kwa damu ya Kristo Yesu. Tunasoma kwamba tunasamehewa kupitia kwa damu ya Kristo Yesu aliyomwagika msalabani kalivari. Hili ni jambo la mjuhimu sana kwa tusije siku hata moja tukaona kwamba lazima tumsaidie Mungu na matendo yetu mazuri ikiwa kweli tutaokoka. Tunaokolewa kupitia kwa zawadi ya pekee Mungu ambaye ilitolewa kama sadaka kwa ajili ya dhambi zetu. Sadaka hii ni Kristo Yesu.

3. Katika mistari ya 12-14, Paulo anamsifu Mungu Roho Mtakatifu kwa kazi yake ya kulinda kwa kutuhaikishia kwamba sisi ni wa Mungu milele.

4. Katika mistari ya 17-18, Ni Mungu ambaye anadhihirisha chochote ambacho tunapaswa kujua kumhusu.Tunapaswa kusoma, kujifunza Biblia kwa uaminifu na kumwomba Mungu Roho Mtakatifu ataufundishi ukweli wa Biblia. Kanisa Afrika ndipo linafanikiwa katika kazi ya kueneza ujumbe wa Injili, ni kuzingatia Biblia pekee kwamba ni neno la Mungu. Tunahitaji tu Biblia pekee na kufanya kazi ya Mungu kwa bidi. Tunapaswa kumwomba Mungu abariki kazi ambayo tunayoifanya na atujaze na hekima ya kufanya kazi yake. Kumbuka kwamba kanisa la kwanza lilijitahidi tu katika kazi ya kuhubiri injili.

5. Waefeso 2:1-10, tunaona mkristo ni mtu wa aina gani. Tunaona kwamba sisi sote wakati mmoja tulikuwa tumekufa jkwa dhambi na tulimfuata shetani kama kiongozi wetu. Katika mstari wa 3, tunasoma kwamba kabla ya kuokoka tulikuwa chini ya ghadhabu ya Mungu.

Tulikuwa tunaenda jahanumu. Lakini katika mistari ya 4-5, tunasoma kwamba kwa sababu ya upendo wake mkuu, Mungu alitukomboa na kutufanya tuwe hai kiroho. Mstari wa 6, tunasoma kwamba tumefanywa kuwa hai na Kristo.

A. Katika mistari ya 8-9, tunasoma jinis tumeokolewa. Ni vyema kufahamu hili kwamba hatuokolewi kwa matendo mazuri.

B. Mstari wa 10, tunasoma kwamba hatujaokolewa kuishi kwa ajili yetu, bali tumeokolewa kutenda matendo mazuri. Tunajua kwamba matendo yetu mazuri hayawezi kutuokoa kwa sababu tunaokolewa kwa neema.

C. Hakuna mtu ambaye anajua siku ile atakufa, hata yule ambaye ameokoka. Lakini ukweli ni kwamba Mungu atatuchukua kutoka katika ulimwengu huu wakati ambao mwenyewe amepanga. Kwa mkristo Mungu atakuewa amekamilisha kazi ya utakatifu katika maisha yake.

6. Waefeso 2:11-22, wakristo ni watu ambao wako pamoja kwa sababu ni Kristo ambaye amewaweka pamoja. Katika mstari wa 19, anasema kwamba sisi sote ni watu wa nyumba moja. Haijalishi wewe ni Myahaudi au mzungu au mwafirka au mwindi; ikiwa umeokoka, wewe ni mtoto wa Mungu na wewe sisi sote ni watu wa nyumba moja. Wakristo ni watu ambao wako na uhusiano wa karibu sana kuliko hata uhusiano wao na watu fam,ilia zao ambao hawajaokoka.

Waefeso 4-6:9, tunasoma jinsi kanisa linapaswa kufanya kazi yake.

1. Waefeso 4:11-16, Paulo anahimiza umoja katika kanisa. Anasema kwamba Mungu ametupatia karama tofauti tofauti na majukumu tofauti tofauti kwa lengo moja la kulijenga kanisa. Tunapaswa kuwasaidia wakristo wengine kukua katika imani ili kama kanisa tuweze kukua pamoja kiroho. Kazi ya wachungaji katika kanisa ni kuwasaidia washirika kukua na kufanya kazi ya Mungu kwa pamoja.

B. Waefeso 4:17-32, tunasoma kwamba hatufai kuishi kama watu ambao hawajaokoka.

i. Mstari wa 25, tunasoma kwamba hatufai kudanganyana badala tunafaa kuwa waaminifu na kuzungumza ukweli pekee kila wakati.

ii. Mstari wa 28, tunapaswa kufanya kazi kwa bidi na wala si kuiba. Kazi hiyo pia imekusudiwa tuwe na kitu cha kluwasaidia wengine.

iii. Mstari wa 29, maneno ambayo tuyazungumza yanafaa kuwa ya kuwajenga wengine badala ya kuwaharibu.

iii. Mstari wa 32, tunasoa kwamba tunapaswa kuufuata mfano wa Kristo kwa kuwa watu wakarimu na wenye kuwasamehe wengine. Msamaha ndio chanzo cha kuwa na uhusiano mwema na wengine. Kila mmoja wetu wakati mmoja au mwingine tunaweza kufanya jambo ambalo linawakasirisha wengine. Lakini ikiwa tutakuwa watu wenye kusamehe kwa haraka, basi tutakuwa na uhusiano mzuri sana na wengine. Ndoa ndio mfano mzuri. Ndoa mzuri ni ndoa ambayo watu wanasameheana kila wakati kwa sababu wanakoseana kila wakati.

2. Waefeso 5, tunapewa jinsi ya kuishi maisha yetu kama watu ambao tumeokoka.

A. Mstari wa 1-2, tunasoma kwamba tunafaa kuiga mfano wa Kristo.

B. Hatufai kujihusisha katika tabia ya dhambi za ulimwengu haswa katika mstari wa 3, dhambi ya zina. Anasema kwa sababu kabla ya kuokoka tulikuwa katika giza na sasa tuko katika nuru.

C. Mstari wa 18, hatufai kulewa kwa sababu tumejazwa na Roho Mtakatifu ambaye anatuongoza katika furaha, shukurani na utiifu.

D. Sehemu ambayo inafuata inashughulika na uhusiano kati ya mume na mke. Haya ni mafundisho muhimu sana kwetu. Baadhi ya mafundisho haya ni kinyume kabisa na jinsi wengi wanavyowaza na kuishi katika ndoa zao leo. Hapa Mungu anapeana jinsi ndoa inapaswa kuwa, ndoa ambayo inamletea utukufu. Kumbuka kwamba Mungu anampenda mke ambaye ameokoka kama tu vile anavyompenda mume ambaye ameokoka.

E. Wacha tuzingatie mafundisho haya ya Mungu kuhusu ndoa.

i. Mistari ya 22-24, maagizo kwa wake kuhusu uongozi katika ndoa. Mume ndiye kiongozi katika ndoa nay eye ndiye amepewa majukumu ya familia yake. Mke anapaswa kutii mume wake.

ii. Mistari ya 25-33, mume anapewa majukumu muhimu sana.

iii. mume anapoongoza familia yake anapaswa kumpenda mke kama tu vile Kristo alivyolipenda kanisa. Je, Kristo alilipenda kanisa kiwango gani? Yeye alikufa kwa ajili ya kanisa. Kristo

hajasema kwamba tufe kwa jili ya wake wetu, lakini anasema kwamba upendo wetu kwao unapaswa kuwa wa kujitolea kabisa.

iv. Kusudi la upendo wetu kwa wake wetu lipaswa kuwa kuwajenga katika Bwana (mistari 26-27). Waume wanapaswa kuwa viongozi wa kiroho katika manyumba zao.

F. Sehemu nyingine katika surah ii inasema kwamba machoni pa Mungu mume na mke ni kitu kimoja. Kila mume anapaswa kumfanyia mke wake jinsi yeye mwenyewe anataka kufanyiwa.

3. Waefeso 6:1-4, tunasoma kuhusu uhusiano kati ya watoto na wazazi wao.

A. watoto wanapswa kuwatii wazazi wao. Hii ndio amri ya nne katika amri kumi za Mungu.
B. Hapa pia kuna majukumu ya wazazi. Tunapswa kuwalea watoto wetu wakifahamu kwamba wao ni wa muhimu sana. 2 Wakorintho 2:14 tunaosma kwamba wazazi tuko na jukumu kubwa juu ya maisha ya watoto wetu. Tunapaswa kuwafundisha watoto wetu kumhusu Mungu. Hili ni jambo la muhimu sana. Ni lazima tuwafundish mafundisho ya Biblia kila siku. Kina baba lazima tusome Biblia na watoto wetu nia yetu ikiwa kuwafundisha na kuwaonyesha njia ya wokovu ambayo ni Kristo. Katika mstari wa 4, tunasoma kwamba tunapaswa kuwalea katika nidhamu. Hii haimaanisha kwamba tunapaswa kuwapiga watoto wetu kila wakati, bali inamaanisha nidhamu ambayo tunawapatia inapaswa kuwa kwa ajili ya kuwarekebisha na wala si kuwaumiza. Ni lazima tuwaeleze watoto wetu sababu ya adhabu ambayo tunawapatia.

4. Mistari ya 5-9, ni uhusiaona katika ya watumwa na mabawana wao. Huu ndio ulikuwa uhusiano katika Agano la kale. Leo huu ni uhusiano katika ya wafanyakazi na wajiri wao. Wafanyakazi wote wanapaswa kuwa waaminifu kwa wajiri wao na wajiri nao wanapaswa kuwashughulikia wafanyakazi kama tu vile Kristo anavyotushughulikia. Malaki 3:5, kuna onyo kwa mwajiri ambaye anakosa anawadanganya wafanyakazi wake. Leo kuna wajiri wengi ambao wanawadanganya wafanyakazi wao kwa kuwapatia mishara duni ambayo haifai. Wengine nao wanawafanyisha kazi nyingi ambayo inazidi kiwango cvha pesa ambacho wanawapatia.

5. Mafundisho ya mwisho katika sura hii yanaanza katika mistari ya 10-18.

A. Tunapaswa kuelewa kwamba wale ambao wameokoa tuko vitani vya kioroho dhidi ya shetani ambaye ni ana nguvu kuliko mwanadamu wa kawaida. Kwa sababu hii tunafaa kupigana na shetani tu kwa kutumia vazi la sila ya Mungu na wala si kwa nguvu zetu. Tusome vazi hili na tutajifunza mengi jinsi ya kumpinga shetani.

6. Paulo katika mstari wa 10, anaonmba kanisa la Efeso limwombee.

Barua za Wafilipi na Wakolosai

Paulo alikuwa gerezani alipokuwa anaandika barua hii kwa kanisa la Filipi ambalo likuwa kasikazini mwa Ugiriki. Alikuwa anataka kuwajulisha hali yake na kuwashukuru kwa usaidizi ambao walimpatia. Pia alikuwa na mafundisho kwao kuhusu majukumu yao na hatari ya mafundisho ya uongo.

Barua kwa Kanisa la Filipi Wafilipi

1. Barua hii iliandikwa kwa wakristo ambao walikuwa katika mjia wa Filipi.

2. Wafilipi 1:1-19, tunaona kwamba kuwa gerezani haikumfanya Paulo akose mkuendelea na huduma wake kwa Mungu. Alitumia wakati huu kuandika baadhi ya barua za Agano Jipya na pia kueneza ujumbe wa injili na wengi hata walinzi wa jera. Paulo nahkushushwa moyo hata wakati alipokuwa gerezani.

3. Paulo anasema kwamba haogopi kifo kamwe. Alijua kwamba yeye angeuliwa wakato wowote, lakini hata hivyo katika mstari wa 21, anasema kwamba ikiwa mtu ambaye ameokoka anakufa, yeye hufaidika zaidi kwa sababu yeye hupoteza maisha yake hapa duniani na anayapata ya mbinguni.

4. Katika mistari ya 20-26, Paulo anasema kwamba hata kama anatamani sana kufa, pia anatamani kuendela kuisi ili aweze kuendelea kulisaidia kanisa. Tunapaswa kuwa na tamaa na kumtumikia Mungu katika kila hali bila kuwa na uoga wa kufa. Tunapaswa kuwa tayari kuteseka kwa jili ya injili (mstari 29).

5. Wafilipi 2, Paulo anajua anawashukuru wafilipi kwa kumshughulikia na pia anawaambai kwamba anawaambea waishi katika umoja. Hili linawezekana ikiwa wao watawaza kama Kristo (mstari wa 5). Mungu ndiye anapasa kuwa wa muhimu sana na kwanza katika maisha yao na wala si jambo lingine.

6. Wafilipi 2:9-11, tunasoma kuhusu ukweli ambao wale ambao hawajaokoka hawawezi kuukubali. Tunasoma kwamba kila mtu atakiri kwamba Yesu ni Bwana. Wale ambao tumeokoka tunafanya hivi kwa mioyo yenye furaha. Yule ambaye hajaokoka atafanya hivi kwa moyo ambao hauna furaha wakati wa hukumu atakapokuwa anahukumiwa kuingia jahanum.

7. Wafilipi 3, Paulo anaonya kuhusu mafundisho ya uongo kuhusu wokovu ambao unapatikana kutokana na matendo ya wanadamu. Katika mstari wa 2, anafafanua watu hawa ambao wanafundisho mafundisho haya kwa kanisa.

A. Katika Wafili 3:3-11, yeye alikuwa akitegemea matendo yake mazuri na sheria kwa ajili ya wokovu. Yeye anasema yale yote ambayo alikuwa ameyafanya kwa ajili ya kupata wokovu wake. Anasema kwamba kama ingewezekana mtu kupata wokovu kwa matendo yake mwenyewe, basi yeye angekuwa mmoja wa wale ambao wangepata wokovu huo. Katika mstari wa 7 anasema kwamba alitambua kwamba matendo yake yote yalikuwa ni bure. Sasa yeye alijua kwamba haki yake inatokana na imani katika Kristo Yesu.

B. Katika mistari ya 12-21, Paulo anasema kwamba lengo letu linapaswa kuwa kumtumikia Kristo na kuwa kama Yeye. Katika mstari wa 20, anasema kwamba sisi ni wenyeji wa mbinguni na kwa hivyo tunamsubiri Kristo ambaye ataibadilishi miili yetu kuwa miili ya utukufu kama wake.

8. Wafilipi 4:1, Paulo anaonyesha moyo wa mchungaji. Mchungaji anapaswa kuwa mut ambaye anawapenda watu wake na anataka kuwa nao. Mchungaji anawapenda na anwajali wale ambao anawachunga. Yeye anajali maisha yao ya nje na ile ya kioroho, na kama Kristo, yeye anawatumikia wale ambao anawachunga nay eye ni mchungaji mzuri.

9. Katika mistari ya 2-3, Paulo anawauliza watu wawili ambao walikuwa wakilumbana kwamba walipaswa kumaliza malumbano yao na kurudi pamoja. Pia anauliza kanisa liwasaidia hawa wawili kutatua malumbano yao ili waweze kufanya kazi ya kanisa kwa pamoja.

10. Sisi sote tunapaswa kuwa na moyo kama wa Paulo. Wafilipi 4:10-13, haijalishi hali yetu ya maisha, tunapaswa kuwa watu ambao tunatosheka. Ikiwa Mungu atakupatia kazi ambayo inahatarisha maisha yako au kazi ambayo ni ngumu sana, unapaswa kuwa mtu ambaye anatosheka.

A. Katika mstari wa 19, tunasoma kuhusu ahadi ya Mungu kwamba Yeye atatupatia mahitaji yetu ya kila siku. Kile anapeana kinaweza kuwa kile ambacho hatukuuliza lakini kila wakati atapeana kile ambacho anajua kinafaa kwetu. Pia hata kama hali ambayo tuko ndani mwake inatuelekeza kwa kifo, tunapaswa kujua kwamba kila wakati mkristo ni mtu wa ushindi (2 Wakorintho 5:8).

Barua kwa Wakolosai

Paulo aliandika barua hii kwa kanisa la Kolose, kanisa ambalo hakuwahi tembelea. Paulo aliandika barua hii wakali alipokuwa gerezani. Aliandika barua na kusudi la kurekebisha uongo ambao ulikuwa umeingia katika kanisa. Mafundisho ya wayahudi yalikuwa yanaleta matatizo katika kanisa. Wao walikuwa wanafundisha kwamba Kristo pekee hatoshi kwa ajili ya wokovu. Paulo aliandika barua hii kurekebisha mafundisha haya.

1. Paulo anaanza kwa kusalimia kanisa na kuwakumbusha watu kwamba yeye alikuwa ameitwa na Mungu kuwa mtume na kwa hivyo mamlaka yake yanatoka kwa Mungu.

2. Hata kama Paulo anaandika kutatua shida, yeye haanzi barua kwa kuzungumza juu ya shida hizo. Badala yake anaanza kwa kutaja mambo mazuri ambayo kanisa hili lilikuwa linayafanya. Hii ni njia mzuri ya kuwasaidia watu wakati wako katika shida fulani fulani. Njia moja mzuri ni kusema ukweli na kuomba kwamba Mungu atatumia ukweli huo kuwarekebisha mahali ambapo wameanguka.
A. Mambo mazuri ambayo walikuwa wamejifunza yalikuwa imani na uoendo na tumaini (mstari wa 4 na 5).

3. Katika mistari ya 13-19, Paulo anafundisha kuhusu hali ya Kristo Yesu.

A. Mistari ya 13-14 tunaosma kwamba Kristo Yesu ndiye Mkombozi wetu.

B. Wakolosai 1:15, Yesu ni mrithi na kiongozi wa kila kitu ambacho kimeumbwa.

C. Mistari ya 16-19, Yesu ndiye mwumbaji wa kila kitu na Yeye ndiye mwanzo wa kila kitu. Yeye ndiye kichwa cha kanisa.

4. Mistari ya 20-23, Yesu ndiye tumaini la pekee la ulimwengu.

5. Wakolosai 1:24-2:3, kila mkristo ana Kristo ndani mwake (mstari wa 26). Tunasoma kumhusu Mungu katika Biblia.

6. Wakolosai 2:4-8, Paulo anasema sababu ya mafundisho haya ni kulinda kanisa dhidi ya mafundisho ya uongo ambayo yangeongoza kanisa katika uongo ambao utawafanya wasiishi maisha kama wakristo wa kweli. Ulinzi halisi dhidi ya mafundisho ya uongo ni mafundisho ya kweli ya Biblia.
7. Mistari ya 9-23 tunafundisho kwamba kwa sababu tuna Kristo, hatuna haja ya kuwa watu wa sheria kama kufuata sheria za vyakula au kuatahiriwa. Ili mtu aweze kuokoka, hahitaji haya yote.

A.Mistari ya 11-13, Katika Kristo tumetahiriwa lakini kutahiriwa huku si kwa mikono ya wanadamu bali ni kutahiriwa kwa moyo (Wakolosai 2:11). Hii ni kazi ya kuzaliwa mara ya pili ambayo ni kazi ya kiroho katika maisha ya yule ambaye anaokolewa. Yule ambaye ni Myahudi wa kweli, ni yule ambaye ametahiriwa moyo wake na Roho Mtakatifu (Warumi 2:29). Hii kazi ya Kristo am,bayo anaifanya katika moyo wa mkristo. Kazi hii si kazi ya mikono ya mwanadamu au kiumbe chochote, bali kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

B. Mstari wa 18, tunasoma kwamba hatufai kutegemea mambo kama unabii au maono ya wanadamu bali tunapaswa kusoma na kutegema tu neno la Mungu.

C. Mstari wa 23, tunaonywa juu ya kutegemea dini ya wanadamu ambayo wengi leo wanafuata.

8. Kwa sababu tumefufuliwa na Kristo 3:1-17, Paulo ansema kwamba tunapaswa kutafuta vitu vya mbinguni, yaani tunapswa kuishi maisha matakatifu. Paulo anasema kile ambacho hatupaswi kufanya na kile ambachi tunapaswa kufanya.

A. Wakolosai 3:5-9, tunapewa orodha ya mambo ambayo tunapswa kuyafanya kwa sababu sasa ni sisi ni watu wapaya nay a kale yameisha.

B. Katika mstari wa 10-11, tunasoma kwamba tunapaswa kuvaa utu upya na maisha ya utu wetu upya.

C. Mstari wa 17, ni mojawapo ya mistari ambayo tunapswa kukariri. Chochote ambacho tunakifanya, tunapaswa kukifanya kwa ajili ya utukufu wa Mungu pekee. Tunapaswa kufanya kila kwa shukurani na utukufu wa Mungu. Hata wakati tunateseka, tunapaswa kumtukuza Mungu (Yakobo 1:2).

9. Wakolosai 3:18-22, Paulo anatoa maagizo kwa familia jinsi wanapswa kuishi. Famili wanafaa kuishi maisha yao kulingana na mafundisho ya Biblia.

10. Wakolosai 4:2-6, Paulo anapeana amri 4 ambazo zinafaa kufuatwa na kila mshirika wa kanisa.

A. Kwanza wanapaswa kuendela katika maombi (mistari ya 2-3).
B. Pili wanapaswa kuwa watu wenye shukurani (mstari wa 2).

C. Tatu, wanapaswa kuishi kwa hekina na wale ambao hawajaokoka. Katika mstari wa 5, Paulo anasema kwamba wanapaswa kuwa wakarimu kwa wale ambao hawajaokoka ili waweze kuwavutia waje kwa Kristo (mistari ya 5-6).

D. Tatu, maneno yao yanapaswa kuwa yamejawa na neema kila wakati (mistari ya 5-6).

11. Paulo anamalizia barua hii kwa kuwaeleza kwamba Tychicus ndiye alikuwa mwakilishi wake ambaye alituma kuwahimiza (4:7-8).

12. katika mstari wa 15, Paulo anataja makanisa manne ambayo yalikuwa yanakutana katika manyumba. Katika sehemu nyingi ulimwenguni makanisa yanakutana katika manyumba. Huu haswa katika mataifa ambapo wakristo wanateswa sana. Nchi kama uchina na Saudi, wakristo wanakutana katika siri katika manyumba.

Barua kwa Wathesalonike.

Barua hizi mbili ziliandikwa na Paulo kwa kanisa la Thesalonike ambalo linapatikana katika kasikazini mwa Ugiriki. Paulo anatumia Barua hizi kwa mafundisho zaidi. Moja wa mambo aliyafundisha katika barua hizi ni kuhusu siku za mwisho. Pia alitumia barua hizi kuwahimiza wakristo katika makanisa haya.

Paulo anaanza barua yake kwa kuwahimiza watu. Wakristo hawa walikuwa wanateseka sana na kwa hivyio walihitaji kuhimizwa sana. Hili ni jambo la muhimu sana kwetu viongozi wa kanisa. Ni jukumu letu kuwahimiza washirika wetu ambao wanapitia magumu sana n ahata kuwasaidia.

1. Katika sura ya 4, anaanza kuzungumza kuhusu shida fulani fulani katika kanisa. Katika mstari wa 1, Paulo anawaeleza wakristo kwamba tunapaswa kuishi maisha yetu kwa kumpendeza Mungu. Hili ndilo linafaa kuwa lengo la kila mkristo kila wakati. Paulo pia katika mstari wa 2, anawaambia wakristo kwamba wanapaswa kumsikiliza na kutii kile ambacho anafundisho kwa sababu mamlaka yake yanatoka mbinguni.

2. Mistari ya 3-8, tunasoma kuhus dhambi ya zina. Hii ni shida kubwa sana katika maisha ya wakristo. Tunaona hivyo katika Agano la Kale na Agano Jipya tunaonywa sana dhidi ya dhambi hii. Kuna viongozi wengi wa makanisa mabao wamekosa kuwa waangalifu na wamejipata wameanguka katika dhambi hii. Tunapaswa kujichunga sana ili tusije tuanguaka katika dhambi hii. Njia moja ya kujilinda ni kusoma neno la Mungu na kuendelea katika maombi na kuhakikshia kwamba hatupatikani katika sehemu ambazo dhambi hii ipo. Pia tuhakikishe

kwamba hatupatikani na watu wa jisni tofauti mahali pa siri au tukiwa peke yetu ikiw wao si wake wetu. Hakikisha kwamba kila wakati unapokuwa na mtu wa jinsi tofautu kuna mashihidi.

A. Kuna wachungaji wengi ambao wameanguka katika dhambi za kutazama picja za ngono kwa mitandao.

B. Kila wakati tunajaribiwa sana kuanguka katika dhambi ya zina na ili tuweze kujilinda kutokana na kuanguka, tunapaswa kufanya jinsi Waefeso 6 inafundisha. Tuvae vazi la silaha za Mungu. Katika Waefeso 4:5, Biblia inasema kwamba hatufai kuishi maisha yetu kama watu ambao hawajaokoka ambao hawana kiasi. Paulo alifundisha katika Warumi 6 kwamba dhambi si bwana wa wakle ambao wameokoka tena. Kwa sababu tunaweza kuwa watu wa kiasi na kujizuia kuanguka katika dhambi ya zina.

C. Paulo katika mstarai wa 8, kila wakati tunapoanguka katika dhambi ya zina, huwa tunakosa kumtii Mungu. Anasema kwamba hatufai kukubali kuanguka katika dhambi hii kwa sababu Mungu ametupatia Roho Mtakatifu ambaye anatusaidia kupinga dhambi na kushinda dhambi.

3. Katika mistari ya 9-12, Paulo anatufundisha mambo mawili:

A. Kwanza kabisa Paulo anawaambia kwamba wanafanya vyema kwa kujaliana, wakionyeshana upendo wa kindugu. Lakini pia anawahimiza kwamba wanapaswa kufanya zaidi.

B.Katika sura ya 4:11-12, kuna wale ambao walikuwa wamekuwa wazembe na walikuwa hawafanyi kazi. Paulo anawaambia kwamba wakristo wanapswa kufanya kazi na wala si kuwa mzigo kwa wengine. Watu wengi katika kanisa hili walikuwa wanatazamia kurudi kwa Kristo na kwa hivyo wao walikataa kujihisha na kazi hii ilikuwa kinyume na mafundisho ya Biblia. Hakuna mtu ambaye anajua siku ile Kristo atarudi na kwa hivyo tunapswa kuendelea na majukumu yetu ya kila siku ambayo Mungu ametupatia kufanya.

4. Katika mistari ya 13-18, Paulo anatuhaikishia kwamna kweli Kristo atarudi. Pia anapeana jinsi mambo yatakavyokuwa kabla ya kurudi kwake Kristo.

A. Katika mstari wa 16, anasema kwamba wale ambao walikufa watafufuliwa kwanza.

B. Katika mstari wa 17, watakapofufuliwa, wale ambao wameokoka pampja na wale ambao watakuwa hai wakati huo, watakutana na Yesu kwa mawingu. Milele hawa wataishi na Kristo. Hii ni himizo kubwa sana kwetu leo kwa sababu tunajua kwamba wakati mpendwa wetu ambaye ameamini Kristo anakufa, siku moja tutakuwa pamoja naye ikiwa sisi wenyewe pia

tumeokoka. Kunamsemo ambao unasema kwamba wakristo huwa hatuagi bali huwa tunasema tutaonana tena baadaye.

5. Sura ya 5:1-2, tunasoma kwamba siku ya Bwana yaja. Je, siku ya Bwana ni siku gani?

A. Neno hili tunalisoma kwanza katika Isaya 13:6, Ombolezeni kwa kuwa siku ya Bwana iko karibu; kama maangamizi kutoka kwa Mungu mwenye Ngungu siku hiyo yaja. Neno hili linatumika mara 23 katika Biblia nzima; katika Agano la kale na Agano Jipya. Katika Yoeli 2:1-11, tunasoma kuhusu maana ya siku ya Bwana; ni siku ya hukumu.

i. Siku ya Bwana inaweza kumaanisha wakati ambapo tunaihsi humu ulimwenguni. Ni siku ya hukumu kali sana kwa sababu ya dhambi. Maisha katika mataigfa mengi yanadhihirisha kwamba tunateseka kwa sababu ya dhambi zetu. Kwa mfano kuteseka kwingi katika ulimwengu kunaletwa na uongozi mbaya ambao ni matokeo ya dhambi.

ii. Mara kwa mara siku ya Bwana inamaanisha wakati ambapo Yesu kristo atarudi tena kuhukumu wanamdamu. Kwa wengi huu utakuwa wakatai wa hukumu mbaya sana.

iii. Siku ya Bwana ni siku ambapo wakristo wote watazawadiwa milele. Zungumza juu ya tofauti ya siku ya Bwana kwa wale ambao wameokoka na kwa wale ambao hawajaokoka. Mkristo anaweza kutazamia siku ya Bwana kwa sababu ni sku ambapo tutaingizwa mbinguni na Bwana yesu Kristo. Yule ambaye hajaokoka, siku yeye ataanza maisha yake huko jahanum milele.

B. Sura ya 5:1-11, Paulo anadem kwamba wale ambao tumeokoka, hatufai kamwe kuogopa siku ya Bwana. Anafanya hivi kwa kuonyesha wazi hatima ya wale ambao tumeokoka na wale ambao hawajaokoka. Tutazame baadhi ya mifano hii:

i. Mstari wa 5, tunahakikishiwa kwamba sisi ni wana wa nuru na wala si wa giza.

ii. mstari wa 9, tunahakikishiwa kwamba hatima yetu si maangamizo.

iii. Mstari wa 10, tunahakikishiwa kwamba tutakuwa na yesu Kristo wakati tunakufa au wakati tunaishi.

C. Sura 5:12-22, tunapata maagizo ya mwisho.

i. Mistari ya 12-13, tunafundishwa kwamba tunapaswa kuwasadia na kuwaheshimu wale ambao wako katika uongozi katika kanisa.

ii. Mstari wa 14, yule ambaye amekua katika imani anahimizwa awahimiza wale ambao hawanyi kile ambacho wanapaswa kufanya na pia amsaidie ndugu ambaye ni mdhaifu katika imani.

B. Mstari wa 15, tunafundishwa jinsi tunapaswa kuwashughulikia wale ambao wanatutesa. Tunapaswa kukumbuka maneno ya Yesu katika Mathayo 5:39. Pia tazama Mithali 25:22 na Warumi 12:22.

7. Katika mistari ya 16-22, Paulo anapeana maagizo.

A. Mstari wa 16, tunapaswa kufurahia kila wakati.

B. Mstari wa 17, tunapaswa kuomba bila kukoma. Tunapaswa kuwa na wakati wa maombi kila wakati na kuwa na nia mzuri katika maombi. Hatupaswi kukosa kuomba kila wakati.

C. Mstari wa 18, tunapaswa kuwa wati wenye kushukuru kila wakati na katika hali zote. Hili ni jambo gumu wakati fulani lakini hata hivyo tunapaswa kukumbuka kwamba hali yoyote haifai kuondoa furaha ya ukristo wako. Kila wakati katika kila hali tunapswa kutazamia mbinguni na kwa sababu hii mioyo yetu inafaa kuwa yenye kushukuru.
D. Mstari wa 19, hatupaswi kuhuzunisha Roho Mtakatifu. Huwa tunafanya hivi wakati tunaenenda katika njia za shetani na kupuuza neno la Mungu.

E. Mstari wa 20, hatupaswi kupuuza unabii. Hii inamaanisha kwamba tunapswa kuwa wenye kupokea mafundisho ya neno la Mungu.

F. Mstari wa 21, tunapswa kujaribu kila kitu. Tunapaswa kuhakikisha kwamba kila kitu kinaenda sawa na neno la Mungu. Tunapswa kujifunza Biblia na ikiwa mtu anafundisho lolote kuhusu Mungu, tunapaswa kuhakikisha kwamba kile anafundisha kinakubaliana na neno la Mungu. Biblia ndio neno la Mungu na ukweli pekee.

G. Mstari wa 21, tunapaswa kushikilia kile ambacho ni kizuri. Tunapaswa tu kukubali yale ambayo ni mazuri machoni pa Mungu. Tunapaswa kufanya kile ambacho ni kizuri machoni pa Mungu.

H. Mstari wa 22, tunapaswa kujitenga na uovu. Tunajifunza kile ambacho ni kizuri kutoka kwa Biblia.

8. Paulo anamalizia mafundisho haya kwa kututeleza katika mstari wa 23, kwamba tunapaswa kutembea na Mungu kwa uaminifu sana. Hatufai kufuata mwovu. Katika mstari wa 24, tunasoma kwamba Yesu atatusaidia katika kufanya mapenzi ya Mungu.

Barua ya Pili kwa Thesalonike.

Barua hii iliandikwa miezi michache baada ya barua ya kwanza labda akijinu mambo ambayo alikuwa ameyapokea kutoka kwa kanisa hili. Ujumbe wa Paulo katika barua unahusu mateso, kurudi kwa Kristo na haja ya kuishi maisha matakatifu.

1. Sura 1:4-12, inahusu kuteseka.

A. Paulo anasema kwamba anafurahia jinsi wao waliendelea kuwa waaminifu kwa Yesu Kristo hata wakati wao walikuwa wanayapitia mateso makali. Hii ilidhihirisha kwamba wao walikuwa waaminifu kwa Yesu (mistari ya 4-5).

B. Wale ambao wanawatesa wakristo watateswa pia na mateso yao yatakuwa ya milele (Mistari ya 6,8-9).

C. mateso yetu ambao tumeokoka ni ya muda mfupi sana (mstari wa 7).
D. Paulo anasena kwamba yeye anatamani kwamba Mungu atatukuzwa katika mateso yetu. Mstari wa 12, hatuelewi kabisa jinis Mungu anavyotukuzwa katika mateso yetu na ufalme wake kueendelea.

2. Sura 2:1-12, mistari hii inashughulika na baadhi ya uwonga wa wengi kwamba Kristo amesharudi na wao walikosa kumwona. Paulo anasema kwamba hili halijafanyika kwa sababu ishara za siku hii bado hazijaonekana.

A. Mojawapo wa ishara ni mtu yule mwovu ambayo bado haijajitokeza. Huyu atakuwa mtu ambaye atakauwa mwovu sana na atajiweka na kuabudiwa badal ya kuabudu Mungu. Kutakuwa na wakati wa uasi mkuu. Katika mstari wa 3, watu wengi katika historia waliwaza kwamba hili lilifanyika. Hatuwezi kabisa kueleza mtu huy mwovu ni nani.

3. Sura ya 3:10-13, Paulo anawahimiza wakristo kwamba hatufai kuwa wazembe. Tunapaswa kufanya kazi ili tuweze kupata chakula chetu cha kila siku. Paulo anasisitiza jambo katika mstari wa 11, kwa kusema kwamba yule ambaye hafanyi kazi, basi naye asile. Paulo alisema hili ili kuwafanya wale ambao ni wazembe waanze kujihusisha na kazi.

A. Katika mstari wa 13m kama tu katika Wagalatia 6:9, tunahimizwa kwamba tunapaswa kuendelea kufanya kazi na tusiochole kumtumikia Mungu. Pia tunapswa kuwa waangalifu kwamba tusifanye kazi bila kupumzika. Kuna wakristo amabo wanajaribiwa kufanya kazi nyingi sana na wanachoka. Baada ya muda wao wanaacha kufanya kazi ya ufalme. Tunapaswa kufanya kazi kwa bidi sana wakati huo pia tukizingatia kupuumzika.

Timotheo-Filemoni

Paulo alinadika barua mbili kwa Timoteo akimhimiza na kumwongoza. Baada ya Timotheo kuokoka, yeye alifanyika mchungaji na alikumbana na changamoto nyingi sana. Paulo aliwaandikia Tiomotheo na Tito ambao walikuwa wachungaji wachanga jinsi ya kuwa wachgania ambao watawasaidia wale ambao wanawachunga. Yeye aliwaonya dhidi ya manabii wa uongo, aliwahimiza wakati wanakumbana na mateso na pia aliwapatia maagizo kuhusu kuabudu na huduma.

1 Timotheo

1. Sura 1:3-11, sehemu ya kwanza ambayo ilihusu onyo dhidi ya mafundisho ya uongo. Paulo alimtaja Hymenaeus na Alexander ambao walikuwa walimu wa uongo (mstari wa 20). Paulo anaposema kwamba waliwapeana kwa shetani anamaanisha kwamba aliwatenga kutoka miongoni mwa washirika wa kanisa. Tunapaswa kujifunza kutoka na hili na kufanya kila jambo ambalo tunaweza kuondoa mafundisho ya uongo miongoni mwa makanisa yetu.

2. Paulo alieza kanisa kwamba lilifaa kuwa kanisa la maombi. Sura ya 2:1-2, Paulo anasema kwamba kanisa lipaswa kuwaombea wengine kama viongozi wan chi ili tuweze kuwa na maisha yenye Amani na utulivu.

3. Sura ya 2:9-15, tunapeawa magizo kuhusu majukumu ya wanawake katika kanisa. Wanawake wanapaswa kuvaa vyema. Katika mstari wa 12, anasema kwamba wanawake hawapaswi kuwa na mamlaka juu ya wanaume.

4. Sura 3, anapeana jinsi makanisa yanapswa kuongozwa.

A. Mistari ya 1-7, kuna afisi moja ya kanisa ambayo ina majina kadhaa: wazee, askofu au mchungaji. Tunaona kwamna huyu anapaswa kuwa mtu ambaye ni mwadilifu. Pia anapaswa kuongoza nyumba yake vyema, Anapaswa kuwa na mke mmoja. Anapaswa kuwa mtu amabye anauwezo wa kufundisha Biblia. Wachungaji wanaongoza kanisa wakiongozwa na Kristo Yesu. Wao wanapswa kuwa mfano mwema kwa kanisa.

B. Mstari wa 5, mtu ambaye hawezi kusuluhisha mambo yake katika maisha yake, hawezi kamwe kuwa mchungaji wa kanisa.

C. Mstari wa 6, mtu ambaye ameokoka juzijuzi, hafai kuwa mchungaji. Tunapaswa kusubiri hadi wakati wao wamekua kiroho na wamedhihirisha kukua kuwao.

D. Wachungaji wako na majukumu mazito sana kwa sababu hiyo wanapaswa kuchaguliwa kwa uangalifu sana. Wao wanapaswa kuwa na mwito kutoka kwa Mungu na mwito kudhihirishwa na kanisa ambamo wanatumikia. Mtu hafai kuchukua afisi ya uchungaji kwa mchezo.

5. Mstari wa 8-13, tunsoma kuwahusu mashamanzi ambao wanahusika katika kazi ya kila siku ya kanisa. Bibnlia inasema kwamba wanapswa kuwa watu wenye kuheshimiwa na wengine. Biblia inaendela kusema kwamba kwanza wanapaswa kujaribiwa (10). Hii inamaanisha kwamba hawafai kuwa watu ambao wameokoka juzijuzi. Wao wanapswa kuonyesha kwamba ni watu ambao wanaishi maisha matakatifu.

6. Sura 3:15, tunsoma kwamba kanisa ni mahali ambapo ukweli kumhusu Kristo unahubiriwa na kufundishwa na kulindwa. Kwanza Paulo alikuwa ameonyesha jinsi watu wanapswa kuishi na jinsi wachungaji wanapswa kuchaguliwa katika kanisa.
7. Sura 4:1-5, tunaonywa kwamba tunapaswa kujilinda sana kutokana na mafundisho ya uongo kwa sababu kuna baadhi ya viongozi wa kanis amabao hawatafuata ukweli wa Biblia.

8. Sura 4:6-16, mchungaji mzuri anapaswa kufundishwa na Biblia. Ndipo tufundishe vyema Biblia tunapswa wenyewe tuwe tumejifunza vyema kabisa Biblia.

A. Mstari wa 7, Biblia inasema kwamba hatupaswi kufundisha chochote ambacho hakitoki katika Biblia. Kumbuka kwamba hatupaswi kuamini lolote kuhusu Mungu kama halijatoka katika Biblia. Tuna jukumu la kufundisha na kuhubiri tu kile ambacho kimetoka katika Biblia pekee. Haya nido maagizo ya Mungu kwetu.

B. Mstari wa 13, tunaagizwa kwamba kusoma Biblia mbele ya wengi na jambo zuri. Ni jambo zuri sana ikiwa kanisa litasoma Biblia kwa sauti wakati wa kuabudu siku ya Jumapili.

C. Mistari ya 15-16, tunasoma kwamba kiongozi wa kanisa anapaswa kufanya kile ambacho huwa anahubiri na wala hafai tu kusema maneno ambayo yeye mwenyewe hayazingatii. Ni lazima awe mfano kwa wale ambao anawaongoza.

9. Sura ya 5, tunafindishwa kuhusu majukumu katika kanisa.

A. Mistari ya 1-2, mchungaji anafundishwa kuheshimu na kuwapenda washirika wa kanisa kama tu watu wa familia yake.

B. Mistari ya 3-16, tunasoma kuhusu jinsi kanisa linapaswa kuwashughulikia wajane.

i. Kwanza kabisa kanisa linapaswa kuwajua kina anani ambao ni wajahe wa kweli. Hawa wanapaswa kuwa wale ambao hawana watu wakuwashulikia. Kumbuka kwamba ni kazi ya familia fulani au jamii fulani kushughulikia watu wake. Ikiwa hakuna watu wa jamii zao wa kuwashughulikia, basi kanisa linaweza kuwashughulikia (16). Je, ikiwa kuna watu wa jamii au familia ambao hawako tayari kuwashughulikia wajane hawa? Je, kanisa l;inapaswa kufanya nini? Kulingana na mawazo yangu, hawa watakuwa kama mayatima na kwa hivyo kanisa liwasaidie (Yakobo 1:27).

ii. Mstari 14, Biblia inasema kwamba ni vyema kwa mjane kuolewa. Mtu akimwoa mjane, ni sawa kabisa.

10. Mafundisho ambayo yanafuata yanafundisha jinsi ya kuwashughulikia wachungaji. 5:17, Biblia inasema kwamba wanapaswa kuheshimiwa na mstari wa 18, wanapaswa kulipwa ili wasikosa mahitaji yao ya kila siku. Kanisa linaweza kuwalipa wachungaji ikiwa linapesa. Ukweli ni kwamba kuna makanisa ambayo hayawezi kwa sababu yanapesa. Lakini hivyo kila mshirika anapaswa kujua kwamba ni jukumu lake kuona kwamba mchungaji wake anapata mahitaji yake ya kila siku. Hii ni amri kutoka kwa Mungu. Ni jambio zuri sana ikiwa kanisa litakuwa na mchungaji ambaye ni wa kila siku ambaye hahitaji kufanya kazi zingine ilia pate chakula cha kila siku.

A. Mistari ya 19-21, inazungumza juu ya kuleta mashitaka ya uongo juu ya mchungaji. Jmabo la kwanza ni, usileta mashitaka ya uongo juu ya mchungaji kama huna mashahidi. Pia hufai kumsengenya mchunagi wa kanisa lako. Nia au tabia juu ya viongozi wa kanisa lako inapaswa kuwa ya kuwasaidia.

B. Kumbuka kwamba wachungaji ni wenye dhambi na mstari wa 20, tunafundishwa kwamba pia wanapaswa kuadhibiwa wakati wananguka katika dhambi na wanakataa kutubu dhambi. Wao wanapaswa kuondolewa katika afisi ya uchungaji ikiwa wanakataa kutubu. Mstari wa 21, tunaonywa kwamba hatufai kufanya hili kwa sababu ya hisia zetu bali tunapaswa kuzingatia ukweli.

C. Tunaweza kuepuka shida nyingi katika kanisa ikiwa tutatumika kama vile mstari wa 22, unasema. Tunapaswa kuwa waangalifu katika kuwachagua viongozi wetu. Tunapaswa kuwachunguza na kuwa na muda wa maombi na kufunga kabla ya kuwachagua. Matendo 14:23 na 1 Timotheo 5:24 inasema kwamba tunaweza kuona dhambi za watu wengine kwa rahisi. Lakini wengine wanaweza kuficha kwa muda mrefu sana. Lazima tuwe waangalifu sana na wakati ambapo dhambi ipo lazima tuikemea na kuiadhibu vikali sana.

11. Katika sura 6:3-10, Paulo anamwambia Timotheo kwamba hafai kushirikiana na wale ambao wanahubiri mafundisho ya uongo na kuleta matatizo katika kanisa (2 Yohana 1:10-11).

A. Paulo anafundisha kwamba mojawapo wa nia ya walimu wa uongo ni kupata pesa. Mstari wa 7,unafundisha jambo ambalo wengi wanatapata vigumu kuamini. Mstari wa 8, tunafundidishwa kuwa watu ambao tumesheka. Mstari wa 9 unafundisha kwamba wale ambao wanatamani kuwa matajiri, huwa wananaswa na kujiletea maangamizi makubwa (mstari 10). Hii ni kwa sababu watu wengi kusudi lao katika maisha haya ni kutafuta utajiri kwa nguvu zao zote.

B. Hapa Paulo anazungumza na viongozi wa makanisa hapa. Ni wazi kwamba maneno yake ni kwa wachunagji wengi wa leo. Anawakemea wote ambao wanatumia makanisa yao kujitajirisha.

12. Katika mstari wa 11, Paulo anaendelea kuwafundisha viongozi wote wa kanisa kwamba hawafai kufundisha mafundisho ya uongo au kutumia nafasi zao katika kutafuta utajiri. Badala yake wanapaswa kutafuta utakatifu na kupigana vita vizuri vya kiroho.

13. Katika mistari ya17-19, Paulo anafundisha kwamba ni vyema kuwa tajiri ikiwa nia yako ya utajiri ni mzuri. Watu hawafai kuwa na kiburi wala kuweka imani yao katika pesa. Wanapaswa kujua kwamba utajiri unatoka kwa Mungu na kwa hivyo wanapaswa kuwa wakarimu na pesa zao. Kuna mfano wa mtu mmoja ambaye alianza kampuni ya katapila. Magari ambayo yanatumika katika kufanya kazi ngumu mno. Asilimia 90 ya mapato yake, aliyapeana kwa kazi ya kanisa na Mungu alimbariki sana.

2 Timotheo

Paulo aliandika barua ili aendelee kumhimiza Tomotheo. Paulo alijua kwamba kulikuwa na siku ngumu ambazo zlikuwa zinakuja na kwa sababu hiyo alitaka kuhimiza Timotheo na kanisa.
Paulo alikuwa gerezani kabla ya kuuliwa wakati alipoandika barua hii. Nero ndiye alikuwa kiongozi wa Roma nay eye alitesa wakristo sana.

1. jambo la kwanza tunalipata katika sura 1:5, tunaona kwamba nyanya na mama wa Timotheo walikuwa wameokoka. Wao ndio walimfunza Timotheo kumhusu Kristo. Kila mzazi ambaye ameokoka ana jukumu la kuwafundisha watoto wake kumhusu Mungu. Kwa mfano zaburi 34:11. Ikiwa wazazi hawatatekeleza jambo hili kwa uaminifu, basi ni wazi kwamba wao watatoa hesabu kwa nini walikataa kutii neno la Mungu. Ukweli ni kwamba mzazi hana nguvu za

kumwokoa mtoto wake, lakini anajukumu la kufundisha mtoto wake neno la Mungu akiwa mtoto. Wengi ambao wameokoka, utapata kwamba waliokoka wakiwa watoto wadogo.

2. Katika sura 1 paulo anaendelea kumhimi Timotheo.

A. Katika mstari wa 7, Paulo anafundisha kwamba hatupaswi kuwa watu ambao wanaogopa.

B. katika mstari wa 8, Paulo anaendelea kuwahimiza wakristo kwamba tunapaswa kusimama imara wakati wa mateso haswa wakati tunateswa kwa ajili ya imani yetu (1 Petro 4:12-16). Paulo anafundisha kwamba tunapaswa kumwamini Kristo atusaidie katika mateso ambayo tunayapitia.

3. Katika sura ya 2, Paulo anaendelea kuwahimiza watu kwamba wanapaswa kuendelea katika uaminifu hata wakati wanateseka. Katika mistari ya 3-4, anasema kwamba wale ambao tumeokoka sisi ni askari wa Mungu. Mateso yetu na upinzani ambao tunapata ni kwa sababu kwamba sisi tuko katika vita vya kiroho. Mstari wa 6-7, tunasoma kwamba kuna zawadi ya milele ikiwa tutavumilia hadi mwisho.

A. Katika 2 Timotheo 2:8-13, Paulo anawahimiza wachungaji kwamba wanapaswa kuvumilia mateso kwa ajili ya watu ambao wanawaongoza. Katika mstari 10, anasema kwamba yeye aliteseka kwa ajili ya kuhubiri injili ya Kristo na kwamba wachungaji wote wanapaswa kuwa tayari kuteseka kwa jaili ya wale ambao Mungu amewachagua kuokoka. Katika mistari ya 11-13, tunasoma kwamba sisi ambao tumokoka tumanapaswa kuteseka pamoja na Kristo ikiwa tunataka kuishi naye. Biblia inasema kwamba ikiwa tutamkaana, Yeye atatukana, onyo kubwa sana dhidi ya kuacha imani ya kweli na kufuata uongo. Katika mstari wa 13, ni mstari ambao unapaswa kutuhimiza sana. Mstari huu unatueleza kwamba wakati sisi tunakosa kuwa waaminifu, Yesu kila wakati Yeye ni mwaminifu. Kumbuka kwamba Kristo mwenyewe aliteseka kwa jili ya sisi. Yeye hakuulizi ufanye kile ambacho hajui.

4. Sura ya 3:1-14, intabiri mateso ya mstari wa 12, ya wakristo na wale ambao wanafundisha mafundisho ya uongo. Biblia inafundisha kwamba tunapaswa kutarajia mateso makali sana humu duniani. Pia tunapaswa kujua kwamba kutakuwa na walimu wengi wa uongo. Katika mistari ya 1-9, Paulo anafafanua hali kanisa katika mataifa mengi humu ulimwenguni.

A. Paulo anasema kwamba tunapaswa kuwa waangalifu sana kwamba wachungaji wetu wawe ni watu ambao wameokoka. Hatupaswi kuwa na ushirika na walimu au wachunagji ambao hawajaokoka. Hii inamaanisha kwamba ni lazima tuwachunguze wale wote ambao wanataka kuwa wachugaji. Tunaweza kufanya hii tukitumia Biblia. Ikiwa mtu anataka kuwa mchungaji

lakini maisha yake ni kinyume na mafundisho ya Biblia, basi mtu huyu hafai kamwe kuwa mchungaji.

5. Sura ya 3:16-17, ni mojawapo wa vifungu vya Biblia ambavyo vinajulikana sana wengi. Biblia kuanzia Mwanzo hadi kitabu cha Ufunuo, ni neno la Mungu, na kwa hivyo lafaa sana. Kusudi la sisi kusoma na kujifunza Biblia linafaa kuwa kukua katika utakatifu na kuishi maisha ambayo yanamtukuza Mungu. Kwa njia hii tutaweza kumtumikia na kumwabudu Mungu itupasavyo.

6. Katika sura 4, Paulo anaendelea kumwagiza Timotheo na wachungaji wote kwamba tunapaswa kuhubiri neno la Mungu kwa uaminifu kila wakti. Katika mistari ya 3-4, tunasoma kuhusu kanisa ya leo mahali ambapo watu wanataka kusikia ujumbe ambao unawapendeza na wala si ukweli kutoka kwa neno la Mungu kama kwamba tunapaswa kuvumilia mateso. Watu wanapenda kudanganywa na ujumbe ambao unawapendeza na wala si neno la Mungu. Kila wakati tunapaswa kuhubiri neno la Mungu kwa utukufu wa Mungu na wala si kumpendeza mwanadamu yeyote. Ikiwa tukihubiri neno la Mungu tutateswa na wanadamu, basi tunapaswa kuvumilia mateso hayo.
A. Katika mistari ya 6-8, Paulo anatuhimiza sana. Paulo alijua kwamba alikuwa anakaribia kufa nay eye alikuwa ametosheka kwamba kazi ambayo Mungu alikuwa amempatia alikuwa ameifanya kwa bidi na kwa uaminifu na kwa hiyo alikuwa tayari kuenda mbinguni. Baada ya tu kuandika barua hii, Paulo aliuliwa.

B. Katika mistari ya We see 9-18, tunaona jambo ambalo kila kiongozi anapaswa kuwa tayari kupitia.

i. Katika mistari ya 10 na 16, tunaona kwamba kila wakati tunapitia majaribu na wakati huo huwa tunahitaji usaidizi wa wakristo wenzetu, lakini huwa wanatuacha (Mathayo 26:31).

ii. Kulingana na mstari wa 14, kun ahata wengine ambao watakupinga na kukuhumiza.

iii. Mungu kila wakati atakuwa pamoja nasi, Yeye ameahidi kwamba hatawahi kutuacha kamwe. Kulingana na mistari ya 17 na 18, anasema kwamba atakuwa pamoja nasi hata wakati wa majaribu makali sana. Kila wakati tunapaswa kumtegemea Mungu.

Tito

Paulo aliandika barua hii miaki kadhaa kabala ya kuandika barua ya 2 kwa Timotheo. Paulo alikuwa anamwandikia Tito ambaye alikuwa kiomngozi wa kanisa. Paulo alisumbuliwa sana na

mafundisho ya uongio ambayo ilikuwa imeingia katika kanisa na ukose wa matendo mazuri katika maisha ya wale ambao walikuwa wamekiri Kristo.

1. Tito 1:5-9, Paulo anamwagiza Tito kwamba awaweka wachungaji. Yeye pia anampatia Tito maagizo kuhusu wachungaji wanapaswa kuwa watu wa aina gani. Mafundisho haya pia tuliyaona katika barua ya kwaza kwa Timotheo. Ni jambo la muhimu sana kwamba kanisa linakuwa na viongozi ambao wanamcha Mungu. Anasema kwamba kiongozi wa kanisa anapaswa kuwa mtu ambaye ana ushuhuda mzuri sana. Hili jambo ambalo aliliangazia tena katika 1 Timotheo. Mchungaji anapaswa kuwa mfano mwema kwa wengine. Katika mstari wa 9, anasema kwamba mchungaji anapaswa kuwa mtu mwaminifu kwa mafundisho ya Biblia na kuwa tayari kuyatetea mafundisho ya Biblia dhidi ya wale ambao wanayapinga.

A.Mistari ya 10-15, tunasoma kuwahusu maadui wa kanisa. Kanisa linahitaji wachungaji waaminifu kwa sababu wanapaswa kulilinda kanisa dhidi ya walimu wa uongo. Paulo anafafanua baadhi ya walimu wa uongo na mafundisho yao. Katika mistari ya 7 na 11, Paulo anafundisha kwamba walimu wa uongo wanafundisha kwa sababu wanapenda pesa. deal with the enemies facing the church and it's leaders. Wale ambao tumeokoka, tunafanya kazi ya Mungu ili tuendeleshe ufalme wa Mungu na wala si kwamba tujifaidishe.

B. Mstari wa 16, tunafundisha kwamba kuna wengi wa viongozi ambao wanakiri kwa vinywa kwamba wao ni wakristo, lakini mwenendo wa maisha yao ni tofauti kabisa na maisha ya ukristo.

2. Tito 2-3, tunapata maagizo kuhusu jinsi tunapaswa kuihsi maisha yetu. Tunapaswa kufanya matendo mazuri kwa sababu sisi tumeokoka na wala si kwamba matendo mazuri yatatuokoa.

A. Mistari ya 1-8, tunapaswa kuishi maisha yetu kama mfano kwa wengine haswa wazee. Katika mstari wa 14, tunapaswa kuwa na tamaa ya kutenda mema.

B. Tito 3:1, tunafundishwa kwamba tunapaswa kuwa wanaichi ambao wanaich ambao wanatii sheria za nchi.

C. Tito 3:10, tunafundishwa kwamba tunapaswa kuwaonya wale ambao wanataka kuleta migawanyiko. Na ikiwa atakataa kutubu, basi hatufai kuwa na ushirika nao kwa sababu wao wanataka kututenganisha. Tunafaa kulilinda kanisa.

Filemoni

Hii ni barua fupi sana ambayo Paulo aliandika kwa ajili ya mkristo ambaye hajakua katika wokovu. Onesimasi alikuwa mtumwa ambaye alikuwa amemwibia bwana wake na akatorokea Roma. Yeye alikutana na Paulo na akaokoka. Paulo alimshawishi Onesimasi kwamba alihitaji kurudi kwa bwana wake. Paulo aliandika barau kwa yule ambaye alikuwa bwana wa Onesimasi ambaye alikuwa Filemoni. Paulo alikuwa anamsihi kwamba amsamehe Onesimasi ambaye sasa alikuwa ameokoka. Hatujuia matokeo ya barua hii ya Paulo.

Barua ndio mwisho wa barua ya 13 za Paulo katika Agano Jipya. Katika barua hizi zote tunaon akwamba alianza kila wakati na salamu na kumaliza kwa kutakiana heri ambaye iliambata na baraka.

Waebrania

Mwandishi wa kitabu hiki hafahamiki. Kitabu kiliandikwa wayahudi. Kiliandikiwa kwa Wayahudi ambao walikuwa wameokoka na walikuwa wanahimizwa waendelee kuwa waaminifu na wasirudi katika tamaduni za Kiyahudi. Kuna mafundisho mengi ya muhimu katika kitabu hiki. Mojawapo wa mafundisho ni kuonyesha ukuu wa Kazi ya Kristo juu ya sadaka za Agano la kale.

1. Waebrania 1:1-4, tunasoma maneno ambayo pia yanapatikana katika Yohana 1:1-5, ambayo yanadhihirisha kwamba Yesu Kristo ni Mungu. Katika mstari wa 2, tunasoma kila kitu kiliumbwa naye. Mwandishi wa waebrania anasisitiza kwamba Kristo ni mkuu. Katika mistari ya 1-2, anazungumza jinis Mungu alivyozungumza kupitia kwa manabii, lakini sasa anazungumza nasi kupitia kwa Yesu kristo ambaye ni mwana wake. Wayahudi walifahamu sana maneno haya, “siku za mwisho” kwa sababu yalihusu siku za Mesiya.

A. Mistari ya 5-14, tunsoam kwamba Yesu kristo ni mkuu kuliko malaika ambao huwa wanamtumikia na wanatutumikia (mstari 6). Malaika ni watumwa wa Kristo (mstari 6). Katika 1 Wakorintho 6:3, tunasoma kwamba sisi wanadamu tutahukumu malaika.

2. Waebrania 2:1-8, tunasoma kuhusu malaika na uhusiano na wanadamu na Yesu. Tunajua kwamba katika mstari 14, malaika wanatutumikia na wanamtumikia Kristo. Katika Waebrania 2:7, tunasoma kwamba Yesu alifanyika kuwa chini kwa muda kidogo kama mwanadamu. Katika 2:2-3, kuna onyo kubwa sana kwetu. Hatufai kukutaa zawadi ya wokovu kutoka kwa Mungu, kwa sababu Mungu anaweza kuiondoa.

A. Mistari ya 9-18, tunasoma kwamba Yesu ni mwanadamu na ni Yeye ambaye anatuunganisha pamoja. Tunafaa kufahamu kwamba Yesu ni Mungu na pia ni mwanadamu. Katika mstari wa 13, tunasoma kwamba Yesu alishiriki mambo mengi nasi kama; alihisi njaa na pia alijaribiwa lakini

hakufanya dhambi. Ni kupitia kwa kifo cha Kristo nguvu za shetani ziliangamizwa, na katika mstari wa 15, tunasoma kwamba tumekombolewa kutoka kwa nguvu za shetani kupitia kwa kifo cha Kristo. Katika mstari wa 16, Yesu alikufa kwa ajili yetu wenye dhambi na wala si kwa ajili ya malaika. Malaika hawaokolewi kutoka kwa dhambi ni wanadamu.

B. Katika mistari ya 17-18, tunapewa sababu kwa nini Kristo alifanyika mwanadamu. Sababu hiyo ni kwamba sadaka yake kwa ajili ya dhambi zetu iweze kukubalika mbele za Mungu. Katika mstari wa 17 tunasoma kwamba sadaka hiyo ilikubalika na Mungu kwa ajili ya dhambi zetu. Kwa ufupi ni kwamba Yesu aliadhibiwa kwa ajili ya wale wote ambao wameokoka na wale ambao watakaookoka. Katika mstari wa 18, sadaka ya kristo ilikubalika na Mungu kwa sababu Yesu hakuwahi tenda dhambi yoyote hata kama yeye alijaribiwa kama sisi kwa kila namna (Waebrania 4:15). Yesu alikuwa mwanadamu kamili kama sisi. Pia yeye alikuwa Mungu kamili. Yesu hakutenda dhambi kama mwanadamu kwa sababu alichagua kumtii Mungu.

3. Waebrania 3:1-6, tunasoma kwamba Kristo ni mkuu kuliko Musa. Wayahudi wengi hawakufamu vyema uhusiano kati Musa na Kristo. Wao waliwaza kwamba Kristo alikuja kuwalazimisha watii sheria ya Musa. Wao walikosa kujua kwamba Kristo alikuwa mkuu sana kuliko Musa. Wao walikosa kujua kwamba Kristo ndiye alikuwa Mungu ambaye aliumba kila kitu. Mstari wa 5-6, tunasoma kwamba Musa alikuwa mtumishi mwaminifu wa Mungu lakini kristo Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Kila mchungaji anapaswa kujau kwamba yeye ni mtumishi na kwa hivyo anapaswa kuwa mwaminifu. Tunapaswa kujau kwamba Kristo pekee ndiye ametukuzwa na ametukuka na kwamba sisi sote tuko chini yake kama watumishi.

A. Mistari ya 7-19, ni onyo kwa wale ambao tumeokoka, kwamba hatufai kuwa na ufahamu tu kumhusu Kristo, bali tunapaswa kuishi maisha yetu kulingana na neno la Mungu. Kujua kwamba Kristo ni Mungu, kujua pekee haimwokoi mtu yeyote. Anapaswa kuwa Yeye ndiye Mungu wetu. Tunapaswa kuishi maisha maisha yetu tukimtumikia na kumwamini na kutii kila jambo ambalo anatuamurisha. Katika Mstari wa 19, tunasoma kwamba webgi wa Waisraeli hakuweza kuingia kanani kwa sababu wao hawakumwamini Kristo. Wao walimwamini Mungu lakini hawakuwa tayari kutii katika maisha yao ya kila siku.

B. Biblia inapewa tofauti ya imani yoyote na imani ambayo inaokoa. Imani ambayo inaokoa ni imani ambayo inamwamini na kumtegemea kristo pekee kwa ajili ya kuingia mbinguni na pia ni imani ambayo inadhihirika kwa matendo. Hili ni jambo ambalo tuntazungumzia zaidi katika kitabu cha Yakobo.

4. Waebrania 4, tunasoma kuhusu kuingia katika pumziko la Mungu jambo ambalo litamfanyikia kila mtu ambaye amemwamini Kristo. Onyo hapa kwetu ni kwamba tusikose kuingia katika pumziko hilo kama wale wengi wa Agano la kale ambao walikataa kutii.

A. Mstari wa 12, ni mstari ambao unajulikana na unazungumza kuhusu nguvu za neno la Mungu, yaani Biblia. Biblia ni neno la Mungu na kuna nguvu katika ujumbe wa Biblia. Chochote ambacho tunataka kujua kumhusu Mungu, kinapatikana katika Biblia. Wale wote ambao tumeokoka, tunapaswa kusoma na kuhubiri ni Neno la Mungu kwa uaminifu sana.

5. Waebrania 4-10, ni mafundisho kuhusu Kristo ambaye ni Kuhani mkuu.

A. Waebrania 4:14, tunasoma kwamba Yesu ni Kuhani wetu mkuu ambaye yuko mbinguni sasa. Yesu Kristo ndiye Kuhani mkuu wetu ambaye amekamilika kwa sababu Yeye alijaribiwa kama sisi lakini hakutenda dhambi. Kwa sababu hii, tumepewa uwezo wa kuja mbele za Mungu kwa sababu tumesafishwa na kufanywa wenye haki kutokana na sadaka ya Kristo kwa ajili yetu.

B. Waebrania 5:1-10, Kristo analinganishwa na kuhani wa kawaida ambaye alitoka katika kabila la Lawi na ambaye alitoa sadaka katika hekalu kwa ajili ya dhambi zake na za watu. Yesu alitoka katika kabila la Yuda na aliwekwa kuwa kuhani Mkuu na Mungu mwenyewe. Kulingana na mstari wa 9, sadaka ya Kristo alitosha kwa ajili msamaha wa dhambi zetu, kwa sababu Yeye hakuwa kama makuhani wengine ambao walihitaji msamaha kwanza. Yeye hakuhitaji msamaha kwa sababu hakuwa ametenda dhambi yoyote.

C. Mistari ya 11-14-waebrania 6, ni maneno ya kukemea wayahudi ambao walikuwa wameokoka. Wao walikuwa hawajakua kiroho na kwa sababu hii wao hawakuwa wanaishi kulingana na mafundisho ya Biblia. Kila mtu ambaye ameokoka, tunapaswa kusoma Biblia ili tuendelee kukua katika imani. Tunapaswa kuishi maisha ambayo yanadhihirisha kwamba kweli sisi tumeokoka.

D. Waebrania 6:4-6, ni onyo kwa wale wote ambao wanadai kwamba wao wameokoka ilhali wao bado. Onyo ni kwamba kwa sababu tunaenda kanisani na kuwa na uhusiano na wale ambao wameokoka, hilo halituokoi. Kuonja uzuri wa kristo haitoshi, tunapaswa kuishi naye kwa utiifu. Wakati watu wanarudi nyuma katika imani, wao huhukumiwa kabisa kwa sababu wamekataa kumwamini Kristo. Hii inamaanisha kwamba mtu kama huyu alijua mengi kuhusu kKristo, lakini alikataa kuokoka.

E. Waebrania 7, Kristo Yesu analinganishwa na Melchizedeki ambaye alikuwa kuhani. Tunajua kwamba huyu kuhani alikuwa mkuu kuliko Abrahamu kwa sababu ni yeye ambaye alimbariki

Abrahamu, na Abrahamu ndiye alitoa fungu la kumi kwake. Melchizedeki alikuwa kuhani na pia alikuwa mfalme wa Salemu, ambalo ndilo jina la mbeleni la Yerusalemu. Jina lake lilikuwa na majina mawili ya Kiebrania; Meleki ambalo linamaanisha mfalme na Zedeki ambalo lilimaanisha mwenye haki.

i. Mistari ya 13-28, tunasoma kuhusu ukuu wa ukuhani wa Kristo. Hii ni kwa sababu Ukuhani wa Kristo ni wa milele.

F. Waebrania 8, tunasoma kwamba Agano Jipya ni kuu sana kuliko lile la kale. Agano la kale lilihusu sana sheria na Agano Jipya linamhusu Kristo. Agano hili limewekwa mhuri na damu ya Kristo. Katikia mstari wa 1, tunasoma kwamba Agano hili ni la mbinguni na la kale ni la hapa duniani. Katika mstari wa 6, tunasoma kwamba Agano Jipya ni kuu sana na liko na ahadi kuu, kwa sababu hii, linaondoa lile la kale.

G. Chapter 9 compares Christ to the tabernacle. In other words, this chapter compares the New Testament or the new covenant with the Old Testament or the old covenant of the law. We see how much superior the new covenant is over the old.

i. Mistari ya 1, 11, 24, hema la kweli liko mbinguni mahali ambapo Mungu yupo.

ii. Mistari ya 7 na 12, tunasoma kwamba Agano Jipya ni la milele na kale hapana.

ii. Mistari ya 12, tunasoma kwamba katika Agano Jipya, dhambi zote zinasamehewa.

iii.Mistari 13-14, tunaambiwa kwamba sadaka za kuteketezwa za wanyama zilonsha tu nje ya mtu. Sadaka kuu ya Kristo inamfanya mtu awe safi kiroho na kutuleta mbele ya Mungu tukiwa wenye haki.

iv. Mistari ya 15-28, inazungumza kuhusu Agano Jipya na Kale. Agano la kale, ni Agano la sheria. Agano Jipya ni Agano la neema. Agano la kale halikuwa la milele, lakini Agano Jipya ni la milele. Sadaka kamilifu ya Kristo Yesu ndiyo sadaka ambayo ilihitajika.

H. Waebrania 10:1-25, tunasoma kwamba sadaka ya Kristo Yesu inatosha kwa ajili ya uondoleo la dhambi. Yesu alipokuwa msalabani, alizilipia dhambi za watu wake wote. Dhambi za wote ambao wanamwamini Kristo zimesamehewa kabisa.

I. Waebrania 10:26-39, ni onyo kwamba hatufai kukataa wokovu ambao tunapewa kupitia kwa Kristo Yesu tukiwaza kwamba kuna njia nyingine ya wokovu kando na Kristo. Msamaha kupitia kwa Kristo yesu ndio njia ya pekee ya wokovu. Katika mstari wa 26, tunaonywa kwamba tunapaswa kuupokea wokovu wakati ambapo tumesikia kwa sababu hakuna wokovu mwingine.

i. Mistari ya 27-31, Kuna hukumu kali sana kwa wale wote ambao wanamkataa Kristo. Mstari wa 31, ni sababu kwa nini tunapaswa kutii na kuokoka. Katika mstari 29, tunasoma kwamba kulikuwa na hukumu kali sana kwa wale ambao walikataa kumtii Musa ambaye alikuwa mwanadamu tu. Je, itakuwa hukumu kubwa ya aina gani ikiwa tunakataa kumtii Kristo ambaye ni Mungu mwenyewe.

6. Waebrania 11, ni sura ambayo inazingatia iamnai. Mstari wa 1, tunafundishwa imani ni nini. Imani ni kuamini kile ambacho hatukioni wala hatukikuzi kama kuwa na imani katika Kristo kwa ajili ya maisha ya milele. Sura inatuptia orodha ya watu katika Agano la kale ambao walikuwa waaminifu na ni vyema kutazama orodha hii kwa sababu inamafundisho mengi kwetu. Katika mistari ya 36-37, inazungumza juu ya jinsi wakristo wengi watakavyoishi maisha ya imani. Mistari hii miwili inafafanua kile ambacho kilifanyika na kile ambacho kitakachofanyika katika maisha ya wakristo wengin. Sisi sote ambao tumeokoka ni lazima tuwe tayari kuteseka n ahata kuuliwa kwa sababu ya imani yetu katika Kristo.

7. Waebrania 12, tunahimizwa kwamba tunapaswa kumtazama Kristo pekee.

A. Mistari ya 1-2, tumepewa mifano ya watu ambao waliishi maisha ya imani ili tujifunze kutoka kwao na tuishi pia maisha ya imani. Pia tunaagizwa tumwamini tu Kristo katika maisha yetu yote. Tunapaswa kuishi maisha yetu kama watu ambao wako kati mashindano yam bio. Kuna wale ambao wanaishi kwa muda mfupi wakiiga maisha ya wakristo lakini baada ya muda wao huacha imani ya kweli. Mkristo wa kweli ni mtu ambaye anamwamini Kristo Kristo amsaidide katika maisha yake yote hadi mwisho hata kama anapitia katika shida na majaribu mengi ya maisha yake. Katika mstari wa 3, tunajifunza kwamba tunapaswa kuwa wavumilivu hadi mwisho.

B. Mstari wa 4, tunapaswa kuwa tayari hata kujitolea kabisa katika vita dhidi ya dhambi. Ni imani katika Kristo ambayo itatusaidia kuvumilia katikam kila hali.
C. Mistari ya 5-13, kuna wakati ambapo tunateseka kwa sababu Mungu anatuadhibu kwa sababu ya dhambi. Adhabu ya Mungu ni ishara kwamba sisi ni wake. Soma Mithali 3:11-12. Ikiwa Mungu hakuadhibu kwa sababu ya dhambi ambayo unakataa kutubu, huenda wewe si wake.

D. Mistari ya 14-17, tunapswa kuishi maisha yetu kwa njia ambayo inaonyesha kwamba sisi ni wa Mungu na wala si wa ulimwengu. Tunapaswa kuwa na ushuhuda mzuri nah ii itawezekana ikiwa tutaishi maisha yetu tukimwiga Kristo. Hatuokoki kwa kutenda matendo mazuri, lakini

wokovu wetu unapaswa kudhihirika kwa matendo mazuri ambao msingi wa ni kristo katika maisha yetu.

E. Mistari ya 18-24, Agano la Kale na Jipya yanalinganishwa.

i. Agano la kale, si Agano lenye kutuhimiza kwa sababu halituleti karibu sana na Mungu. Katika mstari wa 21, tunasoma kwamba hili ni Agano la kutisha sana. Watu walitishwa kwamba watakufa ikiwa Mungu angezengumza nao (Kutoka 20:19). Wao walitishiwa kifo ikiwa hata wangeuguza mlima ambapo uwepo wa Mungu ulikuwa (kutoka 19:13).

ii. Katika mistari ya 22-24, tunasoma kwamba Agano Jipya linatuleta karibu na Mungu kupitia kwa kristo Yesu. Tunaelezwa kuhusu sherehe ya wale ambao wameokoka huko mbinguni. Agano Jipya linaleta furaha na kama si Agano la Kale. Katika Agano la kale, kuhani mkuu ndiye alikuwa mwakilishi kati ya watu na Mungu. Katika Agano Jipya tunaenda katika uwepo wa Mungu wenyewe kupitia kwa Kristo.

F. Sura hii inamalizikia katika mistari ya 25-29, tukihimizwa kwamba hatufai kupuuza onyo kutoka mbinguni, kwa sababu Mungu ambaye anatupatia onyo hizi, ni Mungu ambaye anahukumu vikali kabisa.

8. Waebrania 13:1-6, kitabu hiki kinamalizikia na amri nyingi ambazo tunapaswa kutii.

A. Mstari wa 3, tunasoma kwamba wakristo wote ni mwili mmoja, na wakati mmoja anateseka, huwa tunateseka wote. Kwa mfano ni wakati ambao mkristo anafungwa kwa sababu yeye ni mkristo. Hii ni kama sisi wenyewe tumefungwa na kuteswa. Katika hali hii, tunapaswa kufanya lolote tuwezalo ili kusaidia. Mara kwa mara kil ambacho tunaweza kufanya ni kuomba, na kwa hivyo tunapaswa kuomba wakati huo.

B. Mstari wa 4, tunaelezwa umuhimu wa kuwa na ndoa takatifu.

C. Mstari wa 5, tunasoma kwamba hatupaswi kuwa watu ambao wanapenda pesa, badala yake tuwe watu wenye kutosheka na kile ambacho Mungu ametupatia.

D. Mstari wa 6, tunahimizwa kwamba tunaweza kutii amri hizi zote kwa sababu Mungu ndiye anayetusaidia.

9. Mistari ya 7-17, kuna maagizo zaidi kwetu. Tunapaswa kufuata viongozi ambao ni waaminifu na wala si wale ambao wanafundisho mafundisho ya uongo. Mstari wa 8, unatuhimiza kwamba

tunapaswa kuendelea kumwamini Kristo kwa sababu Yeye huwa habadiliki kamwe. Mstari wa 16, tunahimizwa kwamba tunapaswa kutenda mema, kwa sababu kwa njia hii Mungu anatukuzwa.

10. Mistari ya 18-25, mwandishi anamalizia kitabu hiki kwa kutuhimiza kwamba tuwaombea viongozi wakristo ambao katika mstari wa 17, anasema kwamba tuwatii. Tuwe waaminifu katika kuwaombea viongozi wetu.

A. Mistari ya 20-31, kuna baraka kutoka kwa Mungu ambayo inapeanwa na watumishi wake. Maneno ya baraka hii yanatoka katika Biblia (mambo ya Walawi 9:22-23).

Kusudi kuu la kitabu cha Waebrania:

1. Kuonyesha ukuu wa kristo juu ya viumbe vyote; kama malaika na Musa.
2. Kuonyesha kwamba Yesu kristo ndiye kuhani Mkuu na kwamba Yeye ni mkuu kuliko makuhani wote.
3. Kuonyesha kwamba Agano Jipya ni kuu juu ya Agano la Kale.

Yokobo

Kitabu cha Yakobo, kimejawa na maagizo jinsi wakristo wanapaswa kuishi maiahs yao ya kikristo. Kitabu hiki kiliandikwa kwa wayahudi ambao walikuwa wameokoka na walikuwa wametawanyika ulimwenguni kote. Kusudi la kitabu hiki lilikuwa kuwahimiza wasomaji kuishi maisha yao kwa njia ambayo inafaa na wala si kuzungumza tu kuhusu wokovu. Kuna hekima sana katika kitabu hiki na maagizo ambayo yafaa kwa ajili ya kutenda mema. Ni kitabu kizuri ambacho kinaeleza maisha ya wale ambao wameokoka ni maisha ya aina gani.

1. Yakobo 1:1-8: tunasoma kuhusu majaribu, uvumilivu, hekima na imani.

A. Mistari ya 2-3 yote inaambatana. Mstari wa pili ni amri ambayo wengi hawaielewi. Mafundisho hapa ni kwamba Mungu huwa anaachilia majaribu katika maisha yetu ili atufundishe ukakamavu na tukue katika kiroho. Kwa sababu hii, Biblia inasema kwamba tunapaswa kuwa na furaha. Katika mstari wa 13, tunasoma kwamba Mungu huwa aachilii majaribu katika maisha yetu ili kutujaribu bali ni kwa sababu anataka tuwe watu bora kioroho.

B. Mistari ya 5 na 6, tunasoma kwamba tunafaa kumwomba Mungu atupatie hekima ili tuweze kumwamini katika kila jambo kila wakati. Tunapaswa kuomba Mungu atuongoze na kwa ujasiri tufanye uamuzi wa kufanya yale ambayo anatuamrisha.

2. Yokobo 1:9-18: tunaosma kuhus utajiri, majaribu na kuzaliwa mara ya pili.

A. Mistari ya 9-11, tunasoma kwamba hatufai kujivuna kwa sababu ya utajiri ambao tuko nao kwa sababu utajiri si wa milele. Hata ndugu ambaye ni maskini ana sababu ya kufurahi kwa sababu hatima yake ni mbinguni.

B. Mstari wa 12 unafundisha kwamba mtu ambaye anapinga na kustahimili majaribu ni mtu ambaye amebarikiwa sana na Mungu.

C.Mistari ya 13-15, tunasoma kuhusu majaribu. Mungu huwa hataujaribu. Shetani huwa anatumia tamaa zetu mbaya za dhambi kutuongoza katika dhambi. 1 Wakorintho 7:15 inafundisha kwamba ni shetani ambaye huwa anatujaribu na dhambi. Mungu hutujaribu ili imani yetu idhihirike kwamba ni ya kweli kama jinsi tunavyosoma katika Mwanzo 22 Abrahamu alipoambiwa kwamba kumtoa mwanawe isaki kama sadaka (Pia soma Kutoka 20:20).

i. Ufafanuzi mzuri wa majaribu ni kwamba mtu anakuwa na nafasi ya kufanya dhambi, wakati huwa pia akiwa na uhuru wa kuchagua kutofanya dhambi hiyo.

ii. Pia ni wakati ambapo muda anahimizwa na shetani kwamba afanye dhambi. Mungu huwa hatujaribu kwa njia hii.

iii. Mtu anaweza kufanya uamuzi atende dhambi au asifanye. Hatuwezi kumlaumu yeyote kwa ajili ya dhambi zetu, kwa sababu huwa ni chaguo letu kufanya dhambi.

D. Mstari wa 17, tunasoma kwamba tunapata kila kitu kizuri kutoka kwa Mungu.

3. Yakobo 1:19-27, tunapata maagizo mengine zaidi.

A. Mistari ya 19-21, tunafundishwa kwamba tunapaswa kuwa watu wenye kiasi jambo ambalo tulifundishwa katika wagalatia 5:23, hili ni tunda la Roho Mtakatifu.

B. katika mistari 21-25, tunapaswa kuonyesha imani yetu kwa matendo yetu. Tunapaswa kufanya kile ambacho Biblia inafundisha na wala si kuzungumza tu kuhusu kile ambacho Biblia inafundisha. Dhihirisha imani yako kwa jinsi unapaosihi maisha yako kama, jinsi unapaowasaidia wengine, kutumika katika kanisa na jinsi unaposhughulikia maswala ya pesa.

C. Mistari ya 26-27, tunaosma kuhsu dini ya kweli. Tunasoma kwamba ikiwa mtu hawezi kudhibiti ulimi wake, basi dini yako ni bure. Ulimi ambao haudhibitiwi ni hatari sana na jambo hili Yakobo atalizungumzia tena katika sura ya 3 na 5. Tunasoma kwamba dini ya ukweli ni ile ambayo inazaa matunda ya kiroho na wal si maneno matupu.

4. Yokobo 2:1-13, tunasoma kuhusu dhambi ya kuonyesha upendeleo katika kanisa. Ni jambo la kawaida katika makanisa mengi ambao washirika wanashughulikiwa vitafauti kabisa kulingana na hali yao ya maisha. Tunapaswa kukumbuka kwamba machoni pa Kristo wale wote ambao wameokoka ni watu sawa. Yule ambaye ameokoka na ni maskini ni wa muhimu sana kama tu yule ambaye ni tajiri na ameokoka. Wote ni wa muhimu machoni pa Mungu. Wote ni watu muhimu sana machoni pa Mungu.

5. Yakobo 2:14-26, tunasoma kwamba imani ambayo inaokoa ni imani ambayo inazaa matendo mazuri. Ikiwa kweli mtu ameokoka, yeye atafanya matendo mazuri. Imani ambayo inaokoa ni imani ambayo iko hai na wala haijakufa.

A. Tunaona mifano kadhaa ambayo inaonyesha kwamba imani ambayo inaokoa ni imani ambayo inaonekana katika maisha ya mtu.

i. Mistari ya 15-16, ni vibaya kusema kwamba unajali ikiwa husaidii haswa kama uko na uwezo wa kusaidia. Hatufai tu kusema kwamba tutamwombea mtu lakini hatuko tayari kuwasaidia kutatua hitaji ambalo wako nalo ikiwa tuko na uwezo wa kusaidia.

ii. Mara tatu (17,20,26), Yakobo anasema kwamba kusema tu kwamba umeokoka lakini matendo yako haya dhihirisha jambo hilo ni ishara kwamba imani yako imekufa.

iii. Katika mstari wa 19, yakobo anaonyesha kwamba hata mapepo yanamini kwamba Mungu yupo lakini hayataokoka.

B. Ni jambo la muhimu sana kukumbuka kwamba tunaokolewa kwa imani pekee katika Kristo na wala si kwa matendo yetu mazuri (Waefeso 2:8-9).

C. Tunapaswa kukumbuka kwamba Mathayo 7:21-23, tunaonywa kwamba tunapaswa kujichunguza kuona kwamba kweli tuko katika imani.

D. Hili ni fundisho muhimu sana kwamba huenda katika makanisa mengi kuna wengi ambao hawaendi mbinguni. Kuna wengi ambao hawafanyi lolote kuhusu iamni yao isipokuwa kuhudhuria kanisa siku ya Jumapili. Biblia ni wazi kwamba ni lazima tuwe na imani ya kweli

ikiwa kweli tutaokolewa. Ikiwa kila mtu ambaye anadai kuwa mkristo angekuwa mkristo wa kweli, basi ulimwengu pangekuwa mahali pazuri sana.

6. Yakobo 3:1-12, Yakobo anataja ulimi. Kuna mafundisho ya muhimu sana kuhusu hatari ya ambayo ulimi unaweza kuleta.

A. Mstari wa 1, unatupatia onyo kuhusu majukumu ya kufundisha. Wale ambao tunafundisha tunapaswa kufahamu umuhimu wa kazi hii. Tunaweza kumwongoza mtu karibu na Mungu an awe mbali sana na Mungu na aende jahanum. Walimu wanapaswa kuwa tayari kufundisha na ni lazima tuombe Mungu aongoze kila neno ambalo tunalitumia katika kila fundisho. Neno moja baya linaweza kuleta madhara mabaya sana.

B. Tunasoma mambo mengi sana kuhusu ubaya wa ulimi. Tunasoma kwamba Ulimi ni chombo ambacho ni hatari sana. Maneno kutoka kwa midomo yetu yanaweza kuwaumiza wengine vibaya sana. Maneno ndio chanzo cha migawanyiko ya kanisa na mafarakano. Mistari ya 9-10, tunasoma kuhusu matumizi mazuri ya ulimi. Tunapaswa kutumia ndimi zetu kwa kumsifu Mungu na kuwajenga wandugu katika Kristo.

7. Yakobo 3:13-18, mistari hii inahusu hekima.

A. Katika mstari wa 14, yakobo anazungumza kuhusu baadhi ya mambo mabaya ambayo watu wanayafanya kama kuwa na wivu, ubinafsi, majivuno na kusema uongo. Mstari wa 15, anasema kwamba hii inadhirisha kwamba hekima kama hii inatoka kwa shetani.

B. Mistari ya 17-18, mistari inazungumza kuhusu matendo mazuri ambayo yanatokana na hekima mzuri ambayo inatoka kwa Mungu. Tunapaswa kupata hekima kutoka kwa Mungu na tunaweza kufanya hivi kwa kumwomba Mungu atuongoze katika njia za hekima.

8. Yakobo 4, ni sura ambayo ikon a mambo mengi mazuri ya kuzingatia.
A. Jambo la kwanza ambalo tunaliona hapa liko katika mistari ya 1-2. Kutamani mali ya watu wengine hulata madhara makubwa sana. Amri ya mwisho katika mari 10 inasema kwamba tunapaswa kutosheka na kile ambacho Mungu ametupatia na hatufai kutamani mali ya mtu mwingine.

B. Mstari wa 3 unasema kwamba maombi yetu huwa hayajibiwa kwa sababu huwa tunaomba tu mambo ya ulimwengu. Tunapaswa kufahamu kwamba maombi yetu yanapaswa kuhusu ufalme wa Mungu na wala si tamaa zet.

C. Mistari ya 4-10, mistai hii inarudia kile ambacho Yesu alisema katika Mathayo 6:24, kwamba hatuwezi tukawatumikia mabawana wawili wakati mmoja. Mungu anapaswa kuwa wa kwanza katika maisha yetu. Tunapaswa kumpenda yeye kwanza. Tunapaswa kuchagua kumfurahisha Mungu halfa mambo mengine baadaye. Hatufai kutafuta kutosheleza tamaa zetu.

D. Mistari ya 11-12, kwa mara ya tatu, Yokobo anazungumza kuhusu hatari ya ulimi.

E. Mistari ya 13-17, tunakumbushwa kwamba kila mipango yetu inapaswa kumhusu tu Mungu na mapenzi yake. Ni dhambi kuwaza kwamba sisi ndio tunatawala na wala si Mungu.

8. Yakobo 5, tunapata mafundisho mengine ya muhimu sana.

A. Mistari ya 1-6, hatufai kuishi maisha yetu kwa sababu ya kupata utajiri bali tunapaswa kuishi kwa ajili ya Mungu na kutosheka kile ambacho Mungu ameleta katika maisha yetu. Mstari wa 4 unazungumza kuhusu dhambi kuwa matajiri kutokana na kuwaibia wengine na kwamba Mungu anachukia jambo hili sana.

i. Mstari wa 5, tunasoma kuhusu matajiri ambao wanajifurahisha katika vitu ambavyo wavipata kwa kuwadhulumu wengine. Katika Biblia, Mungu anawaonya wote ambao wanawadanganya wengine ili wapate utajiri. Ninakumbushwa kuhusu hadithi ya Lazaro na tajiri katika Luka 16:19-31. Ni vyema kuwa majiri bora utajiri wetu hautokani na njia za dhambi na pia haturuhusu utajiri huo uendeshe maisha yetu. Tunapaswa kutumia utajiri wetu kumtumikia Mungu.

B. Mstari wa 12, tunasoma tena kuhusu ulimi. Tunapaswa kutumia ulimi wetu kwa njia mzuri. Tunapaswa kutumia ndimi zetu kusema ukweli. Sisi ambao tumeokoka tunapaswa kujulikana kama watu ambao wanasema ukweli. Verse 12 again talks about the tongue.

C. Yakobo 5:13-18, ni sehemu ambayo inahusu kuomba.

i. Katika mstari wa 13, tunasoma kwamba tunapaswa kuomab wakati wamateso. Pia tunapaswa kwamba tunapaswa kumsifu Mungu wakati mambo ni mazuri.

ii. Mistari ya 14-15, wakati tumegonjeka, tunapaswa kuwaita wachungaji wa kanisa watuombee. Kumbuka kwamba ni Mungu ambaye anaponya si wale ambao wanaomba. Pia zingatia hili kwamba hakuna pesa ambayo inalipwa kwa wachungaji wakati wanakuja kuombea.

iii. Mstari wa 16, tunapaswa kutoa hesabu wenye kwa wenye. Ni jambo zuri ikiwa tuna mtu ambaye sisi wenyewe tunaweza kueleza yale ambayo tuyapitia, dhambi zetu na kuomba pamoja.

iv. Mistari ya 17-18, tunapewa mfano wa umuhimu wa maombi. Maombi ya wale ambao wameokoka ni yafaa sana na ni yenye nguvu sana.

D. Mistari ya 19-20, tunaelezwa kuhusu kuwarejesha ndugu katika ushirika wa kanisa ua kuwaongoza wale ambao hawajaokoka kwa Kristo. Tunaona kwamba kuna baraka katika kufanya hili.

1 Petro

Brau hii ya waraka wa kwanza ya Petro aliandikiwa wakristo ambao walikuwa wametawanyika ulimwenguni kote. Kusudi la barua hii ni kuwahimiza wakristo hawa kuvumilia mateso ambayo walikuwa wanayapitia. Patro alihubiri kinyume na wengi leo ambao wanahubiri injili ya afya mzuri na mali ya ulimwengu huu. Katika marua hii tunajifunza kwamba sisi ambao tumeokoka, tutapata mateso mengi katika ulimwengu huu. Lskini pia wakati huo tujue kwamba neema ya Mungu inatutosheleza.

1. 1 Petro 1, paetro anaenleza yeye ni nani: Mtume ambaye alikuwa pamoja na Kristo.

A. 1 Petro 1:4-5, inahimiza sana. Tunasoma kwamba urithi wa wale ambao tumeokoka ni wa milele na umelindwa kwa nguvu za Mungu. is encouraging.

B. Kuanzia mistari ya 6-9, paetro anafundisha juu ya mateso. Huu ni ujumbe ambao Petro ameurudia mara 16 katika barua hii. Kuna mafundisho mengi juu ya mateso katika Agano Jipya kwa sababu Mungu anataka tuwe tarari wakati mateso hayao yanakuja kwetu. Wale ambao wanafundisha kwamba mtu akiwa ameokoka hafai kuwa mgonjwa au kukosa pesa ni ujumbe wa uongo kabisa.

i. Kuna sababu ya kuteseka kwetu. Mstari wa 7, mateso hudhihirisha ukweli wa imani yetu. Tunapaswa kukumbuka kwamba Mungu kila wakati upo upande wetu. Yeye habadiliki hata wakati mambo ni mabaya katika maisha yetu.

C. Mistari ya 10-12, mistari inaeleza kwamba hata manabii hawakuelewa vyema kazi ya wokovu ambao tumefunuliwa kupitia kwa kristo Yesu. Manabii walikuwa na ufahamu lakini si wote kuhusu wokovu ambao ulikuwa unakuja kupitia kwa Kristo Yesu.

D. Mistari ya 13-21, inahusu jinsi tunapaswa kuishi maisha yetu tukimsifu Mungu. Tunakumbushwa katika mstari wa 18-19, kwamba tumenunuliwa kwa damu ya thamni ya Kristo Yesu.

E. 1 petro 1:22-2;10, tunakumbushwa kwamba tuna majukumu manne katika uhusiano wetu na wakristo wengine.

A. Katika mstari wa 22, tunapaswa kupendana kwa kweli, si kwa maneno pekee, lakini hata kwa matendo.

B. Katika mstari wa 2:2, tunapaswa kukua kiroho. Tunaweza kufanya hii kwa kusoma Biblia kila wakati kwa uaminifu sana. Mstariwa 1, tunaambiwa kwamba jkuna dhambi 5 ambazo tunapaswa kuziacha ikiwa tutaweza kukua kiroho.

C. Mstari wa 3, wale ambao tumeokoka ni makuhani matakatifu ambao tumepewa uwezo wa kutoa sadaka za kiroho kwa Mungu. Kulingana na mwandishi mmoja ambaye aliitwa Albert barnes, tunaweza kujitoa kwa Mungu; nafsi na miili kama sadaka ya maisha ambayo inakubalika kwa Mungu; maombi yetu na sifa zetu na matendo mema tunayoyafanya kwa imani; yanatoka na upendo kwa Mungu na tamaa ya kumtukuza.

D. Kulingana na mistari ya 9-10, tunapaswa kutangaza ukweli kumhusu Kristo. Tunafanya hii kwa sababu sis ni watu wake (mstari wa 9). Sisi ni watu wa Mungu ambao tumechaguliwa na kwa sababu tumehurumiwa, tunapaswa kutangaza huruma huu kwa wengine.

3. 1 Petro 2:11-17, tunasoma kwamba tunapaswa kuwashughulikia watu wote sawa. Tunapaswa kuwa na ushuhuda mzuri kila wakati. Tunapaswa kuwatii viongozi wetu.

4. 1 Petro 3:1-7, tunasoma kuhusu uhusiano wa mke na mume.

A. kwanza wake ambao wameokoka wanapaswa kuwa na mwenendo ambao utawavutia waume wao ambao hawajaokoka, ili watamani kuokoka. Hivi pia ndivyo waume ambao wameokoka wanapaswa kuishi maisha yao na wake ambao hawajaokoka (1 Wakorintho 7:13). Lakini tukumbuke vuema kwamba hawa ambao Petro anazungumza nao ni wale ambao walioana wakiwa wote hawajaokoka. Halfa kwa neema ya Mungu mmoja anaokoka. Ikiwa wewe umeokoka, hupaswi kumwoa mtu ambaye hajaokoka Biblia inakataa kabisa (1 Wakorintho 6:13, 19-20).

B. Mstari wa 7, tunafundishwa kwamba sisi wanaume tunapaswa kuishi na wale wetu kwa njia ya heshima (Waefeso 5:25-31). teaches that we men are to treat our wives in a very good way or our relationship with God will be impaired.

5. 1 Petro 3:8-4:6, ni mafudisho kwetu jinsi tunapaswa kuishi maisha yetu.

A. Petero 3:3-11, tunahimizwa kufanya mambo fulani fulani.

B. Petro 3:13-14, biblia inauliza swali je, ni nani atakaye tudhuru ikiwa tunafanya yaliyo mema? Ikiwa tunafanya yaliyo mema, hatutarajii kuumizwa. Lakini pia tukumbuke kwamba tunaweza kuteswa kwa sababu ya hayo mazuri ambayo tumefanya, kwa sababu hii hatufai kuogopa. Mungu atatubariki kwa sababu yay ale mazuri tumefanya kwa ajili ya utukufu wake. Baraka hiz ni kwa wale ambao wameokoka.

C. Katika mstari wa 17, tunasoma kwamba tunapaswa kufanya mazuri hata kama inamaanisha kwamba tutateswa kwa sababu ya kufanya mazuri. Mstari wa 17 unatukumbusha kwamba hata Kristo aliteseka.

D. Mistari ya 20-21, wengi hawaelewi. Maji ya ubatizo ni ishara kwamba tumekufa kwa dhambi na sasa tume fufuka pamoja na Kristo milele.

6. 1 Petro 4:7-11, tunasoma kwamba tunapaswa kila wakati kuwa tayari kwa ajili Yesu anakuja wakati ambao hatujui. Pia anatupatia maagizo jinsi tunapaswa kuihsi maisha yetu tukisubiri kuja kwa Kristo Yesu. Soma maagizo hayo.

7. 1 Petro 4:12-19, tunapata mafundisho mengi kuhusu mateso ya wakristo.

A. Mstari wa 12, tufundishwa kwamba tujitayarishe kuteseka.

B. Mstari wa 14, tunasoma kwamba wale tumeokoka, tumebarikiwa sana na Mungu kwa sababu tuko ndani ya Kristo.

C. Mistari ya 15-16, tunapaswa kuhakikisha kwamba mateso yetu si kwa sababu ya dhambi amnazo tumefanya, bali mateso yanafaa kuwa kwa sababu sisi ni watoto wa Mungu. Tunapaswa kumtukuza Mungu wakati wa mateso. Tunaweza kufanya hivi ikiwa Mungu atatupatia nguvu. Hii inamaanisha kwamba ni lazima tuombe.

D. Mstari wa 19, tuteseka kwa sababu ni Mungu ambaye amekusudia hivyo nas kwa sababu hiyo, lazima tuwe wenye kiasi na tuvumilie mateso yetu kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

8. 1 Petro 5:1-4, ni maagizo jinsi wachungaji wanapaswa kufanya kazi yao. Tunapaswa kuwasaidia wale ambao Mungu ametupatia kwa kuwaongoza katika njia sawa kwa ajili ya uzuri wao kiroho. Kumbuka kwamba washirika wa kanisa si mali ya Mchungaji, bali ni mali ya Mungu. Kwa hivyo hatupaswi kuwatumia kwa njia ambayo ni ya kujifaidisha wenyewe. Mstari wa 2 unasema kwamba tyfanye kazi ya ucvhungaji si kwa sababu ya upendo wa pesa. Mstari wa 3 unasema kwamba tunapaswa kuwa wanyenyekevu na kuwa mfano katika kila jambo. Kuongoza kwetu kusiwa kule kwa kuwafanya washirika kuwa watumwa wetu. Tunapaswa kufanya kazi tukitarajia taji letu ambalo Mungu atatupatia ikiwa tumefanya kazi kwa uaminifu.

9. 1 Petro 5:5-11, tunafundishwa jinsi tunapaswa kuwaheshimu wachungaji wetu. Sisi sote tunapaswa kuwa na nia sawa na tunapaswa kuwa wanyenyekevu. Biblia inafundisha kwamba tunapaswa kuwaheshimu wale ambao ni wazee kwa miaka (mambo ya walawi 19:32).
A. Biblia inatuhimiza kwamba hatufai kuwa na wasiwasi (Mathayo 6:25-34). Katika 1 Petro 5:7, tunasisitiziwa ukweli huu. Hatuna sababu ya kuwa wasiwasi, badala yake tunapaswa kumwamini Mungu atushughulikie.

B. Mistari ya 8-9, tunakumbushwa kwamba shetani anafanya kila kitu kuona kwamba hatufanikiwi, kwa sababu hiyo tunapaswa kumpinga. Tunapaswa kuvaa vazi la sila za Mungu. Katika mstari wa 9 tunaona tena kwamba wakristo tutakumbana na mateso katika ulimwengu huu.

B. mstari wa 10, mateso haya ni ya muda mfupi sana kwa sababu Mungu atatuchukua na kutupeleka mbinguni karibuni. Mbinguni hakuna mateso au shida au kilio.

2 Petro

Petro aliandika barua ili kuonya kanisa dhidi ya mafundisho ya uongo. Yeye anahimiza wakristo kwamba tunapaswa kukua katika imani kwa sababu kwa njia hii tutaweza kujilinda kutokana na walimu wa uongo. Petro aliandika barua muda mfupi kabla ya kuuliwa kwake.

1. 2 Petro 1:1-11, tunafundishwa kwamba njia bora ya kulinda kutokana na walimu wa uongo ni kuhakikisha kwamba tunasoma Biblia. Tunaona jambo hili katika mistari ya 2,4,5,6,8.

2. Mistari ya 12-18, anaonyesha upendo wake kwa wachungaji wa kweli. Wakati yeye alijua kwamba alikuwa karibu kufa. Tunaona hili katika mistari ya 13-15, anasema kwamba anataka

kuhakikisha kwamba wakati yeye anakufa, wasirika wa kanisa wataweza kujilinda kutokana na walimu wa uongo. Mchungaji wa kweli ni mtu ambaye anawajali sana watu ambao anawachunga na wala si yeye wenyewe.

A. Mistari ya 16-18, Petro anatuhakikishia ukweli wa ujumbe wake kwa kutueleza kwamba Yeye alikuwa pamoja na Kristo wakati Kristo alibadilishwa sura.

3. Mistari ya 19-21, Petro anaeleza kuhusu wapi unabii wa kweli ulitoka. Katika mstari wa 20, anasema kwamba unabii wa kweli hautoki kwa mwanadamu bali anasema katika mstari wa 21 kwamba unabii wa kweli unatoka kwa Mungu Roho Mtakatifu ambaye anamwongoza mwanadamu kuandika au kunena maneno ya Mungu. Kwa ufupi ni kwamba unabii wa kweli unatoka kwa Mungu pekee. Biblia indio unabii wa kweli kutoka kwa Mungu na wale wote ambao wanahubiri Biblia kwa kweli, wao pekee ndio waaminifu ambao wanazungumza neno la Mungu.

4. 2 Petro 2:1-3, Petro anaonya kwamba kutakuwa na mafundisho ya uongo. Anasema kwamba walimu hawa wa uongo watafundisha uongo, ambao wanakana Mungu. Mstari wa 1 unasema kwamba walimu hawa watajiletea maangamizi kwa sababu ya mahubiri yao ya uongo. Mstari wa 3 unasema kwamba moja wa sababu za walimu hawa kufundisha uongo ni kwamba waweze kujifaidisha kwa pesa nyingi. Mwalimu wa kweli huwa anaongozwa kufundisha kwa sababu anampenda Mungu na si kwa sababu anapenda pesa. Yeye huwa anaamini kwamba Mungu atamzawadia kutoka mbinguni. Walimu wa uongo wote wanaelekea jahanum. Mwalimu wa uongo ni mtu ambaye anafundisha kuhusu Mungu, lakini mafundisho yake hayatoki kwa Biblia. Mwalimu wa uongo ni yule ambaye anafundisha kutoka kwa Biblia pekee.

5. 2 Petro 2:4-9, tunasoma kwanza jinsi Mungu alivyowaadhibu wenye na malaika hapo awali. Pia anaendelea na kusema kwamba Mungu aliwaokoa pia wale ambao walikuwa ni wenye haki hapo awali. Katika mstari wa 9, Petro anasema kwamba Mungu abado anaendelea kuwaokoa wenye haki na kuwaadhibu wenye dhambi. Wale ambao tumeokoka, tunapaswa kufarijiwa na ukweli kwamba Mungu atatuokoa kutoka kwa majaribu yote. Mstari wa 9, pia unasema kwamba hakikika wale ambao hawajaokoka, Mungu atawahukumu.

6. Katika mistari ya 10-18, Petro anasema kwamba matendo ya wale ambao hawajaokoka ni mabaya sana kiwango kwamba wanastahili hukumu.

A. Mistari ya 10-13, ansema kwamba hawa walimu wa uongo wanatenda dhambi zao kwa ujasiri mkubwa sana ambao hata malaika ambao ni wenye nguvu kuliko wanadamu wanaogopa kufanya dhambi hizo. Hawa watu ni wenye kibuir na wanastahili hukumu ya Mungu.

B. Kuanzi mstari wa 14, Petro anataja dhambi ambazo hawa wanafurahia kufanya. Katika mstari wa 17, tunasoma kwamba Mungu amewawekea nafasi huku jahanum.

7. Katika mistari ya 19-22, Petro anawafunua hawa walimu wa uongo. Anasema kwamba hawa watu ni wale ambao walikuja karibu sana na ufalme na walionekana kuwa ni watu ambao wameokoka, lakini wao walikataa kuokoka. Katika makanisa mengi kuna watu wengi ambao wanajua mambo fulani fulani kumhusu Yesu, lakini ukweli ni kwamba wao hawajaokoka. Tunasoma kuwahusu hawa watu katika Matendo ya Mitume 20:29. Hawa ni wale ambao wanakuja katika makanisa yetu na kuwaongoza watu mbali na Mungu.

8. 2 Petro 3:1-9, Petro anazungumza na walimu wa uongo ambao wanakana kwamba Yesu hatarudi tena. Petroa ansema kwamba hii ni kwamba katika mawazo yao, Yesu amekawia kurudi kwa sababu hii wao wanasema kwamba hatarudi.

A. Mstari wa 8, tunasoma kwamba ufahamu wa Mungu kuhusu wakati ni tofauti sana na ufahamu wetu sisi wanadamu. Mara kwa mara ni jambo gumu kwetu kusubiri wakati ambapo Mungu anafanya jambo, hadi wakati Mungu mwenyewe analifanya.

B. Katika mstari wa 9, tunaona sababu ya kuchelewa kwa kurudi Kristo Yesu. Mungu ni Mungu mwenye huruma na anataka watu wake wote watubu na waokolewe.

9. Mistari ya 10-14, tunapewa onyo kwamba uvumilivu wa Mungu si wa milele, na kwa sababu hii, tunapaswa kuhakikisha tuko tayari kabla ya Kristo kurudi. Mstari wa 10, tunasoma kuhusu siku ya Bwana ambayo itakauwa siku ya hukumu kali ya Mungu kwa wale wote ambao hawajaokoka. Hii ni siku ambayo itafika bila mtu yeyote kujua. Ikiwa watu hawataokoka kabla ya Kristo kurudi, akirudi mlango wa mbinguni utafunhwa na hakuna mtu ambaye ataweza kuokoka tena. Wakati wa kuokoka ni sasa.

10. 2 Petro 3:15-18, Petro anatunnya kwamba tuwe waangalifu juu ya wale wote wanaugeuza ukweli wa Biblia kwa ajili ya manufaa yao wenyewe. Kila wakati tunafaa kusoma Biblia na moyo ambayo unataka kufundishwa. Tunapaswa kuwa na tamaa ya kujifundisha kile ambacho Mungu anasema na wala si kusoma kwa anjia ambayo tunataka tamaa zetu zitoshelezwe. Kwa mfano kuna wengi ambao wamesoma Mwanza 9:25-27 vibaya. Wao wanasema kwamba watu waafrika wamelaaniwa na kwa hivyo ni vyema hata kama wao wadharau na kuwatumia vibaya. Hii ndio sababu katika ulimwengu kuna wengi ambao wanawanyanyasa kwa miaka nyingi sana. Biblia haitupatii ruhusa wa kumdharau au kumnyanyasa mtu yeyote.

A.Katika mstari wa 17, petro anatuonya kwamba tunapaswa kuwa waangalifu sana ili tusiongozwe vibaya. Katika mstari wa 18 anatuhimiza kwamba tukue katika neema na kumjua Kristo zaid. Njia bora ambayo tunaweza kujilinda nayo dhidi ya walimu wa uongo ni kusoma na kutii Biblia. Tunapaswa kuhakikisha kwamba wale ambao wanatufundisha Biblia, wanafundisha kwa uaminifu sana kile ambacho Biblia inafundisha. Ikiwa mwalimu yeyote si mwaminifu katika mafundisha ya Biblia tunapaswa kumweleze awache kufundisha. Ikiwa atakataa, basi tuondoke na tusiendelee kumsikiza mwalimu wa uongo.

Barua za Yohana-Yuda

Mtume Yohana aliandika barua hizi wakati alikuwa anafika mwisho wa maisha yake duniani. 1 Yohana iliandikwa ili kulinda kanisa dhidi ya walimu wa uongo. Hawa walimu wa uongo walidai kuwa na hekima ambayo waliongeza juu ya mafundisho ya Biblia. Wao waliamini kwamba mwili wa mwanadamu ulikuwa na sehemu mbili. Wao waliamini kwamba dhambi ilikuwa tu katika mwili na kwamba nafsi ya mtu ilikuwa tu imejawa na mambo ya Mungu. Wao waliamini kwamba mwili wa mtu angefanya lolote unataka. Wao waliwaza kwamba ni kupitia kwa hekima yao mtu alipata kuwa kiroho. Wao pia waliamini kwamba Yesu hakuwa mwanadamu.

1. 1 Yohana 1:1-4, anaanza kama jinsi alivyoanza injili Yohana. Katika mstari wa 1, tunasoma kwamba yesu ni wa milele. Mstari wa 2 tunasoma kwamba Yesu alikuwa mwanadamu. Yesu alikuwa na mwili wa kawaida wa mwanadamu. Fundisho hili lilenga walimu wa uongo ambao walikuwa wanakataa kwamba Yesu si mwanadamu. Kama yesu hakuwa mwanadamu kamili, basi Mungu Baba hangekubali sadaka yake kwa ajili ya dhambi zetu.

2. 1 Yohana 1:5-10, tunasoma kuhus nuru ya Mungu na dhambi za ulimwengu.

A. mstari wa 5, tunasoma kwamba Yesu ndiye nuru ya ulimwengu na kwamna ndani mwake hamna giza lolote.

B. Katika mstari wa 6, Yohana anasema kwamba ikiwa tutaendelea katika dhambi, hatuwezi kamwe kuwa na ushirika Yesu. Hii inamaanisha kwamba hatuwezi kamwe kuchagua kuendelea katika dhambi ikiwa sisi ni wake. Kila wakati tunapaswa kuepeuka dhambi kwa sababu sisi ni wa Kristo.

C. Mistari ya 8 na 10, tunafundisho kwamba bado ndani mwetu mna dhambi na wakati moja au mwingine tunatenda dhambi. Lakini mstari wa 7 unasema kwamba damu ya Kristo itaendelea

kutusafisha kutoka kwa dhambi. Biblia inasme akwamba ikiwa mtu anasema kwamba yeye hana dhambi, basi ni mwongo na ukweli wa Biblia haumo ndani mwake.

D. Mtu ambaye ameokoka, kila wakati anahuzunika kwa sababu ya dhambi zake na wakati huo anatubu kwa kweli. Mstari wa 9, tunahakikishiwa kwamba tutasamehewa na Mungu ambaye ni mwaminifu. Yeye anatuonsha kutoka na uchafu wa dhambi.

3. 1 Yohana 2:1-17, tunasoma kuhusu kutembea katika dhambi na giza.

A. Ujumbe katika mstari wa 1, ni kwamba mkristo atafanya lolote awezalo kuona kwamba hatendi dhambi na tunavyoendelea kukua katika ukristo, pole pole tutaendelea kuacha dhambi na kumtukuza Kristo zaidi na zaidi. Hii haimainishi kwamba dhambi itakuwa imeondoka kabisa. Ikiwa tutatubu, Mungu ambaye ni mwaminifu atatusamehe.

B. Mstari wa 2, tunapata neno sadaka. Hii inamaansia kwamba adhabu ya Mungu kwa Yesu msalabani iliondoa hasira ya Mungu. Kwa sababu hii Mungu alikubali sadaka hiyo kwa ajili ya dhambhi zetu. Yesu mslabani alilipia dhambi za wale ambao wameokoka na wale ambao Mungu atawaokoa. Mtu ambaye anakataa kuokoka, Mungu atamwadhibu vikali sana jahanum kwa sababu ya dhambi zake.

C. Mistari ya 3-6, tunafundishwa kwamba tunaonyesha upendo kwa Mungu wakati tunatii neno lake. Hii inaonekana wazi kabisa wakati tunaishi maisha yetu kulingana na neno la Mungu.

D. Mistari ya 9-11, tunasoma kwamba wale ambao wameokoka, wanapaswa kupendana na tunapaswa kufanya kazi pamoja. Hii haimaanishi kwamba hatuwezi kuwa na kutoelewana. Kutakuwepo lakini, pia kutakuwa na kupatana kwa sababu tunapendana.

E. Katika mistari ya 12-14, Yohana analisifu kanisa kwa ajili ya ushindi wao dhidi ya dhambi za kale na kwa ajili ya uhusiano wao mzuri na Mungu.

F. Mistari ya 15-17, tunafundishwa kwamba hatufai kuwa na upendo wa dunia. Hatufai kunaswa na upendo wa vitu vya ulimwengu kama pesa, tamaa mbaya na kiburi. Kwa sababu mambo haya yote ni ya juda tu. Mambo mzuri kutoka kwa Mungu ni ya milele.

4. Sehemu ambayo imebaki ya surah ii, inashughulika na mpinga Kristo na wale ambao hawamo katika ufalme wa Mungu.

A. Neno Mpinga Kristo ambalo linapatikana na mstari wa 18, linapatikana katika barua za Yohana pekee. Hatupati mafundisho wazi kabisa kuhusu ishara za mpinga Kristo. Huenda sababu Yohana hakufafanua ni kwa sababu wasikilizaji wake walifahamu vyema alikuwa anazungumza kuhusu nani.

B. Jambo moja ambalo tunaweza kujifunza nalo ni kwamba siku za mwisho ambamo tunaishi, kutakuwepo na wengi ambao watampinga Kristo. Hii inadhihirishwa wazi kutokana na mafundisho mengi ambayo yanafundishwa na yanampinga Kristo.

C. Mistari ya 19 na 24, tunasoma kmhusu mtu ambaye amekuwa katika kanisa kwa muda mrefu na alijifunza mengi kumhusu Mungu. Lakini mgu huyu hakuwa ameokoka na kwa sababu hii, ukweli ambao alisikia haukumfaidi. Huyu mtu hakuwa ameongzwa na Roho Mtakatifu. Yeye alishawishiwa lakini alikataa. Mtu anapaookoka, mstari wa 20 na 27, roho Mtakatifu anakuja na kuihsi ndani mwake. Roho Mtakatifu anamlinda mtu huyu kutokana na mafundiaho ya uongo na pia kwamba hatawahi kumkaana Kristo.

D. Mstari wa 28, tunahimizwa kwamba tunafapaswa kuendelea kuwa waaminifu kwa Kristo Yesu. Mstari 29, tunasoma kwamba watu ambao ni wenye haki ni wale ambao wamepokea haki yao kutoka kwa Kristo Yesu. Kufanywa wenye haki mbele za Mungu ni zawadi ya bure kutoka kwa Yesu Kristo.

5. 1 Yohana 3:4-10, tunasoma kuhsu haki. Yohana anasisitiza sana kuhusu dhambi.

A. Mstari wa 6, mtu ambaye anaendelea kuchagua dhambi, yeye hajaokoka.

B. Mstari wa 8, tunasoma kwambaq yeyotwe ambaye anaendelea kutenda dhambi yeye ni wa shetani.

C. Mstari wa 9, tunasoma kwamba mtu ambaye amezaliwa na Mungu haendelei na tabia dhambi.

D. Linganisha 1 Yohana 1:8 na mstari wa 10 ambayo inasema kwamba ikiwa tutasema kwamba hatuna dhambi, ukweli haumo ndani mwetu.

Maneno yafuatayo yanukuliwa na katika kitabu cha Halley's Bible handbook kurasa ya 812. Je tunawezaje kufafanua kwamba mtu ambaye amezaliwa na Mungu haendelei katika tabia ya dhambi ilhali biblia pia inafundisha kwamba ikiwa tunasema kwamba hatuna dhambi ukweli haumo ndani mwetu? Je, kuna tofauti gani kati ya kwamba sisi ni wadhaifu, dhambi ambayo

tunaifanya kwa kupenda na tabia ya dhambi? Ni kweli kwamba mtu ambaye ameokoka anaweza kuanguka katika dhambi. Klakini hata wakati anaanguka katika, hapotezi wokovu wake. Katika kuandika kwake, Yohana anaweza kuwa alikuwa na watu fulani katika mawazo yake haswa walimu wa uongo kama Jezebeli katika Ufunuo 2:20, ambao wanadai kuwa na ushirika na Mungu na wakati huo huo wanaendelea katika tabia ya uzinzi.

Mtu ambaye ameokoka, yeye anaweza kuanguka katika dhambi, lakini si tamaa yake kwamba atende dhambi. Tamaa yake ni kuepuka dhambi kila wakati. Mtu ambaye hajaokoka anaweza kuendelea katika dhambi kwa muda mrefu sana. Lakini baada ya kuokoka, yeye hatakuwa mtu ambaye anatamani dhambi kwa sababu hii dhambi itaanza kumwachilia. Yeye sasa atakuwa na tabia ambayo si kuendelea katika dhambi kinyume na yule ambaye hajaokoka. Tamaa ya moyo wake itakuwa kwamba hataki kufanya dhambi tena.

6. 1 Yohana 3:13-24, na 4:7-21, tunasoma kuhusu upendo.

A. Mstari wa 13, tunasoma kwamba ulimwengu haupendi kanisa. Ulimwengu unachukia sana kanisa la Kristo. Hii inatusaidia kufahamu kwa nini wakristo wengi wanateswa ulimwenguni kote. Kila wakati tuanchukia na wale ambao si wakristo.

B. Mistari kadhaa katika kifungu hiki inatukumbusha kwamba upendo ni mojawapo wa ishara ya kuwa mkristo. Katika 4:12, biblia inasema kwamba ikiwa tunapendana wakristo kwa wakristo, Mungu anaishi ndani mwetu. Ikiwa huna upendo kwa wengine, 4:20, Biblia inasema kwamba wewe hupendi Mungu.

C. Upendo kati yetu unapaswa kudhihirika kwa matendo. Yakobo 2:14-18, inatufundisha kuhusu upendo ambao ni wa kweli. Ni lazima tusaidiane.

D. 1 Yohana, katika sehemu nyingi tunafundishwa kwamba hata kama tumeokolewa kwa neema ya Mungu, tuna jukumu la kumtii Mungu.

i. Soma 2:3, 2:4, 3:22, 3:23, 3:24, 4:21, na 5:3, na utaona umuhimu wa kumtii Mungu.

7. 1 Yohana 4:1-6, tunasoma kuhusu walimu wa uongo.

A. Mstari wa 1, tunasoma kwamba kuna walimu wenginwa uongo ulimwenguni na kwamba kila mmoja wetu ana jukumu ya kuwatambua.

B. Mstari wa 2, tunaweza kusema ni nani mwalimu wa kweli kulinagana na mafundisho yake. Mwali wa kweli ataleta ujumbe wa kweli kumhusu Mungu ambao unapatikana katika Biblia. Kila mkristo ana jukumu la kuhakikisha kama ujumbe wa mwalimu au mhubiri unatoka kwa Biblia. Hili ndilo jambo ambalo Musa alisema katika Kumbukumbu la Torati 18:22.

C. Mistari ya 4-5, ni wale ambao hawajaokoka ambao wanasikiliza ujumbe ambao hautoki kwa Mungu. Wale ambao tumeokoka tunasikiliza tu ule ujumbe ambao unatoka kwa Biblia ambao unapatikana katika Biblia.

8. 1 Yohana 5, ni sura ambayo inazungumza kuhusu hakikisho la wokovu. Mara kumi katika barua hii Yohana anatumiza neno twajua, ujue au jua kutuhakiksihia kwamba tunaweza kuwa na uhakikka kwamba tumeokolewa. Tazama 2:3, 2:5, 3:2; 3:14, 3:19, 3:24, 4:13, 5:13, 5:15, na 5:19.

A. Katika 5:4-8, kwamba wakristo tunaamini katika Mungu wa Utatu; Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu na kwamba wote wanashuhudia kumhusu Kristo.
B. Mistari ya 9-13, Mungu anatuhakikishia kwamba wote ambao watamwamini Mwanawe Kristo, watapata uzima wa milele na hawatawahi kupoteza uzima huo.

C. Mstari wa 16, tunasoma kuhusu dhambi ambayo haitasamehewa ambayo tulisoma kuhusu katika Mathayo. Hii ni dhambi ya kukataa kutubu na kumwamini Kristo Yesu.

2 Yohana

Barua ina sura moja tu na kuna mambo mawili ambayo ninataka kusisitiza.

1. Mistari ya 1-4, tunasoma neno ukweli mara tano.

A. mstari wa 1, tunasoma kwamba tunapaswa kupenda kwa kweli. Hii inamaanisha kwamba tunapaswa kupenda kwa ukweli na wala si kujifanya.

B. Mstari wa 1 pia unasema kwamba tunapaswa kujua ukweli ambao unapatika katika Biblia pekee.

C. Mstari wa 2, tunasoma kwamba wakristo ni watu wa ukweli na kila wakati tunapaswa kuishi maisha yetu kwa ukweli.

D. Mstari wa 3, tunasoma kwamba neema, huruma na Amani kila wakati mambo haya yatakuwa pamoja nasi.

E. Mstari wa 4, tunasoma kwamba wakristo ni watu ambao wanatembea kwa ukweli. Kila wakati ni lazima tuseme ukweli.

2. Mistari ya 5-6, tunahimiza kwamba ni lazima tupendane kama tu vile Kristo alisema katika Marko 12:31. Mstari wa 6, tunasoma kwamba ni lazima tumtii Mungu na kwamba hii ni amri kutoka kwa Mungu. again order us to love one another just like what Jesus said in Mark 12:31.

A. Katika mistari ya 7 na 8, tunaona kwamba katika ulimwengu huu kuna wapinga Kristo wengi. Tunapaswa kujilinda kabisa kutokana na walimu hawa wa uongo ili wasitatize mwenendo wetu na Kristo. Ikiwa tutatembea kwa karibu sana na Kristo tutazawadiwa na Mungu. Kwa sababu hii hatufai kukubali mafundisho ya uongo itutatize.

B. Tena tunaona hatari ya mafundisho ya uongo. Mungu anataka ahakikishe kwamba tunalindwa vyema kabisa dhidi ya mafundisho ya uongo kwa sababu ni mafundisho ambayo yanaleta maangamizi.

C. Mstari wa 9, tunasoma kwamba uhusiano wetu na Mungu unategemea mafundisho kumhusu Mungu ambayo tunapaswa kuzingatia kabisa. Ikiwa neno la Mungu haliishi ndani mwetu, basi ni wazi kwamba Mungu haumo ndani mwetu pia. Ikiwa tuna neno la Mungu ndani mwetu, pia Mungu yumo ndani mwetu.

ii.Katika mstari wa 10, tunasoma kwamba ikiwa mwalimu wa uongo anakuja kwetu tusimkaribishe wala kumsalimia. Tunapaswa kumfukuzia mbali. Mungu anatakutulinda kutokana na walimu wa uongo.

3 Yohana

Hii barua fupi mno ambayo imejawa na maagizo mengi sana.

1. Mistari ya 2-4, ni ombi. Mtu Yohana anaombea Gayo kwamba Mungu atamfanikisha katika kila sehemu ya maisha yake. Yohana aliombea afya yake ya kiroho na kimwili. Mchungaji wa kweli anawajali watu wake. Yeye hana wivu wakati anawaona wanafunzi wake wakiendelee vyema katika maisha yao, badala yake Yeye anafurahia.

2. Katika mistari ya 5-8, tunasoma kuhusu kukua kwa Gayo kiroho. Tunasoma kwamba yeye aliwashughulikia watu wa Mungu. Tunafundishwa hapa kwamba tunapaswa kuwasaidia kifedha wale ambao wanafanya kazi ya Mungu. Mfano ni mtu ambaye anataka kutumika katika nchi nyingine. Kanisa la kristo linapaswa kujitoa na kusaidia ili kazi ya Mungu endelee. Mfano mwingine ni mchungaji ambaye anajitoa kuchunga kondoo wa Mungu. Usaidizi katika kazi ya Mungu, unatufanya tuwe washirika katika kazi hiyo.

3. Mistari ya 9-10, tunaonywa kuhusu shida fulani ambayo inajitokeza mara kwa mara katika kanisa. Kuna watu kama Deotrefe ambao wanapenda kuleta mafarakano katika kanisa. Wakati mwingi watu kama huwa hawajaokoka na huwa wanaweka tamaa zao mbele badala ya kanisa. Watu kama hawa huwa na kiburi sana. Uongozi wa kanisa kila amara wanapaswa kuwa waangalifu sana juu ya watu kama hawa kwa ajili ya kulilinda kanisa. Ni lazima nidhamu ya kanisa itekelezwe kwa ajili ya kulinda kanisa na kumrejeshe yule katika ushirika ambaye ameanguka katika dhambi.

4. Mstari wa 11, ni shauri kwetu kwamba tutenda mema. Tunaona kwamba mtu ambaye anatenda mema, ni yule ambaye ameokolewa na Mungu. Lakini mtu ambaye anatenda maovu hafai kuwa mmoja wa kanisa.

Yuda

Kitabu kingine kifupi ambacho kinaendeleza mafundisho kuhusu walimu wa uongo.

1. Yuda anaanza kuandika katika mstari wa 1 na anamalizia katika mstari wa 24 akituhakikishia kwamba wokovu wetu ni wa milele. Yule ambaye ameokoka, hawezi kamwe kupoteza wokovu wake. Katika mstari wa 1 anasema kwamba wale ambao wameokoka wamewekwa kwa ajili ya Kristo Yesu. Katika mstari wa 24, anasema kwamba wale ambao tumeokoka Yesu atatulinda na kutuepusha na kumkana na atatuleta kwa Mungu Baba bila doa au makossa yoyote.

2. Katika mistari ya 3-4, anasema kwamba sababu ya kuandika ni kwamba anataka kuwaonya wasikilizaji wake kuhusu walimu wa uongo ambao wako moongoni mwao. Anasema kwamba hawa walimu wa uongo wamejipenyeza ndani mwao. Hili onyo kwetu kwamba lazima tuwe waangalifu kuwahusu wale ambao wanadai kuwa watu wa Mungu, baada ya kuwaamini, wao hubadilika na kuanza kufundisha mafundisho ya uongo. Kuna madhehubu nyingi ambazo hazihubiri ukweli, mwanzoni wao huonekana kuwa watu wazuri ambao wanahubiri Kristo, lakini unapochunguza utapata kwamba wao ni waongo ambao hawazingatii neno la Mungu kamwe. Kwa mfano kuna wale ambao wanajiita kanisa la Kristo la siku za mwisho (Mormons). Hawa mwanzoni wao huonekana kuwa watu wazuri hadi unapochunguza na kufahamu msimamo wa

mafundisho yao ndipi ututambua kwamba wao ni waongo. Kinga bora dhidi ya watu kama hawa ni Biblia, tudumu katika mafundisho ya kweli ya Biblia.

3. Mistari ya 5-7, tunasoma kuhusu adhabu kali ya Mungu kwa wale wote ambao wanaendelea kuasi dhidi ya Mungu.

4. Mistari ya 6-16, kuna aina tofauti za uasi. Hizi ni rahisi kufahamu. Mstari wa 9, ni mojawapo ya mistari ambayo hatuelewi vyema.

5. Mistari ya 17-25, Yuda anamalizia baraua hii kwa kutupatia jinsi tunapaswa kujilinda kutokana na mafundisho ya uongo. Hatufai kuchangazwa na walimu wa uongo, bali kila wakati tunapaswa kuwa tayari kuwapinga.

A. Yuda anapena mambo matatu ambayo yatatufanya tulindwe kutokana na mafundisho ya uongo.
1. Katika mstari wa 20, anasema kwamba tunapaswa kujengwa katika imani takatifu. Tunafanya hivi kwa kusoma Biblia ili walimu wa uongo wasiweze kutudanganya.

2. Katika mstaro wa 20, anasema kwamba tuombe kwa Roho Mtakatifu. Katika Waefeso 6:18 tunaagizwa tuombe kwa Roho Mtakatifu kama njia moja ya kumpinga shetani. Haya ndio maombi ya mkristo kwa sababu tuna Roho Mtakatifu ndani mwetu, Yeye hutusaidia kuomba (Warumi 8:26).

3. Katika mstari wa 21, tunahimizwa kwamba tunafaa kujiweka katika upendo wa Mungu. Tunafanya hili kwa kuwa karibu sana na Mungu wakati tunasoma Biblia, tunaomba, tunakutana pamoja kuabudu na kumaliza muda na wakristo wengine. Pia kujitoa katika kazi na mambo ya Mungu.

4. Mstari wa 21, tunahimizwa kwamba tutegemea huruma wa Mungu ambao unatuongoza katika maisha ya milele. Tunapaswa kuishi maisha yetu tukijua kwamba tunaajibika mbele za Mungu na kwamba wakati wowote tunaweza kufa na kusimama mbele ya Mungu na kuhukumiwa.

B. Mistari ya 23-25, tunahimizwa kwamba tunapaswa kuwahurumia sana wale ambao hawajaokoka. Tunafanya hivi kwa kuwahubiria Kristo na kuwaongoza kwa kristo ili wapate msamaha wa dhamnbi zao.

Ufunuo

Kitabu hiki kiliandikwa na mtume Yohana. Sura ya 1:1, tunaambiwa kwamba kitabu ni ufunuo wa Kristo Yesu. Kitabu hiki kiliandika kuhimiza kanisa la Kristo. JMada ya kitabu hiki ni ushindi mkuu wa Yesu Kristo na kanisa dhidi ya shetani na malaika wake. Yohana aliandika kitabu hiki akiwa katika kisiwa cha Patmo. Kuna kutokubaliana kwingi mingoni mwa wakristo wengi juu ya ujumbe wa kitabu hiki. Hatutasoma mstari kwa mstari kwa sababu masomo yetu ni jumla. Kwa sababu kila mtu anapaswa kujitoa kukisoma kitabu kwa kina sana.

Kuna mambo mengi sana mabyo tunaweza kujifunza kutokana na kitabu cha ufunuo. Kwa mfano maada kuu ni ushinda wa Kristo dhidi ya uovu wote. Shetani na wafanya kazi wake wote watashindwa milele na Mungu. Maada nyingine ni kwamba kuna watu wa aina mbili; kuna wale ambao wameokoka na wako katika ufalme wa Mungu na wale ambao hawajaokoka ambao wako upande wa shetani. Wale ambao wameokoka ndio wao wambao wataishi na Mungu milele. Ni ukweli kwamba maisha ya wokovu si rahisi kwamba ya mateso ambayo tunayapitia kila wakati. Lakini hata hivyo, tunapaswa kuvumilia kwamba kuna zawadi huko mbinguni kwa ajili ya uaminifu wetu. Wale ambai hawajaokoka, ambao ni wa shetani, watakuwa jahanum milele.

1. Ufunuo 1:1-3, ufunuo wa Kristo Yesu. Tunasoma katika mstari wa 1 kwamba kitabu hiki kinahusu maisha ya mebeleni. Katika mstari wa 10, tunasoma kwamba ni Yohana ambaye alikuwa aandike mambo haya ambayo yalikuwa yametukia. Katika mstari wa 1, tunasoma kwamba ujumbe ulipewa Kristo na Mungu Baba na Yesu aliupatia malaika ampatie Yohana.

A. Mstari wa 3, kuna baraka ambazo zinaandiwa kwa wale wote ambao watasoma na kusikiza na kutii mafundisho ya kitabu hiki. Mara kwa mara huwa ninashanga kwa nini kitabu hiki hakisomwi katika makanisa mengi. Neno la Mungu linafaa kuwa msingi wa ibada zetu. Tunapaswa kuwa na wakati ambapo neno la Mungu linasomwa kando na mahjubiri bila kuongeza maneno yoyote juu yake.

2. Mistari ya 4-8, Yohana anayasilimia makanisa saba ambayo lakini katika eneo la Asia. Wakati wa Yohana, mahali ndipo Uturuki ya sasa. Hapa kulikuwa na makanisa mengi sana. Dini ya ukristo ndyo ilikuwa kubwa hapa. Leo ni dini ya Kiislamu.

Tutazama mafundisho muhimu ya kitabu hiki.

Tunasoma, “aliyeko, aliyekuwako na atakayekuja.” Hapa tunasisitiziwa kwamba Mungu ni wa milele.

1. Ashiye milele na milele (4:10).

2. Bwana Mungu, aliyekuwa, aliyeko na atakayekuja (4:8).

3. Alfa na Omega, Mwanzo na mwisho (1:8, 21:6 and 22:13).

4. “Mimi bi Alfa na Omega,” asema Bwana Mungu, “aliye, aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi” (1:8).

5. “Mimi ni Kwanza na wa mwisho. Mimi ni yeye aliye hai, niliyekuwa nimekufa na tazama, ni hai milele na milele! Name nianzo funguo za mauti na kuzimu” (1:17-18).

Tunaishi katika ulimwengu ambapo kila kitu kinabadilika. Hapa tunakumbuhswa kwamba Mungu huwa habadiliki, Yeye ni wa milele. Hili ni jambo la kutuhimiza kwa sababu tunajua kwamba Mungu ambaye tunamtegemea habadiliki kamwe na tunaweza kuendelea kumwamini kila wakati kwa ahadi zake. Ukweli utatusadia wakati tunateswa kukumbana na mateso hayo. Mungu huwa anatupatia hali ya wakati tunaingi mbinguni kwamba hatutakufa tena na hatutabadilika tena milele.

Kristo ndiye Mfalme wa wafalme wa ulimwenguni wote (1:5). Wafalme wa dunia watakufa na mamlaka yao yote itaisha. Kama vile mwandishi mmoja aliandika, hawa wafalme ambao ni wakatili na wauaji na wezi, wote wataangamia jahanum wasipotubu. Kristo Yesu ndiye anatawala ulimwengu wote.

Ambaye ametuweka huru kutoka katika dhambi zetu kwa damu yake(1:5).

1. “kwa damu yako (Kristo) ukamnunulia Mungu watu” (5:9).

2. “Nao wakamshinda (Shetani) kwa damu ya Mwana-kondoo” (12:11).

3. “Hawa ni wale waliotoka katika ile dhiki kuu, nao wamefua mavazi yao katika damu ya Mwana-Kondoo na kuyafanya meupe kabisa” (7:14).

4. “wamebarikiwa wale wafuao mavazi yao, ili wapate haki ya kuuendea huo mti wa uzima” (22:14).

Hapa tunaona wazi kwamba tunaokolewa kupitia kwa damu ya Kristo Yesu.

Utukufu na Uwezo vina Yeye milele na milele Amen (1:6).

1. “Bwana wetu na Mungu wetu, wewe umestahili kupokea utukufu na heshimu ba uweza” (4:11).

2. “Anastahili Mwana-Kondoo, yeye aliyechinjwa, kupokea uweza na utajiri na hekmi na nguvu na heshima na utukufu na sifa”(5:12).

3. “Sifa na heshima na utukufu na uweza ni vyake yeye aketiye juu ya hicho kiti cha enzi na kwa Mwana-kondoo, milele na milele” (5:13; 7:10, 12).

4. “Matendo yako ni makuu…njia zako ni za haki na kweli, Mfalme wa milele (15:2-3).

5. Kuna furaha kubwa sana mbinguni kwa sababu Yesu Kristo anatawala. Tunapaswa kufurahia pia na kumpa Kristo utukufu wote (19:1-7).
Wazee 24 na viumbe 4 (5:4-14), mamilioni ya malaika na umati mkubwa wa wale wote ambao wameokolewa, wanapaza sauti zao na kumsifu Mungu. Hivi tunapswa kufanya kama kanisa leo. Tunapaswa kuongoza makanisa yetu yamsifu Mungu kwa furaha. Sifa hizi zinapaswa kuwa kwa ajili ya utukufu wa kristo na wala is kwa kujifurahisha wenyewe. Hivi ndivyo tutakuwa tunafanya huko mbinguni.

Anakuja kwa mawingu

1. Kila jicho litamwona hata wale ambao walimwumiza (1:7).
2. “lakini shikeni sana mlicho nacho, mpaka nitakapokuja (2:25).
3. “Nitakuja kama mwivu” (3:3).
4. “Nitakuja upesi. Shika sana ulicho nacho, ili mtu asije akaichukua taji yako” (3:11).
5. “Tazama, naja kama mwivi! Amebarikiwa yeye akesheya” (16:15).
6. “Tazama, naja upesi! (22:7).
7. “Tazama naja upesi! Thawabu yangu I mkononi mwangu!”(22:12).
8. “Hakika naja upesi” (22:20).
9. “Amen, Njoo Bwana Yesu. (22:20).

Kuna unabii moja ambao tunaweza kutabiri na huu ni kwamba Kroisto Yesu anarudi kwa sababu Biblia inafundisha hivyo. Yesu Kristo atakuja bila kutarajiwa kama mwizi. Kwa sababu hii ni lazim tujitayarishe kwa sabau tusipojitayarisha, akija hakuna mtu ambaye ataweza kujitayarisha. Kila wakati ni lazima tuwe tayari.

Turudi sasa kwa Ufunuo 1

1. Ufunuo 1:9-20, tunasoma kuhusu Kristo na kanisa lake.

A. Mstari wa 10, tunasoma kuhusu maoni ya Yohana ambayo yananukuliwa hadi katika mstari wa 20. Maoni haya yanatufundisha kwamba Kristo ni mwenye nguvu zote. Yeye atarudi kwa nguvu za ushindi.

i. Mstari wa 13, Yesu Kristo amevaa mavazi ya kuhani mkuu wa Agano la Kale. Hii ni kwa sababu Kristo Yesu ndiye kuhani wetu mkuu.

ii. Kulingana na mstari wa 20, Malaika wako mikononi mwake.

iii. Mstari wa 14, tunasoma kwamba nywele yake ni nyeupe kama sufu, theluji; macho yake ni kama mwali wa moto.

iv. Mstari wa uso wake ni kama jua kali linaling'aa kwa nguvu zake zote.

v. Kutoka katika kinywa chake, kuna upanga uwao uwao wote wenye makali kuwili (Tazama Waebrania 4:12).

2. Ufunuo 2 na 3, tunasoma kuhus barua ambazo ziliandikwa makanisa saba.

A. Yohana anatumia barua hizi kueleza hali ya makanisa haya yote. Kila kanisa leo linapaswa kujichunguza kulinagana na baraua hizi.

Tutazama mawazo ya kristo juu ya makanisa haya.

i. Makanisa ya Smirna na Filadelfia yalikuwa makanisa ambayo yalikuwa mazuri.

ii. Makasi ya Sardi na laodikia yalikuwa na makossa mengi sana.

a. Ufunuo 3:4-5, hata katika makanisa ambayo yalikuwa hayaendelei vizuri sana, Mungu alikuwa na watu humo ambao walikuwa waaminifu kwake.

iv. Makanisa matatu ya Efeso, Pergamo na Thiatira hayakuwa na ukakamavu. Wakati mwingine yaliendelea vyema na wakati mwingi hayakuendelea vyema.

B. Hatuwezi kusoma kila barua kwa ndani sana, lakini kuna mwelekeo wa makanisa haya ambao tunapaswa kujifunza kutokana nao.

i. Utanguliza

ii. Yohana analisifu kanisa. Lakini halisifu kanisa la sardi na Laodikia kwa sababu ya mwenendo wao haukuwa mzuri.

iii. Yohana hakuyakemea makanisa ya Smirna na Filadefia.

iv. Yesu kupitia kwa Yohana anapeana maagizo kwa kila kanisa.

v. Yesu alipeana ahadi kwa makanisa haya.

3. Ufuno 4, maoni ya Mungu akiwa ameketi juu ya kiti chake cha Enzi. Maada ya sura hii ni nguvu kuu za Mungu katika kuumba kila kitu. Yohana alichukuliwa katika maono mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Hapa alihakikishi kwamba haijalishi ni nini ambacho kitafanyika, Mungu bado ameketi juu ya kiti cha Enzi na anawatala kla kitu. Tutatazama yale ambayo Yohana aliona.

A. Mistari ya 2-3, tunasoma kuhusu Mungu akiwa ameketi juu ya kiti chake cha enzi.

B. Mstari wa 4, tunasoma kuwahusu wazee 24.

C. Mistari ya 6-11, tunasoam kuwahusu Viumbe 4. Hawa viumbe huenda ni Cherubim ambao Ezekeili aliona katika Ezekieli 1L10. Katika Ufunuo 10 tunaona kwamba kila mtu mbinguni anamsifu Mungu. Mstari wa 11, ni vizuri kuumbuka katika maombi yetu.

4. Ufunuo 5, tunasoma kuhusu nguvu za Mungu wokovu Yohana anapoendelea kueleza yale ambayo alikuwa anayaona mbinguni.

A. Mistari ya 1-4, tunasoma kuhusu lakiri saba. Lakiri hizi ziko na ujumbe hatari ambao unahusu matukio ambayo yanakuja kufanyika. Kuna kilio kwa sababu hakuna mtu ambaye anaweza kuzifungua lakiri hizi.

B. Mistari ya 5-6, tunasoma kumhusu Kristo ambaye ni simba wa kabila la Yuda na ambaye ndiye Mwana-konodoo.

Kuitwa simba ni dhihirisho la nguvu na Mwana-kondoo dhihirisho la sadaka ambayo ndiye ili leta ushindi. Katika kitabu hiki chote Kristo Yesu anafafanuliwa kama Mwana-kondoo.

i. Mstari wa 5, tunasoma kwamba yule ambaye ana nguvu za kufungua lakiri saba ni Kristo Yesu pekee.

ii.mstari wa 6, pembe 7 zinadhihirsha mamlaka na macho saba yadhihirisha kuwa na hekima yote.

C. Mistari ya 8-14, ni nyimbo za sifa.

5. Ufunuo 6, lakiri za kwanza 6. Zinadhihirisha baadhi ya mateso na majaribi. Kuna wengi ambao wanawaza kwamba haya mamabo hayametendeka. Ishara hizi zinafuata mpangilioa ambayo Yesu alizungumza kuhusu katika Mathayo 24.

A. Mistari ya 1-2, lakiri ya 1. Farasi mweupe, wengi wanawaza kwamba huyu ni Kristo, lakini huenda huyu ni mpinga Kristo. Mathayo 24:3-5, tunasoma kuwahusu walimu wa uongo ambao wanakuja kuwadanganya watu.

B. Mistari ya 3-4, tunasoma kuhusu lakiri ya pili. Farasi mwekundu anadhihirisha vita vya wazi. (Soma Mathayo 24:6).

C. Mistari ya 5-6, tunasoma kuhsu lakiri ya tatu. Farasi mweusi anadhihirisha janga la njaa. (soma Mathayo 24:7).

D. Mistari ya 7-8, lakiri ya nne. Farasi wa kijivujivu ambaye alidhihirsha kifo ambacho kilisababishwa na vita na njaa. Mstari wa 8, tunasoma kwamba robo ya watu wa ulimwengu watakufa (Soma Mathayo 24:7-8, kuhusu vita).

E. Mistari ya 9-11, lakiri ya tano. Tunasoma kuhusu wale ambao waliuliwa kwa sababu ya imani. (Soma Mathayo 24:9-13).

F. Mistari ya 12-17, lakiri ya sita. Tunasoma kuhusu maangamizi dunia mzima kama matetemeko ya aridhi .

6. Ufunuo 7, tunasoma kuhusu repoti mbinguni kwamba kuna kikundi cha watu ulimwenguni ambacho kitalindwa (mstari wa 3). Hii inazungumza kuhusu kulindwa kiroho.

A. Mstari ya 4-8, tunasoma kuhusu 144,000 ambayo wengi wanaona kama idadi ya wale Wayahudi ambao wataokolewa.

B. Mistari ya 2-3, watu wa Mungu watawekwa au wamewekwa ishara ya kuonyesha kwamba wao ni wa Mungu.

C. Mistari 9-17, tunasoma kuhusu wale ambao wataokolewa. Katika mstari wa 9 tunaona kwamba wale ambao wataokolewa watakuwa umati mkubwa sana na watatokla katika kila taifa la ulimwengu huu.

7. Ufunuo 8, tunasoma kuhusu lakiri ya saba ikifunguliwa.

A. Mstari wa 1, kwamba baada ya kufunguliwa kwa lakiri ya saba, kulikuwa na kimya mbinguni kwa nusu saa. Hii ni kwa sababu lakiri hii iko na mapigo ya tarumbeta saba ambayo ni mabaya sana kuliko yale sita.
B. Sura hii inaeleza kuhusu maangamizi ambayo yatatukia kwa sababu ya tarumbeta nne za kwanza.

i. Katika mstari wa 7, tunasoma kuhusu tarumbeta ya kwanza ambayo inahusu kuhusu uharibifu wa kilimo. Haijulikani kama mstari huu unahusu ulimwenguni kote au nchi ya Palastine pekee. The first trumpet in verse 7 tells us that one third of the vegetation will be destroyed.

ii. Katika mstari wa 8, tarumbeta ya pili ilipopigwa, theluthi ya bahari alikuwa damu.

iii. Katika mstari wa 10, tarumbeta ilipopigwa, nyota kubwa iliyokuwa ikiwaka kama taa, ikaanguka kutoka angani, ikaangukia theluthi ya mito na chemichemi za maji na maji hayao yakawa chungu.

iv. Katika mstari wa 12, tunasoma kwamba tarumbeta ya nne ilipopigwa, theluthi ya jua, mwezi na nyota, zikapigwa na ikawa giza.

C. Mstari wa 13, tarumbeta 3 zingine zinatangaza kwamba mambo mabaya sana yanakuja.

8. Ufunuo 9, tunasoma kuhusu tarumbeta ya 5 na 6. Matangazo yake ni mabaya sana.

A. Katika mistari ya 1-11, tarumbeta ya 5, inatangaza kwamba kuna pigo kubwa sana ambalo ni kuja kwa nziga. Hizi ni nziga ambazo zinauma kama ngee lakini hufi. Hii itakuwa mateso

makubwa sana. Nguvu zake zitakuwa kwa miaka mitano na wale wataumwa watasikia uchungu mkubwa sana na wale ambao wataumwa watakuwa wanatamani kufa kama njia ya kuepuka uchungu.

i. Mstari wa 4, tunasoma hawa nzige hawawezi kuwaumiza watu wa Mungu. Watu wa Mungu wamewekwa mhuri (Ufunuo 7:2-3).

B. Mistari ya 12-21, tunasoma kuhusu tarumbeta ya 6 ambayo inatanagaza hatari ya 2.

i. Hatari ya 2, italeta mateso mengi sana kwa sababu theluji moja ya watu itakufa. Kumbuka Ufunuo 6:8 ambapo tunasoma kwamna robo ya watu watakuwa wamekufa.

ii. Hata baada ya taabu hizi, mstari wa 20-21, wale ambao walikuwa wanendelea kuishi walikataa kutubu na kutoka katika njia zao ovu.

9. Ufunuo 10, lakiri ilifunguliwa kati ya tarumbeta ya 6 na ile ya saba. Malaika ambaye alikuwa na lakiri anadhaniwa kuwa Kristo.

A. Mstari wa 6, unasema kwamba mambo haya hayatakawiya, yatafanyika kwa wakati ufao. Wale ambao wanafanya mabaya watapata kwamba wakatai wao wa kuendelea katika uovu, unaendelea ukiisha na wakati wa hukumu kukaribia.

B. Yohana aliamurishwa kwamba badala ya kusoma lakiri ile, alifaa kuikula. Aliambiwa kwamba lakiri hiyo itakuwa kama asali katika mdomo wake, lakini itakuwa chungu sana katika tumbo lake.

i. Lakiri hiyo kuwa chungu ni ishara kwamba kuna habari zingine kuhus mateso zaidi.

ii. Utama wa asali ni ishara ya ushirika mzuri ambao wale tumeokoka tuko nao pamoja na Mungu.

10. Ufunuo 11:1-14, mashahidi wawili wanaendelea na maoni ambayo walipewa. Tarumbeta ya 7 11:15-19. Mambo katika maono haya hayawezi kufahamika kwa rahisi.

A. Mstari wa 3, tunapata mashihidi wawili ambao hawatambuliwi. Kuna wengi ambao wanasema kwamba ni Musa au Eliya, au Enoki. Hawajatajwa. Hawa ni wakilishi wa Mungu.

I. Kama katika Yohana 10:1-11, wakati tunasoma kuhusu mchungaji mwema, tabia yao inapaswa kuigwa na wakristo wote. Kila mkristo anapaswa kuwa tayari kuteswa n ahata kuuliwa kwa ajili ya Kristo.

B. Tunaona hapa kwamba Mungu atakuwa na watu wake kila wakati ahata katika hali ambazo ni mbaya sana. Mfano leo ni kanisa la Kristo ambalo kila siku linapitia mateso makali sana katika nchi nyingi ulimwenguni. Kulingana na utafiti, wakristo 250,000 wanauliwa kila mwaka kwa ajili ya imani katika Kristo.

C. Katika mistari ya 5-6, tunaona kwamba Mungu anawalinda hawa washihidi wawili kwa miaka mitatu na nusu, hadi kazi yao ilipokamilika.

D. Mstari wa 7, tunasoma kwamba wakati kazi yao inamalizika, Mungu anakubali adui wao awaue. Hawa mashihidi wawili walikuwa wamechukiwa sana kiwango kwamba hata miili yao iliachwa katika barabara za mji ili kila mtu aione. Mstari wa 10, tunasoma kwamba watashangilia kwa sababu hawa walikuwa wameuliwa. Hii inatukumbusha kwamba ulimwengu unachukia kanisa.
E. Mistari ya 11-12, tunasoma kwamba Mungu aliwafufua hawa washindi wawili na kuwaleta mbinguni. Hapa tunapata fundisho kwetu ambao tumeokoka jinsi tunapaswa kumtumikia Mungu kwa ujasiri sana hata kama tutateseka na kuteswa, kwa sababu Mungu ni mwaminifu. Mungu atatuleta mbinguni. Kuuliwa kwa mkristo si kushindwa, bali ni ushindi katika Kristo.

f. Mstari wa 14, ndio mwisho wa tarumbeta ya 6 na hatari ya pili. Hatari ya tatu karibu inakuja.

11. Ufunuo 11:15-19, tarumbeta ya saba ilipigwa.

A. Mstari wa18, tunaona hukumu ya mwisho na katika mistari ya 15,17, tunaona ushindi wa Mungu.

B. Mstari wa 19, tunasoma kuhusu kufunguliwa kwa hekalu la Mungu na kufunuliwa kwa sanduka ambcho ndicho kilikuwa kitu cha thamini katika hema. Kufunuliwa kwa sanduku hili ni ishara kwamba Mungu amefunua utukufu na huruma wake kwa watu wote. Kujifunua kwa Mungu kunadhihirisha ukuu wa nguvu za Mungu na kufanywa upya kwa kila kitu (22:1-22:5)

12. Ufunuo 12, tunasoma mwanamke, mtoto na joka.

A. Mwanamke ni ishara ya Israeli. Katika mstari wa 2, tunapata maono ya Isaya 66:7-8 kuhusu mwanamke (Israeli) akimzaa mwana wa kiume likiwa limetimika. Katika mstari wa 5, tunasoma kwamba mwana wa kiume na Yesu ambaye angetawala ulimwengu wote.

B. Mistari ya 3-4, tunasoma kuhusu joka la rangi nyekundu ambaye ni shetani kulingana na mstari wa 9. Joka hili ni ishara za nguvu za giza mstari wa 4. Tunajua kwamba shetani ana nguvu nyingi sana kutuliko sasa wanadamu na hatuwezi kamwe kumshinda kwa nguvu zetu. Yeye tunaweza kumshinda kwa uwezo wa nguvu za Mungu pekee (Waefeso 6:10-18).

C. Mistari ya 7-12, tunasoma kuhusu vita huko mbinguni wakati shetani alitupwa chinni duniani. Mstari wa 5, tunasoma kuhusu ushindi wa Kristo Kalivary dhidi ya shetani. Tunahimizwa kwamba shetani ameshindwa vita. Kulingana na Luke 10:18, tunajua kwamba shetani alikuwa ana ruhusiwa kuingia mbinguni, lakini sasa hana ruhusa hiyo tena. Lakini hata kama shetani amepoteza vita hivi, yeye bado anaendelea kupigana. Katika mstari wa 9, tunasoma kwamba lengo lake ni kuongoza ulimwengu wote dhidi ya Mungu.

D. Mistari ya 13-17, tunasoma kusoma kutoroka kwa mwamke katika jangwa. Baada ya shetani kushindwa na Kristo, sasa anajaribu kuwaangamizwa watu wake, lakini hataweza.

i. Mstari wa 15, tunasoma kwamba shetani anajaribu kuwaangamiza kwa kuwadanganya.

ii. Mstari wa 16, dunia inamlinda mwamke. Kiumbe cha Mungu, kinamzuia shetani na mipango yake kwa njia tofauti tofauti ili asiliangamizi kanisa.

iii. Mstari wa 17, tuna soma kwamba shetani anaendelea kuwatesa wakristo.

13. Ufunuo 13, tunasoma kuhusu majitu wawili. Majitu haya mawili yanaelezwa ambayo kulingana na mstari 4, ulimwengu utaabudu majitu haya.

A. Ufunuo 13:1-10, tunasoma kuhusu jitu la kwanza. Mstari wa 7 unasema kwamba jitu hili lifanya vita dhidi ya kanisa. Hii inazingatia kanisa nyakati ambazo zimepita na nyakati za sasa. Mateso yako kila wakati. Kuna wakati ambapo mates ohayo ni makali sana. Leo mateso ni makalisa nan a karibu ya Kristo yesu kurudi, mateso yatazidi na yatakuwa makali zaidi.

B. Mistari ya 11-18, tunasoma kuhusu jitu la pili. Hili jitu si kama lile la kwanza. Tunasoma kwamba hili jitu linafanana kama mwana-kondoo. Majitu haya mawili yanafanya kazi ya shetani. Shetani anajidhihirisha kuwa kama Mungu.

i. Katika mistari ya 13-14, tunaona kwamba shetani anadanganya kwa kujifanya kwamba yeye anafanya kazi ya Roho Mtakatifu. Jitu hili linaiga kazi ya Roho Mtakatifu ambayo tunasoma kuhusu katika kitabu cha matendo ya Mitume.

ii. Jitu hili la pili linaendeleza kuabudu kwa jitu la kwanza (Ufunuo 13:12), kama tu vile Roho Mtakatifu anaendeleza kuabudiwa kwa Kristo Yesu.

C. Mstari wa 15, tunasoma kwamba wale ambao hawataabudu jitu hili watauliwa. Hivi ndivyo mfalme Nebukaduneza na Warumi walivyowafanyia wakristo. Mstari wa 15-16, tunasom a kwamba wakristo watalazimishwa kuhusika katika ibada za sanamu. Kwa mfano wakristo wanatoa kondi katika nchi mingi na pesa hizi zinatumika katika kuwauwa watoto wachanga ambao wazazi wao hawawataki wazaliwa. Pesa zingine zinatumika katika shule za uma amabzo hazitambui ukuu wa Mungu na zinapinga Biblia na mafundisho yake. Hii ni kama wale ambao wanafundisha kwamba tulitoka kwa wanyama.

D. Katika mistari ya 13-17, tunasoma kuhusu alama ya jitu. Alama si alama ambayo itaonekana na macho ya kiasili. Yaani ni alama ya kiroho. Hii inamaanisha kwamba mtu badala ya kujitoa kwa Kristo, yeye amejitoa kwa shetani na anamtumikia shetani.

E. Mstari wa 18, tunasoma kuhusu 666, kuna vitabu vingi ambavyo vimeandikwa ili kueleza kuhusu nambari, lakini hayao yote hakuna mtu ana uhakika.

14. Ufunuo 14, tunasoma kuhusu Mwana-kondoo na wafuasi wake.

A. mstari wa 15, tunasoma kuhusu 144,000, hii ni ishara ya wale ambao wameokoka katika ukamilifu wao wote. Idadi hii ni mfano wa wakristo wote.

i. Katika mstari wa 2, tunasikia sauti zikitoka mbinguni ambazo ni sauti za watakatifu ambao wanamwabudu Mungu.

ii. mstari wa 3, tunasoma kwamba ni wale ambao wameokoka ambao wanauwezo wa kumwimbia Mungu wimbo mpya. Ukweli ni kwamba wale ambao hawajaokoka, hawawezi kamwe kushirika katika kumwabudu Mungu kwa kweli au kufahamu Biblia. Kuabudu kwa kweli ni kwa wale ambao wameokolewa na Kristo.

B. Katika mistari ya 6-7, tunasoma kuhusu malaika ambaye ana ujumbe wa injili wa milele. Hii inaweza kuwa furusa ya mwisho kwa wale ambao hawajaokoka kusikia neno la Mungu na kuja kwa Kristo Yesu.

C. Mstari wa 8, tunasoma kuhus kuanguka kwa babeli. Babeli ndiye anaye yaongoza mataifa mengi katika dhambi. Yeye anaenda kuanguka.

D. Mistari ya 9-12, wale wote ambao wanaabudu jitu badala ya kumwabudu watahukumiwa na Mungu. Katika mistari ya 11-12, tunafafanuliwa kuhusu hatari ya hukumu ya Mungu kwa wale ambao wanaambudu jitu.

E. Mstari wa 13, tunasoma kuwahusu wale ambao wanakufa wakiwa wameokoka. Tazama tofauti ya hatima ya wale ambao wanakufa wakiwa ndani ya Kristo na wale ambao wanakufa wakiwa nje Kristo.

F. Mistari ya 14-20, tunasoma kuhusu yule ambaye anakaa kama Mwana wa Adamu. Hii ni mfano wa kurudi kwa Kristo ambapo atawakusanya watu wale pamoja. Hiki kifungu kinahusu kuwahukumu wale ambao hawajaokoka na jinsi hatima yao ni mbaya sana.

15. Ufunuo 15-16, tunasoma kuhusu bakuli 7 ambazo zimejawa na ghadhabu ya Mungu. Ufuno 15, tunasoma kuhusu bakuli hizi ambazo zimejawa na mapigo ambayo ndio hukumu ya Mungu ambayo inavunja nguvu za babeli. Babeli ni mwunganiko wa wanasiasa na walimu wa uongo.
A. Ufunuo 15:2-4, tunsoam kuhusu wimbo wa washindi. Hawa ni watakatifu ambao wanafurahia kwa sababu ya ushindi wa Mungu na haki ya Mungu. Mojawapo wa maada ya kitabu hiki ni kwamba kuna watu wa aina mbili: Wale ambao hawajaokoka na wanaenda jahanum na wale ambao wameokoka wataishi katika furaha ya milele.

B. Mabakuli saba ambayo yametajwa katika mstari wa 7, yamejawa na ghadhabu ya Mungu na ndio yanakamilisha ghadhabu ya Mungu.

C. Mstari wa 8, tunasoma kwamba hema limefungwa. Hii inamaanisha kwamba hakuna mtu ambaye anaweza kuingia na kuzuia ghadhabu kwa sababu siku za maobi zimeisha.

D. Ufunuoa 16:2-9, tunasoma kuhushu mabali ya manne ya kwanza. Mabakuli haya ya ghadhabu yalimwaga humu duniani.

i. Ya kwanza ni vidonda ambavyo vinauma sana ambavyo vinawatokea wale wote ambao wanaabudu jitu badala ya kuwabudu Mungu.

ii. Bakuli la pili, liliua kila kitu katika bahari.

iii. Mito na vijito badala ya maji kutoka, damu ndio ilitoka humo kwa sababu bakula la pili.

iv. Bakuli la nne liliwafanya watu wachomeka sana na mot ambao ulisababishwa na jua kali sana.

v. Hata baada ya haya yote, watu bado walikataa kutubu na kuokoka.

E. katika Ufunuo 16:10-11, tunasoma kuhusu bakuli la tano. Ambalo ni giza kuja juu ya nchi nzima. Hata baada ya haya na uchungu kutoka na ghadhabu ambazo zilitangulia, watu waliendelea kumlaani Mungu na kukata kutubu.

F. katika mistari ya 12-16, tunasoma kuhusu bakuli la 6 ambalo linazungumza kuhusu kukutana pamoja kwa madui wa Mungu ili wapigana na Mungu katika vita vya mwisho Amagedoni. Vita hiv vilitabiliwa katika Zaburi 2:2-4.

G. Katika mistari ya 17-21, tunasoma kuhusu bakuli la 7, ambalo linakamilisha ghadhabu zote za Mungu. Mungu alitumia mawe na mtetemeko wa ardhi wenye nguvu sana kuwashinda maadui wake hata kabla ya vita venyewe kuanza.
16. Ufunuo 17, tunasoma kuhusu jumbe wa kwanza wa malika. Tunasoma kuhusu babeli ambaye nidye kahabu mkuu ambaye anawaongoza watu katika dhambi ya zina (mstari wa 4). Kuangamizwa kwa babebli ni mfano wa kuangamizwa kwa nguvu za giza. Babeli hapa si mji, bali jina ambalo linadhihirisha ulimwengu ambao ni mwovu sana.

A. Mistari ya 1-2, haya ni maoni ya hukumu ambayo ilkuwa inakuja kwa babeli na wale ambao walidanganywa naye.

B. Katika mistari ya 3-4, Yohana alipelekwa mahali ambapo aliona kahaba ambaye ni mfano wa dhambi za ulimwengu huu. Kwa muda mfupi katika mstari wa 4, anafurahia vitu vya ulimwengu huu.

i. Mstari wa 4, vita vya nje vimewadanganya kwamba wao wako sana ilhali kiroho wao wako katika hatari kubwa sana.

ii. Mwanake huyu yeye anahidi na kupeana kila aina ya furaha ya ulimwenguni lakini furaha hii ni ya muda mfupi sana na matuko yake ya milele ni mabaya sana.

iii. Warumi 6:23, tunasoma kwamba mshahara wa dhambi ni mauti. Fuaraha ya kukutana kimwili na mtu ambaye ana ukimwi, ni ugonjwa ambao hauna tiba. Utumiaji wa madawa

huonekana kwamba uleta furaha sana, lakini huwafanya wale ambao wanatumia madawa haya kuwa na maisha mabaya sana.

C. Mstari wa 5, unatukumbusha kwamba babeli ni mfano wa miji ambayo imekuja pamoja kumpinga Mungu.

D. Mstari wa 6, dhambi ya babeli kuu ni kuwaua watu wa Mungu.

E. Mistari ya 7-8, tunasoma kuhusu ujumbe wa malaika ambao ni uangamizaji wa babeli.

i. Mstari wa 7, tunaona kwamba mailaka wanatumika kufafanua mambo ambayo hatuelewi sisi.

ii. Mstari wa 8, kuhusu kutumia maneno ambayo yamedhihirisha Mungu, yanatumika na jitu. Maneno haha yanatoka katika Ufunuo 4:8: Mtakatifu Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana Mungu, aliyekuwako, aliyeko na atakayekuja. Jitu linatumia maneno haya kubishana na Mungu juu ya kutawala kila kitu.

iii. Mstari wa 8, watu ambao majina yao hayajaanidikwa katika kitabu cha uzima, wao wanaendelea kuongozwa vibaya na jitu.
iv. Mstari wa 9, tunasoma kuhusu milima ambayo inadhihirisha falme ambazo zimepita na zile za sasa.

v. Mstari wa 10, tunasoma kuwahusu wafalme 7.

vi. Mstari wa 12, tunasoma kuwa wafalme wa mbeleni ambao pamoja na wale wapinga Kristo watapokea nguvu na mamlaka kutoka kwa shetani wakati wa mwisho. Mstari wa 13, uansema kwamba wataungana pamoja.

vii.mstari wa 14, tunasoma kwamba Mwana-kondoo anawashinda kwa sababu Yeye ni Bwana wa bwana na Mfalme wa wafalme.

17. Ufunuo 18, kuna ujumbe ambao unatangaza kuanguka kwa babeli. Mji ulianguka kwa sababu ulikuwa umewaweka watu wa Mungu katika utumwa. Hapa babebli ni mfano wa miji ya ulimwengu ambayo ni miovu sana.

A. Katika mstari wa 2, kuna ujumbe wa pili wa malaika ambao ni maangamizi ya wale ambao wanampinga Kristo.

B. Ujumbe wa tatu wa malaika unahusu onyo kwa wale ambao tumeokoka. Mstari wa 4-8, tunasoma kwamba Mungu anawaita watu wake watoke katika dhambi. Mungu hataki wale ambao tumeokoka tuendelee katika dhambi za ulimwengu huu.

i. Mstari wa 5, tunasoma kwamba wao walifanya dhambi kila wakati.

C. Ufunuo 18:9-20, tunasoma kuhusu vikundi vitatu vya watu jinsi walivyohuzunika kwa sababu ya babeli. Hawa ni watu ambao walipenda sana tabia ya dhambi ya babeli. Wao walitamani anasa za babebli. Hawa ni watu ambao wamepotea pia hata kama hawakuhisika katika dhambi za babeli. Wao walitamani anasa hizi na hawakukataza babebli kuacha kutenda dhambi.

i. Kwa mfano, wezi wanaamua kuiba mali ya gari moja barabarani. Wanapaokuwa wanaiba, hata wewe unakuja na kuchua ile ambayo imebaki. Ukweli ni kwamba wewe hukupanga kuiba lakini umechukua mali ya wizi.

D. Ufunuo 18:21-24, tunasoma kuhusu ujumbe wa mwishi wa kuangamiza babeli. Uangamizi huu ni wa milele.

Tunaelezwa kuhusu anasa za hapo mbeleni ambazo zimekwisha milele.
i. Sura hii inamaliza kwa kusema kwamba uangamizi huu wa bebeli ulisababishwa na jinsi wao walivyoshughulikia watu wa Mungu.

18. Ufunuo 19, tunasoma kuhusu kuangamizwa kwa jitu na walimu wa uongo.

A. Mistari ya 1-10, kila mtu mbinguni anafurahia juu ya kushindwa kwa adui wa Mungu.

B. Mstari wa 7, tunasoma kuhusu upendo wa karibu sana kati ya Kristi na watu wake.

C. Mstari wa 8, mavazi mazuri ambayo ni matendo ya watakatifu wa Mungu.

D. Mstari wa 9, wale ambao wameokoka ni wa Mungu na ndio wamealikwa kwa karamu na Mwana-kondoo wa Mungu.

E. Mistari ya 11-16, tunasoma kuhusu kuja kwa Kristo akiwa juu ya farasi mweupe.

i. Mstari wa 11, Kristo atarudi humu duniani.

F. Katika msitari ya 17-21, tunasoma kuhusu vita vya mwisho vya maangamizi ya jitu na walimu wa uongo. Tunasoma kwamba adui wa Mungu watadharauliwa na miili yao italiwa na ndege wa angani. Wao watatupwa jahanum.

19. Ufunuo 20, tunasoma kuhusu milenia na hukumu. Vile unavyofahamu milenia inataegemea ufahamu wako juu ya miaka 1000.

A. tunaona kwamba mwishowe Mungu alishinda uovu. Tunasoma kuhusu miaka 1000 ambapo shetani na watu wake watakuwa wamefungwa. Yaani hawateweza tena kufanya uovu wao. Wakati Kristo na watu wake watatawala (Isaya 11:6).

B. Mistari ya 1-3, kwa 1000 shetani atakuwa amefungwa (Luka 8:31) na hataweza kutatiza watu.

C. Mistari ya 4-6, tunasoma kuhusu utawala wa Kristo na kanisa lake. Hii inaweza kuwa si miaka 1000 vile sisi tunaona. 2 Petro 3:8, anasema kwamba Mungu haesabu miaka kama sisi.

i. katika mstari wa 4, tunasoma kuhusu vita vya enzi vya hukumu ambavyo ni vita vya watakatifu ambao watatawala Kristo.

D. mstari wa 7-10, shetani anashindwa kabisa. Shetani anaachiliwa kutoka gerezani na anajaribu kuchua utawala. Lakini wakati huu tunasoma kwamba anashindwa kabisa.

i. Mstari wa 8, shetani alipofunguliswa anajikusanyia jeshi kubwa. Gogi na Magogi katika Ezekieli 38-39, ni mfano wa adui wa Mungu ambao walitoka kasikazina. Je, hawa madui wa Mungu wote walitoka wapi? Jibu ni kwamba hawa watu waliihsi wakati wa Milenia na walikuwa na uhuru wa kufanya uamuzi. Kama Adamu na Hawa, wao walichugua kutotii Mungu. Somoni alisema hakuna kipya chini ya jua. Hali ya asili ya mwanadamu nu kuchagua dhambi. Tumaini letu kutoka kwa dhambi ni Kristo pekee.

i. Mstari wa 10, mahali ambapo shetani atakuwa milele na wale ambao wanamfuata. Hatima ya mtu ambaye anakataa kumwamini Kristo ni mbaya sana.

E. Katika mistari ya 11-15, tunasoma kuhusu hukumu ya mwisho juun ya ulimwengu (Mathew 25:31-46; Danieli 7:9-10; Zaburi 7:6-8; 47”8-9).

i. Paulo anazungumza kuhusu hali hii (Warumi 2:16), siku ambayo Kristo atawahuku watu. Kuna watu wa aina mbili dunia; wale wameokoka na wale ambao hawajaokoka. Kila jina na mtu ambaye ameokoka, limo katika kitabu cha uzima. Mstari wa 15, wale ambao hawamo katika kitabu cha uzima watatupwa jahanum.

20. Ufunuo 21:1-8, baraka za mkristo. Mbingu mpya nan chi mpya. Tunahimizwa sana wakati tunasoma mambo haya kuendelea kumwamini Kristo hata wakati tunapitia majaribu makali sana.

A. Kuna hukumu mara mbili. Mstari wa 20 na mstari wa 21.

B. Kuna maoni tofauti tofauti kuhusu mbingu mpya nan chi mpya. Hapa ni mahali ambapo hakuna dhambi.

C. Tutazame baadhi ya baraka ambazo zimetajwa hapa.

i. Mstari wa 3, tutaishi na Mungu

ii. Mstari wa 4,hakutakuwa na huzuni au uchungu. Kila kitu ktakuwa kipya (mstari wa 5).

iii. Mstari wa 5, haya ni ya watakatifu wote.

iv. mstari wa 8, hatari ya wale ambao wanakufa bila kuokoka.

21. Ufunuo 21:9-22:5, tusoma kuhusu Yeruslemu mpya.
A. Mstari wa 9, Yohana alipelekwa kama bibi arusi. Kuna furaha katika uwepo wa Mungu.

B. Mstari wa 11, Yerusalemu mpya ikon a utukufu wa Mungu.

C. Ufunuo 21, tutashughulikiwa na Mungu.

D. Ufunuo 22:1-3, mambo yatakuwa kama yalivyo katika Edeni. Lakini sasa tutakuwa kila tunda kwa kila mtu. Mstari wa 3, hakutakuwa na chochote ambacho kimelaniwa na Mungu.

22. Ufunuo 22:6-21, maandishi ya biblia yanaishia hapa.

A. Mistari ya 5-16, umuhimu wa kitabu hiki. Hili ni neno la Mungu na halipaswi kupuuzwa.

i. Mstari wa 6, maneno ya Biblia ni ya kweli kwa sababu ni maneno ya Mungu.

ii. Mstari wa 10, tunapaswa kusoma Biblia na kujifunza Biblia.

iii. Mstari wa 11, wale wameenda jahanum hawatoki humo na wale wameenda mbinguni nao hawatoki humo. Kila atakapoenda ni kwa sababu alifanya uamuzi huo.

iv. Mistari ya 14-15, kutawanyika kwa wale ambao wameokoka na wale ambao hawajaokoka milele.

v. Mstari wa 16, unabii wote unatuelekeza kwa kristo pekee (Hesabu 24:17).

B. Ufunuo 22:17, mara ya mwisho watu wanalikwa kwa Kristo.

C. Mistari ya 18-19, pamoja na Kumbukumbu la torati 4:2, onyo hatufai kuongeza lolote kwa maneno ya Biblia. Chochote Mungu anataka tujue kumhusu kiko katika Biblia. Hakuna ufunuo mpya kutoka kwa Mungu na hautawahi kuwepo. Lazima tufundishe na tutii tu kile ambacho Mungu ametupatia katika neno lake.

i. Mungu huzungmza nasi kupitia kwa Biblia na wala si ndoto au maono.

ii. Lazima tutii kila kitu ambacho biblia inafundisha. Warumi 1:26-27, tunasoma kwamba dhambi ya usenge ni mbaya, na watu hawafai kuifanya kama tu dhambi zingine zote. Kuna wachungaji na wengi ambao wanadai kwamba ni watu wa Mungu ilhali wanaishi maisha ya dhambi.
D. Mstari wa 20, Kristo anaahidi kurudi tena.

E. Mstari wa mwisho wa Biblia ni baraka ambayo ianapeanwa kwetu. Hii ni baraka kutoka kwa Mungu kwa watu wake. (Hesabu 6:23).